NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

## Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 10 Mei, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Tukae, Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. *(Makofi)*

**MHE. MATTAR ALI SALUM (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):**

Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. *(Makofi)*

**MHE. CECIL D. MWAMBE (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Maji na Umwagiliaji juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Maswali, tutaanza na Ofisi ya Rais (TAMISEMI) na swali linaulizwa na Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 175

### Changamoto ya Wodi ya Wazazi Hospitali ya Vwawa (Mbozi)

**MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza:-

Hospitali ya Vwawa Wilayani Mbozi inakabiliwa na changamoto kubwa ya uhaba wa vitanda vya kulalia wajawazito pamoja na vile vya kujifungulia, pia wodi ya akinamama ni ndogo huku ukizingatia kuwa hospitali hiyo inahudumia Wilaya ya Mbozi na Momba:-

Je, ni lini Serikali itajenga wodi ya akinamama kubwa yenye vifaa vya kutosha ili wanawake hawa waondokane na adha ya kulala wawili wawili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa

Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Wilaya ya Mbozi yaani Vwawa ni hospitali iliyopandishwa hadhi kutoka Kituo cha Afya kuanzia mwaka 2001. Kwa sasa hospitali hiyo inahudumia wagonjwa wengi kutoka Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Wilaya za Momba, Mbozi na Ileje. Ili kuboresha huduma ya uzazi katika hospitali hiyo, Serikali katika mwaka wa fedha 2017/2018, imepanga kutumia jumla ya shilingi milioni 180 kwa ajili ya ukarabati wa wodi ya wazazi baada ya kujifungua (*post natal ward)* ambayo itakuwa na uwezo wa kuhudumia wagonjwa wengi kwa wakati mmoja na kuondoa msongamano uliopo hivi sasa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, swali la nyongeza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Waziri japokuwa niseme kwamba majibu haya hayaridhishi na wala hayajatosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la msingi nilitaka kujua kwamba Serikali ina mpango gani wa kujenga wodi mpya ya akinamama katika Hospitali hii ya Wilaya ya Mbozi ukizingatia kwamba hospitali hii inahudumia wilaya mbili mpaka sasa. Hali halisi ilivyo pale kuna vitanda 25 tu vya akinamama vya kulala baada ya kujifungua lakini kwa siku wanawake wanaozalishwa katika hospitali hiyo ni wanawake 42 mpaka 50. Kwa hiyo, kukarabati hili jengo hakuwezi kusaidia. Kwa hiyo, swali langu la msingi nataka kujua kwamba Serikali ina mpango gani wa kujenga wodi ya akinamama mpya na kubwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, katika swali langu la msingi pia nataka kujua kwamba Serikali ina mpango gani wa kujenga Hospitali ya Wilaya ya Momba? Hili jambo nimekuwa nikilipigia kelele sana katika Bunge hili kwamba mpaka sasa Wilaya ya Momba hawana Hospitali

ya Wilaya. Hali hiyo inapelekea usumbufu sana kwa sababu mara nyingi wanalazimika kuja kutibiwa katika hospitali ya Mbozi ambayo pia nayo jengo lake ni dogo. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie ni lini sasa Serikali itajenga Hospitali ya Wilaya ya Momba? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, haya yote yanatokana na *needs* za Wabunge wenyewe tunavyokaa katika vikao vyetu. Kwenye vikao vyetu ndipo ambapo tunaweka *priority* nini kifanyike. Eneo hili *priority* ya kwanza imeonekana ni lazima tutenge shilingi milioni 180 kwa ajili ya kufanya ukarabati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niseme mipango hii yote inaanzia kwetu sisi Wabunge katika maeneo yetu tunapofanya *needs assessment* au tunapopanga mipango yetu. Hata hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Juliana kwa jinsi anavyopigania haki za akinamama na watoto Serikali tutafanya kila liwezekanalo kuona jinsi gani tutafanya kwa sababu pale Vwawa sasa hivi ndiyo kama Makao Makuu. Licha ya ukarabati huu, lakini tutaangalia nini kingine kifanyike lengo kubwa ni akinamama na watoto hasa wanaozaliwa waweze kuwa katika mazingira salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Hospitali ya Momba, niliongea na Mkuu wa Mkoa wetu wa Songwe, Mama Chiku Gallawa wakati tunafanya mikakati ya ukarabati wa vituo vya afya 100, hili jambo aliweka kama *priority* na aka-*identify* kwamba Momba haina Hospitali ya Wilaya. Tulibadilishana mawazo tukaona lile eneo la awali ambalo limepangwa kuwa Makao Makuu ya Halmashauri ya Momba kile kituo cha afya cha pale tukiwekee miundombinu ya kutosha ili wananchi wa eneo lile waweze kupata huduma ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Juliana kwamba tutafanya kila liwezekanalo kuhusiana na hoja hii na kwamba katika Makao Makuu ya Momba tunaenda kufanya uwekezaji mkubwa sana ndani ya kipindi hiki hiki kabla ya mwezi wa saba. Kilio cha wananchi wa pale ni kwamba wanapata shida na Serikali tumesikia kilio hiki, tutaenda kufanya kazi kubwa na ya kutosha kuwasaidia akinamama na watoto wa maeneo yale. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Matatizo yaliyopo Momba ni sawa kabisa na matatizo yaliyopo katika Mkoa wa Kigoma ikiwa ni katika Wilaya ya Kakonko na Buhigwe. Wilaya hizo ni mpya na zimekuwa zikipata huduma kutoka kwenye Wilaya Mama. Ni lini Wilaya ya Kakonko na Buhigwe zitapatiwa Hospitali ya Wilaya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, anavyosema Mheshimiwa Mbunge Genzabuke ni kweli Kakonko wanatumia Kituo cha Afya cha pale Kakonko, hali kadhalika Buhigwe hawana Hospitali ya Wilaya. Kipindi kile nilivyofika Kakonko na Buhigwe tulifanya makubaliano fulani juu ya nini kifanyike kama mipango ya awali kurekebisha hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika,pale Buhigwe kwanza tunaenda kufanya ukarabati mkubwa wa Kituo cha Afya cha Buhigwe kwa kukipatia wodi ya upasuaji na wodi kubwa ya wazazi na vifaa vyote vinavyowezekana. Jambo hili tunalipanga kama Mungu akijalia kabla ya mwezi Agosti tutakuwa tumelitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tutashirikiana na wenzetu wa Kakonko kuona ni jinsi gani tufanye, lakini nikifahamu fika kwamba jana nilikuwa naongea na Wabunge wahusika wa maeneo haya na Mheshimiwa Mbunge pia na tuliona hata ikama ya Madaktari walioenda kule ni wachache na katika mchakato ule wa ajira zitakazokuja hapo baadaye tutaongeza idadi ya wataalam kwa sababu ukiachia miundombinu lakini suala la *human resources* ni jambo la msingi. Haya yote kwa Mkoa wa Kigoma tutayapa kipaumbele ili wananchi wa mkoa huu waweze kupata huduma za afya ya msingi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, swali la nyongeza.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tatizo linalowakabili wananchi wa Mbozi kwenye suala la Hospitali ya Wilaya kwa kiasi kikubwa linafanana na la Hospitali ya Wilaya ya Hai katika Mkoa wa Kilimanjaro. Hospitali hii ya Wilaya ya Hai ilianza kujengwa zaidi ya miaka 10 iliyopita wakati huo Mji wa Hai ukiwa na wakazi wasiofika 10,000 na Mji wa Hai leo ni mji unaokua kwa kasi kuliko miji yote katika Mkoa wa Kilimanjaro ikiwa katika kipindi cha miaka kumi, Mji wa Hai umefikisha zaidi ya wakazi 50,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali hii imekuwa inajengwa awamu kwa awamu lakini kuna tatizo moja kubwa la msingi ambako wanaume na wanawake wanalala katika wodi moja. Jambo hili nimeli-*witness* mwenyewe na nimetembelea hospitali hii wiki iliyopita kushuhudia hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachomwomba Naibu Waziri katika hatua ya sasa, kutokana na hali ya unyeti wa hospitali hii na ikiwa vilevile ni hospitali ambayo iko katika barabara kuu ya Arusha-Moshi ambayo inahudumia wagonjwa wote wanaopata ajali katika barabara ile, rai yangu kwa Mheshimiwa Waziri ni kutenga muda wake tuweze kutembelea pamoja hospitali hii kwa pamoja tuone uzito

wa tatizo lililopo kisha Serikali itutafutie ufumbuzi wa kudumu kuhusu tatizo hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niseme takriban wiki tisa kama sio kumi zilizopita nilikuwa pale Hai. Nilienda kuitembelea hospitali ile na niliweza kubaini mchakato mkubwa unaofanywa na injinia wetu katika lile jengo la akinamama linalojengwa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nimefarijika na nimefurahi sana kwa mkakati uliopangwa. Kwa kutumia hizi *Force Account* kazi kubwa inafanyika pale. Kwa hiyo, jambo la msingi ni kwamba kama Serikali pale kuna kazi kubwa tunaendelea kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme nimekubali wazo hilo la kwenda pamoja lakini tayari nimeshakwenda na tumesha-*identify* na nimeshatoa maelekezo nini wanatakiwa wafanye. Namshukuru sana *DMO* wetu pale kwa kazi kubwa inayofanywa na menejimenti ya hospitali ile. Hata hivyo, nimetoa maagizo sasa waangalie rasilimali zilizokuwepo kama majengo yaliyokuwepo pale nini kifanyike, wapange mpango mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa tunayokwenda kufanya ni kukamilisha lile jengo kubwa linalojengwa ambalo ni la mfano na mimi nimetolea mfano hata nilivyokwenda Siha kule nikawaambia kwamba igeni kwa wenzenu wa Hai kwa kutumia *Force Account,* kutumia fedha ndogo na kufanya mabadiliko makubwa katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeweka nguvu kubwa pale. Hata hivyo, nina mpango wa kwenda Hai na Waziri wangu amepanga hilo kwa sababu Mheshimiwa Rais ameshaelekeza lazima tukahakiki suala

zima la matumizi ya fedha na miundombinu ya barabara, kwa hiyo, tutakwenda tuone jinsi gani tutafanya ili hospitali ile iweze kuwahudumia vizuri wananchi wetu wa Hai.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndasa, swali la nyongeza.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Matatizo yaliyopo Mbozi Vwawa yanafanana sana na Kituo cha Afya cha Malya. Kituo cha Afya cha Malya kinahudumia Maswa, Malampaka na Kwimba. Kwa sababu Kituo cha Afya cha Malya kwa sasa kimezidiwa, miundombinu ya majengo na vyumba vya kusaidia wazazi havitoshi, Serikali ina mpango gani sasa wa kuwekeza angalau adha zilizopo pale ziweze kupungua?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), majibu mafupi tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii sehemu ya Kwimba ina Majimbo mawili, Jimbo la Mheshimiwa Ndassa na Mbunge mwingine lakini ukiangalia hospitali yetu ya wilaya na kule anakosema Malya ni kweli. Ndiyo maana naomba nimshukuru Mheshimiwa Mbunge, katika *initiative* zake za kutusumbua mimi na Waziri wa Afya alileta Kituo hiki cha Afya cha Malya kiweze kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi TAMISEMI tumeshapitisha bajeti yetu na Wizara ya Afya imeshapitisha yao ni kwamba sasa hivi tunaenda kufanya uwekezaji mkubwa katika Kituo cha Afya cha Malya. Naomba nimhakikishie kwamba ombi lake kama Wizara ya Afya na Wizara ya TAMISEMI tumelichukua, tunaenda kufanya ukarabati mkubwa. Katika vile vituo 100 na Malya ni kimojawapo, tunaenda kuwasaidia wananchi wa jimbo lake.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako sasa aulize swali lake.

Na. 176

## Ahadi ya Kuboresha/Kuchimba Bwawa la Maji –Makambako

**MHE. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Mwaka 2014 Rais wa Awamu ya Nne alipokuja Makambako aliahidi kutoa Sh.600,000,000/= ili zisaidie kuboresha au kuchimba bwawa la maji Makambako litakalotoa huduma ya maji kwa wananchi wa mji huo:-

Je, ni lini fedha hizo zitatolewa ili zifanye kazi iliyokusudiwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Awamu ya Kwanza ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji imekamilisha usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya mradi wa maji Makambako. Mradi huu utahusisha ujenzi wa bwawa eneo la Tagamenda, chujio la kutibu maji, matanki ya kuhifadhi maji na ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji. Mradi huu unatarajiwa kugharimu dola za Marekani milioni 38. Serikali imepata mkopo wa gharama nafuu kutoka Serikali ya India kwa ajii ya utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali wakati inasubiri utekelezaji wa mradi huo mkubwa imechukua hatua za dharura za kuboresha hali ya huduma ya maji mjini Makambako kufuatia ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu

ya Nne alipotembelea Mji wa Makambako. Mradi huu unakadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi milioni 654. Kazi zitakazotekelezwa kwa mradi huu ni pamoja na ujenzi wa kitekeo, tanki, bomba kuu, pampu ya maji na nyumba ya pampu. Kiasi cha shilingi bilioni mbili kimetengwa katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2016/2017 na zabuni imetangazwa tarehe 4/1/2017 na ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2017/2018.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Naishukuru Serikali kwa namna ambavyo imeonesha nia nzuri ya kutatua tatizo kubwa la maji lililoko katika Mji wa Makambako. Swali la kwanza, kwa sababu Serikali imetenga fedha hizo dola ambazo amezitaja hapo, dola milioni 38, nataka kujua ni lini sasa mradi huu utaanza ili wananchi wa Makambako waepukane na tatizo kubwa wanalopata Makambako na hata wawekezaji wa viwanda inashindikana kwa sababu maji hatuna?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa sababu mradi huu mdogo ambao kama alivyosema tenda imetangazwa ambao ni kwa ajili ya bwawa dogo la Makambako, nilipofuatilia Mkoani wanasema tayari iko Wizarani lakini Wizara bado haijarudisha kule ili mkandarasi aanze kazi. Je, ni lini sasa mkandarasi huyu ataanza kazi kwa mradi huu kwa mwaka huu wa fedha 2016/2017?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza anauliza ni lini huu mradi mkubwa wa dola milioni 38 unatarajiwa kuanza. Kwa faida ya Wabunge wengine ambao watafaidika na mradi huu wa dola milioni 500 za mkopo nafuu kutoka Serikali ya India, niseme kwa sasa hatua inayoendelea tayari Hazina

imekamilisha taratibu za kusaini makubaliano ya fedha kwa maana ya *financial agreement*. Pia Wizara inaendelea sasa kufanya manunuzi ya ma-*consultant* watakaokamilisha usanifu na makabrasha ya zabuni kwa ajili ya mradi huu. Mheshimiwa Deo Sanga baada ya kukamilisha taratibu hizi basi tutaendelea na kutangaza tenda na kuhakikisha kwamba mradi huu unaanza kwenye mwaka wa fedha wa 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu tenda inayoendelea ambayo inafanywa na Halmashauri ya Mheshimiwa Deo Sanga, niseme kwamba kwa vile ametoa taarifa kwamba tayari wameshaleta hizo nyaraka Wizara ya Maji, naomba nifuatilie kama kweli zimeshaletwa na tusimamie ili waweze kurudisha haraka ili shughuli iendelee. Mheshimiwa Sanga naomba tuwasiliane kwa hili.

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Saumu Sakala, swali la Nyongeza.

**MHE. SAUMU H. SAKALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu haya ambayo amejibu Naibu Waziri tatizo la maji ambalo lipo Makambako ni sawa kabisa na tatizo la maji ambalo kwa sasa limejitokeza katika Jiji la Tanga na linaendelea kujitokeza ambapo licha tu ya maji kukatika mara kwa mara bila ratiba na bila taarifa lakini pia maji yale takribani mwezi mmoja sasa yamekuwa yakitoka machafu yenye tope.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili nilimfikishia Mheshimiwa Waziri wa Maji, nilimwandikia barua lakini pia nilikwenda kumwona mimi mwenyewe lakini bado linaendelea na majibu ya uhakika bado hatujapata. Maji yamekuwa yakiendelea kutoka machafu, yakiwa na tope na bado pia yanaendelea kukatika mara kwa mara. Serikali itoe tamko sasa ni lini watu wa Tanga watapata maji safi kama walivyozoea na maji ambayo hayakatikikatiki? Ahhsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mbunge alikuja kwangu akilalamikia hali ya maji kuwa na tope katika Jiji la Tanga. Jiji la Tanga ni mojawapo la mamlaka katika nchi ambayo imekuwa siku zote inatoa maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichojitokeza ni kwamba kumetokea hitilafu katika mtambo wa uchujaji maji na hii imetokana na uchafuzi mkubwa wa maji kule kwenye vyanzo kwa sababu wamevamia wachimbaji wa madini kwa hiyo maji yanakuja na tope na rangi. Kwa hiyo, imebidi sasa tutengeneze *design* nyingine ya kuchuja maji yale na tatizo lile tumeshalimaliza sasa hivi Tanga wanapata maji safi kama walivyokuwa wanapata zamani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mary Nagu swali la nyongeza.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Kama ilivyo kwa Bwawa la Makambako, Wizara ya Maji iliahidi Wilaya ya Hanang' kuchimba Bwala la Gidahababieg kwa miaka saba. Naomba niulize ni lini bwawa hilo litachimbwa ili wale watu waliopata matatizo kwa miaka mingi waweze kupata maji? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge ambaye pia ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji, Kilimo na Mifugo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli bwawa hili amekuwa analipigania kwa muda mrefu lakini katika bajeti ya mwaka huu tutaanza kwanza kufanya usanifu ili tuweze kujenga bwawa hilo. Baada ya kujua gharama ya ujenzi ni kiasi gani na michoro itakuwa namna gani, basi tutajenga bwawa hilo kwa mwaka huu wa fedha unaokuja 2017/2018.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litauliuzwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Subira Mgalu.

Na.177

**Mradi wa Umwagiliaji wa Masengwa**

**MHE. SUBIRA K. MGALU (K.n.y. MHE. AZZA H. HAMAD)** aliuliza:-

Je ni lini Serikali itakamilisha ahadi ya kuchimba Bwawa la Mradi wa Umwagiliaji Masengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, skimu ya umwagiliaji ya Masengwa ambayo ilijengwa kati ya mwaka 2004 na 2006 chini ya Programu Shirikishi ya Kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji, ina eneo lililoboreshwa lipatalo hekta 325. Hata hivyo, eneo linalolimwa linafikia hekta 800. Aidha, kutokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi, tumeshuhudia ukame hali ambayo imewafanya wakulima wawe na hitaji la kujengewa bwawa kwa ajili ya kutunza maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hitaji hilo, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara yangu kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Kanda ya Mwanza, imetenga fedha kwa ajili ya kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kutoa gharama halisi kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hilo. Aidha, Wizara ilikwishaainisha maeneo yote nchini yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na kuandaa mpango kabambe wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji

wa mwaka 2002 *(National Irrigation Master Plan)*. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi, hivi sasa Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Japan inaendelea na mapitio ya mpango huo ambao utahusisha ujenzi wa mabwawa madogo, ya kati na makubwa kwa nchi nzima.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza na namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la upembuzi yakinifu limekuwa likijibiwa hata Bunge la Kumi kwenye swali hili la msingi na kwa kuwa hata majibu ya msingi ya swali hili yameonesha hakuna hata kiwango cha fedha kilichotajwa waziwazi kutengwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018, hali inayopelekea wasiwasi wa utekelezaji wa kazi hii. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuambatana na Mbunge Mheshimiwa Azza kutembelea eneo hili la Masengwa ili asikie kilio cha wananchi hawa na ikizingatiwa Mkoa huu wa Shinyanga umekuwa ukiendelea kunyemelewa na janga la ukame?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa matatizo ya maji ya Halmashauri ya Shinyanga yanafanana kabisa na matatizo ya maji ya Halmashauri ya Chalinze yanayotokana na kusuasua kwa mradi wa Chalinze Wami Awamu ya Tatu na kwa kuwa mradi huu pia ulitembelewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu miezi miwili iliyopita na kutoa maelekezo kwa mkandarasi kukamilisha kazi hii kwa siku 100. Je, mpaka sasa Wizara imefikia hatua gani katika ufuatiliaji wa maelekezo ya Waziri Mkuu ili tatizo la maji linaloikumba Halmashauri ya Chalinze hususani Mji wa Chalinze, Ubena na maeneo mengine lipate majibu? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Subira kwamba utaratibu wa utekelezaji wa miradi huwa unaanza na hatua ya awali ambao kwa lugha ya kigeni tunaita *basic concept* baada ya hapo tunakwenda kwenye *feasibility study*. Kumekuwa na lugha ya kiujumla ambayo inafahamika kwa wengi (usanifu wa awali). Kwa hiyo, hiyo iliyokuwa inatajwa mwanzoni ilikuwa ni kwa ajili ya *basic concept* sasa ni kweli tunaenda kwenye *feasibility study* ambao ni usanifu wa awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia amesema hajaona fedha iliyotengwa Mheshimiwa Mbunge leo ndiyo tunaanza kusoma bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2017/2018. Asingeweza kuiona kabla ya hapo lakini kwa leo baada ya kuanza kusoma bajeti nina uhakika ataona tunaelekea wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa ameomba pia tuambatane na Mheshimiwa Azza, ni kazi ya mimi Naibu Waziri kuhakikisha kwamba natembelea Majimbo na Halmashauri zote kujionea utekelezaji wa miradi ya maji safi na salama pamoja na miradi ya umwagiliaji. Kwa hiyo, asiwe na wasiwasi hata huko Shinyanga nitafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa amezungumzia utekelezaji wa mradi wa Chalinze, kwanza nimwambie kwamba sasa hivi mkandarasi ana kasi kubwa ya utekelezaji wa mradi wa Chalinze. Mheshimiwa Waziri pamoja na mimi tunapata taarifa kila siku na taarifa ya jana ni kwamba mkandarasi amefikisha asilimia 44.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni kweli Mheshimiwa Waziri Mkuu alitembelea pale na wakati ule tulitamka siku 100 za kumpima mkandarasi, tunakupa siku 100 ili tuone kama utaongeza *speed* basi tutaendelea na wewe. Sasa anaendelea kuthibitisha kabla ya hizo siku 100 kwamba ameongeza kasi. Kama ataendelea hivyo, tutaendelea naye kuhakikisha kwamba mradi ule unakamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aisharose Matembe, swali la nyongeza.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa wanannchi wa Jimbo la Manyoni Mashariki wanategemea maji ya mabwawa na visima na kwa muda murefu sana wamekuwa wakitaabika na kero kubwa ya ukosefu ya maji safi na salama. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Jimbo la Manyoni Mashariki linapata maji safi na salama kwa uhakika? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumekamilisha awamu ya kwanza ya utekelezaji wa program ya maji hapa nchini na tumeanza awamu ya pili Julai mwaka huu 2017. Tumeweka utaratibu wa kutenga fedha kwa kila Halmashauri ili zenyewe zihakikishe kwamba zinabuni na kutekeleza miradi ya maji. Zaidi ya hapo, kuna bwawa kubwa tumejenga katika Halmashauri ya Manyoni Mashariki ambalo lile litafanya kazi mbili, moja ni umwagiliaji kwa ajili ya kilimo cha mboga mboga, lakini pili litasaidia katika maji ya matumizi ya majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge wala asiwe na wasiwasi, tunaendelea na utelekezaji kuhakikisha kwamba wananchi wa Manyoni Mashariki wanapata maji. Nimshukuru kwa sababu yeye ni mama wananchi wake wa Singida anawapenda ndiyo maana anawatetea. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, swali la nyongeza.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza kwa Waziri Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi takribani wiki mbili inakwenda ya tatu sasa Shinyanga, Kahama maji hayatoki. Wale watu wanatumia maji ya kununua hakuna maji kabisa. Tatizo inasemekana kwamba hamjalipa bili ya umeme kama Mheshimiwa Rais alivyoagiza. Mheshimiwa Waziri wale watu wanapata shida, hivi ni lini mtarudisha yale maji ili watu waendelee ku-*enjoy* tunu za Taifa hili? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wiki mbili zilizopita Mamlaka nyingi za maji zimekumbwa na tatizo la kukatiwa umeme hivyo kufanya mitambo ya kuzalisha maji isifanye kazi, hii ni kwa Shinyanga pamoja na maeneo mengine pia. Kutokana na tatizo hilo, tarehe 8 Wizara ya Maji, Hazina na Mkurugenzi wa *TANESCO* walikaa kikao na kuna makubaliano ambayo yamefikiwa. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya muda mfupi suala hili litatuliwa ili liwe na ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda Mheshimiwa Mbunge ajue kwamba ni kweli kabisa kwamba Mamlaka zimekuwa hazilipi bili za umeme na kama Mamlaka hazilipi bili za umeme *TANESCO* itakufa. Kwa hiyo, tumeweka utaratibu kwamba tuhakikishe tunalipa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wamekuwa na nia nzuri kabisa ya kuwatetea wananchi wao, wengine wanasema kwamba bili ni kubwa na kadhalika lakini bila kuweka bili ya kiwango ambacho kitawezesha hizi Mamlaka ziweze kujiendesha wenyewe tatizo hili tutaendelea kuwa nalo. Kwa hiyo, naomba sana *EWURA* wanapopita kufanya hesabu za maji tuwe waangalifu tunapojaribu kuziingilia zile kwa sababu zinatusababisha tufike kwenye hii hali ambayo tumefika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa suala la lililopo kule Masengwa linafafanana kabisa na bwawa ambalo Serikali imetuahidi katika Kata ya Mnazi na Kivingo kule Lushoto. Je, ni lini sasa Serikali itatenga fedha kuanza mradi huo wa uchimbaji mabwawa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza eneo la Lushoto ni zuri sana, ni *green*, lina mvua za kutosha na linafaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Sasa hivi Wizara yetu imepata fedha kutoka Serikali ya Japan na inashirikiana na wataalam wa Serikali ya Japan kupitia mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba unaainisha maeneo yote yaliyotambuliwa kwa kilimo cha umwagiliaji ili uweze kuweka mkakati na kuweka mbinu kama nilivyozungumza kwenye swali moja la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika huo mpango ambao tunatarajia ukamilike mwaka 2018 maeneo yote yataainishwa na matatizo mengi ambayo yamejitokeza yataangaliwa ili tuhakikishe tunajenga miundombinu ambayo itawezesha kilimo cha umwagiliaji. Nimhakikishie Mheshimiwa Shangazi kwamba katika kazi hii inayoendelea tutahakikisha kwamba tunafika mpaka Lushoto.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Gibson Ole Meiseyeki, Mbunge wa Arumeru Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na.178

### Vyombo vya *PPRA* na *TEMESA* katika Halmashauri

**MHE. GIBSON B. OLE-MEISEYEKI** aliuliza:-

*PPRA* na *TEMESA* vimekuwa vyombo vinavyoisababishia Halmashauri zetu hasara kubwa katika

utekelezaji wa miradi katika utengenezaji magari na mitambo badala ya kusaidia Serikali katika kutimiza majukumu yake kwa bei nafuu:-

Je, Serikali haioni umefika wakati wa kuvifuta vyombo hivyo au kuvibadilishia utaratibu wake wa kufanya kazi ili viweze kuwa na tija kwa Taifa letu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gibson Blasius Ole-Meiseyeki, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Ufundi na Umeme (*TEMESA*) umeanzishwa chini ya Sheria Na. 30 ya mwaka 1997 ya Wakala. *TEMESA* ina majukumu ya kusimamia matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo ya Serikali, matengenezo ya mifumo ya umeme, elektroniki na viyoyozi kwenye majengo ya Serikali pamoja na kutoa huduma ya uendeshaji vivuko vya Serikali na ukodishaji wa mitambo. Aidha, *TEMESA* hutoa huduma za ushauri wa kitaalam kwa Serikali kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013, *TEMESA* ina jukumu la kutoa huduma zake kwa Serikali. Katika kuboresha utendaji wa *TEMESA*, Serikali kila mwaka imekuwa ikiwekeza katika kuboresha karakana za *TEMESA*, ikiwemo kuongeza vitendea kazi vya kisiasa na kuajiri wataalam wenye ujuzi wa magari na mitambo ya kisasa. Kwa sasa *TEMESA* ina jumla ya Wahandisi 78 na mafundi 344. Serikali pia imebadilisha Menejimenti ya *TEMESA* kwa lengo la kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali itahakikisha kuwa huduma za *TEMESA* zinaboreshwa na kutolewa kwa ufanisi bila urasimu wowote kwa kufuata Mkataba wa

Huduma kwa Wateja na Mwongozo wa Matengenezo ya Magari ya Serikali. Vilevile, Serikali itaendelea kusimamia *TEMESA* ili kuhakikisha kuwa kuna usimamizi wa karibu wa ubora wa matengenezo ya magari na karakana zake zinatumia vipuri halisi katika matengenezo ya magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa inayoikabili *TEMESA* ni madeni makubwa ambayo wakala unadai Wizara, Taasisi za Serikali na Halmashauri. Mpaka sasa *TEMESA* inazidai taasisi hizo zaidi ya shilingi bilioni 11. Kuchelewa kulipwa madeni haya kunaipunguzia *TEMESA* uwezo wa kutoa huduma. Napenda kutumia fursa hii kuzitaka Wizara, Taasisi za Serikali pamoja na Halmashauri zote zinazodaiwa na *TEMESA* kulipa madeni yao haraka kabla Serikali haijachukua hatua stahiki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gibson Ole-Meiseyeki, swali la nyongeza.

**MHE. GIBSON B. OLE-MEISEYEKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa matokeo ya utekelezaji kazi wa Wakala hawa wa Serikali imekuwa tofauti kabisa na makusudio ya uundwaji wa sheria hizi, nikiwa na maana kwamba vyombo hivi vinaisababishia Halmashauri na Taasisi za Serikali usumbufu mkubwa wa ucheleweshaji wa utengenezaji wa mitambo lakini pia gharama kubwa za utengenezaji wa mitambo hiyo ukilinganisha na bei zilizoko kwenye masoko ya kawaida. Kwa mfano, *TEMESA* haina kabisa karakana na wataalam wa kutengeneza mitambo yetu hii, kwa maana hiyo Wakala hawa wamekuwa kama kupe wa kufyonza fedha za Serikali badala ya kuisaidia Serikali kuweza kutengeneza miradi kwa gharama nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliuliza kwenye swali langu la msingi kwa nini isifanyiwe marekebisho ya utekelezaji wao wa kazi ili sasa iweze kuleta tija na maendeleo ya haraka katika maeneo yetu badala ya kuweka vyombo ambavyo

vinasababisha gharama kubwa katika utekelezaji wake wa kazi. Kwa hiyo, swali langu linabaki pale pale, kwa nini Serikali isibadilishe utaratibu wa utekelezaji kazi wa mamlaka hizi ili kuweza kuleta tija na ku-*save* fedha badala ya kusababisha gharama kubwa mara mbili, tatu ya gharama sahihi zilizoko mitaani? Kwa nini utaratibu wa utekelezaji wake wa kazi usibadilishwe? Ahsante *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa Mheshimiwa Mbunge nikuambie mimi nimeitumia *TEMESA,* nilikuwa Meneja wa *TANROADS* na nilikuwa Wizara ya Ujenzi, kwa hiyo *TEMESA* naielewa vizuri kwa undani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema kwamba *TEMESA* imekuwa na usumbufu, gharama kubwa na ucheleweshaji, hayo anayoyazungumza ni kweli. Ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimesema kwamba *TEMESA* sasa hivi uongozi umebadilishwa na karakana zilizopo zinaboreshwa kwa kuwekewa vifaa vilivyo bora. *TEMESA* ilikuwa na shida ya namna ya kutumia sheria mliyoiunda ninyi Wabunge ya *PPRA*, sasa hivi wamewekwa wataalam ambao wataitumia ile sheria vizuri. Sheria ni nzuri sana lakini kulikuwa na wafanyakazi ambao sio waadilifu na Serikali hii ya Awamu ya Tano imechukua hatua ya kuhakikisha kwamba inawaondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge wazo lake la kusema chombo hiki kwa sasa kibadilishwe, ukianza kuunda kingine leo utaanza tena kuwafundisha mpaka wafike huko watakakofika. Sasa hivi hawa tayari wameshaiva, tunahakikisha wanaboreshwa ili *TEMESA* iwe na ufanisi mzuri kuliko *garage* nyingine yoyote ya kawaida. Naomba atupe muda na tushirikiane tuendelee kutekeleza suala hili.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe, sasa aulize swali lake.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Kawe, naomba swali langu namba 179 lijibiwe pamoja na marekebisho. Nilikuwa namaanisha taa za kuongoza magari, vilevile taa zile za barabarani kwa ajili ya kutoa mwanga kwenye barabara. Kwa hiyo, ajibu katika muktadha huo.

Na. 179

**Changamoto za Barabara ya Mwenge- Tegeta**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Barabara mpya ya Mwenge- Tegeta kwa kiwango fulani imesaidia kupunguza tatizo la foleni ingawa ina changamoto kadhaa kama kukosekana kwa taa za kuongoza magari kunakosababisha ajali za mara kwa mara; nyakati za mvua barabara hujaa maji sababu ya udogo wa mapokeo na matoleo ya maji ya mvua hususan eneo la Makonde - Mbuyuni hali inayohatarisha uhai wa wananchi na barabara yenyewe; kuna maeneo hatarishi sana ambayo Serikali inatakiwa ama kuweka matuta au vivuko vya waenda kwa miguu ili kuzuia ajali, miongoni mwa maeneo hayo ni eneo la Bondeni (Jeshini Kata ya Mbezi Juu) karibu na njia panda ya kwenda Kawe:-

Je, ni lini changamoto hizi zitapatiwa ufumbuzi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Mbunge Halima James Mdee, Mbunge wa Jimbo la Kawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua umuhimu wa taa za kuongoza magari kwenye makutano ya barabara zetu ili kusaidia kupunguza ajali hususan barabara ya Mwenge-Tegeta. Mkandarasi wa ujenzi wa taa za kuongoza magari kwenye makutano ya Afrikana tayari amepatikana na anatarajia kuanza kazi wakati wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu udogo wa mapokeo na matoleo ya maji ya mvua yanayosababisha kero katika eneo la Makonde hadi Mbuyuni, Serikali inakamilisha taratibu za kusaini mkataba wa ujenzi wa mtaro mkubwa eneo la Mbezi Samaki Wabichi ambao utatatua kero ya barabara kujaa maji nyakati za mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kivuko cha waenda kwa miguu eneo la Kawe Bondeni hadi Jeshini, Kata ya Mbezi Juu na Kawe tayari limeshapatiwa ufumbuzi. Serikali itajenga daraja la juu kwa ajili ya kivuko cha waenda kwa miguu *(Over- Head Pedestrian Bridge)* eneo la Kawe Bondeni. Kwa sasa mkandarasi wa kujenga daraja hilo yupo kwenye hatua za maandalizi *(mobilization)* kwa ajili ya kuanza ujenzi.

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Halima Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya Waziri yanaonesha kwamba watajenga mtaro mkubwa Mbezi Samaki lakini kuna eneo lingine ambalo ni hatarishi na sasa hivi kutokana na mvua zilivyonyesha liko kwenye hali mbaya sana na barabara inaweza ikakatika, ni eneo la Afrikana - Salasala - Kinzudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili tumeshafanya ziara mara kadhaa na Mkurugenzi wa *TANROADS* Mkoa tukashauriana kwamba wauweke mtaro mkubwa, lakini vilevile waweke utaratibu wa kujenga hata mita mia za lami kwenda mbele kwa sababu ile barabara inahudumiwa na Halmashauri ili kuweka mapokeo makubwa ya maji vilevile kuokoa ile barabara. Sasa napenda

Mheshimiwa Naibu Waziri anijibu mahsusi kwa eneo la Afrikana - Salasala - Kinzudi ambapo sasa hivi barabara imechimbika sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni mwaka wa tatu mfululizo Manispaa ya Kinondoni haijapata fedha za Mfuko wa Barabara kutokana na makosa yaliyofanywa na ma-*engineer* wetu ambao walijenga barabara chini ya kiwango. Matokeo yake ni kwamba wananchi wa Kinondoni ikiwemo Jimbo la Kawe wanaathirika kwa sababu barabara ziko katika hali mbaya sana. Hawa ma-*engineer* wameshapewa adhabu zao, wengine wamesimamishwa kazi, wengine wamehamishwa vituo. Nataka Waziri atuambie ni lini fedha husika za miaka mitatu zitakuwa *released* ili maboresho ya barabara za Kinondoni yaweze kufanyika na kupunguza kero ya wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la tafsiri ya mradi, nini maana ya mradi? Mradi unaanza na *basic concept, feasibility study, detail design,* ujenzi lakini mradi pia una *operation* na wakati wa *operation* ni *operation and research.* Nikiri kwamba Mheshimiwa Mbunge aliyoyasema ni kweli, ile barabara na mimi naitumia. Kwanza yeye ni Mbunge wangu maana nakaa Kinondoni. Tangi Bovu, Afrikana, Kilongowima na maeneo mengine maji yanapita pale lakini kipindi cha *operation and research* tayari mpaka sasa hivi Wizara imeshatambua maeneo hayo na inaanza kuingia mikataba. Kwa mfano, eneo la Tangi Bovu mkandarasi amepatikana kwa maana sasa ya kuboresha na kupanua ile sehemu ya kupitisha maji katika eneo la barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo lingine kwamba *TANROADS* inashughulikia eneo la hifadhi yake na kwa eneo lile hifadhi ni mita 80, 40 kila upande kutoka katikati ya barabara, nje ya hapo ni eneo la Halmashauri. Kipindi cha

mvua kutokana na mabadiliko haya, mimi huwa nasema ni mabadiliko ya binadamu, *storm water* yanapotembea yanakuja na takataka nyingi sana zinaingia kwenye yale makalavati zinaziba, matokeo yake sasa maji hayapiti katika dizaini iliyotakiwa yanapita juu ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja yake pia amezungumzia kuhusu *street light,* nazo katika hiki kipindi cha *operation and research need* imeshaonekana. Kwa hiyo, Serikali italifanyia kazi ili wananchi wanaotembea usiku waweze kupata huduma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo hili suala ambalo mwenyewe amekiri kwamba kulikuwa na ubadhirifu na uzembe ama wa wahandisi ama wa watu gani kuhusiana na ujenzi wa barabara, wakajenga barabara ambazo haziko katika *standard* inayotakiwa. Ni kweli, kwani yeye Mheshimiwa Mbunge anapenda? Mtu ambaye anafanya kitu ambacho hakiko kwenye *standard* inayotakiwa lazima achukuliwe hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala kwamba fedha za Mfuko wa Barabara hazijaja mfululizo kwa miaka mitatu kwangu ni geni. Naomba nilichukue, nitaliwasilisha kwa wahusika ili waweze kuliangalia.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na swali linaulizwa na Mheshimiwa Shaaban Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto.

Na. 180

**Hitaji la Chuo *VETA* Wilaya ya Lushoto**

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Serikali iliahidi kujenga vyuo vya *VETA* kwa kila Wilaya ili kuwasaidia vijana kujifunza stadi za kazi mbalimbali:-

Je ni lini Chuo cha *VETA* kitajengwa katika Wilaya ya Lushoto?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shaaban Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaanza ujenzi katika Wilaya ya Lushoto mara baada ya kukamilisha miradi ya Vyuo vya *VETA* iliyoanzwa. Vyuo hivyo ni pamoja na Ludewa, Namtumbo, Kilindi, Chunya, Ukerewe, hiyo ni kutokana na tatizo la upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inashauri kwamba wakati juhudi mbalimbali zinaendelea za kutafuta fedha na ufadhili wa kujenga vyuo, wananchi wa Lushoto waendelee kutumia Chuo cha *VETA* kilichopo katika Mkoa wa Tanga na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(FDCs)* vilivyopo Muheza na Handeni na vyuo vingine vilivyosajiliwa na Mamlaka ya *VETA* nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shaabani Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa Waziri kunijibu majibu mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijauliza maswali mawili ya nyongeza, nitoe pole kwa wananchi wa Jimbo la Lushoto na Wilaya ya Lushoto kwa ujumla kwa mvua zinazoendelea kunyesha maana mpaka sasa hakuna mawasiliano kati ya Dar es Salaam - Lushoto, Arusha – Lushoto na Tanga - Lushoto. Nimeongea na Meneja wa *TANROADS*

Mkoa akaniambia kwamba atashughulikia suala hilo. Hata hivyo, nikiangalia tatizo lile ni kubwa sana, madaraja yamekatika zaidi ya kilometa 32. Kwa hiyo, nipaze sauti Serikali ipeleke msaada maeneo yale haraka iwezekanavyo ili kunusuru maisha ya wananchi wa Lushoto na uchumi unaotegemea barabara ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa pole hiyo kwa wananchi wangu wa Wilaya ya Lushoto na mkoa mzima kwa ujumla basi niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri amenijibu kwamba kwa kuwa Serikali itaanza ujenzi katika Wilaya ya Lushoto mara baada ya kukamilisha miradi ya Vyuo vya *VETA* vilivyoanza. Je, Serikali haioni kwamba itaendelea kulimbikiza vijana wengi wa Wilaya ya Lushoto bila kupata elimu ya *VETA*?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tayari kuna majengo ya kuanzisha Vyuo vya *VETA* je, Waziri yupo tayari kuongozana nami ili kwenda kuona majengo yale kama yanafaa na kutoa tamko la kuanzisha Chuo cha *VETA*? Hata kama *VETA* hiyo itaanzishwa chini ya mti, lakini naomba wananchi wangu hususani vijana wangu waweze kupata elimu hiyo ya *VETA*, hiyo ndio shida kubwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, si lengo la Serikali kudidimiza Jimbo la Lushoto na kimsingi Serikali imekuwa ikijitahidi kuhakikisha kuwa vyuo vilivyopo vinaweza kudahili wanafunzi wengi zaidi na ndiyo maana kwa sasa badala ya kusubiri tu kujenga chuo kipya, tunaona kuna haja pia ya kuongeza idadi ya mabweni katika vyuo vilivyopo ili kuchukua hata wanafunzi wa mbali. Kwa hiyo, lengo ni kuweza kujenga Chuo cha Lushoto muda muafaka utakapofika na fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kuongozana naye kwenda kuona majengo yaliyopo, kwa moyo mkunjufu kabisa niko tayari na endapo majengo haya yataweza kufaa aidha kwa kutumiwa kama *VETA* au Chuo cha Maendeleo ya Jamii tutafanya hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, Mbunge wa Magu, sasa aulize swali lake.

Na. 181

**Sera ya Elimu Bure**

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA** aliuliza:-

Serikali kwa sasa ina Sera ya Elimu Bure kuanzia chekechea hadi kidato cha nne:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu bure kwa kidato cha tano na sita?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kutoa elimu bila malipo kwa wanafunzi wa kidato cha tano na cha sita na badala yake imejikita zaidi katika kuboresha miundombinu ambayo ni pamoja na upungufu wa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, majengo ya utawala pamoja na kumalizia changamoto za uhaba wa Walimu wa sayansi na vifaa vya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na masuala ya TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa miundombinu hiyo itasaidia kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wenye sifa ya kuingia kidato cha tano wanapata fursa ya kuendelea na masomo yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali pamoja na mikakati mizuri ambayo Serikali inaiweka lakini ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa nina imani kwamba Waziri na Maprofesa wote mlioko ndani humu mmesoma bure *A-Level* na kwa sababu watoto hawa wanachaguliwa, wengine wanashindwa kuendelea na masomo haya kwa kukosa fedha, kwa sababu bado ni watoto wa maskini na wengine wamefaulu vizuri masomo ya sayansi pamoja na hesabu, je, Serikali haioni kwamba inapoteza vijana wazuri ambao wanaweza kusaidia Taifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa hawa watoto wanaochaguliwa kuendelea na *A-level* ni wachache kuliko wale ambao wanahudumiwa na Serikali kwa maana ya *O-Level,* je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka sasa wa kuleta bajeti ili tuweze kuwasaidia watoto hawa wa maskini ili waweze nao kusoma bure wafaidi matunda ya Serikali hii? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Serikali ingependa kusomesha wanafunzi katika ngazi zote za elimu bure endapo uwezo ungekuwa wa aina hiyo. Kama nilivyosema ni kwamba awamu ya mwanzo tuliongeza shule za msingi lakini tukaja tukaongeza shule za sekondari kila kata na sasa

hivi tunaendelea kuongeza shule za kidato cha tano na sita *(A-level)* kwa sababu ni chache ukilinganisha na wanafunzi wanaofaulu na hasa baada ya Serikali kuchukua jitihada za makusudi za kuongeza ubora wa elimu, imekuwa sasa wanafunzi wanaofaulu ni wengi na hivyo hatuwezi kuwaacha bila kupata elimu hiyo. Kwa hiyo, kabla hatujaweza kutoa fedha kwa kuwalipia hiyo ada, ina maana kama hawana sehemu ya kusomea itakuwa bado hatujafanya jambo la msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili la kuongeza bajeti, hilo ni suala letu sote kama Wabunge. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais lakini pia Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye tukonaye humu, Wizara yetu ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni kati ya Wizara ambazo zinapewa kipaumbele cha hali ya juu kwa kupewa bajeti kubwa kuliko Wizara nyingine. Kwa hiyo, naamini Serikali itaendelea kufanya hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Raisa Abdallah Mussa, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Yussuf.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Sasa naomba swali la Ukht Raisa, Namba 182, lipatiwe majibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yussuf, hilo ndio jina lake maana huku kuna Raisa Abdallah Mussa, sasa naona umeongeza jina kabla. Hebu turekebishie ili *Hansard* isome vizuri.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, hicho ni cheo kama Alhaj, Dkt. na mambo mengine.

**NAIBU SPIKA:** Tunaomba umshauri Mheshimiwa Raisa akisajili hicho cheo chake ili tuwe tukikisoma rasmi huku kwenye maswali.

Na. 182

## Kuanzisha Vyuo vya Misitu Nchini

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN (K.n.y. MHE. RAISA ABDALLAH MUSSA)** aliuliza:-

Kutokana na umuhimu wa misitu hapa nchini na kwa kuzingatia kuwa theluthi moja ya ardhi ya Tanzania ni misitu; na kwa kuwa, Serikali ina Chuo kimoja tu cha Misitu cha Olmotonyi ambacho sasa kinakaribia kufikisha karne moja tangu kianzishwe:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha vyuo vingine vitakavyotoa taaluma zaidi ya misitu kwa Watanzania?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raisa Abdallah Mussa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania Bara ina eneo la takribani hekta milioni 48 za misitu sawa na 55% ya eneo lote la nchi kavu lipatalo hekta milioni 88.1. Kwa mujibu wa viwango vinavyoratibiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Chakula na Kilimo, inakadiriwa kuwa Afisa Misitu mmoja husimamia wastani wa hekta 5,000 za misitu hivyo, kwa ukubwa wa eneo la misitu katika nchi yetu kiasi cha wataalam wa misitu 9,600 wenye jukumu la kusimamia misitu moja kwa moja ukiondoa watawala na watumishi wa viwandani na kadhalika wanahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina vyuo vitatu vinavyotoa taaluma ya misitu. Vyuo hivyo ni pamoja na Chuo Kikuu cha Sokoine kilichoko Morogoro ambacho kinatoa

Shahada ya Kwanza, Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu katika Fani ya Misitu; Chuo cha Viwanda vya Misitu kilichopo Moshi, ambacho kinatoa Astashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu na Astashahada ya Teknolojia ya Viwanda vya Misitu na Chuo cha Misitu kilichopo Olmotonyi, ambacho kinazungumziwa na Mheshimiwa Mbunge muuliza swali, nacho kinatoa mafunzo ya Astashahada na Stashahada ya Misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kujali vyuo walivyosoma, taaluma mahsusi ya misitu na ngazi za shahada walizohitimu, katika kipindi cha miaka 10 vyuo nilivyovitaja hapo juu vimeweza kuzalisha jumla ya wataalam 3,500 ambao wameingia kwenye soko la ajira. Kufikia mwaka 2020, Serikali inao mpango wa kuongeza udahili, mara mbili ya viwango vya sasa, katika vyuo vilivyopo kwa kutekeleza, pamoja na mambo mengine, uboreshaji miundombinu ya kufundishia, kuongeza ubora na idadi ya wakufunzi na vifaa vya kufundishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, mipango ya Serikali inaonesha uwezekano mkubwa wa kufikiwa kwa malengo ya kupatikana kwa wataalam wa kutosha kwa idadi na uweledi, kwa sasa Serikali haioni umuhimu wa kuongeza vyuo vingine kwa madhumuni hayo.

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Yussuf, swali la nyongeza.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Mheshimiwa Waziri, mimi kama mtaalam wa misitu, naomba hili swali lijibiwe tena, halikujibiwa, la kwanza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na majibu haya ambayo wataalam wa Mheshimiwa Waziri wamejaribu kuzunguka, unaposema *FITI* ni Chuo Cha Misitu, Chuo cha Nyuki kwa nini umekiacha? *FITI* ni *consumers* siyo misitu. Tukisema *foresters* ni yule ambaye unampa mbegu anakupa *product* ama ya *timber* ama ya *log,* huyo ndiyo mwanamisitu, sio unayempa ubao akafanya *processing. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo, hivi kweli Watanzania tunajiangalia kwamba misitu ina umuhimu kwa maisha yetu na vizazi vyetu na viumbe vingine vilivyomo katika ardhi? Hekta 5,000 kuhudumiwa na mtu mmoja, tuko *serious* kweli? Hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, unaposema katika kipindi cha miaka 10…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yussuf tusaidie, swali la pili uulize bila kuchangia tafadhali, muda wetu unakimbia sana.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa. Swali la pili, unaposema una wanataaluma 3,500 katika kipindi cha miaka 10, ni wastani wa 350 kwa mwaka. Hebu tupe mchanganuo kwa sababu katika vyuo vyote darasa halizidi watu 40 na ni madarasa mawili tena ya *certificate,* wanaochukua *degree* hawazidi watu 50 kwa siku. Kwa hiyo, mnatoaje watu 350 kwa mwaka? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utalii na Maliasili, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la kwanza, pamoja na maelezo mengi ya utangulizi aliyotoa, nililoweza kulinukuu kama swali mahsusi ni kwamba, inawezekanaje hekta 5,000 zikahudumiwa na mtaalam mmoja wa misitu. Dunia inaendeshwa kwa sayansi na teknolojia, wataalam na miongozo mbalimbali. Mawazo na maoni ya mtu mmoja-mmoja yanaheshimiwa lakini yanatakiwa yakae ndani ya utalaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nasoma jibu langu nimenukuu kwamba takwimu hizi au viwango hivi vimewekwa kimataifa na vimewekwa na Shirika la Chakula Duniani la *FAO.* Sasa inawezekana Mheshimiwa Mbunge ana maoni mazuri zaidi kuliko yale ya Shirika la Kimataifa la Dunia, basi

nafikiri maoni yake hayo afuate *channels* zinazofaa ili kuweza kwenda kuboresha hali hiyo kwa namna ambavyo ataona inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, nalo pia ni la takwimu. Anasema inampa mashaka kidogo kuona kama kweli tuna wataalam hao 3,500 kwa kuwa, kwa mujibu wa taarifa alizonazo yeye watalaam wanaozalishwa kwa mwaka kwa vyuo vyote ni 350, sasa ni muda gani utakuwa umepita huo kuweza kupata idadi ya watalaam hawa 3,500. Kwa sababu, hili ni swali linalohusiana na takwimu, swali lake hilo ili niweze kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kuweza kumwambia namna gani tumefikia hapo, basi anione kwa wakati muafaka, hata mchana huu nitaweza kumpa mchanganuo mzuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 183

**Kutangaza Vivutio vya Utalii – Katavi**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Mkoa wa Katavi ni miongoni mwa mikoa ambayo ina vivutio vingi vya utalii kama vile Mbuga ya Katavi yenye wanyama wengi, kivutio cha pekee cha twiga weupe ambao hawapatikani mahali pengine popote duniani:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukitangaza kivutio hiki pekee cha utalii?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Katavi ni miongoni mwa mikoa yenye vivutio vingi vya utalii, vikiwemo Mbuga ya Wanyama ya Katavi, Mti wa Mzimu wa Katavi pamoja na vivutio vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Bodi ya Utalii Tanzania na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania, imekuwa ikitangaza vivutio vya utalii vya Katavi kwa ujumla wake kupitia mitandao na tovuti mbalimbali za kijamii. Aidha, Majarida ya Utalii ya *TANAPA* na *TTB* yanayotolewa kwa lugha za Kiswahili, Kingereza, Kidachi, Kichina, Kifaransa na Kirusi ni sehemu ya njia zitumikazo katika kutangaza utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Majarida hayo ni *Selling Tanzania* na *Explore Tanzania* yatolewayo na *TTB* na *TANAPA Today* na Hifadhi za Taifa Tanzania au *Tanzania National Parks* yanayotolewa na *TANAPA.* Aidha, *TANAPA* hutangaza pia utalii kupitia kipindi maalum kiitwacho Hifadhi za Jamii za Taifa kilichorushwa na Kituo cha Luninga cha Taifa *(TBC).* Kipindi hiki hurushwa kila wiki na kupitia kipindi hiki vivutio vinavyopatikana Hifadhi ya Taifa ya Katavi, kikiwemo kivutio pekee cha twiga weupe hutangazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilika kwa ukarabati mkubwa wa Uwanja wa Ndege wa Mpanda kulikofuatiwa na ujio wa Ndege za Shirika la Ndege la Taifa *(ATCL)* kutasaidia sana kuongezeka kwa idadi ya watalii ambao watatembelea maeneo mbalimbali Mkoani Rukwa, ikiwemo Hifadhi ya Katavi. *TTB* na *ATCL* wanakamilisha matayarisho ya kuanzisha safari maalum za siku za mwisho za juma na siku za sikukuu kwa lengo la kuhamasisha na kuwawezesha Watanzania wengi zaidi kutembelea vivutio vya utalii vilivyoko Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Bodi ya Utalii, Shirika la Hifadhi za Taifa la *TANAPA* na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro itaendelea kuboresha mbinu zilizopo na kubuni mbinu mpya, ili kuimarisha utangazaji wa vivutio vya utalii na hatimaye kuvutia watalii wengi zaidi katika sekta ya utalii nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Restituta Mbogo, swali la nyongeza.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninayo maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya mahusiano ya ujirani mwema *TANAPA* Mkoani Katavi wamejitolea kuchimba visima kwenye vijiji vitatu ambavyo ni Kijiji cha Matandarani, Igongwe na Stalike lakini *condition* yao ni wanakijiji wachangie 30%. Gharama ya hivyo visima ni milioni 21, asilimia 30 itakuwa kama kwenye shilingi milioni saba, wanakijiji watatakiwa wachangie ili waweze kuchimbiwa hivyo visima vitatu. Je, *TANAPA* ili kudumisha mahusiano mema na Mkoa wa Katavi na ukizingatia kwamba kule mkoani kwetu vipato viko chini, wananchi hawana uwezo wa kuchangia hiyo shilingi milioni saba, inaonaje ikachukua hiyo gharama ikachimba bila kuwachangisha wananchi? Hilo swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, je, ni lini *TANAPA* itajenga hoteli ya nyota tatu katika Mkoa wangu wa Katavi ili tuweze kupata watalii kutoka nje na ndani ya nchi? Nauliza hivyo kwa sababu mkoa hauna hoteli ya nyota tatu ambayo inaweza kuwawezesha wageni kutoka nje kuja kutalii mkoa wetu na kuangalia huyo twiga mweupe ambaye hapatikani duniani kokote isipokuwa Mkoa wa Katavi? Ukizingatia kwamba sasa hivi uwanja wetu ni mzuri...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Taska Mbogo. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza la uchangiaji kwenye utekelezaji wa miradi ya ujirani mwema na nafikiri niweke vizuri tu hapa kwamba, *TANAPA* hawajitolei bali wanatekeleza wajibu wao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu kwamba pale ambapo kuna wananchi wanaishi

jirani na maeneo ya hifadhi, mahali ambako utalii unafanyika tunao wajibu wa kuweza kutekeleza miradi mbalimbali chini ya utaratibu wa ujirani mwema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango tulioweka wa kuchangia unawafanya wananchi waweze kwanza kushiriki moja kwa moja kwenye shughuli za uhifadhi lakini pia kujisikia kwamba na wenyewe ni sehemu ya uhifadhi lakini sehemu pia ya kufanya shughuli za maendeleo. Kwa hiyo, kwa kuwa utaratibu huu uko kwa mujibu wa kanuni, ikiwa Mheshimiwa Mbunge ana maoni bora zaidi ya haya aliyotuambia au ana namna bora zaidi ya kueleza kwa kirefu maoni hayo, basi anaweza kuyaleta Wizarani tukapitia utaratibu mzima wa utekelezaji wa miradi ya ujirani mwema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, je, ni lini *TANAPA* itajenga hoteli ya nyota tatu Mkoani Katavi na kwa kweli anauliza kwamba kwa nini *TANAPA* wasijenge hoteli ya nyota tatu ili kuweza kuboresha shughuli za utalii Mkoani Katavi. Kwa ufupi tu ni kwamba, Serikali haijengi hoteli kwa ajili ya matumizi ya watalii au kwa ajili ya matumizi mengine yoyote kwenye sekta ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Serikali ni kuweka mazingira mazuri ya kuwawezesha wawekezaji ambao wanatoka *private sector* kuweza kuwekeza kwenye eneo hilo. Kwa hiyo, nimshauri tu Mheshimiwa Mbunge aungane na Serikali kuwashawishi wadau kutoka mahali popote pale waweze kuja kwenye Mkoa wa Katavi kuwekeza na kujenga hoteli si ya nyota tatu tu, hata kama wanaweza ya nyota nne, nyota tano, ili mradi kuwe na mazingira ambayo yatawawezesha watalii kuvutiwa na kuja kutalii wakiwa katika hali ambayo ni bora zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, Mbunge wa Ushetu, sasa aulize swali lake.

Na. 184

## Msako wa Waganga wa Kienyeji Nchini

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA** aliuliza:-

Polisi wamekuwa wakifanya msako na kamatakamata ya waganga wa kienyeji sehemu nyingi hapa nchini:-

(a) Je, ni waganga wangapi wa kienyeji walikamtwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu?

(b) Je, ni waganga wa kienyeji wangapi walifikishwa Mahakamani na kutiwa hatiani katika kipindi hicho katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, waganga wa kienyeji waliokamatwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu ni 26 na kushtakiwa kwa makosa ya kufanya biashara ya uganga bila kibali na kupatikana na nyara za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015 jumla ya waganga 16 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani. Kati ya hao, waganga saba walipatikana na hatia kwa kufungwa miaka miwili kila mmoja au kulipa faini ambapo jumla ya watuhumiwa sita katika kesi tofauti walilipa faini ya jumla ya Sh.1,250,000/=. Mtuhumiwa wa kesi moja alihukumiwa miaka miwili bila yeye kuwepo Mahakamani, juhudi za kumsaka zinaendelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Elias Kwandikwa, swali la nyongeza.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na pia nimshukuru kwa kutupa Kituo cha Wilaya cha Polisi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Sheria Na.23 ya mwaka 2002 inatoa fursa kwa msajili kwa ajili ya kusimamia hawa waganga wa tiba asili na tiba mbadala lakini kwa kuwa kamatakamata hii imesababishwa na wale waganga wasio waadilifu na hawajasajiliwa ambao kimsingi wamesababisha kuwa na mgongano na kusababisha mauaji ya vikongwe. Kwa mfano, katika Halmashauri ya Ushetu kuna watu 25 wameuawa katika kipindi cha mwaka 2012 na 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa kuwa, kamatakamata hii inaleta usumbufu kwa waganga wanaofanya shughuli hii kihalali, je, Serikali imejipangaje kuliimarisha Baraza hili la Tiba Asili au Tiba Mbadala ili lishirikiane na vyombo vingine kama polisi na kuwaondoa kabisa waganga wanaowachonganisha wananchi na kuwalinda vikongwe hawa dhidi ya mauaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni lini Serikali itafungua vituo vya usajili mikoani ili kurahisisha usajili na kudhibiti waganga hawa na kuweza kushughulikia kabisa wasiokuwa na sifa na kuboresha huduma hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli utaratibu wa kusajili waganga wa kienyeji ambao kimsingi wanasajiliwa na Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Wazee na Watoto, baada ya mganga kuthibitishwa na Baraza hilo ndipo anapatiwa usajili, kwa hiyo, ni utaratibu mzuri tu. Kupitia utaratibu huu na mabaraza haya, nishauri waganga wote ambao wanajishughulisha na tiba asili kujisajili kisheria ili

waweze kutambulika kihalali. Nina hakika watakapofanya hivyo hata kazi ya Jeshi la Polisi kuwabaini waganga wachochezi wanaopiga ramla chonganishi itakuwa ni nyepesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na hoja ya kupeleka vituo hivi vya usajili mikoani, nadhani ni wazo zuri na kama Serikali tutalichukua na tutalifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nafasi ya mwisho kabisa ataipata mwakilishi wa waganga wa kienyeji humu ndani, Mheshimiwa Musukuma. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kutambua uwakilishi wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu nimekuwa nikisikia Wabunge wanalalamika na kuwatetea sana wasanii pindi wanapopata matatizo kwamba tunawatumia kwenye chaguzi lakini baada ya chaguzi hatuwasaidii. Hata hivyo, waganga wa kienyeji kwa karama niliyonayo nikiangalia humu ndani wakati wa uchaguzi wawili, watatu hamkupita kwao labda Mzee Selasini...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilinde.

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Na siyo Wabunge peke yake ni jamii nzima na waganga hawa baada ya chaguzi...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa uliza swali lako.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Sawa Mheshimiwa Spika. Waganga hawa baada ya chaguzi tunawatelekeza na kuwatumia Polisi.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Atutake radhi huyo hakuna Mbunge mchawi humu.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga chuo cha kuwasaidia waganga hata kama ni kwa elimu ndogo? *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, majibu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Musukuma kwa swali lake la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba nchi yetu inathamini na kuheshimu kazi za waganga wa asili na ndiyo maana tumepitisha Sera ya Waganga wa Asili na Tiba Mbadala ya 2002 lakini pia kanuni. Lengo la sera hii ni kuendeleza tiba asili na tiba mbadala kwa sababu ni kweli asilimia 60 ya Watanzania wanatumia huduma za waganga wa tiba asili na tiba mbadala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, siyo tu kujenga chuo lakini tunalo pia Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala ambalo linafanya mafunzo ya mara kwa mara kwa waganga wetu *especial* katika kuhifadhi dawa zao na kufanya ufumbuzi. Sasa hivi tumeweka mfumo mzuri wa kuwasajili waganga wetu, tumewateua ma-*DMO* wote kuwa ni wasajili wasaidizi kwa ajili waganga wetu wa asili na tunaendelea kuwaenzi kwa sababu wana mchango mkubwa sana katika kutatua huduma za afya kwa wananchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Nitaleta kwenu matangazo yaliyotufikia, tunaanza na tangazo linalohusu wageni. Wapo wageni kumi na mbili wa Spika wa Bunge, Mheshimiwa Job Ndugai ambao ni Wabunge wa Bunge la Umoja wa Ulaya wakiongozwa na Mheshimiwa

David Martin – Kiongozi wa Msafara, Mheshimiwa Balozi Roeland Van De Geer - Mwakilishi Mkuu wa Umoja wa Ulaya nchini Tanzania na Afrika Mashariki. Wageni hawa wameambatana na wafanyakazi wa Bunge la Ulaya na Ofisi ya Umoja wa Ulaya nchi Tanzania. *Thank you very much for coming and we believe we will have a chance to chat with you during the cocktail. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Mheshimiwa Injia Gerson Lwenge, Waziri wa Maji na Umwagiliaji kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji wakiongozwa na Injinia Emmanuel Kalobelo ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, Injia Mbogo Futakamba ambaye ni Katibu Mkuu Mstaafu, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Balozi Job Lusinde ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Maji Dodoma na Profesa Nuhu Khatib ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Taifa ya Umwagiliaji. Waheshimiwa Wabunge, pia wameambatana na Wenyeviti wa Bodi, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara, Taasisi, Vitengo na Maafisa mbalimbali waliopo chini ya Wizara hiyo. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wageni wengine wa Mheshimiwa Injinia Gerson Lwenge ni familia yake na ndugu zake ambao wameongozwa na mtoto wake Ndugu Tulalumba Gerson Lwenge. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni mbalimbali wa Wahemishiwa Wabunge pamoja na wanafunzi waliotembelea Bunge kwa ajili ya Mafunzo Bungeni. Karibuni sana wageni wetu pia na wanafunzi tunaamini mtapata mawili, matatu juu ya namna Bunge linavyofanya kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la pili, linatoka kwa Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Tanzania *(TWPG),* anawatangazia Wabunge wanawake wote kuwa leo tarehe 10 Mei, 2017 kutakuwa na kikao kwa ajili ya Wabunge wanawake wote kitakachofanyika katika Ukumbi wa

Zahanati ya zamani ya Bunge. Kikao kitafanyika kuanzia saa 7.00 mchana. Waheshimiwa Wabunge kwa sababu yako makundi mbalimbali pia ambayo yanakutana leo kadri mtakavyoona hapa matangazo, wanawake wote mnaombwa muende kwanza kuhudhuria semina hii ya wanawake wote halafu ndiyo mtawanyike muelekee kwenye mikutano mingine ya makundi mengine. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni ambaye ni Mwenyekiti wa Tawi la *CPA* Tanzania, anawatangazia kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati ya Utendaji ya *CPA,* Tawi la Tanzania leo tarehe 10 Mei, 2017, saa 5.00 asubuhi. Ni kikao cha muda mfupi ukumbi namba 229, ghorofa ya pili, jengo la Utawala. Mheshimiwa Dkt. Chegeni kwa kuwa mnakutana saa tano asubuhi naamini kwamba mmeshapata kibali cha Mheshimiwa Spika maana wakati huo Bunge litakuwa halijasitishwa bado, lakini kikao kimetangazwa saa tano.

Waheshimiwa Wabunge, lipo pia tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza ambaye ni Mwenyekiti wa *Tanzania Young Parliamentary Forum* anawaomba Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe Jukwaa la Wabunge Vijana kuwa leo tarehe 10 Mei, 2017 kutakuwa na semina ya pamoja na ujumbe wa Bunge la Ulaya uliopo hapa nchini. Semina hiyo itafanyika *New Dodoma Hotel* kuanzia saa 7.00 mchana hadi saa 10.00 jioni. Waheshimiwa Wabunge ambao ni wajumbe wa hili jukwaa kwa maana ya kwamba na wao ni Wabunge vijana basi Mwenyekiti wenu anawatangazia mkutano huo. (*Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo lingine ambalo ni taarifa ya mabadiliko ya ratiba ya Mkutano wa Saba wa Bunge. Kamati ya Uongozi imekutana leo tarehe 10 Mei, 2017 kwa ajili ya kujadili mapendekezo ya mabadiliko ratiba ya Mkutano huu wa Saba ili ratiba yetu iendane na mabadiliko ya tarehe ya kusomwa bajeti ya Serikali. Bajeti ya Serikali sasa itasomwa tarehe 8 Juni, 2017 badala ya tarehe 15 Juni, 2017.

Kutokana na mabadiliko hayo, tarehe za baadhi ya Wizara kuwasilisha bajeti zao zitabadilika kama inavyoonekana kwenye ratiba mpya ambayo itasambaswa hapa ukumbini. Aidha, tumeongeza baadhi ya siku za Jumamosi ili zitumike kwa ajili ya shughuli za Bunge. Hata hivyo, mabadiliko hayo hayataathiri siku ya kuhitimisha Mkutano huu ambayo inabaki kuwa tarehe 30 Juni, 2017. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa ajili ya kurahisisha rejea mtakapoletewa hiyo ratiba Jumamosi tatu ndizo ambazo zitaguswa na haya mabadiliko. Jumamosi ya tarehe 13 Mei, 2017; 20 Mei, 2017 na 27 Mei, 2017 kutakuwa na Bunge siku hiyo. Kwa hiyo, ratiba nyingine mtakapoletewa mtagundua mengine yote yamebaki kama yalivyo isipokuwa hizo Jumamosi tatu ndizo ambazo Bunge litaendelea na vikao vyake.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa tunaendelea.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**WABUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaanza kuwataja ili mseme miongozo, mkumbuke wazi kanuni yetu ya 68(7) inazungumzia miongozo ambayo inauliza Kiti kitoe maelekezo ikiwa jambo lililofanyika linaruhusiwa ama haliruhusiwi. Kwa hiyo, sasa tutaendelea, Mheshimiwa Dkt. Semesi.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na ahsante kwa kutukumbusha kwa mwongozo huo wa Kanuni ya 68(7), ni jambo ambalo linaendelea kutokea na limeshatokea jana usiku ila sikupata nafasi, kwa hiyo, naomba nilisemee tena leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa kanuni hiyo hiyo ili nipate mwongozo wako na kuweza kutusaidia kwenye hili. Tuko kwenye Bunge la Bajeti na kwa miezi hii tuliyo hapa tunasimamia na kupitisha bajeti hizo. Sasa kuna *trend*

inayoendelea na bado naendelea kwa kusimamia kanuni ambazo zinatuongoza kwenye majadiliano hayo ya bajeti ya 99 – 103, tangu tuanze kujadili hii bajeti tunapofika Kamati tunashika shilingi ya Waziri, wanachaguliwa wajumbe kutoka upande wa CCM wanne na wajumbe kutoka upande wetu wa Upinzani wawili. Naona sasa imekuwa ni *strategy* au ni *trend* kwamba tunapoteza muda pale kwenye majadiliano ya kushika shilingi halafu ghafla tunakwenda kwenye *guillotine* lakini hatuitendei haki bajeti ya Wizara husika na sauti zetu upande wa upinzani zinakuwa zimegandamizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako, hii *trend* naomba iachwe sababu pia tuna uwezo wa kusogeza muda. Bunge la bajeti lililopita tulikaa hapa mpaka saa tano usiku lakini sasa hivi tunaongeza tu nusu saa halafu tunajikuta sisi upande wa pili huku tukishika zile shilingi hatufikii *stage* ya hitimisho tunakuwa tumeenda kwenye *guillotine* na bajeti ya Wizara husika inakuwa imepita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mwongozo wangu unakita kwa Kanuni hiyo hiyo ya 68(7) kwa jambo ambayo limetokea jana wakati wa majumuisho ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani kuhusu hali ya usalama barabarani na tulipokea taarifa kwamba kuna ajali nyingine ilitokea huko kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vya habari leo vimeripoti kwamba mmiliki wa Shule ya Lucky Vincent amekamatwa na yuko chini ya mikono ya Jeshi la Polisi kwa ajili ya mahojiano. Mwongozo wangu ni kwamba basi kutoka shuleni pale mpaka kufika sehemu ilipotokea ajali kuna *road block* za *traffic* na polisi zaidi ya nne. Kama kweli nia ya Serikali ilikuwa ni kuwajibisha watu juu ya masuala yatokanayo na

ajali tungesikia vilevile *RTO - Regional Traffic Officer* wa Mkoa wa Arusha pamoja Ma-*traffic* wote waliokuwa barabarani wamekuwa *responsible. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ukweli hata wewe ukiondoka sasa ukaenda Arusha utasimamishwa zaidi ya mara ishirini mpaka unafika Arusha. Sasa unajiuliza kuna *road block* Kisongo, Miserani, Makuyuni, Mto wa Mbu, *traffic* wote hawa hawakuona basi lilikuwa limezidisha watoto au watoto walikuwa hawakufunga mkanda? Sasa leo anayewajibishwa ni mmiliki wa shule ambaye wala hakuwepo shule badala ya *RTO* kuwajibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako juu ya *double standard* ya maamuzi katika jambo hili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kunipa nafasi na mimi nipate mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo ninaouomba ni mwongozo ambao niliuomba wiki iliyopita lakini sikupata majibu ya kuridhisha. Mwongozo wangu ni kuhusu zoezi la bajeti linaloendelea ambalo limeathiri kupunguza fedha za Mfuko wa Jimbo kwa majimbo yetu. Ninavyofahamu fedha hizi tunapewa kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Jimbo, Na.16 ya mwaka 2009 na kifungu cha 5(3) kinasema kwamba fedha hizi tunapewa katika majimbo yetu kwa vigezo vya idadi ya watu asilimia 45, lakini asilimia 20 ni *poverty margin,* asilimia 10 ni kwa ajili ya *size* ya *constituency,* lakini hili limefanyika wakati tunaendelea na bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo huu kabla hatujafika kwenye bajeti kuu ya Serikali ili kama kuna marekebisho yanaweza yakafanyika yafanyike mapema kwa sababu sisi Wabunge wa Majimbo tuliomba fedha hizi tuongezewe na wenzetu wa Viti Maalum waliomba pia

wapatiwe. Mimi upande wangu nimepunguziwa kutoka shilingi milioni 54 napewa shilingi milioni 30 shilingi milioni 24 zimepunguzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako ni kwa nini Serikali au Waziri wa TAMISEMI anayehusika na Mfuko huu, asikae na Wabunge wa Majimbo atuambie ni kwa nini fedha hizi zimepunguzwa badala ya kuongezwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo wa mwisho Mheshimiwa Mussa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mimi nasimama kwa Kanuni ya 68(7) ambapo jana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wakati akiwasilisha hotuba yake alizungumza hali iliyojitokeza Tanga ya mafuriko ambapo familia nyingi, wafanyabiashara na hata shule ilibidi zisitishe shughuli zake kutokana na mafuriko yaliyotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako ili Waziri mwenye dhamana kama sikosei ni Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye ndiye anahusika na masuala ya mazingira na mambo kama hayo, nataka kujua Serikali inaweza ikawasaidia vipi wale wananchi ambao wameathirika na mafuriko, nyumba zimefunikwa na maji, magari yamesombwa, masoko yamejaa maji na bidhaa mbalimbali zimekwenda. Nataka kujua Serikali inawasaidia vipi kwa sababu wengi wanaishi katika shule, misikiti na makanisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi kuhusu jambo ambalo limekuwa likijitokeza mara kwa mara ambapo

katika maelezo yake jambo hili limetokea jana pia wakati bajeti ya Mambo ya Ndani ya Nchi ikipitishwa na Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, wakati akitoa maelezo yake ametoa maelezo kwamba wakati wa kushika mshahara wa Waziri ambapo mtu anaweza kusema anatoa shilingi kwa mujibu wa kanuni zetu, Wabunge wanne wa CCM hupewi nafasi na Wabunge wawili wa upande wa Upinzani hupewa nafasi.

Kimsingi amezungumzia mambo mawili, moja ni kwamba sauti za upinzani zinaminywa na jambo la pili ni kwamba tunapotumia huo utaratibu unapunguza muda wa kupitia vifungu vya bajeti husika na hivyo kuingia kwenye utaratibu wa kupitisha bajeti kwa namna ya kusoma mafungu yote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hizi nafasi zinavyopangwa, kwa kuwa hili ni jambo ambalo linajirudia na litaendelea kujirudia kwa sababu tatizo ni sisi wenyewe Wabunge. Kwanza kwenye suala la sauti za upinzani kuminywa halipo kwa sababu Wabunge wa Upinzani humu ndani ni wachache kwa uwiano, CCM wako asilimia 70 na Upinzani wako asilimia 30. Kwa hiyo, wanapogawa hizi nafasi si kwa upendeleo wala si kwa lengo la kuminya nafasi za Upinzani ni kwa ajili ya kuangalia uwiano. Kwa hiyo, suala la kuminya upande wa Upinzani kwa kupewa nafasi mbili halipo ni katika kuangalia nafasi zilizopo na uwiano uliopo Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, suala la pili la kwamba nafasi inakuwa haitoshi kwa sababu watu tunatumia muda mrefu sana kuzungumzia kwenye kifungu cha mshahara wa Waziri halafu muda wa kupitia mafungu mengine unakuwa haupo. Sisi hili ni Bunge la Kumi na Moja, Mabunge hayo mengine yaliyopita ilikuwa akisimama mtu akisema anashika shilingi anasimama mtu mmoja tu na akiishika hiyo shilingi Bunge zima litaunga mkono ama litakataa baadaye lakini ni kwamba mjadala utakuwa kwenye hoja hiyo. Sasa hivi watu kumi wanasimama wote wanataka kushika mshahara wa

Waziri na kila mtu anatoa shilingi. Utagundua kwamba sisi wenyewe Wabunge ndiyo tuliosababisha kushika shilingi kuwe hakuna maana yoyote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama sisi Wabunge ndiyo tuliosababisha na tunasimama kumi, kwa mujibu wa Kanuni zetu Kiti hakina namna ya kusema kwamba Waheshimiwa tutatakiwa kwenda kwenye vifungu vingine kwa hiyo watu wasiruhusiwe kushika shilingi. Utashangaa mara nyingi Wabunge wanaolalamika muda kutotosha ni wale wale ambao kwenye Kamati ya Matumizi kila wakati wanasimama wanataka kushika shilingi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sisi wenyewe ni kama Bunge hatujajiwekea utaratibu wa kutaka kupitia bajeti ya Serikali kwa umakini ndiyo maana tunataka tu tuangalie mshahara wa Waziri, mafungu mengine yanapita. Sisi wenyewe tujiwekee utaratibu mtu akishika shilingi awe mmoja, hoja ijadiliwe tuendelee kwenye mafungu mengine ili tuweze kuona fedha zimetengwa au hapana. Kwa sababu yapo mazingira ambayo fedha zinakuwa zimeandikiwa sifuri, wewe utaona saa ngapi wakati umekazana na kushika shilingi? *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, sisi wenyewe ndiyo tatizo na tulimalize wenyewe kwanza, tuache utaratibu wa kila mtu kusimama anataka kushika shilingi ili tupate muda wa kupitia bajeti sawasawa. Kwa hiyo, mwongozo wangu ni huo sisi wenyewe Wabunge na ndiyo tupo humu ndani tuweke utaratibu wenyewe, kwa sababu kanuni zipo vizuri, tuweke utaratibu akishika shilingi mtu mmoja kama tunataka kuchangia tuchangie tuendelee na bajeti, lakini ukisema kwamba watu kumi kila mtu asimame na kila mtu anataka hoja yake ijadiliwe ndio maana hatufiki mahali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Godbless Lema amezungumzia kuhusu kukamatwa kwa mmiliki wa shule ambayo wanafunzi waliofariki Arusha walikuwa wakisoma yaani mmiliki wa Lucky Vincent. Mwongozo wake anaomba kwenye mazingira ya kuonesha kwamba Polisi ambao

wanasimamia usalama barabarani hakuna taarifa zinazoonesha kwamba wamechukuliwa hatua wakati wao pia walikuwepo barabarani wakati basi likipita na wangeweza kuona kwamba wale wanafunzi hawakuwa wamefunga mikanda kwa maana kwamba basi halikuwa na usalama wa kuwasaidia hawa watoto waweze kufika waendapo ama hata kama wangepata ajali pengine madhara yasingekuwa makubwa sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maelezo yake nimehesabu ameonesha kwamba kulikuwa na vizuizi kama vinne kabla ya kufika sehemu ambayo basi lilipata ajali. Akaeleza pia kwamba jana kuna ajali nyingine imetokea mahali kwingine, sasa anataka mwongozo wa Spika kuhusu namna ambavyo upande wa Serikali unashughulika na mmiliki wa Lucky Vincent wakati yeye hakuwepo lakini barabarani kulikuwa na Polisi walioruhusu gari kupita. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni yetu hiyo ya 68(7) jambo hili halijatokea hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa pia na mwongozo na Mheshimiwa Pauline Gekul kuhusu jambo ambalo aliliombea mwongozo wiki iliyopita. Kwa maelezo yake ni kwamba hakupata majibu na mwongozo wake aliouomba wakati huo ulikuwa unahusu kupungua kwa fedha za Jimbo ambazo Waheshimiwa Wabunge wenye Majimbo wanapewa kwa mujibu wa sheria ambayo tumeiweka wenyewe. Ametoa maelezo kwamba kwa yeye Jimbo lake fedha zimepungua kutoka shilingi milioni 54 mpaka shilingi milioni 30 na hana maelezo ya kwa nini fedha hizo zimepungua wakati sheria iko vile ilivyokuwa tangu mwanzo.

Waheshimiwa Wabunge, hili lipo wazi, Mheshimiwa Pauline Gekul anasema aliomba mwongozo huu wiki iliyopita. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI yupo hapa, kama yeye atataka kulifanyia kazi anaweza kufanya hivyo lakini Kiti hakina mwongozo juu ya jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo mwingine nimeombwa na Mheshimiwa Mussa ambaye ni Mbunge wa Tanga Mjini, anaeleza kwamba jana Mwenyekiti wa Kamati inayohusika na Ulinzi na Usalama alizungumzia mafuriko Tanga. Anauliza Serikali itasaidia vipi hawa wananchi ambao wako katika hali ya taharuki kwa sababu soko na nyumba maji zimejaa maji na magari yamechuliwa pia.

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo wangu kwenye hili ni kwamba kama hili jambo lilisemwa jana na Waziri anayehusika yupo hapa atakuwa alilisikia.

Waheshimiwa Wabunge, nitoe maelezo ya jumla. Unaposimama kuomba mwongozo siyo nafasi ambayo unaipata ili tu uzungumze. Ukitumia Kanuni inayohusu mwongozo tafadhali sana uzungumzie jambo lililotokea Bungeni mapema na unataka kujua linaruhusiwa ama haliruhusiwi, ndiyo kanuni zetu zinavyosema na Kiti hakina shughuli zingine zaidi ya kusimamia Kanuni.

Kwa hiyo, tafadhali sana tufuate utaratibu, kama una jambo ambalo unataka Bunge lisikie basi tumia Kanuni zingine zinazohusika unaweza hata kutoa Maelezo Binafsi ili upewe muda kwa sababu kanuni zinakuruhusu, utapewa muda tena wa kutosha tu ili ujieleze jambo lako Serikali isikie. Ukitumia nafasi hii ya kuomba mwongozo ili tu upate nafasi ya kuzungumza humu ndani tunakuwa sisi wenyewe hatujitendei haki lakini pia hatuwatendei haki wananchi maana sisi wenyewe ndiyo tunaolalamika kwamba muda wetu hautoshi.

Mheshimiwa Lema hukuwepo muda mrefu, umerudi uwe na adabu Kiti kimesimama usiwe unazungumza, usizungumze Kiti kikiwa kimesimama tafadhali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nawasihi sana tutumie Kanuni zetu mahsusi kwa jambo lile linalohusika ili tupunguze kutumia muda wetu vibaya.

Baada ya kusema hayo, tunaendelea, Katibu. *(Makofi)*

**NDG. RAMADHAN I. ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe maelezo ya Hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge chini ya Kanuni 28(2)(15) na Kanuni ya 153(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

KWA KUWA, miongoni mwa shughuli zilizopangwa kufanyika leo katika Kikao hiki cha Ishirini na Moja cha Mkutano huu wa Saba ni pamoja na uchaguzi wa Wabunge wawili wa Bunge la Afrika Mashariki kwa Kundi la Vyama vya Upinzani na hasa CHADEMA.

NA KWA KUWA, Kanuni ya 28(2) inaelekeza kwamba vikao vya Bunge huanza saa 3.00 asubuhi hadi saa 7.00 mchana na kurejea saa 11.00 jioni hadi saa 1.45 usiku.

NA KWA KUWA, Bunge likirejea saa 11.00 jioni hakutakuwa na muda wa kutosha kwa ajili ya shughuli ya mjadala wa hoja ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji pamoja na Uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki.

HIVYO BASI, ili kuleta utekelezaji bora wa kikao cha leo, naomba Bunge lako liridhie Kanuni ya 28(2) itenguliwe ili Bunge likisitishwa saa 7.00 mchana leo lirejee saa 10.00 jioni badala ya saa 11.00 jioni ili kuwezesha Bunge kupata muda wa kutosha kuendelea na mjadala wa hoja ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji pamoja na kufanya uchaguzi wa Wabunge la Afrika Mashariki kama nilivyoeleza hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Bunge Kurudia Saa 10.00 Jioni badala ya Saa 11.00 Jioni kwa siku ya leo ilikubaliwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waliosema ndiyo wameshinda, kwa hivyo, Kanuni yetu hiyo kwa leo imebadilika. Tunaendelea, Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Wizara ya Maji na Umwagiliaji**

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Bunge lako Tukufu limepokea taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji iliyowasilishwa na Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang, kuhusu Makadiro ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kawaida na maendeleo ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati hiyo kwa kupokea na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa 2016/2017 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2017/2018. Maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji yamezingatiwa wakati wa maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli; Makamu wa Rais, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan; na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa kwa uongozi thabiti waliouonesha katika mwaka wa kwanza wa

Serikali ya Awamu ya Tano pamoja na juhudi zao kwenye ukusanyaji wa kodi; kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ya Serikali; mapambano dhidi ya rushwa, ufisadi na madawa ya kulevya. Vilevile, nichukue fursa hii kuwapongeza viongozi hao kwa azma yao ya dhati ya kuipeleka Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati kupitia viwanda. Hii ni ishara tosha ya uzalendo walionao kwa nchi yetu na imani yao katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata maendeleo ya haraka na ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya ambao ni Mheshimiwa Juma Ali Juma aliyechaguliwa kuwa Mbunge kupitia Jimbo la Dimani; Mheshimiwa Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare na Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge kuwa Wabunge kupitia Viti Maalum pamoja na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Abdallah Majura Bulembo, Mheshimiwa Profesa Kabudi na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete walioteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, kwa masikitiko makubwa, naomba kutoa pole kwako wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, familia za marehemu, ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa misiba iliyotupata kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Dimani, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir na Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dkt. Elly Marko Macha. Michango ya Wabunge hao katika shughuli za maendeleo ya Taifa letu itakumbukwa milele. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa naomba kutoa pole kwa wananchi wote na Taifa kwa ujumla kwa msiba wa wanafunzi na walimu wa Shule ya Lucky Vincent uliotokea tarehe 6 Mei, 2017 katika ajali mbaya ya gari Mkoani Arusha. Msiba huu umeleta pengo kubwa sio kwa shule hiyo tu bali kwa Taifa zima. Mwenyezi Mungu azipumzishe roho za marehemu hao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile natoa pole kwa wananchi wa maeneo mbalimbali nchini waliokumbwa na majanga katika mwaka wa fedha 2016/2017 ya kupoteza ndugu, marafiki na mali zao. Kwa namna ya pekee natoa pole kwa wahanga wa tetemeko la ardhi lililotokea katika Mkoa wa Kagera na kuleta madhara makubwa. Namwomba Mwenyezi Mungu awape nguvu na moyo wa subira wahanga wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nichukue fursa hii kumshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Majaliwa Kassim kwa hotuba yake mahiri aliyoiwasilisha hapa Bungeni ambayo inatoa dira na mwongozo wa utekelezaji wa kazi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hiyo imeonesha mapitio ya uendeshaji wa shughuli za Serikali ya Awamu ya Tano kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 na mpango na bajeti kwa mwaka 2017/2018 pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2015 – 2020. Vilevile, nawapongeza Mawaziri wenzangu wote walionitangulia kuwasilisha hoja zao na Wabunge wote waliochangia hoja hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara yangu yenye maeneo makuu yafuatayo:-

(i) Hali ya Sekta za maji na umwagiliaji nchini;

(ii) Mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 na malengo ya sekta kwa 2017/2018;

(iii) Ushiriki wa sekta binafsi katika kutekeleza miradi ya sekta za maji na umwagiliaji;

(iv) Pamoja na changamoto na hatua zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo haya yamezingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa, sera, mikakati na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2015 – 2020. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji huo yameainishwa kwenye aya zifuatazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hotuba yangu yote kamili iweze kuingia kwenye *Hansard* kwa sababu naweza nisisome yote ka ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya sekta ya maji na umwagiliaji nchini. Wizara inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maji na umwagiliaji kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa mujibu wa Sera ya Maji ya mwaka 2002; Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2010 pamoja na Sheria na Kanuni za Maji na Umwagiliaji. Utekelezaji huo pamoja na masuala mengine unazingatia maelekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa miaka mitano na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mipango hiyo, umeboresha hali ya huduma za maji na umwagiliaji ambazo ni kichocheo kikubwa katika kufikia azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwa na "Tanzania ya viwanda" na kuelekea kuwa nchi ya kipato cha uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Hali halisi katika sekta hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji. Usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini unafuata taratibu za usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji kupitia Bodi za Maji za Mabonde tisa yalipo nchini. Takwimu za rasilimali za maji zilizopo nchini zinaonesha kuwa maji yanayofaa kwa matumizi mbalimbali yanaendelea kupungua kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hiyo inatokana na mwenendo usioridhisha wa upatikanaji wa mvua kwenye

baadhi ya maeneo nchini ambao umesababisha ongezeko dogo la viwango vya maji katika vyanzo mbalimbali kama inavyoonyeshwa katika Jedwali Na.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, inaandaa Mfumo wa Tahadhari kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa taarifa za hali ya hewa kwa wakati zitakazowasaidia wananchi kuandaa mikakati ya kukabiliana na majanga yatakayojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya maji vijijini. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya vijijini ambapo hadi mwezi Machi 2017, jumla ya miradi ya maji 1,333 imekamilika. Kukamilika kwa miradi hiyo kumewezesha watu 22,951,371 sawa na asilimia 72.58 ya wananchi waishio vijijini kupata huduma ya maji safi na salama. Vilevile, vyombo vya watumiaji maji 1,799 vimesajiliwa na kuimarishwa ili kuhakikisha huduma ya maji inakuwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya maji mijini. Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia Mamlaka za Maji Mijini imeendelea na ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi katika maeneo ya miji husika. Kwa upande wa Miji Mikuu ya Mikoa, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji imeendelea kuimarika na kupunguza kero ya uhaba wa majisafi kwa wananchi wa miji hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuimarika kwa huduma hiyo, idadi ya wateja waliounganishwa kwenye mtandao wa majisafi imeongezeka kutoka 405,095 mwezi Machi 2016 hadi wateja 432,772 mwezi Machi, 2017. Hadi Machi, 2017 upatikanaji wa maji mijini umefikia wastani wa asilimia 86.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo, upatikanaji wa huduma ya maji umeongezeka kutoka asilimia 68 hadi kufikia asilimia 75 kwa sasa. Ongezeko hilo limetokana na kukamilika kwa maboresho ya mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini ambapo uzalishaji wa maji umeongezeka kutoka lita milioni 300 hadi lita milioni 504 kwa siku. Vilevile upotevu wa maji umeendelea kupungua kutoka asilimia 47 mwezi Machi, 2016 hadi asilimia 38 Machi, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Miji Mikuu na Miji Midogo uzalishaji wa maji umeongezeka kutoka lita milioni 99.5 kwa siku mwezi Machi, 2016 hadi lita milioni 99.7 kwa mwezi Machi, 2017. Kwa upande wa miradi ya maji ya kitaifa uzalishaji wa maji umeongezeka kutoka lita milioni 57.2 hadi lita milioni 59.5 kwa siku. Kuongezeka kwa uzalishaji huo kumeboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kufikia asilimia 62 katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya umwagiliaji; Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002 ulibaini kuwa nchi yetu ina eneo la hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Eneo hilo lina uwezekano tofauti wa kumwagiliwa ambapo hekta milioni 2.3 zina uwezekano mkubwa, hekta milioni 4.8 zina uwezekano wa kati na hekta milioni 22.3 zina uwezekano mdogo. Hadi mwezi Machi, 2017 eneo linalomwagiliwa limeongezeka kutoka hekta 461,326 kwa mwaka 2015/2016 hadi kufikia hekta 468,338. Eneo hilo linachangia asilimia 24 ya mahitaji yote ya chakula nchini kwa sasa. Lengo ni kuongeza eneo la umwagiliaji kufikia hekta milioni moja katika skimu za wamwagiliaji wadogo, wa kati na wakubwa ifikapo mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Fungu 49 – Wizara ya Maji na Umwagiliaji iliidhinishiwa jumla ya shilingi 939,631,302,771 na kati ya fedha hizo, shilingi 24,437,365,000 zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi 915,193,937,771 zilikuwa ni fedha za maendeleo. Hadi mwezi Machi jumla ya shilingi 181,209,813,609 sawa na asilimia 19.8 ya fedha zote za

maendeleo zilipokelewa ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 95,506,951,632 zilipatikana kupitia Mfuko wa Maji. Aidha, shilingi 14,436,952,900 sawa na asilimia 58 ya fedha za matumizi ya kawaida zilipokelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa Fungu la 5 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji iliidhinishiwa jumla ya shilingi 39,876,143,028. Kati ya fedha hizo shilingi 4,506,613,600 zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi 35,369,629,428 zilikuwa ni fedha za maendeleo. Hadi mwezi Machi, 2017 jumla ya shilingi 2,986,101,292 sawa na asilimia 8.4 ya fedha za maendeleo zilipokelewa na shilingi 2,532,329,224 sawa na asilimia 56 ya fedha za matumizi ya kawaida zilipokelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2016/2017 na malengo ya mwaka 2017/2018; katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara yangu ilitekeleza miradi inayohusu usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini, kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi na usafi wa mazingira vijijini na mijini, uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji na kutekeleza malengo ya masuala mtambuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/2017 na malengo ya mwaka 2017/ 2018 yamefafanuliwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara yangu iliendelea kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji nchini na maji shirikishi kwa kuchunguza na kutathmini wingi na ubora wa maji juu na chini ya ardhi; kuandaa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali hizo pamoja na kufanya usanifu na kusimamia ujenzi wa miundombinu ya kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara yangu imeendelea kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji kwa kuimarisha vituo vya kupima wingi na ubora wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi kwenye

mabonde yote nchini. Katika kuboresha upatikanaji wa takwimu na taarifa sahihi, jumla ya vituo 13 vilijengwa na vituo 56 vilikarabatiwa. Vilevile kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, Wizara yangu imeendelea kuvitambua, kuviwekea mipaka na kuvitangaza vyanzo vya maji kuwa maeneo tengefu ambapo vyanzo tisa vimetangazwa katika Gazeti la Serikali. Vyanzo hivyo ni Bwawa la Mindu na Mito ya Halewa - Swaya, Mfwizimo - Iziwa, Nzovwe, Ivumwe, Imeta, Hanzya, Mfwizimo/Lunji na Sisimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara yangu imeendelea kutafuta vyanzo mbalimbali vya maji na kuhakikisha vinabainishwa na kufanyiwa tathmini ili viweze kuendelezwa na kuongeza upatikanaji wa maji nchini. Jumla ya maeneo 174 kwenye mabonde ya maji yalifanyiwa utafiti wa maji chini ya ardhi kwa ajili ya kuendelezwa kuwa vyanzo vya maji. Vilevile, tathmini ya fidia kwa wananchi watakaoathirika na ujenzi wa Mabwawa ya Kimkakati ya Farkwa, Ndembera pamoja na Kidunda inatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2017. Kwa upande wa Bwawa la Kidunda tathmini kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi waliolalamikia malipo ya awali imekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kusimamia matumizi bora ya rasilimali za maji, Wizara yangu kupitia Bodi za Maji za Mabonde ilitoa jumla ya vibali vipya 914 vya kutumia maji na vibali 12 vya kutiririsha majitaka kwenye vyanzo vya maji. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara itaendelea kupokea maombi na kutoa vibali vya matumizi ya rasilimali za maji kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi za Maji za Mabonde zimeendelea kujengewa uwezo na kuimarishwa ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwa ni pamoja kukusanya maduhuli yatokanayo na ada za matumizi ya maji. Hadi mwezi Machi, 2017 jumla ya shilingi 2,953,466,917 zilikusanywa sawa na asilimia 78 ya lengo la shilingi 3,806,000,000 kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Katika mwaka

wa fedha 2017/2018 Bodi za Maji za Mabonde zimelenga kukusanya kiasi cha shilingi 4,145,000,000 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato kama ilivyoainishwa katika Jedwali Namba 02.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017 migogoro 32 ya watumia maji ilijitokeza. Kati ya hiyo, migogoro 25 imesuluhishwa na migogoro mingine saba ipo katika hatua mbalimbali za usuluhishi. Serikali itaendelea kutoa elimu kuhusu matumizi, ugawaji na utunzaji wa rasilimali za maji ili kupunguza migogoro ya watumia maji pamoja na kuitatua kadri itakavyojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa rasilimali za maji shirikishi; nchi yetu ina rasilimali za maji tunazoshirikiana na nchi nyingine ambazo ni Mto wa Ruvuma, Mto Kagera, Mto Mara, Mto Umba, Mto Momba, Mto Songwe pamoja na Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Ziwa Natron, Ziwa Chala na Ziwa Jipe. Ushirikiano huo unatekelezwa kupitia taasisi za kikanda na utekelezaji wa miradi na programu za baadhi ya taasisi hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Utunzaji na Uendelezaji wa Bonde la Mto Songwe; nchi za Tanzania na Malawi zimeanza utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Programu ya Utunzaji na Uendelezaji wa Bonde la Mto Songwe ambayo inatarajiwa kuanza kutekelezwa kwa pamoja na Nchi za Malawi na Tanzania. Mradi huo utasimamiwa na Kamisheni ya Kudumu ya Bonde la Mto Songwe itakayoanzishwa baada ya nchi washirika kusaini mkataba. Taratibu za kuridhia mkataba huo zipo katika hatua za mwisho na nchi hizo zinaendelea na jitihada za kutafuta fedha kutoka kwa wafadhili na wawekezaji mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza miradi iliyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bonde la Mto Nile; Umoja wa Ushirikiano wa Nchi za Bonde la Mto Nile ni chombo cha mpito kuelekea uundwaji wa Kamisheni ya Bonde la Mto Nile, jumla ya nchi 11 zinaunda umoja huo. Tanzania ilipewa heshima ya kuwa mwenyeji wa maadhimisho ya 11 ya siku

ya Nile yaliyofanyika tarehe 22 Februari, 2017 ambapo mgeni rasmi alikuwa Makamu wa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan. Kaulimbiu ya Maadhimisho hayo ilikuwa "Kuhakikisha Usalama wa Upatikanaji wa Chakula, Maji na Nishati ya Umeme kwa Jamii inayozunguka Bonde hilo."

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Sekretarieti ya *AMCOW* iliandaa Maadhimisho ya Sita ya Wiki ya Maji ya Afrika na Mkutano Mkuu wa 10 wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Afrika, kuanzia tarehe 18 – 22 Julai, 2016 Jijini Dar es Salaam. Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa "Kufikia Lengo la Sita la Maendeleo Endelevu kuhusu Usalama wa Maji na Usafi wa Mazingira." Mgeni rasmi kwenye maadhimisho hayo alikuwa Makamu wetu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maadhimisho hayo, tarehe 22 Julai, 2016 ulifanyika Mkutano wa Baraza ambao ulipitisha Azimio la Dar es Salaam lililotoa mwelekeo wa utekelezaji wa majukumu mbalimbali kwa nchi za Afrika kuhusu usalama wa maji na usafi wa mazingira. Mwelekeo huo ulipendekeza maeneo 12 ya utekelezaji kulingana na Lengo la Sita la Maendeleo Endelevu la Ajenda ya 2030. Katika Mkutano huo, nikiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nilikabidhiwa Urais wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Afrika kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia Julai, 2016 hadi Juni, 2018 na Rais aliyemaliza muda wake ambaye ni Waziri wa Maji wa Senegal. Vilevile Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli amekuwa ndiye Msemaji Mkuu *(champion)* wa masuala ya maji katika Bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini yameainishwa kuanzia ukurasa wa 15 hadi ukurasa wa 30 wa kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya majukumu ya Wizara yangu ni kuhakikisha ubora na usalama wa maji katika vyanzo vya maji kwa lengo la kulinda afya za wananchi na mazingira. Katika mwaka 2016 Wizara ilipanga

kukagua vyanzo vya maji kwa kuchunguza sampuli 10,000 za maji ili kuhakiki ubora wake. Vilevile sampuli 1,500 za majitaka zilipangwa kukusanywa na kuchunguzwa ubora wake kwa lengo la kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji na mfumo wa ikolojia. Hadi mwezi Machi, 2017 sampuli 4,288 za maji kwa matumizi mbalimbali na sampuli 264 za majitaka zilikusanywa na kuhakikiwa ubora wake. Maelezo ya ubora na usafi wa maji kwa matumizi mbalimbali yakiwemo ubora wa maji kwa matumizi ya majumbani, viwandani na ujenzi, ubora wa dawa za kusafishia maji na kutibu maji, uondoaji wa madini ya *floride* katika maji ya kunywa na kupikia na maabara za maji kupata ithibati, yameainishwa kwa kina kuanzia ukurasa wa 30 mpaka 39 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza miradi ya maji vijijini kupitia Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Hadi sasa jumla ya miradi 1,333 imekamilika na miradi 477 inaendelea kujengwa na ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Vyanzo vya maji vya miradi hiyo ni pamoja na visima vifupi, visima virefu, mabwawa na maji mtiririko. Kukamilika kwa miradi hiyo kumeongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma ya maji kutoka 21,900,000 mwezi Machi, 2016 hadi kufikia wananchi 22,951,371 mwezi Machi, 2017. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya kimkakati, mradi wa Maji Tabora; ujenzi wa mradi wa maji Tabora, umetekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa maji katika vijiji 31 kwenye Wilaya zote saba za Mkoa wa Tabora. Mradi huo umehusisha ujenzi wa visima 111 vya pampu za mkono na miradi minne ya maji ya bomba yenye vituo 60 vya kuchotea maji. Mradi umekamilika na kuzinduliwa rasmi na Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan tarehe 29 Aprili, 2017 na umehudumia wananchi 40,000 katika vijiji hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe; Serikali kwa kushirikiana na *BADEA, OFID* na *Kuwait Fund* inaendelea kutekeleza mradi

wa Same – Mwanga – Korogwe ambao umelenga kusambaza maji katika Miji ya Same na Mwanga pamoja na vijiji 38 vilivyo kando ya bomba kuu katika Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe. Mradi huo umegawanyika katika awamu mbili na ujenzi umeanza kwa awamu ya kwanza ambayo inatekelezwa katika vipande vinne vitakavyohusisha ujenzi wa chanzo, mitambo ya kusafisha maji na miundombinu ya kupeleka na kusambaza maji katika miji ya Mwanga na Same.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipande cha kwanza kinahusu ujenzi wa chanzo cha maji, mtambo wa kusafisha maji na ulazaji wa bomba kuu la urefu wa kilometa 12.8. Gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 92.7 na gharama za usimamizi ni shilingi bilioni 1.65. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa Mradi huu wa Same – Mwanga – Korogwe yanapatikana kuanzia ukurasa wa 41 hadi ukurasa wa 43 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Maji wa Masoko – Wilaya ya Rungwe; awamu ya kwanza ya mradi huo inaendelea kutekelezwa ambapo ujenzi wa tanki la kuhifadhia maji lenye mita za ujazo 90 katika kijiji cha Ikama umekamilika. Kazi inayoendelea ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha Mbaka, ujenzi wa tanki lenye mita za ujazo 370 katika kijiji cha Lufumbi, kulaza mabomba yenye urefu wa kilometa 12.6 na kujenga vituo sita vya kuchotea maji. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Masoko yanapatikana ukurasa wa 43 wa kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Maji Mkoani Kigoma; Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Ubelgiji itatekeleza mradi wa maji utakaohusisha Halmashauri zote za Mkoa wa Kigoma. Mradi huo utatekelezwa katika vijiji 26 vya kipaumbele kwa kipindi cha miaka mitano na utawanufaisha wananchi wapatao 200,000 wa Mkoa huo. Mradi utagharimu jumla ya shilingi bilioni 21.6 na kati ya fedha hizo, Serikali ya Ubelgiji itatoa shilingi bilioni 19.68 na kiasi cha shilingi bilioni 1.91 kitatolewa na Serikali ya

Tanzania. Hadi mwezi Machi 2017, Serikali ipo kwenye hatua za mwisho za kusaini mkataba wa makubaliano ili ujenzi wa mradi huo uweze kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kw aupande wa Miradi yenye Kuleta Matokeo ya Haraka *(quickwins),* Mradi wa Maji kwa Vijiji 100 Vitakavyopitiwa na Bomba Kuu kutoka Ziwa Victoria hadi Kahama – Shinyanga; Wizara inaendelea kutekeleza ujenzi wa miradi ya maji katika vijiji vilivyopo pembezoni mwa bomba kuu la maji kutoka Ziwa Victoria hadi Miji ya Kahama na Shinyanga. Ujenzi wa miradi ya maji katika vijiji 40 umeanza ambapo upimaji na usanifu katika vijiji 32 umekamilika. Kati ya hivyo, ujenzi wa miradi ya maji umekamilika katika vijiji 14 na wananchi wanapata huduma ya maji. Maelezo ya kina ya utekelezaji wa mradi yanapatikana katika ukurasa wa 44 hadi 45 wa kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Maji wa Ntomoko; mradi huu unatekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa katika vijiji kumi kwenye Halmashauri za Wilaya za Kondoa na Chemba. Vijiji hivyo ni Makirinya, Lusangi, Kinkima, Kirere, Chang'ombe, Churuku, Hamai, Songolo, Jangalo, Jinjo na Madaha. Maelezo ya kina ya utekelezaji wa mradi huu yanapatikana ukurasa wa 45 hadi 46 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati na ujenzi wa mabwawa; katika mwaka 2016/2017 Serikali imeendelea na ujenzi pamoja na ukarabati wa mabwawa katika maeneo mbalimbali nchini. Mabwawa hayo ni pamoja na Bwawa la Habiya lililopo Wilayani Itilima, Seke Ididi lililopo katika Wilaya ya Kishapu, Kawa – Nkasi, Matwiga – Chunya, Iguluba – Iringa, Wegero – Butiama, Mwanjoro – Meatu, Kidete – Kilosa, Dongo – Kiteto na Bwawa la Sukuro lililopo katika Wilaya ya Simanjiro. Hatua za utekelezaji zimeoneshwa katika ukurasa wa 47 mpaka 50 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika,kuhusu Mradi wa Kutumia Teknolojia ya Nishati Jadidifu *(renewable energy);* Wizara kwa

kushirikiana na Benki ya Dunia kupitia *Global Partnership on Output Based Aid* inakamilisha maandalizi ya mradi wa kutumia teknolojia ya nguvu ya jua. Lengo la mradi huo ni kupunguza gharama za uendeshaji na matengenezo ya miradi ya maji vijijini. Awamu ya kwanza ya mradi itaanza kwa majaribio katika vijiji 280 kwenye mikoa 12 ya Dodoma, Morogoro, Geita, Kagera, Mara, Shinyanga, Mtwara, Rukwa, Singida, Tabora, Arusha na Manyara kwa gharama ya shilingi bilioni 9.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi wa kuimarisha uendelevu wa huduma ya maji kupitia Mfumo wa Malipo kwa Matokeo *(Payment by Results - PBR);* Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Uingereza kupitia *DFID* imeendelea kutekeleza mradi unaolenga kuimarisha uendelevu wa huduma ya maji vijijini kupitia Mfumo wa Malipo kwa Matokeo. Jumla ya Paundi za Uingereza milioni 78.6 sawa na shilingi bilioni 214 zimetengwa kutumika kwa miaka mitatu. Hadi mwezi Machi 2017, jumla ya Halmashauri 74 ziliwasilisha taarifa za miradi ili kupata fedha kutoka kwenye mradi huo. Kati ya hizo, Halmashauri 57 zilikidhi vigezo na kupatiwa jumla ya shilingi bilioni 1.74, Halmashauri 17 hazikukidhi vigezo ambapo zilipatiwa shilingi milioni 232.05. Kwa ajili ya kujenga uwezo, Wizara itaendelea kutekeleza mradi huo ili kuhakikisha huduma ya maji vijijini inakuwa endelevu kwa maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uvunaji wa maji ya mvua; Serikali inaendelea kuhamasisha wananchi kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua kwa kujenga matanki ya mfano katika taasisi za umma, kutoa maelekezo kwa Halmashauri kutunga sheria ndogo zenye kuzitaka taasisi za kijamii, asasi na watu binafsi kujenga miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua na kutoa mafunzo kwa wananchi kuhusu uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia teknolojia rahisi. Jumla ya wananchi 795 wamepata mafunzo kuhusu teknolojia rahisi ya uvunaji wa maji ya mvua.

Vilevile matanki 29,059 ya ukubwa tofauti yamejengwa katika Halmashauri mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha miradi ya maji vijijini inakuwa endelevu, Serikali imetoa mwongozo wa usajili wa vyombo vya watumiaji maji kwa Halmashauri unaohusu uendeshaji, usimamizi na matengenezo ya miradi ya maji vijijini. Hadi mwezi Machi 2017 jumla ya vyombo 1,799 vya watumia maji vimeundwa na kusajiliwa katika Halmashauri mbalimbali nchini. Vilevile Serikali imeandaa kanuni na taratibu mbalimbali pamoja na mkakati wa uendelevu wa miradi ya maji vijijini kwa ajili ya uendeshaji wa vyombo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara itaendelea kukamilisha ujenzi wa miradi inayoendelea, kujenga miradi mipya, kupanua miradi, kukarabati miundombinu ya maji iliyochakaa pamoja na kutekeleza miradi ya maji katika maeneo kame yenye uhaba mkubwa wa maji. Vilevile Wizara itaendelea kuhamasisha ujenzi wa mitambo midogo ya kutibu maji kwa kutumia teknolojia rahisi pamoja na matumizi ya nishati mbadala. Jumla ya shilingi bilioni 341.83 zimepangwa kutumika kutekeleza miradi hiyo, angalia Jedwali namba 5(a), (b) na (c). Maelezo ya kina kuhusu huduma ya maji vijijini yameainishwa kuanzia ukurasa wa 39 mpaka ukurasa wa 54 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma ya maji mijini; katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara imeendelea kutekeleza miradi ya maji mijini inayohusu ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka pamoja na kuzijengea uwezo Mamlaka za Maji za Mijini. Lengo ni kuwapatia wakazi wa mijini huduma ya majisafi na usafi wa mazingira, hivyo ubora na uendelevu, miradi iliyotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maji katika miji saba; Manispaa za Bukoba na Musoma; Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa inatekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya majisafi katika Manispaa za Bukoba na Musoma. Gharama za mradi huu ni shilingi bilioni 27 kwa Bukoba na shilingi bilioni 40.6 kwa Musoma.

Kwa Manispaa ya Bukoba mradi umekamilika na kuongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 8.82 hadi lita milioni 18 kwa siku na kuwezesha huduma ya maji kupatikana kwa saa 24. Kwa upande wa Manispaa ya Musoma mradi unalenga kuongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 10.14 za sasa hadi lita milioni 34 kwa siku. Utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 90 na upo katika hatua za majaribio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Manispaa za Lindi, Kigoma na Sumbawanga; Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani na Umoja wa Ulaya inatekeleza miradi ya maji safi na usafi wa mazingira katika Manispaa za Lindi, Kigoma na Sumbawanga. Gharama za mkataba wa Lindi ni *Euro* milioni 11.7 sawa na shilingi bilioni 25.7, Kigoma ni sawa sawa na shilingi bilioni 36 na Sumbawanga sawa sawa na shilingi bilioni 33. Utekelezaji wa miradi katika miji hiyo ni kama inavyooneshwa kuanzia ukurasa wa 56 hadi ukurasa wa 58 wa hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Manispaa za Mtwara na Babati; Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani kupitia *KfW* imeanza kutekeleza miradi ya kuboresha miundombinu ya kusambaza maji safi katika Miji ya Mtwara na Babati kwa gharama ya shilingi bilioni 46.5. Mtaalam Mshauri amewasilisha taarifa ya awali ya usanifu katika mwaka 2016/2017, kazi ya usanifu wa kina, kuandaa makabrasha ya zabuni pamoja na kuwapata wakandarasi itafanyika ili kazi ziweze kuanza katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya maji ya kukidhi mahitaji ya muda mrefu; mradi wa maji Jijini Arusha; Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika inatekeleza mradi wa kuboresha miundombinu ya usambazaji majisafi na uondoaji wa majitaka katika Jiji la Arusha na baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Arumeru kwa gharama ya shilingi bilioni 476. Ujenzi wa mradi utaanza katika mwaka wa fedha 2017/2018 na utakapokamilika, uzalishaji wa maji utaongezeka kutoka lita milioni 40 za sasa hadi lita milioni 200 kwa siku na huduma ya uondoaji wa majitaka kutoka asilimia 7.6 za sasa hadi asilimia 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji Morogoro Mjini; Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika la Maendeleo la Ufaransa *(AFD)* itatekeleza mradi wa kuongeza uzalishaji wa maji katika Manispaa ya Morogoro kwa gharama ya shilingi bilioni 150. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuongeza urefu wa tuta la Bwawa la Mindu kwa mita 2.5 na kujenga chujio la maji lenye uwezo wa kuzalisha lita milioni 54 kwa siku. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2017/2018. Vilevile katika hatua za muda mfupi za kuboresha hali ya huduma ya maji Serikali imechimba visima vitatu kati ya visima vitano vilivyopangwa na visima viwili vilivyobaki pamoja na miundombinu ya usambazaji maji vitakamilishwa katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa kutoa maji kutoka Mto Ruvuma kupeleka Manispaa ya Mtwara Mikindani; Serikali inatekeleza mradi wa kutoa maji kutoka Mto Ruvuma kupeleka Manispaa ya Mtwara Mikindani na vijiji 26 pamoja na vitongoji vilivyopo ndani ya kilometa 12 kutoka eneo la bomba kuu utakaogharimu shilingi bilioni 425.4. Hadi mwezi Machi 2017, mkandarasi wa ujenzi wa mradi huo amepatikana na Serikali inaendelea na majadiliano na Serikali ya China kwa ajili ya kuweza kukamilisha suala la upatikanaji wa fedha za mradi huo. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni tisa za sasa hadi lita milioni 120 kwa siku na kutosheleza mahitaji ya viwanda mbalimbali katika Manispaa ya Mtwara Mikindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kutoa Maji kutoka Mto Malagarasi kwenda Miji ya Urambo, Kaliua na Nguruka; Wizara imepanga kutekeleza mradi wa kutoa maji Mto Malagarasi kupeleka miji ya Urambo, Kaliua, Nguruka na Usoke pamoja na vijiji 68 vilivyopo kando kando ya bomba kuu. Mtaalam Mshauri anaendelea na usanifu wa kina pamoja na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni, kazi ambazo zinatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2017. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo unaotarajiwa kunufaisha wakazi wapatao 607,086.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika inaendelea kutekeleza mradi wa maji na usafi wa mazingira wa Ziwa Victoria katika Miji ya Sengerema, Nansio na Geita kwa gharama ya dola milioni 30.4. Kazi zilizotekelezwa katika miji hiyo ni pamoja na hatua za utekelezaji inapatikana kwenye ukurasa wa 62 mpaka 64 wa hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maji safi na usafi wa mazingira katika Jiji la Mwanza, miji ya Lamadi, Magu, Misungwi pamoja usafi wa mazingira katika miji ya Bukoba na Musoma. Serikali inatekeleza mradi wa uboreshaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Mwanza na Miji ya Magu, Misungwi na Lamadi pamoja na mradi wa uondoaji wa majitaka katika Mji ya Bukoba na Musoma. Miradi hiyo inatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya na Shirika la Maendeleo la Ufaransa kwa gharama ya shilingi bilioni 245.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jiji la Mwanza na Miji ya Magu, Misungwi na Lamadi utekelezaji wa miradi umeanza na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Februari, 2019. Mradi huo utakapokamilika utaongeza hali ya upatikanaji wa maji katika miji hiyo ambapo kwa Jiji la Mwanza itaongezeka kutoka asilimia 90 za sasa hadi asilimia 100. Kwa Mji wa Magu kutoka asilimia 23 ya sasa hadi asilimia 90, Misungwi asilimia 39 ya sasa hadi asilimia 60 na kwa Mji wa Lamadi kutoka asilimia 20 ya sasa hadi asilimia 95.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi wa huduma ya uondoaji wa majitaka katika Miji ya Musoma na Bukoba kwa gharama ya shilingi bilioni 24. Katika Mji wa Musoma mkandarasi wa mradi huo amepatikana na ujenzi utaanza Juni, 2017 na utakapokamilika asilimia 30 ya wakazi wa Mji wa Musoma wataunganishwa kwenye huduma ya mtandao wa majitaka. Kwa upande wa Mji wa Bukoba taratibu za kumpata mkandarasi zinaendelea na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2017. Mradi huo utakapokamilika asilimia 12 ya wakazi wa Mji wa Bukoba wataunganishwa kwenye huduma ya mtandao wa majitaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali inaendelea kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Miji ya Mpanda, Njombe na Bariadi ambayo ina uhaba mkubwa wa maji. Utekelezaji wa miradi katika miji hiyo pamoja na fedha zilizotengwa kwa mwaka 2017 zimeainishwa katika ukurasa wa 66 mpaka 68 wa hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miradi ya kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka miji mbalimbali; Miji ya Busega, Bariadi, Lagangabilili, Maswa na Mwanhuzi; Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Miji ya Busega, Bariadi, Lagangabilili, Maswa na Mwanhuzi. Mradi huo utatekelezwa kwa awamu mbili na utahudumia wakazi 834,204 katika miji hiyo. Ujenzi wa awamu ya kwanza utahusisha Miji ya Nyashimo-Busega, Bariadi, Lagangabilili pamoja na vijiji vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka eneo la bomba kuu na unatarajiwa kuanza mwezi Septemba 2017 kwa gharama ya shilingi bilioni 258.3 ambapo Benki ya *KfW* ya Ujerumani itatoa shilingi bilioni 61.5 na *Green Climate Fund* shilingi bilioni 196.8. Awamu ya pili ya ujenzi itagharimu shilingi bilioni 511, fedha ambayo zinatarajiwa kutolewa na *Green Climate Fund*. Awamu hiyo itahusisha Miji ya Mwanhuzi pamoja na Maswa. Fedha za kutekeleza awamu ya kwanza zimeshapatikana na ujenzi utaanza katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miji ya Isaka na Kagongwa; Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa maji kwenda katika miji ya Isaka na Kagongwa kwa kutumia chanzo cha maji kutoka Ziwa Victoria kupitia bomba kuu la Kashwasa kwa gharama ya shilingi bilioni 24.42. Wakandarasi wameshapatikana na ujenzi wa miradi unatarajiwa kuanza mwezi Mei, 2017. Mradi huo utakapokamilika hali ya upatikanaji wa maji utaongezeka kutoka asilimia 26 hadi asilimia 90 kwa Mji wa Isaka, na asilimia 24 hadi asilimia 95 kwa Mji wa Kagongwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miji ya Mwadui, Kishapu, Kolandoto na Maganzo; mradi wa kupeleka maji

katika miji ya Mwadui, Kishapu, Kolandoto na Maganzo unaotekelezwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia Mamlaka ya *KASHWASA* umekamilika na wakazi wa miji hiyo wanapata huduma ya maji. Katika jitihada za kuongeza uhifadhi wa maji ya kutosha katika Mji wa Kishapu, Wizara inaendelea na ujenzi wa tanki kubwa lenye uwezo wa lita milioni 1.2. Hadi mwezi Machi 2017, ujenzi wa tanki hilo ulifikia asilimia 90 na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mradi wa kuwapatia huduma ya maji wakazi wa miji ya Tabora, Uyui, Igunga, Nzega, Tinde na Sikonge pamoja na vijiji 89 vilivyopo kwenye eneo la kilometa 12 kutoka bomba kuu la mradi wa *KASHWASA.* Awamu ya kwanza ya mradi itahusisha Miji ya Tabora, Uyui, Igunga, Nzega na Tinde ambapo Wakandarasi wameshapatikana na ujenzi unatarajiwa kuanza Mei, 2017. Gharama ya mradi huo ni dola za Marekani milioni 268 sawa sawa na shilingi bilioni 600, ikiwa ni mkopo wenye masharti nafuu kutoka Serikali ya India. Awamu ya pili ya mradi itahusu kupeleka maji katika Mji wa Sikonge kutoka Ziwa Victoria na inatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kutekeleza miradi ya maji katika Jiji la Dar es Salaam ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji hilo pamoja na Miji ya Kibaha na Bagamoyo. Kukamilika kwa upanuzi wa mtambo wa Ruvu chini pamoja na miundombinu yake kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 300 kwa siku hadi lita milioni 500 kwa siku, hivyo kufikisha wastani wa huduma ya maji kuongezeka kutoka asilimia 72 hadi asilimia 75. Miradi mingine inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na miradi ya uchimbaji wa visima ya Kimbiji na Mpera, ukarabati na upanuzi wa mfumo wa kusambaza maji safi, mfumo mpya wa kusambaza maji, kuboresha miundombinu ya uondoaji maji taka na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa kwa miradi hiyo inapatikana ukurasa wa 71 hadi 75 wa hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maji katika baadhi

ya Miji Mikuu ya Wilaya na Miji midogo; Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya kuboresha huduma ya maji katika Miji wa Kilosa, Turiani, Mvomero, Gairo, Bunda, Mugumu na Orkesumet. Taarifa za miradi hiyo inapatikana ukurasa wa 75 hadi ukurasa wa 79 wa hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuboresha huduma ya maji katika miradi ya maji ya Kitaifa ya Chalinze, Mugango, Kiabakari, Makonde, *Handeni Trunk Main* na Wanging'ombe. Taarifa ya utekelezaji wa miradi, fedha zilizotengwa na hatua iliyofikiwa imeelezwa kwenye ukurasa wa 80 hadi ukurasa wa 83.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018, jumla ya shilingi bilioni 273 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maji mijini. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 143 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 130 ni fedha za nje. Jedwali Namba Sita linaonesha mgawanyo wa fedha zilizotengwa kutekeleza miradi ya maji mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa maboresho ya huduma ya maji katika Miji 17 ya Tanzania Bara na Zanzibar kwa kutumia fedha za mkopo dola milioni 500 kutoka Serikali ya India. Miji hiyo ni Muheza, Wanging'ombe, Makambako, Kayanga, Songea, Zanzibar, *HTM*, Njombe, Mugumu, Kilwa Masoko, Geita, Chunya, Makonde, Manyoni, Sikonge, Kasulu na Rujewa. Hatua iliyofikiwa ni kufanya manunuzi ya Mhandisi mshauri atakayefanya mapitio ya usanifu. Mchanganuo wa fedha wa miji hiyo husika uko kwenye ukurasa wa jedwali namba 7. Maelezo ya kina kuhusu huduma ya maji mijini yameainishwa kuanzia ukurasa wa 54 hadi ukurasa wa 85 wa hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Tume ya umwagiliaji imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya umwagiliaji ikiwemo programu ya kuendeleza sekta ya kilimo, mradi wa kuendeleza zao la mpunga, mradi wa Kuendeleza skimu ndogo ndogo za umwagiliaji, programu ya kukabiliana na changamoto za uhaba wa chakula duniani *(feed the future)* na mradi wa kujenga uwezo katika kuendeleza

umwagiliaji nchini. Utekelezaji wa baadhi ya miradi hiyo imeelezwa kwa kina ukurasa wa 85 mpaka 90 wa hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali itaendelea kukamilisha ujenzi wa miradi ya umwagiliaji inayoendelea kukarabatiwa, miradi iliyopo katika maeneo mbalimbali nchini, kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi ya mabwawa na skimu za umwagiliaji, kufanya utafiti wa teknolojia za umwagiliaji zinazotumia maji kwa ufanisi na kuwajengea uwezo wataalam na wakulima wadogo. Lengo la Serikali ni kuongeza eneo la umwagiliaji kufikia hekta 1,000,000 ifikapo mwaka 2020. Maelezo ya kina kuhusu huduma za sekta ya umwagiliaji Nchini yameainishwa kuanzia ukurasa wa 85 hadi ukurasa wa 90 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu taasisi zilizo chini ya Wizara nakwanza ni Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Maji; Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Maji ni Taasisi yenye jukumu la kukusanya mapato, kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji na kufuatilia matumizi yake. Lengo la mfuko ni kusaidia uwekezaji kwenye miradi ya maji, utoaji wa huduma ya maji na usimamizi wa maeneo ya vyanzo na vidakio vya maji, kipaumbele ikiwa ni kwenye maeneo yenye uhaba mkubwa wa huduma ya maji hususani maji vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Namba 12 ya Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009, inaeleza kuwa vyanzo vya mapato vya mfuko ni fedha zitakazoidhinishwa na Bunge, misaada pamoja na fedha nyingine zitakazolipwa kwenye mfuko kwa mujibu wa sheria nyingine. Hadi sasa chanzo pekee cha mapato ya mfuko ni tozo ya shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta ya dizeli na shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta ya petroli.

Mheshiwa Naibu Spika, hadi Machi, 2017 mfuko umepokea jumla shilingi bilioni 95.6 kutoka tozo ya mafuta. Fedha hizo zimetumwa katika Halmashauri 99 pamoja na mamlaka 17 za majisafi na usafi wa mazingira kwa ajili ya upanuzi wa miundombinu ya maji katika pembezoni mwa

miji husika. Vilevile fedha hizo zilitumwa kwenye miradi inayosimamiwa na Wizara, jedwali namba 9(a), (b) na (c) linaelezea kwa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda tumetoa maelezo kwenye hotuba yangu kuhusu Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati, *(EWURA),* tumetoa pia maelezo kuhusu Chuo cha Maji, tumetoa maelezo juu ya Wakala wa Uchimbaji Visima na Mabwawa, na pia tumetoa maelezo kuhusu masuala mbalimbali ya mtambuka ambayo yanahusu rasilimali za watu, mapambano dhidi ya rushwa. Tumetoa maelezo pia ujenzi wa ofisi za Wizara, tumetoa maelezo juu ya uratibu wa programu ya maendeleo ya sekta ya maji na kwa sababu ya muda naomba hotuba yangu yote iweze kuingizwa kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee baadhi ya changamoto ambazo tunazo; kupungua kwa rasilimali za maji. Rasilimali za maji zimeendelea kupungua kutokana na uchafuzi na uvamizi wa vyanzo vya maji, matumizi holela ya maji na mabadiliko ya tabianchi. Kupungua kwa rasilimali hizo kumeathiri shughuli za kijamii na kiuchumi. Kwa hiyo, maelezo mengi unaweza kuyapata kwenye hotuba yangu. Pia tumetoa maelezo kiwango kikubwa cha upotevu wa maji na kwa sababu ya uchakavu wa miundombinu kwamba tunahitaji kuwekeza zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumetoa maelezo kuhusu madeni makubwa na ankara za maji kwa Taasisi za Serikali. Taasisi za Serikali kwa muda mrefu zimekuwa hazilipi mpaka madeni yameweza kufikia bilioni 39. Sasa tumefika changamoto kwamba *TANESCO* wameanza kukata huduma ya umeme kwenye miundombinu yetu ya maji, basi ni vizuri Wabunge mkatusaidia tukapata idhinisho ya bajeti hii ili tuweze kulipa madeni hayo ili tuweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kidogo kuhusu shukrani; napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru wadau wote waliochangia kwa njia moja ama nyingine kufanikisha

majukumu ya Sekta za Maji na Umwagiliaji katika kipindi cha mwaka 2016/2017 zikiwemo nchi rafiki. Nchi hizo ni pamoja na Serikali za Ujerumani, Uholanzi, Uingereza, Marekani, Japan, Ufaransa, China, Uswisi, Ubeligiji, Ireland, Korea Kusini, Sweden, Denmark, Norway, India na Misri. Vilevile natoa shukrani kwa Taasisi za fedha za kimataifa na mashirika ya kimaendeleo yakiwemo Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza *(DFID),* Shirika la Maendeleo la Ujerumani, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Maendeleo ya Ujerumani, Benki ya Maendeleo ya Ufaransa, Benki ya Uwekezaji pamoja na Ulaya, Benki ya Kiarabu *(BADEA)*, Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait *(Kuwait Fund),* Mfuko wa Mandela wa Nchi zinazozalisha Mafuta *(OPEC)*, Mfuko wa Maendeleo wa Saudia, Umoja wa Ulaya, Shirika la Maendeleo la Ubelgiji, Shirika la Marekani la Changamoto za Milenia *(MCC),* Benki ya Dunia, Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa, Shirika la Ushirikiano la Kimataifa la Japan, Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Makazi Duniani *na* Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF),* Shirika la Misaada ya Maendeleo la Sweden *(SIDA)* na Shirika la Misaada la Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kutambua mchango wa asasi mbalimbali za Kiserikali**,** naomba sasa nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mhandisi Isack Aloyce Kamwelwe - Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji; Profesa Kitila Alexander Mkumbo - Katibu Mkuu; Mhandisi Emmanuel Masasi Kalobelo - Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, wataalam na watumishi wote wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji; pamoja na watendaji wote na mashirika yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie shukrani zangu kwa wananchi wote wa Wilaya ya Wanging'ombe kwa kuendelea kuniamini na kuniunga mkono katika kuleta maendeleo ya Wilaya yetu. Naomba niendelee kuwaahidi kwamba tutatekeleza ahadi zote ambazo mimi niliwaahidi wakati wa kampeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi

672,223,100,937 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2017/2018, ili niweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii. Mchanganuo wote ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 49, jumla ya shilingi 648,064,207,707 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya Sekta ya Maji kwa mwaka 2017/2018. Kati ya fedha hizo Matumizi ya Kawaida ni shilingi 24,457,459,705 ambapo shilingi 6,636,613,705 sawa na asilimia 27 ni kwa ajili ya kugharamia matumizi mengineyo na shilingi 17,820,941,000 sawa na asilimia 73 ni kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wa Wizara na Chuo cha Maji. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni shilingi 623,606,748,000 ambapo kati ya fedha hizo shilingi 408,617,643,000 sawa na asilimia 66 ni fedha za ndani na shilingi 214,989,105,000 sawa na asilimia 34 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu la 05, jumla ya shilingi 24,158,893,232 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya Sekta ya Umwagiliaji kwa mwaka 2017/2018. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni shilingi 4,055,481,082 ambapo shilingi 585,184,082 sawa na asilimia 14.4 ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo na shilingi 3,470,297,000 sawa na asilimia 85.6 ni kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni shilingi 20,103,412,150 ambapo kati ya fedha hizo shilingi 5,600,000,000 sawa na asilimia 27.9 ni fedha za ndani na shilingi 14,503,412,150 sawa na asilimia 72.1 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nitoe shukrani zangu kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara kwa anwani www.maji.go.tz.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI MHE. ENG. GERSON HOSEA LWENGE (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI KWA MWAKA 2017/2018 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

**1.** **Mheshimiwa Spika**, leo hii Bunge lako Tukufu limepokea taarifa ya Mwenyekiti wa **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo**, **Mifugo na Maji**, **Mheshimiwa Daktari Mary Michael Nagu**, **Mbunge wa Hanang'**, inayohusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Naomba sasa, kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2017/2018.

**2.** **Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati hiyo kwa kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2017/2018. Maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa na **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo**, **Mifugo na Maji** yamezingatiwa wakati wa maandalizi ya bajeti ya Wizara yangu.

**3.** **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kumpongeza **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, **Mheshimiwa Daktari John Pombe Joseph Magufuli**, **Makamu wa Rais**, **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** na **Waziri Mkuu**, **Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa** kwa uongozi makini na thabiti waliouonesha katika mwaka wa kwanza wa Serikali ya Awamu ya Tano pamoja na juhudi zao kwenye ukusanyaji wa kodi; kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ya Serikali; pamoja na mapambano dhidi ya rushwa, ufisadi,

na madawa ya kulevya. Vilevile, nichukue fursa hii kuwapongeza viongozi hao kwa azma yao ya dhati ya kuipeleka Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati kupitia viwanda. Hii ni ishara tosha ya uzalendo walionao kwa nchi yetu na imani yao katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata maendeleo ya haraka na ya uhakika.

4. **Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya ambao ni **Mhe. Juma Ali Juma (Mb)** aliyechaguliwa kuwa Mbunge kupitia Jimbo la Dimani na **Mhe. Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare (Mb)** kuwa Mbunge kupitia Viti Maalum. Nawapongeza pia **Mhe. Anne Kilango Malecela (Mb), Mhe. Abdallah Majurah Bulembo (Mb)**, **Mhe. Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb)** na **Mhe. Salma Rashid Kikwete (Mb)** walioteuliwa na **Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

5. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa pole kwako wewe mwenyewe Mhe. Spika, Bunge lako Tukufu, Familia za Marehemu, Ndugu, Jamaa na Watanzania wote kwa misiba iliyotupata kwa kuondokewa na aliyekuwa **Mbunge wa Dimani**, **Mhe. Hafidh Ali Tahir** pamoja na aliyekuwa **Mbunge wa Viti Maalum**, **Mhe. Dkt. Elly Marko Macha**. Michango ya Wabunge hao katika shughuli za maendeleo ya Taifa letu itakumbukwa milele daima. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu hao mahali pema peponi. **Amin**.

6. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, natoa pole kwa wananchi wa maeneo mbalimbali nchini waliokumbwa na majanga katika mwaka 2016/2017 ya kupoteza ndugu, marafiki na mali zao. Kwa namna ya pekee natoa pole kwa wahanga wa tetemeko la ardhi lililotokea katika Mkoa wa Kagera na kuleta madhara makubwa. Namwomba Mwenyezi Mungu awape nguvu na moyo wa subira wahanga wote.

7. **Mheshimiwa Spika**, naomba pia nichukue fursa hii kumshukuru, **Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa**

**Tanzania**, **Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa (Mb)** kwa hotuba yake mahiri aliyoiwasilisha hapa Bungeni ambayo inatoa dira na mwongozo wa utekelezaji wa kazi za Serikali. Hotuba hiyo imeonesha mapitio ya uendeshaji wa shughuli za Serikali ya Awamu ya Tano kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 na Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2017/2018 pamoja na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2015 – 2020). Vilevile, nawapongeza Mawaziri wenzangu wote walionitangulia kuwasilisha hoja zao na Wabunge waliochangia hoja hizo.

8. **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara yangu yenye maeneo makuu manne yafuatayo:- Hali ya Sekta za Maji na Umwagiliaji Nchini; Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 na Malengo ya Sekta kwa mwaka 2017/2018; Ushiriki wa Sekta Binafsi katika kutekeleza miradi ya Sekta za Maji na Umwagiliaji; pamoja na Changamoto na Hatua zilizochukuliwa. Maelezo ya maeneo hayo yamezingatia Mpango wa Maendeleo wa Taifa; Sera, Mikakati na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2015 – 2020). Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji huo yameainishwa kwenye sehemu zifuatazo katika hotuba hii.

## 2.0 HALI YA SEKTA ZA MAJI NA UMWAGILIAJI NCHINI

9. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maji na umwagiliaji kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa mujibu wa Sera ya Maji ya mwaka 2002; Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2010; pamoja na Sheria za Maji na Umwagiliaji na Kanuni zake. Utekelezaji huo unazingatia maelekezo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2016 - 2030; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020; na ahadi mbalimbali za Serikali. Utekelezaji wa mipango hiyo, umeboresha hali ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji; upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya vijijini na mijini;

pamoja na kuongeza eneo lenye miundombinu ya umwagiliaji.

10. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na maboresho hayo, Sekta za Maji na Umwagiliaji zimeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo kupungua kwa rasilimali za maji kunakosababishwa na uharibifu wa mazingira, mabadiliko ya tabianchi na matumizi mabaya ya maji; ongezeko la watu lisilowiana na kiwango cha uwekezaji katika Sekta hizo; na kuongezeka kwa mahitaji ya maji kutokana na ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii. Serikali imeendelea kukabiliana na changamoto hizo kwa kuimarisha hali za upatikanaji wa huduma za maji na umwagiliaji katika maeneo mbalimbali nchini. Kuimarika kwa huduma hizo ni kichocheo kikubwa katika kufikia azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuwa na **"Tanzania ya Viwanda"** na kuelekea kuwa nchi ya kipato cha uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

11. **Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za maji na umwagiliaji, Wizara yangu imeendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji pamoja na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwa upande wa Umwagiliaji kwa kuzingatia Sera, Sheria na Kanuni zilizopo. Hali halisi katika Sekta hizo ni kama ifuatavyo:-

## 2.0 2.1 SEKTA YA MAJI

12. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ulikamilika mwezi Juni, 2016. Kwa sasa, Wizara inatekeleza Awamu ya Pili ya Programu hiyo iliyoanza mwezi Julai, 2016. Awamu hiyo inatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano na imegawanyika katika programu ndogo tano ambazo ni Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji; Huduma ya Maji Vijijini; Huduma ya Maji Mijini; Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira; na Kujenga Uwezo wa Taasisi. Kwa sasa, programu ndogo hizo zipo katika hatua zifuatazo:-

### 2.1.1 Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

13. **Mheshimiwa Spika**, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini unafuata taratibu za usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji kupitia Bodi za Maji za Mabonde tisa yaliyopo nchini, ambapo mabonde saba kati ya hayo yanahusisha majishirikishi kati ya nchi yetu na nchi jirani. Kutokana na rasilimali hizo za maji, takwimu zilizopo zinaonesha kuwa maji yanayofaa kwa matumizi mbalimbali ni **kilomita za ujazo 96.27** na kila mwananchi ana uwezo wa kupata maji wastani wa **mita za ujazo 1,800** kwa mwaka. Aidha, kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa kila mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa ni **mita za ujazo 1,700**. Iwapo hatua madhubuti hazitachukuliwa, kiwango hicho kitapungua hadi kufikia **mita za ujazo 883** katika mwaka 2035. Serikali inaendelea na jitihada za kukabiliana na changamoto ya kupungua kwa rasilimali za maji ikiwa ni pamoja na uhamasishaji wa uvunaji wa maji ya mvua ili nchi yetu isifikie kiwango kikubwa cha uhaba wa maji na kusababisha athari kwa maendeleo ya nchi.

14. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa kihaidrolojia ulioanza mwezi Novemba 2015 hadi mwezi Oktoba 2016, hali ya mvua katika mabonde ya maji nchini ilitofautiana kutokana na tabia tofauti za hali ya hewa. Pamoja na muonekano wa kuwepo kwa mvua kubwa katika baadhi ya maeneo nchini, kwa ujumla hali ya mvua katika kipindi hicho imeendelea kuwa chini ya wastani. Kiwango cha maji katika maziwa, mito na mabwawa mbalimbali kwa kipindi hicho ni kama inavyooneshwa katika ***Jedwali Na.1***.

15. **Mheshimiwa Spika**, mwenendo usioridhisha wa upatikanaji wa mvua kwenye baadhi ya maeneo nchini umeathiri shughuli za maendeleo zikiwemo kilimo, ufugaji na uzalishaji wa umeme. Kutokana na hali hiyo, kumekuwa na mvutano baina ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa maji. Katika kukabiliana na hali hiyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, imeanza kuandaa Mfumo wa Tahadhari (*Early Warning System*) ambao utahusu ufungaji wa vifaa vya kuchunguza mwenendo wa

hali ya hewa kwenye maeneo mbalimbali nchini. Lengo la Mfumo huo ni kuboresha taarifa za hali ya hewa ambazo zitawasaidia wananchi kuandaa mikakati ya kukabiliana na majanga yatakayojitokeza.

### 2.1.2 Huduma ya Maji Vijijini

**16.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya vijijini kupitia Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kwa kujenga, kupanua na kukarabati miundombinu ya maji, kujenga miradi ya visima virefu na vifupi pamoja na kujenga mabwawa katika maeneo kame. Utekelezaji wa Programu hiyo umeboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini ambapo hadi mwezi Machi 2017, jumla ya watu **22,951,371** sawa na **asilimia 72.58** ya wananchi waishio vijijini wanapata huduma ya maji safi na salama katika umbali usiozidi mita 400 kama Sera ya Maji ya Mwaka 2002 inavyoelekeza.

**17.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kuhamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika kupanga, kujenga na kuendesha miradi ya maji katika maeneo yao, ikiwa ni pamoja na kuunda na kuimarisha Vyombo vya Watumiaji Maji (*Community Owned Water Supply Organizations - COWSOs*). Lengo la kuunda na kuimarisha vyombo hivyo ni kuhakikisha kuwa huduma ya maji inakuwa ya uhakika na endelevu. Hadi mwezi Machi 2017, uhamasishaji uliofanyika umeleta mafanikio na mwamko wa wananchi katika kumiliki na kugharamia uendeshaji wa miradi ya maji vijijini kupitia jumla ya Vyombo vya Watumiaji Maji **1,799** vilivyosajiliwa.

### 2.1.3 Huduma ya Maji Mijini

**18.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji Mikuu ya Mikoa, Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Maji ya Kitaifa imeendelea na ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi

katika maeneo ya miji hiyo. Kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015 - 2020), malengo ya Serikali ni kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Miji Mikuu ya Mikoa kutoka **asilimia 86** hadi kufikia **asilimia 95**; Miji Mikuu ya Wilaya, Miji midogo na Miradi ya Kitaifa kutoka **asilimia 60** hadi **asilimia 75**; na katika Jiji la Dar es Salaam kutoka **asilimia 72** hadi **asilimia 95** ifikapo mwaka 2020. Kwa sasa, hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka mijini ni kama ifuatavyo:-

**(a) Huduma ya Majisafi Mijini**

**(i) Miji Mikuu ya Mikoa**

**19.** **Mheshimiwa Spika**, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Miji Mikuu ya Mikoa imeendelea kuimarika na kuweza kupunguza kero ya uhaba wa maji safi kwa wananchi wa miji hiyo. Idadi ya wateja waliounganishiwa huduma hiyo imeongezeka kutoka **405,095** mwezi Machi 2016, hadi wateja **432,772** mwezi Machi, 2017 ambapo **asilimia 97** ya wateja hao wamefungiwa dira za maji ili kulipia huduma ya maji kulingana na matumizi.

**20.** **Mheshimiwa Spika**, kupungua kwa wingi wa maji katika vyanzo vya maji mbalimbali nchini kumesababisha kushuka kwa wastani wa uzalishaji wa maji katika miji mikuu ya mikoa kutoka **lita milioni 470** kwa siku mwezi Machi 2016 hadi kufikia **lita milioni 400** kwa siku mwezi Machi, 2017. Hali hiyo imesababisha wakazi katika baadhi ya miji mikuu ya mikoa kupata huduma ya maji kwa mgao. Katika jitihada za kuimarisha vyanzo vya maji, Wizara inaendelea kuhamasisha wananchi kuhusu utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji pamoja na utafutaji wa vyanzo vingine vya maji ikiwemo ujenzi wa mabwawa ya kimkakati na uchimbaji wa visima virefu.

**(ii) Jiji la Dar es Salaam**

**21.** **Mheshimiwa Spika**, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na

Bagamoyo imeimarika kutokana na kukamilika kwa maboresho ya mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini ambapo uzalishaji wa maji umeongezeka kutoka **lita milioni 300** hadi **lita milioni 504** kwa siku. Aidha, mahitaji ya maji yameongezeka kutoka **lita milioni 450** mwezi Machi, 2016 hadi **lita milioni 544** mwezi Machi, 2017.

**22.** **Mheshimiwa Spika**, idadi ya maunganisho kwenye mtandao wa majisafi imeongezeka kutoka wateja **155,000** mwezi Machi, 2016 hadi kufikia wateja **182,721** mwezi Machi, 2017. Hali hiyo imechangia kuongezeka kwa makusanyo ya maduhuli yanayotokana na mauzo ya maji kwa mwezi kutoka wastani wa **Shilingi bilioni 7.1** mwezi Machi, 2016 hadi **Shilingi bilioni 8.3** mwezi Machi, 2017. Vilevile, upotevu wa maji umeendelea kupungua kutoa **asilimia 47** mwezi Machi, 2016 hadi **asilimia 38** mwezi Machi, 2017. Lengo ni kupunguza upotevu huo kufikia **asilimia 25** ifikapo mwaka 2020. Wizara inaendelea kukamilisha ujenzi wa miradi ya kuongeza uzalishaji wa maji pamoja na miradi ya miundombinu ya kusambaza maji ili kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo mengi zaidi ya Jiji la Dar es Salaam pamoja na Miji ya Kibaha na Bagamoyo.

**(iii) Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Maji ya Kitaifa**

**23.** **Mheshimiwa Spika**, uzalishaji wa maji katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo umeongezeka kutoka **lita milioni 99.5** mwezi Machi, 2016 hadi **lita milioni 99.7** kwa siku mwezi Machi, 2017 ikilinganishwa na mahitaji ya maji ya **lita milioni 273** kwa siku. Kwa upande wa miradi ya maji ya Kitaifa uzalishaji wa maji umeongezeka kutoka wa **lita milioni 57.2** hadi kufikia **lita milioni 59.5** ambapo mahitaji ya maji ni **lita milioni 119** kwa siku. Pamoja na ongozeko hilo la uzalishaji wa maji bado mahitaji ya maji ni makubwa katika maeneo ya Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Maji ya Kitaifa ikilinganishwa na uzalishaji uliopo. Kutokana na hali hiyo Wizara inaendelea kuwekeza katika miundombinu ya maji pamoja na kuzijengea uwezo mamlaka za maji ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama na kuboresha huduma za kiuchumi na kijamii katika maeneo hayo.

**(b) Uondoaji wa Majitaka Mijini**

**24. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya majitaka katika Miji Mikuu **10** ya Mikoa yenye mtandao wa majitaka ambayo ni Arusha, Dodoma, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Tabora, Moshi, Tanga, Songea na Iringa. Idadi ya wateja waliounganishwa kwenye mitandao ya majitaka katika miji hiyo imeongezeka kutoka **25,361** mwezi Machi, 2016 hadi kufikia wateja **26,636** mwezi Machi, 2017 na kuweza kupunguza kero ya majitaka kutiririka ovyo katika miji hiyo. Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam, idadi ya wateja waliounganishwa kwenye mtandao wa majitaka imeongezeka kutoka **18,436** mwezi Machi, 2016 hadi kufikia wateja **19,034** mwezi Machi, 2017. Kwa sasa wastani wa utoaji wa huduma ya uondoaji majitaka katika miji hiyo ikijumuisha Jiji la Dar es Salaam ni **asilimia 20**. Wizara imeweka mkakati wa kuhakikisha kuwa miradi yote ya majisafi itakayotekelezwa ni lazima kuwepo na kipengele cha mradi wa usafi wa mazingira utakaohusisha miundombinu ya uondoaji wa majitaka ikiwemo mabwawa ya kutibu majitaka pamoja na ununuzi wa magari ya huduma ya uondoaji majitaka. Mkakati huo unatarajiwa kuongeza huduma ya uondoaji majitaka kufikia **asilimia 30** ifikapo mwaka 2020.

**3.0 2.1.4 Kujenga Uwezo wa Taasisi**

**25. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kujenga uwezo wa Taasisi zinazotekeleza Programu za Maendeleo ya Sekta ya Maji na Sekta ya Kilimo kwa upande wa umwagiliaji, kwa kuzipatia Sekta hizo watalaam wa kada mbalimbali hususan wahandisi na mafundi sanifu watakaofanikisha utekelezaji wa programu hizo. Hadi mwezi Machi 2017, Wizara imepata kibali cha kuajiri jumla ya Watalaam **243** wa Sekta ya Maji ambao watapangiwa vituo vya kazi katika ngazi ya Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya. Vilevile, kibali cha kuajiri Wataalam **40** wa Sekta ya Umwagiliaji kimetolewa. Watalaam hao watakaoajiriwa watasaidia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Sekta hizo kwenye maeneo mbalimbali nchini. Aidha,

Wizara imeendelea kuzijengea uwezo Taasisi zake kwa kuzijengea ofisi, kuzipatia watumishi na vitendea kazi ili kuongeza ufanisi wa utoaji huduma za maji na umwagiliaji nchini.

## 4.0 2.2 SEKTA YA UMWAGILIAJI

**26. Mheshimiwa Spika**, Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002 ulibaini kuwa nchi yetu ina eneo la **hekta milioni 29.4** zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Eneo hilo lina uwezekano tofauti wa kumwagiliwa ambapo **hekta milioni 2.3** zina uwezekano mkubwa, **hekta milioni 4.8** zina uwezekano wa kati na **hekta milioni 22.3** zina uwezekano mdogo. Hadi mwezi Machi 2017, eneo linalomwagiliwa limeongezeka kutoka **hekta 461,326** kwa mwaka 2015/2016 na kufikia **hekta 468,338**. Eneo hilo linachangia **asilimia 24** ya mahitaji yote ya chakula nchini kwa sasa. Lengo ni kuongeza eneo la umwagiliaji kufikia **hekta 1,000,000** katika skimu za wakulima wadogo, wa kati na wakubwa ifikapo mwaka 2020.

**27. Mheshimiwa Spika**, Serikali imekamilisha utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Programu Ndogo ya Umwagiliaji katika Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo. Awamu ya Pili inatarajiwa kuanza kutekelezwa mwaka 2017/2018 kwa kipindi cha miaka mitano. Katika Awamu hiyo, Serikali imepanga kukamilisha ujenzi wa miundombinu katika skimu **176**, ukarabati wa skimu **205**, ukarabati wa mabwawa **30** na kujenga mabwawa mapya **40** ili kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na matumizi mengine kwenye maeneo mbalimbali nchini.

## 4.1 3.0 MAPATO YA FEDHA KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2016/2017

**28. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Fungu 49 – Wizara ya Maji na Umwagiliaji liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 939,631,302,771** na kati ya fedha hizo **Shilingi 24,437,365,000** zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na **Shilingi 915,193,937,771** zilikuwa ni fedha za maendeleo. Hadi

mwezi Machi 2017, jumla ya **Shilingi 181,209,813,609** sawa na **asilimia 19.8** ya fedha za maendeleo zilipokelewa ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi 95,506,951,632** zilipatikana kupitia Mfuko wa Maji. Aidha, **Shilingi 14,286,952,966** sawa na **asilimia 58.5** ya fedha za matumizi ya kawaida zilipokelewa.

**29.** **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 39,876,143,028**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 4,506,613,600** zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na **Shilingi 35,369,529,428** zilikuwa ni fedha za maendeleo. Hadi mwezi Machi 2017, jumla ya **Shilingi 2,986,101,292** sawa na **asilimia 8.4** ya fedha za maendeleo zilipokelewa; na **Shilingi 2,532,329,224** sawa na **asilimia 56.2** ya fedha za matumizi ya kawaida zilipokelewa.

## 4.2 4.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2016/2017 NA MALENGO YA MWAKA 2017/2018

**30.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Wizara yangu ilitekeleza miradi inayohusu usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini; kuongeza upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini na mijini; uendelezaji wa miundombinu ya umwagiliaji; na kutekeleza malengo ya masuala mtambuka. Mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/2017 na malengo ya mwaka 2017/2018 yamefafanuliwa katika sehemu zifuatazo za hotuba hii:-

## 5.0 4.1 USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA RASILIMALI ZA MAJI

**31.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Wizara yangu iliendelea kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji nchini na majishirikishi kupitia Bodi za Maji za Mabonde, Ofisi za Mabonde Madogo na Jumuiya za Watumia Maji. Usimamizi huo ulihusu kuchunguza na kutathmini wingi na ubora wa maji juu na chini ya ardhi; kuandaa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali hizo; pamoja na kusanifu na kusimamia ujenzi wa miundombinu ya kipaumbele.

#### 4.1.1 Mwenendo wa Rasilimali za Maji

32. **Mheshimiwa Spika**, katika kusimamia mwenendo wa rasilimali za maji nchini, Wizara yangu imeendelea kuimarisha vituo vya kupima wingi na ubora wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi ili kuboresha upatikanaji wa takwimu na taarifa sahihi. Takwimu na taarifa hizo husaidia kutambua hali ya maji kwa nyakati tofauti kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini, hivyo kukamilisha uandaaji wa mipango na maamuzi sahihi ya ugawaji wa rasilimali za maji kwa matumizi mbalimbali.

33. **Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Machi 2017, jumla ya vituo **55** vilifanyiwa ukarabati kwenye mabonde ya Ziwa Victoria **(17)**, Rufiji **(12)**, Wami-Ruvu **(9)**, Pangani **(9)**, Ruvuma na Pwani ya Kusini **(5)**, Bonde la Kati **(2)** na Ziwa Nyasa **(1)**; na vituo **13** vya hali hewa vilijengwa katika mabonde ya Pangani **(9)**, Rufiji **(2)**, Ziwa Tanganyika **(1)** na Ruvuma na Pwani ya Kusini **(1)**. Vilevile, takwimu za hali ya maji nchini zilikusanywa na kuchambuliwa kutoka vituo **215** vya kupima maji katika mito, **156** vya mvua, **81** vya hali ya hewa, **30** vya kupima usawa maji chini ya ardhi na vituo **5** vya kupima usawa wa maji kwenye maziwa na mabwawa. Katika mwaka 2017/2018, Wizara imepanga kujenga vituo **90** na kukarabati vituo **35** katika mabonde yote pamoja na kuboresha ukusanyaji wa takwimu za rasilimali za maji.

#### 4.1.2 Uhifadhi wa Mazingira na Vyanzo vya Maji

34. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuvitambua, kuviwekea mipaka na kuvitangaza vyanzo vya maji kuwa maeneo tengefu ili kuvilinda na kuvihifadhi kwa ajili ya kuzuia uharibifu na uchafuzi wa vyanzo hivyo. Hadi mwezi Machi 2017, jumla ya vyanzo **73** vimewekewa mipaka na kati ya hivyo, **18** ambapo vyanzo vimetangazwa katika Gazeti la Serikali kuwa maeneo tengefu ambapo vyanzo **tisa (9)** vimetangazwa katika mwaka 2016/2017. Maeneo hayo ni Bwawa la Mindu lililoko Bonde la Wami-Ruvu pamoja na Mito ya Halewa/ Swaya, Mfwizimo/Iziwa, Nzovwe, Ivumwe, Imeta, Hanzya,

Mfwizimo/Lunji na Sisimba iliyoko Bonde la Ziwa Rukwa. Vyanzo hivyo ni kwa ajili ya matumizi ya maji majumbani. Katika mwaka 2017/2018, Wizara yangu itaendelea kuweka mipaka na kutangaza maeneo ya vyanzo vya maji yaliyoainishwa ili kuyakinga dhidi ya uharibifu wa mazingira na kuhakikisha usalama wa vyanzo na uhakika wa upatikanaji wa maji kwa maendeleo endelevu.

#### 4.1.3 Kudhibiti Uchafuzi wa Vyanzo vya Maji

**35.** **Mheshimiwa Spika**, katika kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji, Bodi za Maji za Mabonde hufanya ukaguzi, kupima na kuchakata takwimu zinazoonesha ubora wa maji katika vyanzo mbalimbali vya maji pamoja na majitaka kutoka maeneo mbalimbali ya uzalishaji. Katika mwaka 2016/2017, sampuli **241** za maji kutoka vyanzo mbalimbali vya maji katika mabonde ya Ziwa Victoria **(93)** na Wami-Ruvu **(148)** zilipimwa na kuchakatwa ili kupata hali ya ubora wa maji katika vyanzo hivyo. Matokeo ya uchunguzi wa sampuli **82** kutoka maeneo ya Bonde la Ziwa Victoria yalionesha kukidhi viwango vinavyokubalika isipokuwa sampuli **11** za maji kutoka baadhi ya vyanzo vya visima vifupi vinavyozunguka mgodi wa North Mara na Mto Tighite zilionekana kuwa na vimelea vya vijidudu. Maeneo yaliyobainika kuwa na maji yenye vimelea vya vijidudu, ilishauriwa kusitishwa kwa shughuli za kibinadamu ambazo zimesababisha uchafuzi wa vyanzo vya maji kwenye maeneo hayo. Vilevile, Wizara ilihakiki maeneo ya kujenga mabwawa ya majitaka ya migodi **mitano (5)** ya *Nyarugusu Mine, Aura Minerals (Tz) Limited, New Luika Gold Mine, Gengetatu Extech Co.Ltd* na *Nyamahuna Medium Scale Gold Mine*. Katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kufanya uchunguzi katika vyanzo vya maji na ukaguzi kwenye maeneo ya uzalishaji kama viwanda na migodi na kuchukua hatua stahiki.

#### 4.1.4 Kutafuta Vyanzo Vipya vya Maji

**36.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Wizara yangu imeendelea kutafuta vyanzo mbalimbali vya maji na

kuhakikisha vinabainishwa na kufanyiwa tathmini ili viweze kuendelezwa na kuongeza upatikanaji wa maji nchini. Utafiti wa maji chini ya ardhi ulifanyika kwenye maeneo **174** katika mabonde ya Ruvuma na Pwani ya Kusini **(72)**, Bonde la Kati **(21)**, Ziwa Victoria **(20)**, Pangani **(39)**, Wami-Ruvu **(15)**, Rufiji **(3)** na Ziwa Tanganyika **(4)** na kubaini kuwa maeneo hayo yanafaa kuendelezwa kuwa vyanzo vya maji. Vilevile, Wizara imekamilisha maandiko ya miradi ya mabwawa ya kimkakati ya Farkwa na Ndembera kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi. Tathmini ya fidia kwa wananchi watakaoathirika na miradi ya ujenzi wa mabwawa hayo inaendelea na inatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2017. Katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa hayo pamoja na kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi katika maeneo mengine nchini.

### 4.1.5 Udhibiti wa Uchimbaji Holela wa Visima

**37.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu ina jukumu la kuratibu na kusajili kampuni za utafiti na uchimbaji wa visima vya maji ili kudhibiti uchimbaji holela wa visima hivyo. Vilevile, Bodi za Maji za Mabonde zimepewa mamlaka ya kuratibu na kutoa vibali vya uchimbaji visima katika maeneo mbalimbali nchini. Utaratibu huo unalenga kuhakikisha misingi ya kitaalam inafuatwa katika uchimbaji wa visima kwenye maeneo husika. Katika mwaka 2016/2017, maombi **19** ya leseni kutoka kampuni za uchimbaji visima na kampuni **mbili (2)** za utafiti wa maji chini ya ardhi yalipokelewa. Kati ya maombi hayo, leseni **15** kwa kampuni za uchimbaji visima na leseni **moja (1)** ya kampuni ya utafiti wa maji chini ya ardhi zilitolewa. Hadi mwezi Machi 2017, vibali vya kuchimba visima **441** vya maji katika maeneo mbalimbali nchini vilitolewa ambapo visima **242** vilichimbwa na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa na visima **199** vilichimbwa na makampuni binafsi.

### 4.1.6 Matumizi Bora ya Rasilimali za Maji

**38.** **Mheshimiwa Spika**, matumizi ya rasilimali za maji yanazingatia kanuni za ugawaji maji kwa matumizi

mbalimbali kwa mujibu wa Sheria **Na. 11** ya mwaka 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji. Katika mwaka 2016/2017, Wizara yangu kupitia Bodi za Maji za Mabonde ilitoa jumla ya vibali vipya **914** vya kutumia maji katika Bonde la Kati vibali **154**, Wami-Ruvu **(152)**, Rufiji **(149)**, Pangani **(126)**, Ziwa Rukwa **(115)**, Ziwa Nyasa **(60)**, Ziwa Victoria **(57)**, Ziwa Tanganyika **(55)** pamoja na Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini vibali **46**. Vilevile, vibali **12** vya kutiririsha majitaka katika Bonde la Pangani vibali **9**, Rufiji **(2)** na Wami-Ruvu **(1)** vilitolewa. Katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kupokea maombi na kutoa vibali vya matumizi ya rasilimali za maji kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

### 4.1.7 Mipango ya Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

**39.** **Mheshimiwa Spika**, Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji imekamilika katika Mabonde ya Ruvuma na Pwani ya Kusini, Ziwa Rukwa, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika, Rufiji na Bonde la Kati. Utekelezaji wa mipango hiyo utaanza baada ya kufanyiwa Tathmini ya Kimkakati ya Kimazingira na Kijamii (*Strategic Environment and Social Assessment*). Hadi mwezi Machi 2017, rasimu ya mwisho ya Tathmini ya Kimkakati ya Kimazingira na Kijamii katika Bonde la Rufiji imekamilika na kuwasilishwa kwa wadau na sasa Mtaalamu Mshauri anafanyia kazi maoni ya wadau. Aidha, Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kutayarisha tathmini hiyo kwa mabonde mengine **matano (5)** yaliyokamilisha mipango shirikishi amepatikana na rasimu ya mkataba imeandaliwa. Katika mwaka 2017/2018, Wizara itakamilisha uandaaji wa mipango shirikishi katika mabonde ya Wami-Ruvu, Pangani na Ziwa Victoria pamoja na tathmini za kimkakati kwa mipango iliyokamilika.

### 4.1.8 Mradi wa Kufanikisha Uhakika wa Maji Eneo la SAGCOT

**40.** **Mheshimiwa Spika**, awamu ya kwanza ya mradi wa kufanikisha uhakika wa maji kwenye eneo la *Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania* (*SAGCOT*) unaofadhiliwa na **Shirika la Maendeleo la Kimataifa la**

**Serikali ya Uingereza (*Department for International Development - DFID)*** inaendelea kutekelezwa kwenye Bonde la Rufiji katika maeneo ya Usangu na Kilombero. Katika mwaka 2016/2017, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilika kwa utafiti wa kuangalia mwingiliano wa maji ya juu na chini ya ardhi, wingi na ubora wake katika eneo la Usangu (Mbarali) kwa kutumia *Isotope Sampling* pamoja na kutambua vyanzo vya maji (*Water Source Mapping)* katika mabonde madogo ya Kilombero na Usangu. Awamu hiyo imekamilika mwezi Desemba, 2016. Awamu ya pili ya mradi itakayotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano itagharimu **Paundi za Uingereza milioni 31.7** na inatarajiwa kuanza baada ya kupatikana kwa fedha. Awamu hiyo itahusisha kazi zitakazotekelezwa katika ngazi ya Wizara pamoja na mabonde ya Rufiji na Pangani.

### 4.1.9 Kuimarisha Bodi za Maji za Mabonde

**41.** **Mheshimiwa Spika**, Bodi za Maji za Mabonde zimeendelea kujengewa uwezo na kuimarishwa ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Katika mwaka 2016/2017, ujenzi wa ofisi kwa ajili ya Bodi za Maji za Mabonde ya Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika umekamilika. Vilevile, ujenzi na ukarabati wa ofisi za Bodi za Maji za Mabonde ya Kati, Ruvuma na Pwani ya Kusini, Ziwa Rukwa, ofisi Ndogo ya Ziwa Nyasa pamoja na ofisi za Jumuiya za Watumia Maji Likonde na Mto wa Mbu unaendelea. Aidha, usanifu na makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Bonde la Wami/Ruvu na Pangani umekamilika na wakandarasi wamekabidhiwa maeneo ya ujenzi. Ujenzi wa ofisi zote za Bodi za Maji za Mabonde unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2017/2018.

### 4.1.10 Makusanyo ya Maduhuli

**42.** **Mheshimiwa Spika**, Bodi za Maji za Mabonde hukusanya maduhuli yatokanayo na ada za matumizi ya maji pamoja na kazi mbalimbali za utafiti na kutumia mapato hayo katika usimamizi, utunzaji na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini. Hadi mwezi Machi 2017, jumla ya **Shilingi 2,953,466,917** zilikusanywa sawa na **asilimia 78** ya lengo la

**Shilingi 3,806,000,000** kwa mwaka 2016/2017. Katika mwaka 2017/2018, Bodi za Maji za Mabonde zimelenga kukusanya kiasi cha **Shilingi 4,145,000,000** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato kama ilivyoainishwa katika ***Jedwali Na. 2***.

### 4.1.11 Udhibiti wa Migogoro katika Matumizi ya Maji

**43.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, migogoro **32** ya watumia maji ilijitokeza katika Bonde la Mto Pangani **(29)**, Wami-Ruvu **(1)**, Ziwa Victoria **(1)** na Ziwa Tanganyika **(1)**. Kati ya hiyo, migogoro **25** katika Bonde la Mto Pangani imesuluhishwa na migogoro mingine **7** ipo katika hatua mbalimbali za usuluhishi. Katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea kutoa elimu kuhusu matumizi, ugawaji na utunzaji wa rasilimali za maji ili kupunguza migogoro ya watumia maji pamoja na kuitatua kadri itakavyojitokeza.

### 4.1.12 Usimamizi wa Rasilimali za Majishirikishi

**44.** **Mheshimiwa Spika**, nchi yetu ina rasilimali za maji tunazoshirikiana na nchi nyingine ambazo zipo katika mabonde saba kati ya tisa. Mabonde hayo ni Bonde la Ziwa Victoria, Bonde la Ziwa Tanganyika, Bonde la Ziwa Nyasa, Bonde la Ziwa Rukwa, Bonde la Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini, Bonde la Mto Pangani na Bonde la Kati. Rasilimali za majishirikishi ni pamoja na Mito ya Ruvuma, Kagera, Mara, Umba, Momba na Songwe; na Maziwa ya Chala, Jipe, Victoria, Tanganyika, Nyasa na Natron. Ushirikiano huo baina ya Tanzania na nchi nyingine unatekelezwa kupitia Mikataba na Makubaliano ambayo yameanzisha Kamisheni au Taasisi za Kikanda zikiwemo *SADC*, *Nile Basin Initiative (NBI)*, Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria (*Lake Victoria Basin Commission - LVBC*), Mamlaka ya Ziwa Tanganyika, Kamisheni ya pamoja ya Maji ya Mto Ruvuma na Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi (*ZAMCOM*). Vilevile, Tanzania ni mwanachama wa Baraza la Mawaziri wa Maji Barani Afrika (*Africa Ministers Council of Water - AMCOW*) ambapo Baraza hilo lina jukumu kuu la kusimamia utekelezaji wa Lengo Namba 6 la Malengo ya Maendeleo Endelevu yanayohusu usalama

wa maji na usafi wa mazingira. Utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali zinazohusu majishirikishi ni kama ifuatavyo:-

**(a) Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria**

**45.** **Mheshimiwa Spika**, Awamu ya Pili ya Mradi wa Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria (*Lake Victoria Environmental Management Program - LVEMP II*) inatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Serikali za Burundi, Kenya, Rwanda na Uganda. Hadi mwezi Machi 2017, miradi **243** ya jamii imekamilika na kati ya hiyo miradi **160** imefanyiwa tathmini na kukabidhiwa kwa Halmashauri husika kwa ajili ya uendeshaji. Aidha, miradi **83** inatarajiwa kufanyiwa tathmini ili ikabidhiwe kwa Halmashauri. Vilevile, miradi **98** iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Miradi mikubwa **20** (*Co-Management Interventions)* kati ya **24** iliyofadhiliwa na *LVEMP II* kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Taasisi mbalimbali za Serikali imekamilika na miradi **minne (4)** ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**46.** **Mheshimiwa Spika**, mradi wa uunganishaji wa majitaka ya majumbani kwenye mtandao mkuu wa majitaka Jijini Mwanza unaendelea na umefikia **asilimia 55**, ukarabati wa machinjio ya Jiji la Mwanza umefikia **asilimia 80** na ujenzi wa mfumo wa kutibu majitaka ya machinjio ya Jiji la Mwanza umefikia **asilimia 75**. Aidha, ukarabati wa Maabara za Maji za Mwanza na Musoma pamoja na ujenzi wa Maabara ya Bukoba unaendelea.

**47.** **Mheshimiwa Spika**, mradi wa *LVEMP II* umefanikiwa kupunguza uwepo wa gugumaji katika Ziwa Victoria kutoka **hekta 518** mwaka 2009 hadi **hekta 116** mwezi Novemba, 2016 kwa kutumia njia za kibaiolojia (*introduction of weevils*) pamoja na nyenzo rahisi za mikono. Kupungua kwa gugumaji kumesaidia kuongeza ubora wa maji na kurahisisha usafirishaji katika Ziwa. Vilevile, mradi umeipatia Idara ya Uvuvi boti **nne (4)** za doria ambazo zimegawiwa katika Mikoa ya Mwanza, Kagera na Mara ili kuimarisha ulinzi wa rasilimali za samaki ziwani. Katika mwaka 2017/2018, mradi huo

umepanga kukamilisha ujenzi wa miradi ya kupunguza uchafuzi wa Ziwa pamoja na mfumo wa kutibu majitaka katika Jiji la Mwanza; kuongeza thamani ya mazao ya miradi ya jamii; na kuanza maandalizi ya awamu nyingine ya mradi. Awamu ya Pili ya mradi wa *LVEMP* inatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Desemba, 2017.

### (b) Programu ya Utunzaji na Uendelezaji wa Bonde la Mto Songwe

**48.** **Mheshimiwa Spika**, nchi za Tanzania na Malawi zimeanza utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Programu ya Utunzaji na Uendelezaji wa Bonde la Mto Songwe ambapo miradi ya uwekezaji inatarajiwa kutekelezwa kwa pamoja na nchi zote. Kazi zitakazotekelezwa katika awamu hiyo ni pamoja na ujenzi wa Bwawa la Songwe Chini kwa ajili ya kuzalisha umeme **(180.2 MW)** na matumizi mengine; skimu mbili za umwagiliaji **hekta 6,200 (**ambapo kwa Tanzania ina **hekta 3,150** na Malawi **hekta 3,050)**; ukarabati wa mkondo wa mto katika uwanda wa chini wa mafuriko; ujenzi wa mradi wa maji ya kunywa kwa ajili ya wananchi wanaoishi katika miji midogo ya Kasumulu (Tanzania) na Songwe (Malawi) pamoja na jamii inayoishi kwenye uwanda wa chini wa Mto; na kutekeleza mipango iliyobainishwa ya miradi ya maji, umeme, maendeleo ya uvuvi, barabara na utalii vijijini. Kazi hizo zitasimamiwa na Kamisheni ya Kudumu ya Bonde la Mto Songwe itakayoanzishwa baada ya Nchi Washirika kusaini Mkataba *(Convetion on the Establishment of the Songwe River Basin Commision)*. Taratibu za kuridhia mkataba huo zipo katika hatua za mwisho na nchi hizo zinaendelea na jitihada za kutafuta fedha kutoka kwa wafadhili na wawekezaji mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza miradi iliyopangwa.

### (c) Bonde la Mto Nile

**49.** **Mheshimiwa Spika**, Umoja wa Ushirikiano wa Nchi za Bonde la Mto Nile *(Nile Basin Initiative – NBI)* ni chombo cha mpito kuelekea uundwaji wa Kamisheni ya Bonde la Mto Nile. Jumla ya nchi **11** zinazounda umoja huo ni Burundi,

Ethiopia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Misri, Rwanda, Sudan, Sudan Kusini, Uganda na Tanzania na nchi ya Eritrea ikiwa ni Mtazamaji (Observer). Nchi hizo zinashirikiana katika matumizi ya Mto Nile ambao moja ya chanzo chake ni Ziwa Victoria. Madhumuni ya kuanzishwa kwa umoja huo ni kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji, mazingira, nishati, kilimo, mafunzo na kujenga uwezo kwa taasisi zilizopo katika nchi husika.

**50.** **Mheshimiwa Spika**, Tanzania ilipewa heshima ya kuwa mwenyeji wa maadhimisho ya 11 ya siku ya Nile ambayo yalifanyika tarehe 22 Februari, 2017 na Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo alikuwa **Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**. Kaulimbiu ya Maadhimisho hayo ilikuwa ni '*Our Shared Nile: Source of Energy, Food and Water for All*' yenye maana ya kuhakikisha usalama wa upatikanaji wa chakula, maji, na nishati ya umeme kwa jamii inayozunguka Bonde hilo. Jumla ya washiriki **600** kutoka nchini na nchi washirika wa Bonde la Mto Nile walihudhuria maadhimisho hayo. Maadhimisho hayo hufanyika kila mwaka ili kukuza uelewa kuhusu umuhimu wa ushirikiano baina ya nchi zote wanachama, miradi inayotekelezwa na faida inayotokana na matumizi bora ya rasilimali za maji katika Bonde la Mto Nile.

**51.** **Mheshimiwa Spika**, kuna miradi mbalimbali inayoendelea kutekelezwa chini ya Bonde la Mto Nile, mojawapo ni mradi wa Bonde dogo la Mto Kagera. Bonde hilo linachangia kiasi kikubwa cha maji katika Bonde la Mto Nile na linahusisha nchi **nne** za Burundi inayomiliki **asilimia 22**, Rwanda **(asilimia 33)** Tanzania **(asilimia 35)** na Uganda inamiliki **asilimia 10**. Utekelezaji wa miradi na shughuli mbalimbali katika Bonde hilo unasimamiwa na chombo cha Programu ya nchi za Maziwa Makuu katika Bonde la Mto Nile *(Nile Equatorial Lakes Subsidiary Action Program- NELSAP)*. Hadi mwezi Machi 2017, tathmini ya athari za kimazingira na kijamii kwa ajili ya miradi inayotekelezwa katika Bonde la Mto Ngono na Bonde la Mto Mara inaendelea. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na *NELSAP* inaendelea na taratibu za kupata

Mkandarasi wa ujenzi wa Bwawa la Borenga na miundombinu ya umwagiliaji katika Bonde la Mto Mara; pamoja na kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji katika maeneo yaliyopo kando ya Bonde la Mto Ngono. Mradi wa umwagiliaji katika Bonde la Mto Ngono utatekelezwa katika vijiji **24** vya Wilaya za Bukoba na Missenyi na inakadiriwa jumla ya **hekta 11,000** zitatumika katika kilimo cha umwagiliaji. Vilevile, bwawa hilo litatoa huduma ya maji kwa matumizi ya majumbani, mifugo pamoja na kuzalisha umeme wa **Megawati 1.5**. Katika mwaka 2017/2018, Serikali kwa kushirikiana na *NELSAP* itaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa mradi huo.

**52.** **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Bonde dogo la Mto Mara, miradi inayotekelezwa husimamiwa na Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria *(Lake Victoria Basin Commission-LVBC).* Bonde hilo linahusisha nchi mbili za Kenya inayomiliki **asilimia 65** ya bonde pamoja na Tanzania inayomiliki **asilimia 35**. Katika mwaka 2016/2017, Serikali za nchi hizo mbili kupitia Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria ziliendelea kuimarisha ushirikiano uliopo kwa kulinda, kusimamia na kuendeleza rasilimali asili za Bonde hilo. Vilevile, maadhimisho ya tano ya *'Siku ya Mara'* yalifanyika tarehe 15 Septemba, 2016 nchini Kenya katika *County* ya Bomet, yalihusu maonesho ya shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na jamii inayoishi kando ya Bonde dogo la Mto Mara ili kubadilishana uzoefu katika masuala ya rasilimali za maji.

### (d) Mamlaka ya Ziwa Tanganyika

**53.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea na usimamizi wa pamoja wa rasilimali za maji ya Ziwa Tanganyika kwa kushirikiana na Serikali za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (*DRC*) na Zambia. Nchi ya *DRC* inamiliki **asilimia 45**, Tanzania **(asilimia 41)**, Burundi **(asilimia 8)** na Zambia inamiliki **asilimia 6** ya rasilimali hiyo. Kwa kipindi kirefu kumekuwa na changamoto ya kushuka kwa kina cha maji ya Ziwa Tanganyika kutokana na kubomoka kwa banio la maji kwenye Mto Lukuga, hivyo kuathiri miundombinu ya

bandari katika nchi hizo pamoja na chanzo cha maji kilichopo Mji wa Kigoma/Ujiji. Katika mwaka 2016/2017, timu ya wataalam kutoka Benki ya Dunia na kamati za kiufundi kutoka Tanzania na *DRC* zilifanya ziara katika eneo la ujenzi wa Banio la Mto Lukuga na kukusanya taarifa kwa ajili ya kuona uwezekano wa Benki ya Dunia kufadhili ujenzi wa banio hilo. Serikali za Tanzania na *DRC* zinaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa banio la Mto Lukuga.

**(e) Bonde la Mto Zambezi**

**54. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine inaendelea na utekelezaji wa Mkataba wa Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi *(Zambezi Watercourse Commission - ZAMCOM*) ulioanza kutekelezwa rasmi kisheria mwaka 2011 kwa kushirikisha nchi saba zilizo katika Bonde hilo. Nchi hizo ni Angola, Botswana, Msumbiji, Namibia, Zambia, Zimbabwe na Tanzania. Majukumu ya Sekretarieti ya *ZAMCOM* ni kuandaa mikakati ya utekelezaji wa mipango ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji za Bonde la Mto Zambezi kwa kuzingatia maamuzi ya vikao vya Baraza la Mawaziri wa Maji wa *SADC* na lile la nchi wanachama wa *ZAMCOM*. Katika mwaka 2016/2017, Sekretariati ya *ZAMCOM* imesimamia zoezi la uundwaji wa kamati mbalimbali za kitaifa na kikanda kwa ajili ya kurahisisha majadiliano ya hoja mbalimbali za uhifadhi wa Bonde hilo. Hadi mwezi Machi 2017, Kamati ya Kitaifa ya Wadau *(ZAMCOM National Stakeholders Committee)* imeundwa, ambapo vikao **vinne (4)** vya kamati vimefanyika na kujadili namna ya kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za Bonde. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na kutathmini hali ya mazingira ya Bonde la Mto Zambezi *(Zambezi Environmental Outlook)*; kuandaa mwongozo wa kubadilishana takwimu *(Guidelines for Data Sharing)*; na kuandaa mfumo wa kubadilishana, kutumia na kuhifadhi takwimu za rasilimali za maji (*Zambezi Water Resources Information system)*.

**55. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2017/2018, Serikali kwa kushirikiana na Serikali za nchi zilizo chini ya Mkataba wa *ZAMCOM* itaendelea na utekelezaji wa shughuli

zilizopangwa kufanyika kulingana na mkataba huo; kuandaa Mpango Mkakati wa *ZAMCOM*; pamoja na kutoa mafunzo kwa nchi wanachama kuhusu namna ya kutumia mifumo iliyoandaliwa.

**(f) Baraza la Mawaziri wa Maji wa Afrika (*AMCOW*)**

**56.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Sekretarieti ya *AMCOW* iliandaa Maadhimisho ya 6 ya Wiki ya Maji ya Afrika na Mkutano Mkuu wa 10 wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Afrika, kuanzia tarehe 18 - 22, Julai 2016 Jijini Dar es Salaam. Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ilikuwa ni '**Kufikia Lengo la Sita la Maendeleo Endelevu (*SDGs Goal 6*) kuhusu Usalama wa Maji na Usafi wa Mazingira**'. Washiriki wa maadhimisho hayo walitoka katika Serikali za mataifa mbalimbali, Taasisi za Kikanda, Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na vyombo vya habari vya kitaifa na kimataifa. Mgeni Rasmi kwenye maadhimisho hayo alikuwa ni **Makamu** wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan.

**57.** **Mheshimiwa Spika**, Mkutano wa Mawaziri uliofanyika tarehe 22 Julai 2016, ulipitisha "**Azimio la Dar es Salaam**" lililotoa mwelekeo wa utekelezaji wa majukumu mbalimbali kwa nchi za Afrika kuhusu Usalama wa Maji na Usafi wa Mazingira (*Roadmap for Achieving the N'gor Commitments on Water Security and Sanitation in Africa*). Mwelekeo huo ulipendekeza maeneo **12** ya utekelezaji kulingana na Agenda 2030 ya Lengo la Sita la Maendeleo Endelevu. Katika Mkutano huo, nikiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nilikabidhiwa **Urais wa Baraza la Mawaziri wa Maji wa Afrika** kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia Julai, 2016 hadi Juni, 2018 na Rais aliyemaliza muda wake ambaye ni Waziri wa Maji wa Senegal. Vilevile, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, **Mheshimiwa Daktari John Pombe Joseph Magufuli** amekuwa ndiye Msemaji Mkuu (*Champion*) wa masuala yanayohusu maji Barani Afrika. Katika mwaka 2017/2018, Sekretarieti ya *AMCOW* kwa kushirikiana na nchi wanachama wataandaa Mpango

Mkakati wa miaka 10 wa *AMCOW* na Mpango Mkakati wa Mawasiliano na Uhamasishaji.

## 4.2 HUDUMA ZA UBORA NA USAFI WA MAJI

**58.** **Mheshimiwa Spika**, mojawapo ya majukumu ya Wizara yangu ni kuhakiki ubora na usalama wa maji katika vyanzo vya maji kwa lengo la kulinda afya za wananchi na mazingira. Uchunguzi wa ubora wa maji katika vyanzo na mitandao ya usambazaji wa maji hutekelezwa na Maabara za Maji nchini na kutoa ushauri wa kitaalam kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira, Vyombo vya Watumiaji Maji, Bodi za Maji za Mabonde, Taasisi pamoja na watu binafsi kuhusu umuhimu wa kuzingatia viwango vinavyokubalika kwa matumizi yaliyokusudiwa. Takwimu na taarifa zinazopatikana hutumika katika maamuzi mbalimbali ikiwemo tafiti na utekelezaji wa mikakati ya kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji. Katika mwaka 2016/2017, Wizara ilipanga kukagua vyanzo vya maji kwa kuchunguza sampuli **10,000** za maji ili kuhakiki ubora wake. Vilevile, sampuli **1,500** za majitaka zilipangwa kukusanywa na kuchunguzwa ubora wake kwa lengo la kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji na mfumo wa ikolojia.

**59.** **Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Machi 2017, jumla ya sampuli **4,288** za maji zilikusanywa na kuhakikiwa ubora wake. Kati ya hizo, sampuli kwa ajili ya matumizi ya maji majumbani ni **3,554**, viwandani **(221)**, kuratibu mwenendo wa ubora wa maji katika vyanzo **(133)**, shughuli za utafiti **(355)** na ujenzi sampuli **25**. Kwa upande wa majitaka jumla ya sampuli **264** zilikusanywa na kufanyiwa uchunguzi. Matokeo ya uchunguzi wa sampuli hizo na hali ya ubora wa maji kwa matumizi mbalimbali ni kama ifuatavyo:-

### 4.2.1 Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Majumbani

**60.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakiki ubora wa maji kwa matumizi ya majumbani jumla ya sampuli **3,554** zilikusanywa na kufanyiwa uchunguzi kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya maji vijijini na mijini. Matokeo yalionesha

kuwa sampuli **2,878** sawa na **asilimia 81** zilikidhi viwango vinavyokubalika na sampuli **676** sawa na **asilimia 19** hazikukidhi viwango vinavyokubalika. Hali hii imetokana na uwepo wa vimelea vya vijidudu (*bacteria*), kiasi kikubwa cha chumvichumvi pamoja na madini mbalimbali. Madini hayo ni *Chloride* katika maeneo ya Kasulu; *Fluoride* (Maji ya Chai na Bomang'ombe); *Nitrate* (Bahi na Kiteto) pamoja na madini ya Chuma na *Manganese* katika maeneo ya Mtwara, Masasi, Newala na Nanyamba. Ushauri stahiki ulitolewa kwa wahusika katika maeneo hayo. Kwa upande wa Halmashauri za Wilaya hali ya ubora wa maji si ya kuridhisha kutokana na miradi mingi iliyokamilika kutokuwa na miundombinu ya kutibu maji. Wizara imezielekeza Halmashauri husika kutumia teknolojia rahisi za kutibu maji, kutoa mafunzo kwa wataalam, kufuatilia na kutathmini matumizi ya dawa za kutibu maji pamoja na kuwaelimisha wananchi kuhusu matumizi ya majisafi na salama ili kupunguza changamoto hiyo.

### 4.2.2 Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Viwanda naUjenzi

61. **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha maji yanayotumika viwandani na kwenye shughuli za ujenzi yanakidhi viwango vya ubora, Wizara imeendelea kuhakiki ubora wa maji kwa matumizi hayo. Katika mwaka 2016/2017, jumla ya sampuli **221** za maji zilikusanywa na kuhakikiwa ubora wake kutoka kwenye viwanda vya kusindika vyakula vya *Kagera Sugar, Kagera Fish, Vic Fish, Tanica, KBG Soft Drink, Musoma Fish, Tanzania Fish, Omega Fish Processors, Bahari Food Ltd, Nileperch* na *Tanperch*. Sampuli **saba (7)** ambazo ni sawa na **asilimia 3.2** maji yake hayakukidhi viwango vya ubora kutokana na uwepo wa vimelea vya vijidudu (*bacteria*). Vilevile, jumla ya sampuli **25** za maji kwa ajili ya ujenzi zilikusanywa katika mikoa ya Morogoro, Kigoma, Mwanza, Arusha na Rukwa na kuhakikiwa ubora wake. Matokeo ya uchunguzi yalionesha sampuli **moja (1)** haikukidhi viwango vya ubora kwa matumizi ya ujenzi kutokana na kiwango kikubwa cha chumvichumvi. Katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea kufuatilia ubora wa maji yanayotumika kwenye viwanda ili kuhakikisha yanakidhi viwango kwa lengo la kulinda afya za wananchi.

### 4.2.3 Ushiriki wa Wizara katika Ufuatiliaji na Udhibiti wa Ugonjwa wa Kipindupindu Nchini

**62.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Mamlaka za Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa; na wadau wengine katika kukabiliana na ugonjwa wa kipindupindu kwa kufuatilia ubora wa maji katika maeneo mbalimbali yakiwemo yaliyoathirika na ugonjwa wa kipindupindu. Katika mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Maabara za Ubora wa Maji nchini ilikagua uwekaji wa madawa ya kutibu maji katika Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira za Mikoa ya Dodoma, Mbeya, Mara, Kagera, Arusha, Shinyanga, Simiyu, Mtwara, Lindi, Morogoro, Tanga na Iringa. Matokeo yalionesha kuwa maji yaliyotibiwa yalikuwa na kiwango cha *chlorine* kinachokubalika kwa matumizi ya majumbani. Wizara imezielekeza Mamlaka hizo kuzingatia matumizi sahihi ya madawa pamoja na kiwango sahihi cha *chlorine* kwenye mtandao wa kusambaza majisafi ili kudhibiti magonjwa yatokanayo na matumizi ya maji yasiyo safi na salama. Vilevile, katika jitihada za Serikali za kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama, Wizara imeandaa mafunzo kuhusu matumizi sahihi ya madawa ya kutibu maji kwa Mamlaka za Maji na Halmashauri za Wilaya nchini.

### 4.2.4 Utekelezaji wa Mipango ya Usalama wa Maji

**63.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Wizara imeandaa Mipango ya Usalama wa Maji (*Water Safety Plans*) kwa Mamlaka ya Maji Kigoma na Chombo cha Watumiaji Maji – Mbande (Mbande *COWSO* - Dodoma). Taasisi hizo zitatumika kama maeneo ya majaribio (*pilot sites*) na utekelezaji wa mipango hiyo kwenye maeneo hayo utaanza mwaka 2017/2018. Kukamilika kwa majaribio hayo kutaiwezesha Wizara kufahamu njia bora ya kutekeleza mipango ya usalama wa maji katika maeneo mengine ya nchi. Lengo la mipango hiyo ni kuboresha huduma za upatikanaji wa maji safi na salama kwa Mamlaka za Maji na Vyombo vya Watumiaji Maji Vijijini (*COWSOs*) kuanzia kwenye chanzo cha maji hadi kwa mtumiaji.

### 4.2.5 Ubora wa Majitaka Yanayorudishwa kwenye Mazingira

64. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia maabara za maji nchini, imekuwa ikifuatilia kwa karibu ubora wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira vikiwemo vyanzo vya maji pamoja na kubaini ufanisi wa miundombinu ya kutibu majitaka katika taasisi mbalimbali. Hadi mwezi Machi 2017, jumla ya sampuli za majitaka **264** zilikusanywa na kuhakikiwa ubora wake. Kati ya hizo, sampuli **150** ni kwa ajili ya majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira na sampuli **114** ni kwa ajili ya kubaini ufanisi wa miundombinu ya kutibu majitaka. Kwa upande wa majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira, sampuli **92** sawa na **asilimia 61** hazikukidhi viwango vya ubora unaokubalika. Matokeo hayo yanaashiria kuwepo kwa mahitaji ya kuongeza jitihada katika ufuatiliaji wa viwango vya ubora wa majitaka yanayotiririshwa kwenye mazingira hususan vyanzo vya maji. Kwa kuzingatia hilo, Wizara imetoa ushauri wa kitaalam katika miji, viwanda na taasisi mbalimbali ili kuongeza ufanisi wa mabwawa na mitambo ya kusafisha majitaka kwenye maeneo yao. Katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kufuatilia ubora wa majitaka katika miji, viwanda na taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam kwa lengo la kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

### 4.2.6 Ubora wa Madawa ya Kusafisha na Kutibu Maji

65. **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Maabara za Maji nchini imeendelea kuchunguza ubora wa madawa ya kusafisha na kutibu maji yanayotumiwa kwenye Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa lengo la kuhakiki ubora wake. Katika mwaka 2016/2017, jumla ya sampuli **16** za madawa ya kusafisha na kutibu maji kutoka Mamlaka hizo zilihakikiwa. Sampuli hizo ni dawa aina ya *Calcium Hypochlorite* sampuli **6**, *Aluminium Sulphate* **(5)**, *Polyaluminium Chlorite* **(3)**, *Polymerbinder* **(1)** na *Pollyacryl Amide* sampuli **(1)** ambazo hutumika kusafisha maji na kuua vijidudu. Matokeo ya uchunguzi huo yalionesha kuwa sampuli zote za dawa zilikidhi viwango vinavyokubalika kwa ajili ya

kusafisha na kutibu maji kwa matumizi ya majumbani. Katika mwaka 2017/2018, Wizara imepanga kuendelea kufuatilia na kuhakiki ubora wa madawa ya kutibu maji katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira pamoja na Taasisi zinazohusika na usambazaji wa madawa hayo.

#### 4.2.7 Uondoaji wa Madini ya *Fluoride* katika Maji ya Kunywa na Kupikia

**66. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya kuondoa madini ya *fluoride* kwenye maji ya kunywa na kupikia kwa kutumia mkaa wa mifupa ya ng'ombe (*bone char*) katika ukanda ulioathirika na madini hayo. Katika mwaka 2016/2017, Wizara imesambaza jumla ya mitambo **473** ya kuondoa madini ya *fluoride* kwenye ngazi ya kaya katika kata **12**. Kata hizo ni Bwawani, Engikareet, KIA, Kisongo, Maji ya Chai, Kati, Olmotonyi, Oldonyowas, Oldonyosambu, Olrtormet, Shambarai na Uwiro ambapo jumla ya wananchi **3,784** wamepata maji safi na salama kupitia teknolojia hiyo. ***Jedwali Na. 3*** linaonesha mchanganuo wa mgawanyo wa mitambo na wananchi walionufaika. Katika mwaka 2017/2018, Wizara imepanga kusambaza mitambo **2,000** ya mkaa wa mifupa ya ng'ombe katika maeneo yenye kiwango kikubwa cha *fluoride*.

**67. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kukusanya takwimu kwenye vyanzo vya maji juu na chini ya ardhi katika maeneo yaliyopo kwenye ukanda wenye madini ya *flouride*. Hadi mwezi Machi 2017, jumla ya vyanzo **355** vya maji kutoka maeneo ya Ikungi, Itigi, Kishapu, Ushetu, Buchosa, Msalala na Iramba vilikaguliwa kwa kufanyiwa uchunguzi wa madini ya *fluoride*. Matokeo yalionesha kuwa vyanzo **32** kati ya hivyo ambavyo ni sawa na **asilimia 9** vina kiwango kikubwa cha madini ya *fluoride* ikilinganishwa na viwango vinavyokubalika kwa matumizi ya majumbani. Vilevile, Wizara inaendelea na taratibu za kumpata Mtaalamu Mshauri atakayeandaa kanzi data ya maeneo yaliyoathirika na madini ya *fluoride*. Mfumo huo wa takwimu utasaidia upatikanaji kwa wakati wa taarifa sahihi zinazohusu maeneo yaliyoathirika na madini hayo katika kutekeleza miradi ya maji.

### 4.2.8 Maabara za Maji kupata Ithibati (*Accreditation*)

**68.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara imepanga kuongeza idadi ya maabara za maji zenye ithibati (*accreditation*) kutoka maabara **moja (1)** hadi **tano (5)** ifikapo mwaka 2019. Katika kutekeleza mpango huo, Maabara za Maji za Dar es Salaam na Iringa zimeendelea na taratibu za kupata ithibati katika vipimo vya kemikali (*Chemical analysis to ISO/IEC 17025: 2005*). Hadi mwezi Machi 2017, rasimu za Mwongozo wa Usimamizi wa Ubora (*Quality Management Manuals)* kwa ajili ya Maabara hizo pamoja na mpango kazi zimeandaliwa. Mpango huo umebainisha mambo muhimu ya kutekeleza ikiwa ni pamoja na upungufu uliopo, kurekebisha upungufu uliopo (*implementation of corrective action*), kufuatilia na kukagua utendaji kazi wa maabara pamoja na kukamilisha matakwa ya tathmini itakayofanywa na *Southern African Development Community Accreditation Service* (*SADCAS*).

**69.** **Mheshimiwa Spika**, vilevile, maabara zote za Ubora wa Maji nchini zimeshiriki katika zoezi la kupima uwezo na ufanisi wa maabara hizo (*Proficiency Testing*) linaloratibiwa na *Shirika la Maji la Namibia (NAM WATER PT Provider-Namibia Water Corporation)* chini ya mpango wa *Southern Africa Development Community Measurement Traceability (SADCMET***)**. Katika zoezi hilo, Maabara zote zilishiriki kufanya uchunguzi wa vimelea vya vijidudu (*bacteria*) na kati ya hizo maabara **11** zilifanya pia uchunguzi wa viashiria vya kifizikia na kikemia. Matokeo yameonesha kuwa maabara zimeendelea kufanya vizuri katika upimaji wa viashiria mbalimbali vya kemikali na vijidudu kwenye maji. ***Jedwali Na. 4*** linaonesha Maabara zilizoshiriki katika zoezi la kujipima uwezo wa kufanya uchunguzi wa vijidudu kwenye maji. Katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kushiriki katika zoezi la kupima uwezo wa ufanisi wa maabara ambapo maabara zote **16** zitashiriki katika vipimo vya bakteriolojia, fizikia na kemikali.

### 4.2.9 Ujenzi na Ukarabati wa Maabara za Maji

**70.** **Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuboresha mazingira ya kazi, Wizara inaendelea na kazi ya ujenzi na ukarabati wa maabara za maji ili ziweze kukidhi mahitaji ya mwongozo wa viwango vya kimataifa vya *ISO 17025:2005*. Katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea na kazi ya upanuzi (*extension*) na ukarabati wa jengo la Maabara Kuu ya Dar es Salaam na Maabara za Musoma na Songea ambapo utekelezaji umefikia wastani wa **asilimia 85** kwa Dar es Salaam, **asilimia 98** kwa Musoma na Songea **asilimia 40**. Aidha, ujenzi wa jengo la maabara ya Kigoma umekamilika na ujenzi wa majengo ya maabara nyingine unaendelea ambapo Singida umefikia **asilimia 80**, Bukoba **(65)**, Mwanza **(50)**, Sumbawanga **(50)**, Mbeya **(50)** na Mtwara **asilimia 50**.

**71.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendela kuzijengea uwezo maabara za maji kote nchini kwa kukarabati na kujenga majengo pamoja na kuzipatia vifaa vya kisasa ili kukidhi mahitaji ya mwongozo wa *ISO 17025* na kulinda afya za watumishi. Vilevile, Wizara itaendelea kutekeleza mkakati wa usimamizi wa ubora wa maji ambapo itachunguza sampuli **10,000** za maji kutoka vyanzo mbalimbali na sampuli **1,500** za majitaka kutoka katika migodi, viwanda na taasisi mbalimbali ili kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji nchini.

## 6.0 4.3 HUDUMA YA MAJI VIJIJINI

**72.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali inatekeleza miradi ya maji vijijini kupitia Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Katika utekelezaji wa Awamu ya Kwanza ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, jumla ya miradi **1,333** imekamilika na miradi **477** inaendelea kujengwa na ipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Utekelezaji wa miradi hiyo unatumia vyanzo vya visima vifupi, visima virefu, mabwawa na maji mtiririko kwenye maeneo mbalimbali nchini.

**73.** **Mheshimiwa Spika**, katika Awamu ya Pili ya

Programu ambayo imeanza kutekelezwa mwezi Julai 2016, Serikali imepanga kujenga, kukarabati na kufanya upanuzi wa miradi ya maji katika vijiji **4,105** na itakapokamilika itawanufaisha wananchi **19,080,000**. Katika awamu hiyo, Serikali imeweka kipaumbele katika kukamilisha miradi inayoendelea ambayo ujenzi wake haukukamilika kwenye Awamu ya Kwanza; maeneo ambayo miradi haikutekelezwa kutokana na kukosa vyanzo vya maji vya uhakika; na maeneo kame na yenye shida kubwa ya maji.

**74.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, jumla ya **Shilingi bilioni 421.56** zilikasimiwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji vijijini, kati ya fedha hizo **Shilingi bilioni 373.34** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 48.22** ni fedha za nje. Hadi mwezi Machi 2017, jumla ya **Shilingi bilioni 80.41** zilitolewa sawa na **asilimia 19.07** ili kutekeleza miradi ya maji vijijini. Kupatikana kwa fedha hizo kumewezesha kukamilika kwa miradi **123** na kuongeza idadi ya wananchi wanaopata huduma ya maji kutoka **21,900,000** mwezi Juni, 2016 hadi kufikia wananchi **22,951,371** mwezi Machi, 2017. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali yameainishwa katika aya zifuatazo:-

### 7.0 4.3.1 Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijijini

**75.** **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa miradi ya maji vijijini unahusisha ujenzi wa miradi ya kimkakati, miradi yenye kuleta matokeo ya haraka na ujenzi wa mabwawa. Hatua zilizofikiwa ni kama ifuatavyo:-

#### (a) Miradi ya Kimkakati

#### (i) Mradi wa Maji Tabora

**76.** **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa mradi wa maji Tabora, umetekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa maji katika vijiji **31** kwenye Wilaya zote saba za Mkoa wa Tabora. Mradi huo umehusisha ujenzi wa visima **111** vya pampu za mkono na miradi **4** ya maji ya bomba yenye vituo **60** vya kuchotea maji.

Mradi umekamilika na kuzinduliwa rasmi na **Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** tarehe 29 Aprili, 2017 na unahudumia wananchi **40,352** katika vijiji hivyo.

**(ii) Mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe**

**77.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na ***BADEA***, ***OFID*** na ***Kuwait Fund*** inaendelea kutekeleza mradi wa Same-Mwanga-Korogwe ambao umelenga kusambaza maji katika Miji ya Same na Mwanga pamoja na vijiji **38** vilivyo kando ya bomba kuu katika Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe. Mradi huo umegawanyika katika awamu mbili na ujenzi umeanza kwa awamu ya kwanza ambayo inatekelezwa katika vipande vinne vitakavyohusisha ujenzi wa chanzo, mitambo ya kusafisha maji na miundombinu ya kupeleka na kusambaza maji katika Miji ya Mwanga na Same.

**78.** **Mheshimiwa Spika**, kipande cha kwanza kinahusu ujenzi wa chanzo cha maji, mtambo wa kusafisha maji na ulazaji wa bomba kuu la urefu wa **kilomita 12.8**. Gharama za ujenzi ni **Dola za Marekeni milioni 41,36** na gharama za usimamizi ni **Dola za Marekeni milioni 0.51** na **Shilingi milioni 381.72**. Hadi mwezi Machi 2017, ujenzi wa chanzo, mtambo wa kusafisha maji na tanki kubwa la kuhifadhi maji kwa ajili ya usambazaji umefikia **asilimia 15.8** na unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2017/2018.

**79.** **Mheshimiwa Spika**, kipande cha pili kinahusu ujenzi wa miundombinu katika vijiji **tisa (9)** vinavyozunguka mradi na kipande cha tatu kinahusu ujenzi wa mtambo wa kusukuma maji kutoka kwenye tanki la Kisangara hadi Kiverenge, miundombinu ya matanki ya kuhifadhi maji na mabomba ya kusambaza maji katika Mji wa Mwanga. Utekelezaji wa kipande cha pili na cha tatu bado haujaanza kutokana na ukosefu wa fedha pamoja na kutokamilika kwa taratibu za manunuzi.

**80.** **Mheshimiwa Spika**, kipande cha nne kinahusu ujenzi wa miundombinu ya maji kwa ajili ya usambazaji wa maji

katika Mji wa Same ikiwemo tanki la **mita za ujazo 7,500** katika Mlima Kiverenge, ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji katika Mji wa Same. Ujenzi utagharimu **Dola za Marekani milioni 35.25** na **Shilingi bilioni 1.67**. Mkandarasi ameanza maandalizi ya ujenzi na kazi hizo zinatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2018.

**81.** **Mheshimiwa Spika**, awamu ya pili ya mradi huo itahusu kupeleka maji kwenye vijiji **29** vilivyopo kando ya bomba kuu kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 97.61**. Utekelezaji haujaanza kutokana na ukosefu wa fedha. Vijiji hivyo ni pamoja na Hedaru, Mabilioni, Gavao, Makanya, Mgwasi, Bangalala, Chajo, Mwembe, Njoro, Ishinde, Ruvu Mferejini, Ruvu Jiungeni, Majengo, Bendera, Mkonga, Ijinyu na Mgandu vilivyopo katika Wilaya ya Same; Vijiji vya Kifaru, Kiruru, Ibwejewa, Kisangara, Lembeni, Kiverenge, Kiti cha Mungu, Mbambua, Kileo, Kivulini, Kituri, Mgagao, Handeni, Lang'ata Bora, Lang'ata Kagongo, Nyabinda, Kirya na Njia Panda vilivyo katika Wilaya ya Mwanga; na Vijiji vya Bwiko, Mkomazi, Nanyogie, Manga - Mtindilio na Manga Mikocheni vilivyopo katika Wilaya ya Korogwe. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za utekelezaji wa mradi huo kutoka katika vyanzo vyake vya ndani pamoja na Wadau mbalimbali wa Maendeleo.

**82.** **Mheshimiwa Spika**, mradi wa maji Same- Mwanga-Korogwe utakapokamilika utakuwa na uwezo wa kuhudumia wananchi wapatao **456,931** kutoka katika Wilaya za Same wananchi **264,793**, Mwanga **(177,085)** na wananchi **15,053** katika Wilaya ya Korogwe.

**(iii) Mradi wa Maji wa Masoko – Wilayani Rungwe**

**83.** **Mheshimiwa Spika**, mradi wa maji wa Masoko Wilayani Rungwe unaotarajiwa kuhudumia jumla ya vijiji **15** ni miongoni mwa miradi inayojengwa chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa fedha za ndani. Awamu ya kwanza ya mradi huo inaendelea kutekelezwa ambapo ujenzi wa tanki la kuhifadhia maji lenye **mita za ujazo 90** katika Kijiji cha Ikama umekamilika. Kazi zinazoendelea ni pamoja

na ujenzi wa chanzo cha Mbaka, ujenzi wa tanki lenye **mita za ujazo 370** katika Kijiji cha Lufumbi, kulaza mabomba yenye urefu wa **kilomita 12.6** na kujenga vituo **vitano (5)** vya kuchotea maji. Hadi mwezi Machi 2017, ujenzi wa mradi kwa ujumla umefikia **asilimia 50**.

**84.** **Mheshimiwa Spika**, awamu ya pili ya mradi inatarajiwa kuanza katika mwaka 2017/2018 na utagharimu jumla ya **Shilingi bilioni 5.3**. Mradi utahusisha ulazaji wa bomba lenye urefu wa **kilomita 92.1** na ujenzi wa vituo **135** vya kuchotea maji na utakapokamilika utawanufaisha wananchi wapatao **19,624** katika vijiji vya Bulongwe, Ngaseke, Igembe, Ntandabala, Lupando, Bujesi, Lufumbi, Nsyasa, Ikama, Itagata, Busisya, Mbaka, Isabula, Lwifa na Nsanga.

**(iv) Mradi wa Maji Mkoani Kigoma**

**85.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na **Serikali ya Ubelgiji** itatekeleza mradi wa maji utakaohusisha Halmashauri zote za Mkoa wa Kigoma. Mradi huo utatekelezwa katika vijiji **26** vya kipaumbele kwa kipindi cha miaka mitano na utawanufaisha wananchi wapatao **200,000** wa Mkoa huo. Mradi utagharimu jumla ya **Euro milioni 8.8** na kati ya fedha hizo, Serikali ya Ubelgiji itatoa **Euro milioni 8** na kiasi cha **Euro milioni 0.8** kitatolewa na Serikali ya Tanzania. Hadi mwezi Machi 2017, Serikali ipo kwenye hatua za mwisho za kusaini Mkataba wa Makubaliano ili ujenzi wa mradi uweze kuanza.

**(b) Miradi yenye Kuleta Matokeo ya Haraka (*quickwins*)**

**(i) Mradi wa Maji kwa Vijiji 100 Vinavyopitiwa na Bomba Kuu kutoka Ziwa Victoria hadi Kahama-Shinyanga**

**86.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kutekeleza ujenzi wa miradi ya maji katika vijiji vilivyopo pembezoni mwa bomba kuu la maji kutoka Ziwa Victoria hadi Miji ya Kahama na Shinyanga. Ujenzi wa miradi ya maji katika vijiji **40** umeanza

ambapo upimaji na usanifu katika vijiji **32** umekamilika. Kati ya hivyo, ujenzi wa miradi ya maji umekamilika katika vijiji **14** vya Nyang'homango, Runele, Gatuli, Nyashimbi, Magobeko, Kakulu, Butegwa, Ng'homango, Jimondoli, Kadoto, Lyabusalu, Mwajiji, Ichongo na Bukamba na wananchi wanapata huduma ya maji. Vilevile, ujenzi unaendelea katika vijiji vya Mwakatola na Mwasekagi katika Halmashauri ya Shinyanga ambapo ujenzi umefikia asilimia 65.

**(ii) Mradi wa Maji wa Ntomoko**

**87. Mheshimiwa Spika**, hali ya huduma ya maji kutoka chanzo cha Ntomoko imeshindwa kukidhi mahitaji kutokana na ongezeko kubwa la watu kutoka **23,400** mwaka 1973 waliolengwa kwenye mradi huo hadi kufikia watu **55,397** kwa sasa. Mradi ulilenga kutoa huduma katika vijiji **18** vya Wilaya za Kondoa na Chemba. Kutokana na mradi huo kutototosheleza mahitaji, iliazimiwa kuwa vijiji **10** kati ya hivyo vipate maji kutoka mradi wa maji wa Ntomoko. Vijiji hivyo ni Makirinya, Lusangi, Kinkima, Kirere cha Ngómbe, Churuku, Hamai, Songolo, Jangalo, Jinjo na Madaha.

**88. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Machi 2017, utekelezaji wa mradi katika vijiji hivyo 10 unaendelea ambapo kazi zilizokamilika ni ujenzi wa chanzo, chujio la maji, tanki lenye **mita za ujazo 100**, vituo vya kuchotea maji, nyumba ya mlinzi, uzio wa eneo la **mita za mraba 120**; ukarabati wa matanki yenye ukubwa wa ujazo mbalimbali katika vijiji husika; ulazaji wa bomba kuu urefu wa **kilomita 17** kati ya **kilomita 21**; pamoja na ujenzi wa malambo mapya ya kunyweshea mifugo katika vijiji hivyo. Vilevile, mabomba ya kusambaza maji yamelazwa katika vijiji vya Makirinya, Hamai, Songolo, Kinkima, Churuku na Lusangi. Kutokana na kukamilika kwa kazi hizo, vijiji **viwili (2)** vya Makirinya na Lusangi vimeanza kupata huduma ya maji. Kazi zinazoendelea ni kukamilisha ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji katika vijiji vya Kirere cha Ng'ombe, Kinkima, Churuku, Hamai, Songolo, Madaha, Jinjo na Jangalo na kuyaunganisha kwenye bomba kuu. Kazi hiyo imefikia **asilimia 90** na inatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2017

ambapo wananchi wapatao **34,000** wa vijiji hivyo watanufaika na huduma ya maji safi.

**89.** **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa vijiji **nane (8)** vilivyobaki ambavyo vilipendekezwa vipate maji kutoka vyanzo vingine, vijiji **vinne (4)** vya Mlongia, Njenjeluse, Goima na Mtakuja vinapata huduma ya maji kupitia visima vilivyochimbwa. Kwa vijiji vya Itolwa, Mapango, Chandama na Igunga, Serikali ipo katika hatua mbalimbali za kutekeleza miradi ili kuhakikisha kuwa wananchi wa vijiji hivyo wanapata huduma ya maji.

**(iii) Mradi wa Maji Chiwambo**

**90.** **heshimiwa Spika**, mradi huo unahusu ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya maji katika Kata za Lulindi, Lupumbulu, Namalenga, Chiungutwa, Sindano, Mchauru na Mbuyuni zilizopo Halmashauri ya Wilaya ya Masasi. Mradi ukikamilika, wananchi wapatao **84,082** wa kata hizo watanufaika na huduma ya maji safi na salama. Utekelezaji wa mradi kwa sasa upo katika hatua mbalimbali ambapo katika kipande cha Chiwambo Nagaga kazi zinazoendelea ni pamoja na ulazaji wa bomba la inchi 8 urefu wa **mita 500**, bomba la inchi 3 **(kilomita 3.3)**, bomba la inchi 6 **(kilomita 3.6)**, na bomba la inchi 4 lenye urefu wa **mita 400**. Utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 75**. Katika kipande cha Nagaga - Mpeta, kazi zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 21**, ulazaji wa bomba la kusambaza maji lenye urefu wa **kilomita 3**, ukarabati wa matanki matatu ya **lita 25,000** kila moja na ujenzi wa vituo **21** vya kuchotea maji. Utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 67**.

**91.** **Mheshimiwa Spika**, kazi zinazoendelea kutekelezwa za kujenga miundombinu ya maji kwenye Kata ya Chiungutwa ni pamoja na ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita 50,000**, ujenzi wa vituo **13** vya kuchotea maji, ulazaji wa bomba la kusambaza maji lenye urefu wa **kilomita 4.2** pamoja na ukarabati wa tanki lenye ujazo wa **lita 25,000**. Utekelezaji wa Mradi huo umefikia **asilimia 65**. Katika kipande cha

Nagaga - Mitesa kazi zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 8**, ulazaji wa bomba la kusambaza maji lenye urefu wa **kilomita 4.9**, ukarabati wa nyumba ya pampu, ukarabati wa *sump well*, ujenzi wa vituo **17** vya kuchotea maji, ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita 50,000**, ukarabati wa tanki la maji lenye ujazo wa **lita 150,000** na ujenzi wa ofisi ya Jumuiya ya Watumia Maji. Utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 75**.

**92.** **Mheshimiwa Spika**, kazi zinazoendelea kutekelezwa katika kipande cha Nagaga hadi Milewe ni ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 25** ambapo **kilomita 13.2** zimekamilika na ulazaji wa bomba la kusambaza maji lenye urefu wa **kilomita 5**. Ukarabati wa matanki mawili ya ujazo wa **lita 25,000** kila moja umekamilika. Utekelezaji wa kipande hicho umefikia **asilimia 60**. Aidha, ukarabati wa mradi katika Kijiji cha Mpeta unaendelea na umefikia **asilimia 90**.

### (c) Ukarabati na Ujenzi wa Mabwawa

**93.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Serikali imeendelea na ujenzi pamoja na ukarabati wa mabwawa katika maeneo mbalimbali nchini hususan kwenye maeneo kame kwa lengo la kuwapatia wananchi huduma ya maji kwa matumizi ya kijamii na kiuchumi. Hadi mwezi Machi, 2017 hatua za utekelezaji wa mabwawa hayo ni kama ifuatavyo:-

**(i)** **Mabwawa ya Habiya na Seke Ididi**: Ujenzi wa Bwawa la Habiya lililopo Wilayani Itilima Mkoa wa Simiyu na Seke Ididi lililopo katika Wilaya ya Kishapu Mkoani Shinyanga umekamilika. Ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji kutoka kwenye mabwawa hayo hadi maeneo ya wananchi umepangwa kutekelezwa katika mwaka 2017/2018;

**(ii)** **Bwawa la Kawa**: Ujenzi wa Bwawa la Kawa lililopo katika Halmashauri ya Nkasi mkoani Rukwa umekamilika. Halmashauri ya Wilaya hiyo inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya maji kupeleka katika vijiji vya Nkundi, Kalundi na Fyengereza;

(iii) **Bwawa la Matwiga**: Bwawa la Matwiga lipo Halmashauri ya Wilaya ya Chunya katika Mkoa wa Mbeya, ujenzi wa bwawa hilo umefikia **asilimia 94**. Mradi huo ulisimama kwa muda kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha kwenye maeneo hayo na ujenzi unatarajiwa kuendelea baada ya mvua hizo kukatika;

(iv) **Bwawa la Mwanjoro**: Taratibu za kupata Mkandarasi wa kukamilisha ujenzi wa bwawa la Mwanjoro lililopo Halmashauri ya Wilaya ya Meatu mkoani Simiyu zinaendelea. Rasimu ya Mkataba wa ujenzi imewaslishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkataba unatarajiwa kusainiwa ifikapo mwezi Juni, 2017;

(v) **Bwawa la Iguluba**: Wizara imefanya tathmini ya awali kuhusu uwezo wa Bwawa la Iguluba lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ili kubaini kama litaweza kukidhi mahitaji ya matumizi yaliyokusudiwa. Baada ya kufanya tathmini hiyo, imeonekana kuwa bwawa hilo halitakuwa endelevu hivyo, Wizara imepanga kufanya tathmini ya kina ili kupata chanzo mbadala kwa ajili ya kuhudumia vijiji vilivyokusudiwa. Taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kufanya tathmini hiyo ikiwa ni pamoja na upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi huo zinaendelea;

(vi) **Bwawa la Wegero**: Wizara imefanya tathmini ya kina kuhusu uwezo na uendelevu wa Bwawa la Wegero lililopo Wilaya ya Butiama na kuonekana kuwa bwawa hilo halitatosheleza mahitaji ya maji kwa maeneo yaliyolengwa na siyo endelevu. Katika mwaka 2017/2018, Serikali itaajiri Mtaalam Mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kupata chanzo cha maji mbadala kwa ajili ya kuhudumia maeneo yaliyokusudiwa;

(vii) **Bwawa la Kidete**: Serikali imesitisha Mkataba wa Mkandarasi wa ujenzi wa Bwawa la Kidete lililopo Wilaya ya Kilosa Mkoani Morogoro baada ya kushindwa kutekeleza Mkataba huo. Hadi mwezi Machi 2017, Wizara inaendelea kufanya mapitio ya upimaji na usanifu wa bwawa hilo na

kazi hiyo itakapokamilika, ujenzi wa bwawa hilo utaanza; na

**(viii) Bwawa la Dongo na Bwawa la Sukuro**: Bwawa la Dongo linatarajiwa kujengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto Mkoani Manyara na kuhudumia Wilaya tatu za Kiteto, Gairo na Kongwa. Upembuzi yakinifu wa awali umekamilika na katika mwaka 2017/2018, Wizara imepanga kufanya usanifu na kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mradi huo. Kwa upande wa Bwawa la Sukuro lililopo Wilayani Simanjiro katika Mkoa wa Manyara linatarajiwa kuanza kufanyiwa ukarabati katika mwaka 2017/2018 ambapo jumla ya **Shilingi milioni 100** zimetengwa.

**(d) Miradi ya Maji katika Maeneo ya Maziwa Makuu**

**94. Mheshimiwa Spika**, kwa sasa Wizara imetangaza kazi kwa ajili ya kuandaa miradi ya kimkakati ambayo itahudumia wananchi wengi zaidi katika maeneo ya maziwa makuu ikiwemo Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika. Zabuni kwa ajili ya kuwapata Wataalam Washauri imetangazwa.

**(e) Mradi wa Kutumia Teknolojia ya Nishati Jadidifu *(Renewable energy)***

**95. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na **Benki ya Dunia** kupitia ***Global Partnership on Output Based Aid (GPOBA)*** inakamilisha maandalizi ya mradi wa kutumia teknolojia ya nguvu za jua. Lengo la mradi huo ni kupunguza gharama za uendeshaji na matengenezo ya miradi ya maji vijijini. Awamu ya kwanza ya mradi itaanza kwa majaribio katika vijiji **280** kwenye Mikoa **12** ya Dodoma, Morogoro, Geita, Kagera, Mara, Shinyanga, Mtwara, Rukwa, Singida, Tabora, Arusha na Manyara kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 4.2**. Vilevile, Wizara inaendelea na majadiliano na Chuo Kikuu cha Ohio kilichopo Marekani ili kutekeleza sehemu ya mradi huo katika vijiji vingine **125** katika mikoa hiyo.

**(f) Mradi wa Pamoja na Mgodi wa Bulyanhulu**

**96. Mheshimiwa Spika**, mradi wa maji wa Bulyanhulu unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Mgodi wa Dhahabu wa Bulyanhulu (*ACACIA*); Halmashauri za Shinyanga na Msalala kwa Mkoa wa Shinyanga; na Halmashauri ya Nyang'hwale kwa Mkoa wa Geita. Mradi huo unahusu upanuzi wa miundombinu ya maji kutoka bomba kuu la maji la mradi wa maji *KASHWASA* ili kuvipatia huduma ya maji vijiji **13** vilivyopo katika Halmashauri za Wilaya za Shinyanga, Nyang'hwale na Msalala. Vijiji vitakavyonufaika na mradi huo ni pamoja na Mwenge, Nyugwa, Kharumwa, Mwamakiliga, Izunya, Kafita, Lushimba, Rwabakanga, Kakola Namba 9, Bushing'we, Kakola, Bugarama na Ilogi. Mkataba wa Makubaliano ya utekelezaji wa mradi huo umesainiwa na utekelezaji unatarajiwa kuanza mwezi Mei, 2017.

**(g) Mradi wa Kuimarisha Uendelevu wa Huduma ya Maji Vijijini kupitia Mfumo wa Malipo kwa Matokeo *(Payment by Results - PbR)***

**97. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na **Serikali ya Uingereza** kupitia *DFID* imeanza kutekeleza mradi unaolenga kuimarisha uendelevu wa huduma ya maji vijijini kwenye miradi inayojengwa na kusimamiwa na Halmashauri kupitia Mfumo wa Malipo kwa Matokeo. Mfumo huo unahusisha utoaji wa malipo kwa Halmashauri kulingana na ufanisi, usimamizi na uendeshaji wa vituo vya kuchotea maji vilivyopo kwenye miradi. Hadi mwezi Machi 2017, jumla ya Halmashauri **57** zilifanyiwa tathmini na kukidhi vigezo vya kupata fedha hizo ambapo kiasi cha **Paundi za Uingereza 637,900** zilitolewa kwa Halmashauri hizo. Aidha, Halmashauri **17** ziliwasilisha taarifa za miradi lakini hazikukidhi vigezo vyote vilivyohitajika. Hivyo, Halmashauri hizo zilipatiwa **Paundi za Uingereza 85,000** kwa ajili ya kujenga uwezo ili ziweze kukidhi vigezo vinavyohusika kwa mwaka ujao. Katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kutekeleza mradi huo ili kuhakikisha huduma ya maji vijijini inakuwa endelevu kwa maeneo yote nchini.

### (h) Uvunaji wa Maji ya Mvua

**98. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuhamasisha wananchi kutumia teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua kwa kujenga matanki ya mfano katika Taasisi za Umma. Vilevile, Serikali imetoa mwongozo kwa Halmashauri zote nchini kutunga Sheria ndogo zenye kuzitaka Taasisi za Kijamii, Asasi na Watu Binafsi kujenga miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua kwenye mapaa ya majengo yao. Aidha, Serikali imeendelea kutoa mafunzo kwa wananchi kuhusiana na uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia teknolojia rahisi kupitia mapaa ya majengo yao. Jumla ya wananchi **795** wamepata mafunzo kuhusu teknolojia rahisi ya uvunaji wa maji ya mvua. Vilevile, matanki **29,059** ya ukubwa tofauti yamejengwa katika Halmashauri mbalimbali nchini.

### 4.3.2 Uendeshaji na Matengenezo

**99. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha miradi ya maji vijijini inakuwa endelevu, Serikali imetoa mwongozo kwa Halmashauri kuhusu usajili wa Vyombo vya Watumiaji Maji (*COWSOs*) ambavyo vinapaswa kusimamia uendeshaji na matengenezo ya miradi ya maji vijijini. Hadi mwezi Machi 2017, jumla ya vyombo **1,799** vya watumiaji maji vimeundwa na kusajiliwa katika Halmashauri mbalimbali nchini. Vilevile, Serikali imeandaa kanuni na taratibu mbalimbali pamoja na Mkakati wa Uendelevu wa Miradi ya Maji Vijijini (*National Rural Water Supply Sustainability Strategy*) kwa ajili ya uendeshaji wa vyombo hivyo.

### 4.3.3 Mpango wa Utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijijini kwa Mwaka 2017/2018

**100. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kukamilisha ujenzi wa miradi inayoendelea, kujenga miradi mipya, kupanua miradi, kukarabati miundombinu ya maji iliyochakaa, kutekeleza miradi ya maji katika maeneo kame na yenye uhaba mkubwa wa maji pamoja na kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi hiyo. Vilevile, Wizara itaendelea kuhamasisha ujenzi wa

mitambo midogo ya kutibu maji kwa kutumia teknolojia rahisi pamoja na matumizi ya nishati mbadala ikiwemo nishati ya jua katika uendeshaji wa miradi ya maji vijijini. Jumla ya **Shilingi bilioni 341.83** zimepangwa kutumika kutekeleza miradi hiyo ambapo fedha za ndani ni **Shilingi bilioni 220** na **Shilingi bilioni 121.83** ni fedha za nje. Mchanganuo wa fedha za maendeleo zilizotengwa katika mwaka 2017/2018 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji vijijini umeoneshwa kwenye ***Jedwali Na. 5(a), 5(b)*** na ***5(c)***.

## 9.0 4.4 HUDUMA YA MAJI MIJINI

**101.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kutekeleza Programu Ndogo ya Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini inayohusisha ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka pamoja na kuzijengea uwezo Mamlaka za Maji za Dar es Salaam, Miji Mikuu ya Mikoa, Miji ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Maji ya Kitaifa. Lengo ni kuwapatia wakazi wa miji hiyo huduma ya majisafi na usafi wa mazingira iliyo bora na endelevu. Miradi iliyotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

## 10.0 4.4.1 Kuboresha Huduma za Maji Mijini

### (a) Miradi ya Maji katika Miji Saba

**102.** **Mheshimiwa Spika**, miradi ya maji katika miji saba ya Bukoba, Musoma, Lindi, Kigoma, Sumbawanga, Mtwara na Babati inaendelea kutekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na **Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AFD*)**, **Serikali ya Ujerumani** kupitia **Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (*KfW*)** na **Umoja wa Ulaya**. Miradi hiyo inahusisha uboreshaji wa miundombinu ya majisafi na usafi wa mazingira katika miji hiyo na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:-

### (i) Manispaa za Bukoba na Musoma

**103.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na **Shirika la Maendeleo la Ufaransa *(AFD)***, imekamilisha mradi

wa ujenzi wa miundombinu ya majisafi katika Manispaa ya Bukoba. Kukamilika kwa mradi huo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 8.82** hadi **lita milioni 18** kwa siku na kuwezesha huduma ya maji kupatikana kwa saa 24. Kwa sasa, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bukoba Mjini inaendelea na jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji katika maeneo ambayo hayana miundombinu hiyo pamoja na kufanya ukarabati wa mabomba yaliyochakaa.

**104.** **Mheshimiwa Spika**, mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika Manispaa ya Musoma unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AFD*) kwa gharama ya **Shilingi bilioni 45**. Mradi huo unalenga kuongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 10.14** za sasa hadi kufikia **lita milioni 34** kwa siku ambazo zitakidhi mahitaji ya maji kwa Manispaa ya Musoma hadi mwaka 2025. Hadi mwezi Machi 2017, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 90** na upo katika majaribio ya uzalishaji maji. Mradi huo unatarajiwa kukamilika katika mwaka 2017/2018 na kunufaisha wakazi wapatao **145,288** wa Manispaa ya Musoma.

**(ii) Manispaa za Lindi, Kigoma na Sumbawanga**

**105.** **Mheshimiwa Spika**, miradi ya majisafi na usafi wa mazingira katika Manispaa za Lindi, Kigoma na Sumbawanga inatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na **Serikali ya Ujerumani** na **Umoja wa Ulaya** kwa gharama ya **Euro milioni 62.59** ambapo **Euro milioni 19.58** ni kwa ajili ya ushauri wa kitaalam na **Euro milioni 43.01** ni kwa ajili ya ujenzi wa miradi. Utekelezaji wa miradi katika miji hiyo ni kama ifuatavyo:-

**106.** **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa mradi wa maji katika Manispaa ya Lindi unaendelea na utekelezaji wake umefikia **asilimia 85**. Hadi mwezi Machi 2017, kazi iliyokamilika ni uchimbaji wa visima virefu **10** na kazi zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa chujio lenye uwezo wa kusafisha maji **lita milioni 7.5** kwa siku; ujenzi wa matanki **mawili (2)** ya maji

ya ujazo wa **lita milioni 3** na **lita milioni 2**; ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 11.5**; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa **kilomita 27**; ujenzi wa **vituo 85** vya kuchotea maji; ujenzi wa mabwawa **mawili (2)** ya kutibu majitaka; na ununuzi wa gari la huduma ya uondoaji majitaka. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2017 kwa gharama ya **Euro milioni 11.7**. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 1.5** za sasa hadi **lita milioni 9** na kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Lindi. Jumla ya wakazi wapatao **81,343** wa Mji huo watanufaika na huduma hiyo.

**107.** **Mheshimiwa Spika**, mradi wa majisafi na usafi wa mazingira katika Manispaa ya Kigoma unatekelezwa kwa gharama ya **Euro milioni 16.32**. Hadi mwezi Machi 2017, ujenzi wa kidakio cha maji umefikia **asilimia 60.5**; ujenzi wa matanki **matano (5)** yenye ujazo wa **lita milioni 2** kila moja na tanki moja lenye ujazo wa **lita 500,000** umefikia **asilimia 87**; ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita milioni 2** umefikia **asilimia 95**; ujenzi wa kituo cha kusukuma maji chenye pampu **9 (asilimia 40)**; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji urefu wa **kilomita 122.8 (asilimia 83)**; ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 22 (asilimia 90)**; ujenzi wa vituo **75** vya kuchotea maji **(asilimia 11)**; ujenzi wa mabwawa **mawili (2)** ya kutibu majitaka **(asilimia 40)**; na gari la huduma ya uondoaji majitaka limenunuliwa. Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 69** na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2017. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji maji kutoka **lita milioni 1.3** hadi kufikia **lita milioni 42** pamoja na kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kufikia **asilimia 95** ya wakazi wa Manispaa ya Kigoma.

**108.** **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa mradi wa majisafi na usafi wa mazingira katika Manispaa ya Sumbawanga uliotekelezwa kwa gharama ya **Euro milioni 14.99** umekamilika na umeanza kutoa huduma kwa wakazi wa Manispaa hiyo. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na uchimbaji wa visima virefu **14**; ujenzi wa *sump tank* lenye ujazo wa **lita**

**milioni 1**; upanuzi wa chujio la maji; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa **kilomita 68** na bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 16**; ujenzi wa matanki **sita (6)** ya maji yenye jumla ya ujazo wa **lita milioni 7**; ujenzi wa vituo **56** vya kuchotea maji; ujenzi wa mabwawa **mawili (2)** ya kutibu majitaka na ununuzi wa magari **mawili (2)** ya uondoaji wa majitaka. Mradi huo umeongeza kiwango cha uzalishaji maji kutoka **lita milioni 4.8** hadi kufikia **lita milioni 13** na wakazi wapatao **209,793** wananufaika na huduma ya majisafi.

**(iii) Manispaa za Mtwara na Babati**

**109. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na **Serikali ya Ujerumani** kupitia ***KfW*** imeanza kutekeleza miradi ya kuboresha miundombinu ya kusambaza majisafi katika Miji ya Mtwara na Babati kwa gharama ya **Euro milioni 18.9**. Hadi Machi 2017, Mtaalam Mshauri amewasilisha taarifa ya awali ya usanifu na katika mwaka 2017/2018, kazi ya usanifu wa kina, kuandaa makabrasha ya zabuni pamoja na kuwapata Wakandarasi itakamilika ili kuanza ujenzi wa miradi ya maji katika miji hiyo.

**(b) Miradi ya Maji ya Kukidhi Mahitaji ya Muda Mrefu**

**(i) Mradi wa Maji Jijini Arusha**

**110. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na **Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*)** inatekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji majisafi na uboreshaji wa huduma ya uondoaji wa majitaka katika Jiji la Arusha na baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Arumeru. Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 233.9** na kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na uchimbaji wa visima; ujenzi wa matanki; ujenzi wa mtambo wa kutibu maji; ujenzi wa mtandao wa mabomba ya majisafi; ujenzi wa mabwawa mapya ya majitaka; ujenzi wa ofisi ya Mamlaka; ununuzi wa vitendea kazi na mafunzo kwa watumishi.

**111.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeajiri Wataalam Washauri wawili ambapo Mtaalam mmoja anaendelea na usanifu wa kina na uandaaji wa makabrasha ya zabuni ya mradi na anatarajiwa kukamilisha kazi hiyo ifikapo mwezi Juni, 2017. Mtaalam Mshauri mwingine anaendelea na kazi ya kutafuta vyanzo vya maji vya uhakika katika Jiji la Arusha na vitongoji vyake na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2017. Ujenzi wa mradi utaanza katika mwaka 2017/2018. Mahitaji ya maji kwa sasa ni **lita milioni 93.27** na mradi utakapokamilika utaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 40** kwa siku za sasa hadi **lita milioni 200** kwa siku. Vilevile, muda wa upatikanaji wa huduma ya majisafi utaongezeka kutoka **saa 12** za sasa hadi **saa 24** kwa siku pamoja na kuongeza huduma ya uondoaji wa majitaka kutoka **asilimia 7.6** za sasa hadi **asilimia 30**.

**(ii) Mradi wa Maji Morogoro Mjini**

**112.** **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na upungufu wa maji uliojitokeza katika Manispaa ya Morogoro ambao umesababishwa na uharibifu wa vyanzo vya maji vilivyopo, Serikali imeanza kutekeleza mpango wa muda mfupi wa uchimbaji wa visima **vitano (5)** katika Halmashauri ya Morogoro. Hadi mwezi Machi 2017, visima **vitatu (3)** vimechimbwa na vimepata maji. Visima **viwili (2)** vilivyobaki vinatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2017. Katika mwaka 2017/2018, Serikali imetenga **Shilingi milioni 500** kwa ajili ya kuendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Manispaa ya Morogoro.

**113.** **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mpango wa muda mrefu, Serikali kwa kushirikiana na **Serikali ya Ufaransa** kupitia **Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AFD*)** itatekeleza mradi wa kuongeza uzalishaji wa maji na kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika Manispaa ya Morogoro kulingana na mahitaji yaliyopo sasa na ya baadaye. Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mradi huo ni pamoja na kuongeza urefu wa tuta la Bwawa la Mindu kwa **mita 2.5** ili kuongeza ujazo wa maji kutoka **lita bilioni 12** hadi kufikia **lita bilioni 20**; upanuzi wa mtandao wa

kusambaza maji; ujenzi wa chujio lenye uwezo wa kuzalisha **lita milioni 54** za maji kwa siku; na ujenzi wa miundombinu ya majitaka. Hadi mwezi Machi 2017, Mtaalam Mshauri anaendelea kupitia usanifu uliofanyika awali na kuandaa gharama mpya za mradi pamoja na makabrasha ya zabuni. Kazi hiyo itakamilika mwezi Julai, 2017 na ujenzi wa mradi utaanza katika mwaka 2017/2018.

**(iii) Mradi wa KutoaMaji Mto Ruvuma Kupeleka Manispaa ya Mtwara Mikindani**

**114. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatekeleza mradi wa kutoa maji kutoka Mto Ruvuma kupeleka Manispaa ya Mtwara Mikindani na vijiji **26** pamoja na vitongoji vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka eneo la bomba kuu utakaogharimu **Dola za Marekani milioni 189.9**. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa kidakio cha maji; chujio la kutibu maji; nyumba ya mtambo wa kusukuma maji; matanki **26**; tanki la ujazo wa **lita milioni 30** ambalo litajengwa eneo la Mangamba; vituo vya kuchotea maji **234**; na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji lenye urefu wa **kilomita 63**. Hadi mwezi Machi 2017, Mkandarasi wa ujenzi wa mradi huo amepatikana na Serikali inaendelea na majadiliano na Serikali ya China kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi wa mradi huo. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 9** hadi **lita milioni 120** kwa siku na kutosheleza mahitaji ya watu na viwanda mbalimbali katika Manispaa ya Mtwara Mikindani.

**(c) Mradi wa Kutoa Maji Kutoka Mto Malagarasi Kwenda Miji ya Urambo, Kaliua na Nguruka**

**115. Mheshimiwa Spika**, Wizara imepanga kutekeleza mradi wa kutoa maji Mto Malagarasi kupeleka miji ya Urambo, Kaliua, Nguruka, Usoke pamoja na vijiji **68** vilivyopo kando ya bomba kuu. Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa kidakio cha maji, ujenzi wa mitambo ya kutibu maji, ujenzi wa matanki ya maji, ulazaji wa bomba kuu kutoka Mto Malagarasi hadi miji ya Urambo na Kaliua na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji

kwenye miji hiyo. Mtaalam Mshauri anaendelea na usanifu wa kina pamoja na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni unaotarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2017. Vilevile, taratibu za kumpata Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii zinaendelea na anatarajiwa kupatikana mwezi Mei, 2017. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo, unaotarajiwa kunufaisha wakazi wapatao **607,086** wa Miji ya Urambo, Kaliua na Nguruka pamoja na vijiji 68.

**(d) Mradi wa Maji katika Miji ya Sengerema, Nansio na Geita**

116. **Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na **Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*)** inaendelea kutekeleza mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Ziwa Victoria (*LVWATSAN II*) katika Miji ya Geita, Sengerema na Nansio kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni** na unasimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza. Kazi zinazotekelezwa katika Miji hiyo ni kama ifuatavyo:

**(i) Mji wa Sengerema**

117. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi wa kujenga miundombinu ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Sengerema uliogharimu **Shilingi bilioni 20.06** umekamilika. Kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa kidakio cha maji cha Nyamazugo katika Ziwa Victoria; ujenzi wa matanki **matano (5)** ya kuhifadhi maji yenye jumla ya **lita milioni 2.6**; na kulaza mabomba yenye urefu wa **kilomita 71.3**. Kwa upande wa mradi wa usafi wa mazingira, kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka eneo la Iyogelo; kujenga vyoo kwenye shule **tatu (3)** za msingi za Ibondo, Ngweli na Mwabaluhi pamoja na kujenga dampo la kisasa kwa ajili ya kutupa taka ngumu eneo la Ibondo. Mradi umekamilika na uzalishaji wa maji umeongezeka kutoka **lita milioni 2.34** kwa siku za hapo awali hadi **lita milioni 6.02** kwa siku za sasa. Mradi upo katika kipindi cha majaribio na utaboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka

**asilimia 33** hadi **asilimia 85** kwa wakazi wapatao **138,000** wa Mji huo.

### (ii) Mji wa Nansio

**118.** **Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa miundombinu ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Nansio umekamilika mwezi Oktoba, 2016 kwa gharama ya **Shilingi bilioni 10.9**. Kukamilika kwa mradi huo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita 700,000** hadi **lita milioni 3** kwa siku na kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 41** hadi **asilimia 70** kwa wakazi wa Mji huo.

### (iii) Mji wa Geita

**119.** **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi wa kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Geita unaendelea kwa gharama ya **Shilingi bilioni 6.67**. Hadi mwezi Machi 2017, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na uchimbaji wa visima virefu **vitatu (3)** na kununua pamoja na kufunga mitambo ya kusukuma maji kwenye visima **vinane (8)**, kazi hizo zimefikia **asilimia 50**; ujenzi wa matanki **manne (4)** ya maji yenye **ujazo wa lita 500,000** ambao umefikia **asilimia 90**, **ujazo wa lita 135,000 (asilimia 90)**, **ujazo wa lita 135,000 (asilimia 91)** na **ujazo wa lita 45,000** umefikia **asilimia 92**; kununua dira za maji **3,608**; ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 5.2** kati ya **kilomita 16**; na mabomba ya kusambaza maji yamelazwa urefu wa **kilomita 16** kati ya **kilomita 38**. Aidha, kwa upande wa kuboresha huduma za usafi wa mazingira mradi wa ujenzi wa vyoo **viwili (2)** kwenye Shule za Msingi za Mbugani na Nyankumbu umekamilika; ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka eneo la Usindakwe umefikia **asilimia 90**; na ujenzi wa dampo la kisasa la kutupa taka ngumu eneo la Usindakwe umefikia **asilimia 50**. Kwa ujumla ujenzi wa mradi umefikia **asilimia 65** na unatarajiwa kukamilika mwaka 2017/2018. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 3.8** kwa siku za sasa hadi **lita milioni 5.7** kwa siku na kuboresha hali ya upatikanaji wa maji kutoka

**asilimia 35** hadi **asilimia 70** kwa wakazi wapatao **135,359** wa Mji wa Geita.

**(e) Miradi ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Mwanza na Miji ya Lamadi, Magu na Misungwi pamoja na Miradi ya usafi wa mazingira katika Miji ya Bukoba na Musoma**

**120. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatekeleza mradi wa uboreshaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Mwanza na Miji ya Magu, Misungwi na Lamadi pamoja na mradi wa uondoaji wa majitaka katika Miji ya Bukoba na Musoma. Miradi hiyo inatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na **Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (*European Investment Bank-EIB)*** na **Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*French Development Agency-AFD*)** kwa gharama ya **Euro milioni 104.5**. Mchango wa Serikali ni **Euro milioni 14.5**, na *EIB* pamoja na *AFD* wanachangia jumla ya **Euro milioni 90**. Mkataba wa ujenzi wa mradi wa uboreshaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Mwanza na Miji ya Magu, Misungwi na Lamadi umesainiwa tarehe 16/02/2017. Ujenzi wa mradi umeanza na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Februari, 2019. Kazi zinazotekelezwa ni kulaza mabomba yenye vipenyo vya ukubwa tofauti, ujenzi wa matanki ya kuhifadhia maji, miundombinu ya kusambaza maji, mitambo ya kutibu maji na kujenga vituo vya kuchotea maji katika miji hiyo.

**121. Mheshimiwa Spika**, mradi huo utakapokamilika utaongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika miji hiyo ambapo kwa Jiji la Mwanza itaongezeka kutoka **asilimia 90** za sasa hadi **asilimia 100**; Mji wa Magu (**asilimia 23** hadi **asilimia 90**); Misungwi (**asilimia 39** hadi **asilimia 60**); na kwa Mji wa Lamadi kutoka **asilimia 20** hadi **asilimia 95**. Kukamilika kwa miradi hiyo kutawanufaisha wakazi **105,649** katika maeneo ya Nyasaka, Bugarika, Nyegezi, Capripoint, Mjimwema, Nyakabungo na Kitangiri katika Jiji la Mwanza; wakazi **23,315** waishio Misungwi mjini na kijiji cha Nyahiti; wakazi **45,340** waishio Magu Mjini na vijiji vya Ilungu na Kipeja; pamoja na wakazi **23,540** wa Mji wa Lamadi.

122. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mradi wa huduma ya uondoaji wa majitaka katika Miji ya Musoma na Bukoba utakaogharimu **Shilingi bilioni 24.87** utekelezaji wake umeanza. Katika Mji wa Musoma Mkandarasi wa mradi huo amepatikana na ujenzi utaanza mwezi Juni, 2017 na utakapokamilika **asilimia 30** ya wakazi wa Mji wa Musoma wataunganishwa kwenye huduma ya majitaka. Kwa upande wa Mji wa Bukoba taratibu za kumpata Mkandarasi zinaendelea na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2017. Mradi huo utakapokamilika **asilimia 12** ya wakazi wa Mji wa Bukoba wataunganishwa kwenye huduma ya majitaka.

### 4.4.2 Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji ya Mpanda, Njombe na Bariadi

123. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Serikali imeendelea kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Miji ya Mpanda, Njombe na Bariadi ambayo ina uhaba mkubwa wa maji. Utekelezaji wa miradi katika miji hiyo ni kama ifuatavyo:-

**(a) Mji wa Mpanda**

124. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika Mji wa Mpanda kwa gharama ya **Shilingi bilioni 2**. Kazi zinazotekelezwa ni ujenzi wa kidakio; ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 10** kutoka kwenye chanzo cha chemichemi zilizopo maeneo ya Kanoge na Barabara ya Kwanza hadi kitakapojegwa kidakio katika eneo la Manga; na bomba lenye urefu wa **kilomita 17** kutoka Manga hadi Hospitali ya Wilaya ya Mpanda. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 3.2** hadi **lita milioni 4.6** kwa siku pamoja na kupunguza tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya Makanyagio, Madukani na Majengo B. Katika mwaka 2017/2018, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1** ili kukamilisha mradi huo.

**(b) Mji wa Njombe**

**125. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Serikali imeendelea kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Njombe kwa kutekeleza mradi wa maji wa *Kibena Howard*- Awamu ya Kwanza kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.1**. Kazi ya ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilomita 2 imekamilika na kazi zinazoendelea ni ujenzi wa kidakio cha maji pamoja na ununuzi na ufungaji wa pampu mbili. Hadi mwezi Machi 2017, ujenzi wa mradi umefikia **asilimia 55** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2017. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita 480,000** hadi **lita milioni 1.1** kwa siku na kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji katika Hospitali ya Kibena, Chuo cha Uuguzi na maeneo mengine ya Kibena. Katika mwaka 2017/ 2018, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1** kwa ajili ya kukamilisha mradi huo.

**126. Mheshimiwa Spika**, katika mpango wa muda mrefu wa kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji wa Njombe, Serikali itatekeleza mradi wa maji kutoka Mto Hagafilo kwa ajili ya kutoa huduma ya maji kwa wakazi wa Mji wa Njombe na maeneo ya pembezoni. Usanifu wa mradi huo umekamilika na kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa kidakio cha maji, chujio la maji, matanki ya kuhifadhia maji pamoja na mabomba ya kusambaza maji. Mradi huo utagharimu **Dola za Marekani milioni 13.5** ikiwa ni mkopo nafuu kutoka Serikali ya India. Fedha hizo zinatarajiwa kupatikana katika mwaka 2017/2018.

**(c) Mji wa Bariadi**

**127. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Bariadi upo katika hatua za mwisho kukamilika. Hadi mwezi Machi 2017, kazi zilizokamilika ni pamoja na kuunganisha visima vipya **vitano (5)** kwenye mtandao wa maji; kujenga matanki **mawili (2)** ya maji yenye ujazo wa **lita 135,000** katika eneo la Somanda na **lita 680,000** eneo la Sima; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa **kilomita 11.2** katika maeneo ya Sima, Malambo na Somanda; kujenga nyumba ya mtambo wa kusukuma

maji; kulaza bomba kuu la kupandisha maji kwenye matanki; ujenzi wa vituo vya kuchotea maji; na kufunga dira za maji kwa wateja **400**. Katika mwaka 2017/2018, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1** kukamilisha mradi ikiwa ni pamoja na ununuzi wa pampu **tano (5)** zitakazofungwa kwenye visima pamoja na kupeleka umeme kwenye eneo la visima ili mradi uanze kutoa huduma ya maji kwa wakazi wapatao **59,500** wa Mji wa Bariadi. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita 443,000** za sasa hadi **lita milioni 1.56** kwa siku na kuongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 30** za sasa hadi kufikia **asilimia 75**.

#### 4.4.3 Miradi ya Kutoa Maji Ziwa Victoria Kupeleka Miji Mbalimbali

##### (a) Miji ya Busega, Bariadi, Lagangabilili, Maswa na Mwanhuzi

**128.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Miji ya Busega, Bariadi, Lagangabilili, Maswa na Mwanhuzi. Mradi huo utatekelezwa kwa awamu mbili zitakazogharimu **Euro Milioni 313** na utahudumia wakazi **834,204**. Mtaalam Mshauri amekamilisha upembuzi yakinifu na anaendelea na usanifu wa kina unaotarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2017. Mradi utahusisha ujenzi wa kidakio cha maji, mitambo ya kutibu majisafi, na tanki lenye ujazo wa **lita milioni 30** eneo la Ngasamo; ulazaji wa bomba kuu kutoka Ziwa Victoria hadi miji husika na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji kwenye miji hiyo. Awamu ya kwanza ya mradi itahusisha Miji ya Nyashimo (Busega), Bariadi, Lagangabilili pamoja na vijiji vipatavyo **253** vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka eneo la bomba kuu. Ujenzi wa awamu ya kwanza ya mradi unatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2017 kwa gharama ya **Euro milioni 105** ambapo Benki ya *KfW* ya Ujerumani itatoa **Euro milioni 25** na *Green Climate Fund (GCF)* **Euro Milioni 80**. Awamu ya pili ya mradi itagharimu **Euro milioni 208** na itahusisha Miji ya Mwanhuzi na Maswa, fedha ambazo zinatarajiwa kutolewa na *Green Climate Fund*. Awamu hiyo itaanza baada ya fedha kupatikana.

**(b) Miji ya Isaka na Kagongwa**

**129. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa maji kwenda katika miji ya Isaka na Kagongwa kwa kutumia chanzo cha maji kutoka Ziwa Victoria kupitia bomba kuu la *KASHWASA*. Wakandarasi wa ujenzi wa mradi wa maji katika miji hiyo wamepatikana na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Mei, 2017. Mradi huo utakapokamilika jumla ya wakazi wapatao **115,000** wa Miji ya Isaka na Kagongwa watanufaika na huduma ya maji ambapo hali ya upatikanaji wa huduma ya maji itaongezeka kutoka **asilimia 26** za sasa hadi **asilimia 90** kwa Mji wa Isaka, na **asilimia 24** hadi **asilimia 95** katika Mji wa Kagongwa.

**(c) Miji ya Mwadui, Kishapu, Kolandoto na Maganzo**

**130. Mheshimiwa Spika**, mradi wa kupeleka maji katika miji ya Mwadui, Kishapu, Kolandoto na Maganzo, uliotekelezwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia Mamlaka ya *KASHWASA* umekamilika na wakazi wa miji hiyo wanapata huduma ya maji. Katika jitihada za kuongeza uhifadhi wa maji ya kutosha katika Mji wa Kishapu, Wizara inaendelea na ujenzi wa tanki la maji lenye ujazo wa **lita milioni 1.2**. Hadi mwezi Machi 2017, ujenzi wa tanki hilo umefikia **asilimia 90** na unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2017.

**(d) Miji ya Tabora, Uyui, Igunga, Nzega, Tinde na Sikonge**

**131. Mheshimiwa Spika**, mradi huo unalenga kuwapatia huduma ya maji wakazi wa miji ya Tabora, Uyui, Igunga, Nzega, Tinde na Sikonge pamoja na Vijiji **89** vilivyopo kwenye eneo la kilomita 12 kutoka bomba kuu la mradi wa *KASHWASA*. Mradi ni wa malengo ya muda mrefu ya kuwapatia huduma ya maji ya uhakika wananchi wapatao **milioni 1.1** wa maeneo hayo. Ujenzi wa mradi umegawanyika katika awamu mbili. Awamu ya kwanza itahusisha kupeleka maji katika Miji ya Tabora, Igunga, Uyui,

Nzega na Tinde. Kazi zitakazotekelezwa katika awamu hiyo ni pamoja na ujenzi wa bomba kuu kutoka Kijiji cha Solwa; ulazaji wa mabomba; na ukarabati wa mitandao ya usambazaji maji katika miji hiyo. Wakandarasi wamepatikana na ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwezi Mei, 2017 kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 268.35** kutoka Serikali ya India kama mkopo wenye masharti nafuu. Mradi huo ukikamilika utaongeza hali ya upatikanaji wa maji katika Mji wa Tabora kutoka **asilimia 80** hadi **asilimia 100**; Uyui **(asilimia 30** hadi **asilimia 100)**; Igunga **(asilimia 62** hadi **asilimia 100)**; Nzega **(asilimia 58** hadi **asilimia 100)**; na Mji wa Tinde kutoka **asilimia 45** hadi **asilimia 68**. Awamu ya pili ya mradi itahusu kupeleka maji katika Mji wa Sikonge kutoka Ziwa Victoria.

### 4.4.4 Miradi ya Kuboresha Huduma ya Maji katika Jiji la Dar es Salaam

**132.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kutekeleza miradi ya maji katika Jiji la Dar es Salaam ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya majisafi katika Jiji hilo pamoja na Miji ya Kibaha na Bagamoyo. Miradi inayoendelea kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

### (a) Ujenzi wa Bwawa la Kidunda

**133.** Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa Bwawa la Kidunda unaogharimu **Dola za Marekani milioni 215**. Mradi huo ni wa kimkakati wenye lengo la kuhakikisha kuwa maji katika Mto Ruvu ambao ni chanzo kikubwa cha maji kwa Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo yanapatikana katika kipindi chote cha mwaka. Mradi huo utajumuisha ujenzi wa bwawa la kuhifadhi maji lenye **mita za ujazo milioni 190**; ujenzi wa kituo cha kufua **megawati 20** za umeme; ujenzi wa njia ya msongo mkubwa wa umeme kutoka Kidunda hadi Chalinze; na ujenzi wa barabara yenye urefu wa **kilomita 75** kutoka Ngerengere hadi Kidunda. Usanifu wa bwawa na barabara umekamilika na kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mradi huo.

**(b) Mradi wa Visima vya Kimbiji na Mpera**

134. **Mheshimiwa Spika**, uchimbaji wa visima virefu 20 vya maji vinavyotarajiwa kuzalisha **lita milioni 260** kwa siku katika maeneo ya Kimbiji na Mpera unaendelea na unagharimu **Shilingi bilioni 18**. Hadi mwezi Machi 2017, Mkandarasi amechimba visima **17**. Uchimbaji wa visima **vitatu (3)** unaendelea na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2017. Visima vya maeneo ya Mpera vitahudumia wakazi wa maeneo ya Gongo la Mboto, Chanika, Luzando, Pugu, Mpera, Chamanzi, Kitunda, Ukonga, Kinyerezi, na Uwanja wa Ndege; na visima vya maeneo ya Kimbiji vitahudumia wakazi wa maeneo ya Temeke, Kisarawe, Kibada, Kimbiji, Kigamboni, Tuangoma, Mkuranga, Kongowe, Mbagala, Kurasini, Mtoni, Tandika, Keko na Chang'ombe. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya kusambaza maji kutoka kwenye visima hivyo kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 158** katika maeneo yatakayohudumiwa na visima vya Mpera na **Dola za Marekani milioni 307** kwa maeneo yatakayohudumiwa na visima vya Kimbiji.

**(c) Ukarabati na Upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Majisafi**

135. **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi wa ukarabati na upanuzi wa mfumo wa kusambaza majisafi katika maeneo ya Changanyikeni, Tegeta hadi Mpiji, Mpiji hadi Bagamoyo na Mbezi hadi Kiluvya unaendelea kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 32.93**. Hadi mwezi Machi 2017, kazi zinazoendelea ni ujenzi wa tanki jipya katika eneo la Changanyikeni na kituo cha kusukuma maji Makongo ambapo kazi hizo zinatarajiwa kukamilika katika mwaka 2017/2018. Kukamilika kwa mradi huo kutanufaisha Mji wa Bagamoyo na vitongoji vyake, eneo la uwekezaji la Bagamoyo (*EPZ*), Mpiji, Bunju, Mabwepande, Boko, Mbweni, Tegeta, Ununio, Wazo, Salasala, Kinzudi, Matosa, Mbezi Juu, Goba, Changanyikeni, Makongo, Kiluvya, Kibamba, Mbezi, Msakuzi, Makabe, Malamba mawili na Msigani. Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na **Benki ya Dunia** itatekeleza mradi wa

ujenzi wa mabomba madogo ya kusambaza maji na kuunganisha wateja katika maeneo ya Changanyikeni hadi Mpiji na Mpiji hadi Bagamoyo. Mradi huo utagharimu **Dola za Marekani milioni 50** na ujenzi utaanza katika mwaka 2017/2018.

**(d) Mfumo Mpya wa Kusambaza Maji Katika Maeneo Yasiyokuwa na Mtandao wa Mabomba**

**136. Mheshimiwa Spika**, katika Jiji la Dar es Salaam na miji ya Kibaha na Bagamoyo, yapo maeneo ambayo hadi sasa hayana mtandao wa mabomba ya kusambaza majisafi. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imeanza kutekeleza mradi wa kulaza mabomba ya kusambaza maji kwenye maeneo hayo yakiwemo Mkuranga, Chamazi, Msongola, Chanika, Gongo la mboto, Pugu, Kitunda, Uwanja wa Ndege, Kinyerezi, Vituka, Kiwalani na Vingunguti. Maeneo mengine ni pamoja na Kimbiji, Kibada, Kigamboni, Tuangoma, Kongowe, Mbagala, Kurasini, Temeke na Bandarini. Hadi mwezi Machi 2017, usanifu pamoja na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi umekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo.

**(e) Kuboresha Miundombinu ya Uondoaji Majitaka**

**137. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na **Serikali ya Korea Kusini** imeanza kutekeleza awamu ya kwanza ya mradi wa kuboresha huduma ya uondoaji majitaka katika Jiji la Dar es Salaam kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 90.09**. Ujenzi wa mradi huo utahusisha maeneo ya Magomeni, Jangwani na katikati ya Jiji ikiwa ni pamoja na kuhamisha mfumo wa kumwaga majitaka baharini kwenda kwenye mtambo mpya wa kusafisha na kutibu majitaka utakaojengwa eneo la Jangwani. Kazi ya usanifu na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni imekamilika. Taratibu za kumpata Mkandarasi zinaendelea na ujenzi utaanza katika mwaka 2017/2018. Awamu ya pili ya mradi huo itatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni**

**65**. Awamu hiyo itahusu upanuzi wa miundombinu ya majitaka kwenye maeneo ya Mbezi Beach, Kawe na Kilongawima. Taratibu za kumpata Mkandarasi zinaendelea na mradi unatarajiwa kuanza mwaka 2017/2018.

### (f) Miradi Mingine ya Maji Jijini Dar es Salaam

**138.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuchimba visima ili kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam ambayo wananchi wake hawapati huduma kutoka mtandao wa kusambaza maji wa *DAWASCO.* Hadi mwezi Machi 2017, uchimbaji wa visima **34** umekamilika na vinatoa huduma ya maji katika maeneo ya Mavurunza A, Kilungule A, Kilungule B, King'ongo I, King'ongo III, Sandali, Mpogo, Mwemberadu, Mburahati, Kipunguni, FFU Ukonga, Mongo la Ndege, Segerea, Chanika, Yombo, Saranga I, Saranga II, Chang'ombe A, Unubini, Chang'ombe Toroli, Keko Magurumbasi na Keko Mwanga. Wizara itaendelea kutekeleza miradi ya namna hiyo ili kupunguza kero ya maji wakati wa kusubiri kukamilika kwa mradi mkubwa wa kusambaza maji katika Jiji la Dar es Salaam.

## 4.4.5 Huduma ya Maji katika Baadhi ya Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo

### (a) Miji ya Kilosa, Turiani, Mvomero na Gairo

**139.** **Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi mahitaji ya maji kwa wakazi wa miji ya Kilosa, Turiani, Mvomero na Gairo, Serikali imeendelea na ujenzi wa miradi ya maji katika miji hiyo. Kazi zinazotekelezwa katika miradi hiyo ni uchimbaji wa visima, ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji, ufungaji wa umeme kwenye nyumba za mitambo, ujenzi wa matanki na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji. Hadi mwezi Machi 2017, utekelezaji wa miradi hiyo katika miji tajwa ni kama ifuatavyo:-

**(i) Mji wa Kilosa**

**140. Mheshimiwa Spika**, mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Kilosa unaendelea kutekelezwa ambapo uchimbaji wa visima **viwili (2)** umekamilika. Kazi zinazoendelea ni pamoja na ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji ambapo **kilomita 22.31** zimelazwa kati ya **kilomita 24.26**; ujenzi wa nyumba **tano (5)** za mitambo umefikia **asilimia 70**; ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji lenye ujazo wa **lita milioni 1** eneo la Uzunguni **(asilimia 95)**; ukarabati wa tanki lenye ujazo wa **lita 135,000** katika eneo la Uzunguni na tanki lenye ujazo wa **lita 225,000** eneo la Manzese "B" **(asilimia 90)**; ujenzi wa nyumba kwa ajili ya kuhifadhi madawa **(asilimia 85)**; ujenzi wa kituo cha kusukuma maji umefikia **asilimia 78;** na taratibu za ununuzi wa pampu **nane (8)** za kusukuma maji unaendelea. Kwa ujumla ujenzi wa mradi umefikia **asilimia 80** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2017. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 59** hadi **asilimia 85** na kuwanufaisha wakazi wapatao **32,120** wa Mji wa Kilosa.

**(ii) Mji wa Turiani**

**141. Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Turiani ambapo uchimbaji wa kisima **kimoja (1)** katika eneo la Madizini na ujenzi wa tanki la maji lenye ujazo wa **lita 300,000** umekamilika. Kazi zinazoendelea ni pamoja na kusafisha visima **viwili (2)** eneo la Madizini ambayo imefikia **asilimia 85**; ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji ambapo **kilomita 26.2** zimelazwa kati ya **kilomita 41.5**; ujenzi wa tanki la maji lenye ujazo wa **lita milioni 2 (asilimia 8)**; ujenzi wa nyumba ya kuhifadhi mitambo **(asilimia 81)**; ukarabati wa kingo za maji katika chanzo cha mserereko **(asilimia 90)**; na ujenzi wa nyumba kwa ajili ya kuhifadhi madawa ambao umefikia **asilimia 39**. Kwa ujumla ujenzi wa mradi umefikia **asilimia 80** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2017. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 60** hadi

**asilimia 75** na kuwanufaisha wakazi wapatao **48,113** wa Mji huo.

**(iii) Mji wa Mvomero**

**142. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Mvomero unaendelea ambapo uchimbaji wa **kisima** katika eneo la Dibamba umekamilika. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa tanki la maji lenye ujazo wa **lita 500,000** ambao umefikia **asilimia 89**; ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji ambapo **kilomita 14.5** zimelazwa kati ya **kilomita 19.9**; ujenzi wa nyumba ya kuhifadhi mitambo umefikia **asilimia 85.5**; na ujenzi wa nyumba kwa ajili ya kuhifadhi madawa ambao umefikia **asilimia 73**. Aidha, taratibu za ununuzi wa pampu **mbili (2)** za kusukuma maji zinaendelea. Kwa ujumla ujenzi wa mradi umefikia **asilimia 80** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2017. Mradi huo utakapokamilika utaongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 42** hadi **asilimia 60** na kutanufaisha wakazi wapatao **15,795** wa Mji huo.

**(iv) Mji wa Gairo**

**143. Mheshimiwa Spika**, uchimbaji wa visima **saba (7)** vya maji katika Mji wa Gairo umekamilika. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa tanki la maji lenye ujazo wa **lita milioni 1** ambao umefikia **asilimia 95**; ujenzi wa matanki **mawili (2)** ya maji yenye ujazo wa **lita 300,000** kila moja **(asilimia 85)**; ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji ambapo **kilomita 31** zimelazwa kati ya **kilomita 43**; ujenzi wa kituo cha kusukuma maji **(asilimia 94)**; ujenzi wa nyumba ya kuhifadhi mitambo **(asilimia 95)**; na ujenzi wa nyumba kwa ajili ya kuhifadhi madawa ambao umefikia **asilimia 98**. Ujenzi wa mradi huo kwa ujumla umefikia **asilimia 81** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2017. Mradi utakapokamilika utaongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 50** hadi **asilimia 74** na utawanufaisha wakazi wapatao **27,180** wa Mji huo.

**144.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Serikali itaajiri Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na utafiti wa kina kwa ajili ya kupata vyanzo vingine vya maji vya uhakika ambavyo vitaondoa kero ya maji katika miji ya Mkoa wa Morogoro.

**(b) Mji wa Bunda**

**145.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kutekeleza awamu ya pili ya mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika Mji wa Bunda kwa kujenga mtandao wa kusambaza maji pamoja na vituo vya kuchotea maji. Hadi mwezi Machi 2017, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 95** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2017. Vilevile, taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mtambo wa kutibu maji zinaendelea. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 35** hadi **asilimia 65** na kunufaisha wakazi wapatao **23,632** wa Mji wa Bunda.

**(c) Mji wa Mugumu**

**146.** **Mheshimiwa Spika**, mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika Mji wa Mugumu unagharimu **Shilingi bilioni 1.6** na unahusisha ujenzi wa mtambo wa kusafisha maji, kulaza mabomba ya kusambaza maji na ujenzi wa *sump well* ya **lita 100,000**. Hadi mwezi Machi 2017, ujenzi umefikia **asilimia 60** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2017. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kutoka **asilimia 30** hadi **asilimia 78** na kuwanufaisha wakazi wapatao **25,000** wa Mji huo.

**(d) Mji wa Orkesumet**

**147.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na **Benki ya Maendeleo ya Nchi za Kiarabu (*BADEA*)** na ***OPEC Fund for International Development (OFID)*** inatekeleza mradi wa majisafi utakaohudumia Mji wa Orkesumet. Mradi huo utagharimu **Dola za Marekani milioni 18.4** ambapo *BADEA* watatoa **Dola za Marekani milioni 8**, *OFID* watatoa **Dola za**

**Marekani milioni 8** na mchango wa Serikali ni **Dola za Marekani milioni 2.4**. Mradi huo umegawanyika katika vipande (*lots*) viwili. Kipande cha kwanza kinahusu ujenzi wa kidakio cha maji na mtambo wa kutibu na kusafisha maji ambapo hadi mwezi Machi 2017, taratibu za kumpata Mkandarasi zinaendelea. Ujenzi unatarajiwa kuanza mwaka 2017/2018.

Aidha, kipande cha pili kinahusu ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji; ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji; ujenzi wa vituo vya kuchotea maji pamoja na miundombinu ya kunyweshea mifugo. Hadi mwezi Machi 2017, Mkandarasi wa ujenzi wa kipande hicho cha mradi ameanza maandalizi ya ujenzi na mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2019. Mradi huo utakapokamilika utaongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kutoka **asilimia 48** hadi **asilimia 82** na kuwanufaisha wakazi wa Mji wa Orkesument pamoja na mifugo yao.

### 4.4.6 Miradi ya Maji ya Kitaifa

**148.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Maji ya Kitaifa ili kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya miradi hiyo. Miradi inayoendelea kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

#### (a) Mradi wa Maji Chalinze

**149.** **Mheshimiwa Spika**, mradi wa majisafi wa Chalinze Awamu ya III unatekelezwa kupitia mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 41.3**. Mradi unahusisha upanuzi wa kidakio katika chanzo; kujenga matanki ya kuhifadhia maji katika vijiji **20**; kulaza bomba kuu na upanuzi wa mtandao wa mabomba ya kusambaza maji; kujenga tanki kubwa la kuhifadhi maji katika Mlima Mazizi; na kujenga vituo vya kuchotea maji katika maeneo ambayo hayakufikiwa na huduma ya maji wakati wa ujenzi wa Awamu ya I na II. Hadi mwezi Machi 2017, ujenzi wa mradi umefika **asilimia 21** ingawa kulingana

na Mkataba ulitarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2017. Kutokana na Mkandarasi kushindwa kukamilisha mradi kwa wakati, Wizara imeanza kumtoza gharama za ucheleweshaji wa mradi (*liquidated damages*) kuanzia tarehe 23/2/2017 kulingana na makubaliano ya Mkataba. Vilevile, Mkandarasi amepewa notisi ya siku 100 kuongeza kasi ya utekelezaji vinginevyo mkataba wake utasitishwa iwapo hatafikisha **asilimia 75** ya ujenzi ifikapo tarehe 31/05/2017. Aidha, Wizara yangu inafuatilia kwa karibu utekelezaji wa agizo hilo. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 5** kwa siku hadi **lita milioni 9** kwa siku na kuwanufaisha wananchi wapatao **397,384**.

### (b) Mradi wa Mugango – Kiabakari

**150. Mheshimiwa Spika**, mradi wa maji wa Mugango-Kiabakari-Butiama unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na **Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika *(BADEA)*** na **Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*Saudi Fund for Development - SFD)*** kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 30.69**. Hadi mwezi Machi 2017, Mtaalam Mshauri amekamilisha usanifu wa kina na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi. Taarifa hizo zimetumwa *BADEA* kwa ajili ya kupata kibali cha ujenzi unaotarajiwa kuanza mwaka 2017/2018. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na upanuzi wa kidakio cha maji; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kusukuma maji; ujenzi wa matanki **matatu (3)**; kulaza bomba kuu kutoka Mugango, Kiabakari hadi Butiama umbali wa **kilomita 32**; kukarabati mitambo ya kusukuma maji ya Kiabakari; na kulaza mabomba ya mtandao wa kusambaza maji kutoka Butiama hadi Bisarye. Mradi huo utakapokamilika utawanufaisha wananchi wapatao **80,000** waliopo katika eneo la mradi pamoja na vijiji vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka eneo la bomba kuu.

### (c) Mradi wa Makonde

**151. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatekeleza mradi mkubwa wa kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi katika maeneo yanayohudumiwa na mradi wa maji

wa Kitaifa wa Makonde. Ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kuanza katika mwaka 2017/2018 kwa gharama ya **Euro milioni 87.41** ikiwa ni mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India. Vilevile, kwenye mpango wa muda mfupi ambao umepangwa kutekelezwa katika mwaka 2017/2018, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1** kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya maji ili kupunguza upotevu wa maji na kuongeza uzalishaji, hivyo kupunguza kero ya uhaba wa maji kwa wananchi wanaohudumiwa na mradi huo.

**(d) Mradi wa *Handeni Trunk Main* (*HTM*)**

**152. Mheshimiwa Spika**, kwa mpango wa muda mfupi wa kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo yanayohudumiwa na mradi wa *HTM*, usanifu umekamilika na ukarabati unatarajiwa kuanza mwaka 2017/ 2018. Ukarabati huo utahusisha ubadilishaji wa mabomba chakavu, ukarabati wa tanki na upanuzi wa chanzo ambapo Serikali imetenga **Shilingi bilioni 2** kwa ajili ya kuanza kutekeleza kazi hizo. Katika mpango wa muda mrefu, Serikali kwa kushirikiana na **Serikali ya India** itatekeleza mradi mkubwa wa maji utakaogaharimu **Dola za Marekani milioni 84.4**. Mradi huo unatarajiwa kuanza katika mwaka 2017/2018 na kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa chanzo na mitambo ya kusafisha maji; ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji; na ulazaji wa mtandao wa mabomba ya kusambaza maji. Kukamilika kwa mradi huo kutaboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 44** ya sasa hadi **asilimia 80**.

**(e) Mradi wa Wanging'ombe**

**153. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2016/ 2017, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya maji kwenye maeneo yanayohudumiwa na Mradi wa Wanging'ombe. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na ulazaji wa mabomba ya maji, kufunga vitoa upepo (*air valves*), kufunga maboya kwenye matanki, kukarabati baadhi ya maeneo korofi kwenye makorongo na kufunga dira za maji kwa wateja hasa vituo vya umma na malambo. Kukamilika kwa kazi hizo kumepunguza upotevu wa maji kutoka **asilimia**

**77** hadi **asilimia 75** na kuwezesha wananchi **16,548** wa Vijiji vya **Kijombe, Lyamluki**, **Uhenga**, **Luduga**, **Igwachanya**, **Chalowe**, **Mtapa** na **Idindilimunyo** kupata huduma ya maji. Katika mwaka 2017/2018, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 4** ili kuendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa maji katika maeneo yanayohudumiwa na mradi huo.

**154.** **Mheshimiwa Spika**, kwa mpango wa muda mrefu Serikali kwa kushirikiana na **Serikali ya India** itatekeleza mradi wa kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo yanayopata huduma hiyo kutoka mradi wa kitaifa wa Wanging'ombe pamoja na Mji wa Igwachanya kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 48.99**, ambapo mradi huo utatekelezwa katika mwaka 2017/2018. Kazi zinazotarajiwa kutekelezwa ni pamoja na ukarabati wa chanzo cha Mbukwa na Mtitafu; kulaza bomba kuu kutoka chanzo cha Mbukwa umbali wa **kilomita 112**; ukarabati wa matanki **59**; kulaza bomba kuu kutoka chanzo cha Mtitafu umbali wa **kilomita 15**; ujenzi wa tanki la ujazo wa **lita 200,000** katika eneo la Igwachanya; na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji. Kukamilika kwa mradi huo kutaboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 77** ya sasa hadi **asilimia 90**.

### 4.4.7 Kuzijengea Uwezo Mamlaka za Maji Mijini

**155.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Serikali imekamilisha ujenzi wa jengo la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Tunduma na kuzinduliwa rasmi tarehe 22/12/2016. Katika mwaka 2017/2018, Serikali itaanza ujenzi wa Ofisi katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Mpanda ambapo Mkandarasi amepatikana na anaendelea na taratibu za maandalizi ya ujenzi. Kwa upande wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira mjini Geita taratibu za kumpata Mkandarasi zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2017. Aidha, Wizara imefanya mafunzo kwa ajili ya Wajumbe wa Bodi za Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji Mikuu ya Mikoa na Miradi ya Maji ya Kitaifa. Mafunzo hayo yatawasaidia Wajumbe kuzisimamia Mamlaka kwa ufanisi zaidi ili kutoa huduma iliyo bora kwa wateja wa Mamlaka hizo.

**156.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Wizara imetangaza zabuni **77** za ujenzi wa miradi ya maji mijini ili kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji katika Miji mbalimbali nchini. Katika mwaka 2017/2018, jumla ya **Shilingi bilioni 273** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maji mijini. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 143** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 130** ni fedha za nje. ***Jedwali Na. 6*** linaonesha mgawanyo wa fedha zilizotengwa kutekeleza miradi ya maji mijini. Vilevile, katika mwaka 2017/2018, Serikali kwa kushirikiana na **Serikali ya India** itatekeleza miradi **17** ya kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na usafi wa mazingira katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo, Miradi ya Maji ya Kitaifa pamoja na Zanzibar kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 503.04** ikiwa ni mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India. Orodha ya miradi hiyo na mchanganuo wa gharama umeainishwa katika ***Jedwali Na. 7***.

**157.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, kwa upande wa huduma ya maji mijini, Serikali imepanga kukamilisha miradi inayoendelea kujengwa pamoja na kuchukua hatua za kisheria kwa Wakandarasi wote ambao watashindwa kukamilisha miradi kwa wakati kulingana na mikataba. Aidha, Wizara kupitia Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira Mijini, itahakikisha kuwa katika utekelezaji wa miradi mipya, maeneo ambayo hayana huduma ya majisafi na usafi wa mazingira yanapewa kipaumbele. Vilevile, Mamlaka hizo zimeelekezwa kutumia fursa ya uwepo wa Sekta Binafsi kupitia utaratibu wa ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*PPP*) pamoja na Taasisi za Kifedha ili kufanikisha uwekezaji katika miradi ya kuboresha huduma ya maji pamoja na kuongeza mitandao ya kusambaza maji kwenye maeneo wanayoyahudumia.

## 4.5 HUDUMA YA UMWAGILIAJI

### 4.5.1 Utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*)

**158.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Wizara

kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilipanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu **103** na maghala **53** pamoja na kuendelea kujenga skimu **37** ambazo ujenzi wake haukukamilika. Hadi mwezi Machi 2017, upembuzi yakinifu na usanifu unaendelea katika skimu za Kilosa kwa Mpepo kwenye Halmashauri ya Malinyi, Simbo (Igunga) na skimu ya Ibanda iliyopo kati ya Halmashauri za Sengerema na Geita pamoja na Bwawa la Gidahababierg lililopo Halmashauri ya Hanang'. Vilevile, usanifu katika skimu za Rudewa (Kilosa) na Endagaw (Mbulu) umekamilika. Wizara inaendelea na ujenzi katika skimu za Ussoke Mlimani **(hekta 530)** katika Halmashauri ya Urambo na Mforo **(hekta 290)** katika Halmashauri ya Mwanga. Aidha, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa skimu za Hangangadinda **(hekta 250)** katika Halmashauri ya Madaba na Igongwa **(hekta 300)** katika Halmashauri ya Misungwi zinaendelea. Wizara pia imeendelea kupitia Mpango Kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002 ili kubaini maeneo yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na kazi hiyo itakamilika katika mwaka 2018/2019.

**159.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara imepanga kukamilisha ujenzi wa mabwawa ya Itagata Wilayani Manyoni, Dongobesh na Tlawi (Mbulu); skimu za Igenge (Misungwi), Kirya (Mwanga), Itete (Malinyi) na Mkula (Kilombero); pamoja na kukarabati skimu ya Segeni iliyopo Wilayani Rufiji. Vilevile, Wizara itakamilisha upembuzi yakinifu na usanifu katika skimu za Luiche iliyopo Wilayani Kigoma, Muhongo (Ngara), Mwamukulu (Mpanda), Kilosa kwa Mpepo (Malinyi), skimu ya Lupiro (Kilombero) pamoja na mabwawa ya umwagiliaji katika maeneo ya Gidahababierg (Hanang') na Igwachanya katika Wilaya ya Wanging'ombe. Wizara pia itafanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa skimu za umwagiliaji za Chiumo katika Bonde la Mto Ruvuma na Kitere kwenye Bonde la Mto Kitere.

**160.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea kuwajengea uwezo wakulima na wataalam kuhusu usimamizi na uendeshaji wa miundombinu ya umwagiliaji; kusajili vyama vipya **100** vya wamwagiliaji katika

skimu za wakulima wadogo; na kuimarisha vyama **442** vya umwagiliaji vilivyopo. Vilevile, Wizara itafanya utafiti ili kubaini teknolojia za umwagiliaji zenye ufanisi zaidi katika matumizi ya maji kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na tija ya mazao. Katika kufanikisha azma hiyo, Wizara imepanga kuanzisha kituo cha mafunzo na utafiti wa teknolojia mbalimbali za umwagiliaji.

### 4.5.2 Mradi wa Kuendeleza Zao la Mpunga (*Expanded Rice Productivity Project - ERPP*)

**161. Mheshimiwa Spika**, Wizara ilipanga kufanya mapitio ya usanifu, ukarabati wa skimu na kutoa mafunzo kwa wakulima kuhusu Kilimo Shadidi cha Mpunga (*Systems of Rice Intensification - SRI*). Hadi mwezi Machi 2017, mapitio ya mahitaji ya maji na upimaji wa ardhi kwa ajili ya kuanza kufanya usanifu wa miundombinu inayohitajika katika skimu hizo yamekamilika. Usanifu wa miundombinu ya umwagiliaji ikiwa ni pamoja na mifereji na matupio (*drains*) unaendelea na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2017. Vilevile, jumla ya wakulima **264** walipatiwa mafunzo kuhusu uendeshaji na kutunza miundombinu ya umwagiliaji pamoja na uanzishwaji na uboreshaji wa vyama vya wamwagiliaji. Wakulima hao walitoka katika Skimu za Njage **(34)**, Msolwa Ujamaa **(38)**, Mvumi **(38)**, Kigugu **(56)** na Mbogo **(98)**. Katika mwaka 2017/2018, Wizara itajenga Skimu hizo ili kuwawezesha wakulima kuzalisha kwa tija.

### 4.5.3 Mradi wa Kuendeleza Skimu za Umwagiliaji za Wakulima Wadogo (*Small Scale Irrigation Development Project - SSIDP*)

**163. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa mradi wa kuendeleza skimu za umwagiliaji za wakulima wadogo kwa awamu tatu katika Halmashauri **68**. Awamu ya kwanza ilihusisha ujenzi na ukarabati wa skimu **45**, awamu ya pili skimu **63** na awamu ya tatu itahusisha ujenzi na ukarabati wa skimu **11**. Katika mwaka 2016/2017, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya **32** imeendelea

kusimamia ukarabati na uboreshaji wa skimu **45** za umwagiliaji za awamu ya kwanza zenye jumla ya **hekta 13,722**. Hadi mwezi Machi 2017, ukarabati na ujenzi wa skimu **45** za awamu ya kwanza umekamilika. Kukamilika kwa ukarabati na uboreshaji wa skimu hizo kumeongeza eneo la umwagiliaji kutoka **hekta 461,326** hadi kufikia **hekta 468,338** (sawa na ongezeko la **hekta 7,012**).

**164.** **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi unahusisha ujenzi na ukarabati wa skimu **63** ambapo ukarabati na ujenzi wa skimu **43** unaendelea; na taratibu za kuwapata Wakandarasi wa skimu **20** zilizobaki zinaendelea katika Halmashauri husika. Katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kukamilisha ukarabati na ujenzi wa skimu hizo. Orodha ya skimu na hatua zilizofikiwa inaoneshwa katika ***Jedwali Na. 8***.

### 4.5.4 Programu ya Kukabiliana na Changamoto za Uhaba wa Chakula Duniani (*Feed the Future*)

**165.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na **Serikali ya Marekani** inaendelea kutekeleza Programu ya *Feed the Future* inayolenga kuendeleza miradi ya umwagiliaji na barabara za kuunganisha masoko katika Skimu ya Dakawa yenye jumla ya **hekta 2,000** Mkoani Morogoro. Hadi mwezi Machi 2017, kazi zilizokamilika ni pamoja na ununuzi wa pampu **6**; ujenzi wa nyumba ya wasimamizi na ofisi ya skimu; ukarabati wa tuta kuu la kuzuia mafuriko; na ukarabati wa barabara yenye urefu wa **mita 360**. Kazi zinazoendelea ni ufungaji wa pampu hizo; uchimbaji na ujenzi wa mfereji wa maji ya matupio wenye urefu wa **kilomita 11.5** ambao umefikia **asilimia 80**; ukarabati wa barabara za mashambani zenye urefu wa **kilomita 35 (asilimia 80)**; ujenzi wa vigawa maji **50** vya mashambani **(asilimia 50)** pamoja na usakafiaji wa mfereji mkuu wenye urefu wa **kilomita 7.3** ambao umefikia **asilimia 55**. Katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Marekani (*USAID*) ili kukamilisha mradi huo.

### 4.5.5 Mradi wa Kujenga Uwezo katika Kuendeleza Umwagiliaji Nchini (*TANCAID*)

**166.** **Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na **Serikali ya Japan** kupitia **Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (*JICA)*** inatekeleza mradi wa Kujenga Uwezo kwa Maendeleo ya Umwagiliaji Tanzania (*Tanzania Capacity Building for Irrigation Development - TANCAID)*. Mradi huo unalenga kujenga uwezo kwa Wataalam wa Kanda za Umwagiliaji, Halmashauri za Wilaya na Wakulima kwa kutumia Mwongozo Yakinifu wa Umwagiliaji (*Comprehensive Guidelines II - CGL II*). Hadi mwezi Machi 2017, mradi umetoa mafunzo ya uibuaji wa miradi; uendeshaji na utunzaji wa miundombinu ya skimu za umwagiliaji; pamoja na utumiaji wa mwongozo wa usimamizi wa miradi ya ujenzi kwa Wataalam wa Wilaya na Kanda. Vilevile, mafunzo kwa vitendo ya uendeshaji na utunzaji wa miundombinu ya skimu za umwagiliaji yalitolewa kwa Wakulima kupita Vyama vya Umwagiliaji katika skimu za Ulyanyama, Nyida, Msemembo na Lemkuna. Jumla ya Wataalam **21** kutoka Kanda 7 za umwagiliaji na Wataalam **14** kutoka Halmashauri za Wilaya za Misungwi, Shinyanga, Manyoni, Simanjiro, Tabora (Mjini), Sikonge na Urambo wamenufaika katika mafunzo hayo. Kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na uandaaji wa Mwongozo wa Ugawaji Maji kwenye Skimu za Umwagiliaji; na Muundo wa Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu za Umwagiliaji.

**167.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea kukamilisha ujenzi wa miradi ya umwagiliaji inayoendelea; kukarabati miradi iliyopo katika maeneo mbalimbali nchini; kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi ya mabwawa na skimu za umwagiliaji; kufanya utafiti wa teknolojia za umwagiliaji zinazotumia maji kwa ufanisi; na kuwajengea uwezo Wataalam na Wakulima Wadogo. Lengo la Serikali ni kuongeza eneo la umwagiliaji kufikia **hekta 1,000,000** ifikapo mwaka 2020.

## 4.6 TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

### 4.6.1 Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Maji

**168. Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Maji (*National Water Investment Fund - NWIF*) ni taasisi yenye jukumu la kukusanya mapato, kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji na kufuatilia matumizi yake. Mfuko huo umeanzishwa chini ya Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira **Na. 12** ya mwaka 2009 (Kifungu 44(1)) kwa lengo la kusaidia uwekezaji (*Provisions of "investment support"*) kwenye miradi ya utoaji wa huduma ya maji na usimamizi wa maeneo ya vyanzo na vidakio vya maji, kipaumbele ikiwa ni kwenye maeneo yenye uhaba mkubwa wa huduma ya maji hususan maji vijijini.

**169. Mheshimiwa Spika**, Sheria **Na. 12** ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009 inaeleza kuwa vyanzo vya mapato vya Mfuko ni fedha zitakazoidhinishwa na Bunge, misaada pamoja na fedha nyingine zitakazolipwa kwenye Mfuko kwa mujibu wa Sheria nyingine. Hadi sasa, chanzo pekee cha mapato ya Mfuko ni tozo ya **Shilingi 50** kwa kila lita ya mafuta ya dizeli na **Shilingi 50** kwa kila lita ya mafuta ya petroli.

**170. Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu, Wizara ilikuwa inakabiliwa na madeni makubwa ya Wakandarasi wa miradi ya maji. Hali hiyo ilichangia miradi mingi kutokamilika kwa wakati na hata baadhi ya wakandarasi kuondoka katika maeneo ya miradi. Kuanzishwa kwa Mfuko huo kumesaidia ulipaji wa madeni ya Wakandarasi na kuharakisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji nchini. Hadi mwezi Machi 2017, Mfuko umepokea jumla ya **Shilingi bilioni 95.5** kutoka katika tozo ya mafuta. Fedha hizo zimetumwa katika Halmashauri **99** kwa ajili ya kuwalipa Wakandarasi na Wataalam Washauri wa miradi; na Mamlaka **17** za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa ajili ya upanuzi wa miundombinu ya maji katika maeneo ya pembezoni mwa miji husika. Malipo hayo yameleta mafanikio makubwa katika kuhakikisha miradi ya maji inakamilika na wananchi wanapata huduma ya maji

pamoja na kuondokana na kero ya uhaba wa maji ambayo ni kilio kikubwa nchini. ***Jedwali Na. 9(a)***, ***9(b) na 9(c)*** linaonesha Halmashauri na Mamlaka za Maji zilizopelekewa fedha za Mfuko pamoja na fedha zilizotumwa katika miradi inayosimamiwa na Wizara.

**171. Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, uwekezaji katika miradi ya maji unakabiliwa na uhaba wa fedha. Chanzo cha Shilingi 50 kwa kila lita ya petroli na Shilingi 50 kwa lita ya dizeli, hakikidhi mahitaji yaliyopo ya uwekezaji kwenye miradi ya maji kwa sasa. Kutokana na chanzo hicho, Mfuko unapata wastani wa **Shilingi bilioni 125** kwa mwaka wakati mahitaji ya fedha za uwekezaji wa miradi mipya ya maji vijijini kwa mwaka ni **Shilingi bilioni 354**. Kutokana na hali hiyo, kuna umuhimu wa kuongeza wigo wa mapato ya Mfuko ili kuendelea kuboresha zaidi huduma ya maji nchini.

### 4.6.2 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*EWURA*)

**172. Mheshimiwa Spika,** *EWURA* inatekeleza majukumu yake kulingana na Kifungu **Na. 414** cha Sheria **Na.11** ya *EWURA* ya mwaka 2001. Sheria hiyo inaitaka *EWURA* kudhibiti utoaji wa huduma kwenye Sekta za Maji na Nishati katika maeneo ya maji na usafi wa mazingira, umeme, mafuta ya petroli pamoja na gesi asilia. Majukumu ya *EWURA* ni pamoja na kutoa leseni, kusimamia utekelezaji wa masharti ya leseni, kudhibiti ubora na ufanisi wa utoaji huduma, kutathmini na kupitisha bei za huduma na kutatua migogoro baina ya watoa huduma na wateja wao. Katika mwaka 2016/2017, kwa upande wa Sekta ya Maji, *EWURA* imeendelea na udhibiti wa huduma za upatikanaji wa majisafi na usafi wa mazingira katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini.

**173. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, *EWURA* ilitathmini na kuidhinisha bei mpya za huduma za maji kwa Mamlaka **12** kati ya maombi **19** yaliyopokelewa. Mamlaka zilizoidhinishiwa bei ni Songe, Utete, Korogwe, Pangani, Liwale, Ruangwa, *MANAWASA*, Kilwa Masoko, Igunga,

Kisarawe, Morogoro (*Water Tankers*) na Mwanga. Tathmini ya maombi ya bei inaendelea kwa Mamlaka **tano (5)** za Katesh, Biharamulo, Sumbawanga, Makambako na Kibaya. Maombi ya bei ya Mamlaka mbili za Mwanza kuhusu usafi wa mazingira na Mamlaka ya Kishapu kuhusu majisafi yalirudishwa kwa Mamlaka husika ili kuwasilisha taarifa zaidi zitakazokidhi haja ya maombi yao. Aidha, *EWURA* ilipokea rasimu za mikataba ya huduma kwa wateja kutoka Mamlaka **25** za Majisafi na Usafi wa Mazingira na kuidhinisha Mikataba **tisa (9)** ya Mamlaka za Moshi, Mwanza, Mtwara, Tanga, Chalinze, Kilwa Masoko, Katesh, Muheza na Utete. Vilevile, *EWURA* ilikagua miundombinu inayotoa huduma ya majisafi na majitaka katika Mamlaka **82** na kuzishauri kuhusu utaratibu bora wa matengenezo, ukarabati na uboreshaji wa miundombinu yao kwa huduma endelevu. *EWURA* ilipokea jumla ya malalamiko **32** yaliyohusu ankara za majisafi na majitaka zilizokosewa, ukosefu wa maji, kukatiwa huduma ya maji kimakosa na huduma hafifu kwa wateja. Kati ya malalamiko hayo, **16** yamepatiwa ufumbuzi na **16** yapo katika hatua mbalimbali za utatuzi.

**174.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, *EWURA* imetoa taarifa za utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa mwaka 2015/2016. Taarifa hizo husaidia Wizara pamoja na Wadau wa Sekta ya Maji katika kuandaa na kutekeleza mipango mbalimbali ya kuimarisha na kuboresha huduma za majisafi na usafi wa mazingira. Katika taarifa hizo Mamlaka zilionesha ufanisi katika viashiria vya ufungaji wa dira za maji, kuongezeka kwa wateja na wastani wa saa za upatikanaji wa huduma ya maji. Pamoja na mafanikio hayo, Mamlaka hizo zinakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo mahitaji makubwa ya maji kuliko kiasi cha maji kinachozalishwa, uondoaji wa majitaka, upotevu wa maji pamoja na ongezeko kubwa la madeni kwa watumiaji maji hususan kwa Taasisi za Serikali. Serikali imeendelea kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa changomoto hizo ili wananchi waweze kupata huduma endelevu na iliyo bora ya majisafi na usafi wa mazingira.

**175.** **Mheshimiwa Spika**, *EWURA* ilikuwa mwenyeji wa

Mkutano wa Mwaka wa Umoja wa Wadhibiti wa Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika *"Eastern and Southern Africa Water and Sanitation Regulators Association (ESAWAS)* inayojumuisha nchi za Kenya, Rwanda, Zambia, Msumbiji, Lesotho na Tanzania. Katika Mkutano huo mada mbalimbali zilizojikita kwenye masuala ya udhibiti wa utoaji huduma za majisafi na majitaka ziliwasilishwa. Kaulimbiu ya Mkutano ilikuwa 'Udhibiti kwa Kizazi Kijacho kwa Kushirikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu'. Aidha, *EWURA* iliendesha mafunzo kwa Mamlaka **27** za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini ambayo yalihusu uandaaji wa Mipango ya Kibiashara inayoziwezesha Mamlaka kujitathimini na kubuni mikakati na miradi ya kuboresha hali ya huduma iliyopo pamoja na kujiwekea malengo ya miaka mitatu.

**176.** **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Sekta Ndogo za Umeme, Petroli na Gesi Asilia, *EWURA* imeendelea kusimamia Sekta hizo ili kuhakikisha uwepo wa ubora na usalama wa huduma hizo kwa kuandaa kanuni na taratibu zinazovutia uwekezaji. Katika mwaka 2016/2017, *EWURA* iliidhinisha leseni **nane (8)** za kuzalisha umeme zikiwemo **tatu (3)** za muda mrefu za uzalishaji, leseni **moja (1)** ya muda mfupi ya kuzalisha umeme na leseni **nne (4)** za muda mfupi za kuzalisha umeme kwa matumizi binafsi. Vilevile, *EWURA* ilitoa leseni **462** za ufungaji mifumo ya umeme.

**177.** **Mheshimiwa Spika**, katika Sekta Ndogo ya Mafuta, hadi mwezi Machi 2017, *EWURA* ilikuwa imetoa leseni **1,245** kwa vituo vipya vya mafuta; leseni za biashara ya kuagiza kwa jumla mafuta ya petroli kwa kampuni mpya **115**; leseni **moja** (**1**) kwa kiwanda cha kusafisha mafuta ya petroli; leseni 28 za uagizaji na usambazaji wa jumla wa vilainishi (*lubricants*); leseni **saba (7)** kwa viwanda vyenye miundombinu ya mafuta kwa ajili ya matumizi binafsi; na vibali **54** vya kuruhusu ujenzi wa miundombinu mipya ya petroli. Vilevile, Mamlaka imetoa leseni kwa ajili ya uagizaji na usambazaji wa gesi ya *LPG* kwa jumla kwa kampuni **12**. Aidha, *EWURA* imeendelea kupanga bei kikomo za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa yanayouzwa kwenye vituo vya mafuta na kuendelea kupima ubora wa mafuta hayo.

Lengo ni kuhakikisha kuwa mtumiaji anauziwa mafuta yaliyo bora kwa bei ambayo siyo zaidi ya bei kikomo.

**178.** **Mheshimiwa Spika**, *EWURA* imeendelea kukagua miundombinu ya kuchakata, kusafirisha na kusambaza gesi asilia ili kubaini kuwa ni salama kwa matumizi na mazingira. Aidha, utayarishaji wa rasimu za kanuni za udhibiti na kanuni ndogo za udhibiti wa Sekta Ndogo ya Gesi Asilia umeanza baada ya kupitishwa kwa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015. Kukamilika kwa nyenzo hizo kutaisaidia *EWURA* kutoa leseni mbalimbali za uwekezaji kwenye Sekta hiyo ndogo ya Gesi Asilia.

**179.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, *EWURA* iliendelea kutunga kanuni na miongozo ya kuimarisha uelewa kwa watoa huduma na umma kuhusu nyenzo za udhibiti ikiwemo ubora na huduma inayotakiwa kutolewa na taratibu mbalimbali zinazotumika kwenye udhibiti ili kuimarisha utawala bora. Kanuni na miongozo inayoendelea kutungwa ni pamoja na Mwongozo wa kuishirikisha Sekta binafsi katika utoaji wa huduma za maji safi na uondoaji majitaka (*PPP Guidelines for Urban Water Sub-Sector*) na Mwongozo wa maunganisho mapya ya maji kwa wateja (*Guidelines on New Water Connections)*.

**180.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, *EWURA* imelenga kuimarisha udhibiti wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira nchini kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo: kushamirisha uwekezaji wa Sekta Binafsi katika Sekta za Nishati na Maji; kuanzisha na kuimarisha ofisi za *EWURA za* Kanda ambapo ofisi zilizoanzishwa hadi sasa ni za Kanda ya Kaskazini (Arusha), Kanda ya Ziwa (Mwanza), Kanda ya Kati (Dodoma) na Nyanda za Juu Kusini (Mbeya); kufuatilia utendaji wa Mamlaka za Maji Mijini kwa kuchambua na kuhakiki taarifa za utendaji kazi wa Mamlaka hizo; kufuatilia utekelezaji wa mipango ya kibiashara (*Business Plans*) ya Mamlaka kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa na *EWURA*; na kuimarisha utoaji wa elimu kwa umma kuhusu masuala ya kiudhibiti, haki na wajibu wa watumiaji wa huduma zinazotolewa na Mamlaka. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana

na *EWURA* itakamilisha Mwongozo wa Ushirikishaji wa Sekta Binafsi katika Utoaji wa Huduma za Maji ili uanze kutumika.

**181.** **Mheshimiwa Spika**, *EWURA* ni Mamlaka ya udhibiti wa Sekta kuu mbili za Maji na Nishati. Ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi, *EWURA* itaendeleza ushirikiano wa karibu kwa kupokea na kutekeleza miongozo inayotolewa na Wizara zinazosimamia Sekta hizo kulingana na Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

### 4.6.3 Chuo cha Maji

**182.** **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Maji ni Wakala unaosimamiwa na Bodi ya Ushauri ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Chuo hicho kina jukumu la kutoa na kuendeleleza wataalamu wanaohitajika katika Sekta za Maji na Umwagiliaji kwa njia ya mafunzo. Majukumu mengine ni kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa kuzingatia Sera na miongozo ya Wizara pamoja na Baraza la Taifa la Vyuo vya Ufundi (*NACTE*).

**183.** **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Maji hutoa mafunzo katika fani **tano (5)** kwa ngazi ya Stashahada na fani **moja (1)** katika ngazi ya Shahada. Fani zitolewazo katika ngazi ya Stashahada ni Uhandisi wa Maji na Usafi wa Mazingira (*Water Supply and Sanitation Engineering*), Haidrolojia na Hali ya hewa (*Hydrology and Meteorology*), Haidrojiolojia na Uchimbaji wa Visima (*Hydrogeology and Water Well Drilling*), Uhandisi wa Umwagiliaji (*Irrigation Engineering*), pamoja na Teknolojia ya maabara na ubora wa maji (*Water Quality Laboratory Technology*). Katika ngazi ya Shahada, Chuo hutoa shahada katika fani ya Uhandisi wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji (*Bachelor of Engineering in Water Resources and Irrigation Engineering*). Vilevile, Chuo kinatoa mafunzo ya muda mfupi kulingana na mahitaji ya wadau kwenye Sekta za Maji na Umwagiliaji.

**184.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Chuo kilidahili wanafunzi **707** wa stashahada ya fani mbalimbali kwa ajili ya mafundi sanifu kwa Sekta ya Maji (*water*

*technicians*) na wanafunzi **241** wa shahada ya kwanza ya Uhandisi wa Rasilimali za Maji na Umwagiliaji (*Bachelor of Engineering in Water Resources and Irrigation Engineering*) na kufanya jumla ya wanafunzi wote Chuoni kuwa **1,849**. Kati ya hao, wanafunzi **1,292** wako katika mafunzo ya ngazi ya Stashahada na wanafunzi **557** ni wa ngazi ya Shahada. Vilevile, jumla ya wanafunzi **313** wa Stashahada walihitimu mafunzo yao. Chuo kimekuwa kikiongeza udahili wa wanafunzi na idadi ya wahitimu mwaka hadi mwaka kama inavyooneshwa kwenye ***Jedwali Na. 10*** na ***Jedwali Na. 11***.

**185.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa idadi ya wanafunzi wa kike kwenye fani za sayansi inaongezeka, Mamlaka ya Elimu Tanzania (*TEA*) ilifadhili wanafunzi wa kike **120** katika kozi ya kuwawezesha kujiunga na masomo ya Stashahada (*pre-entry course*). Vilevile, Mfuko wa Mafundi Sanifu (*Water Technicians Fund*) ulifadhili jumla ya wanafunzi **252** na kati yao wanafunzi **97** ni wanafunzi wa kike. Juhudi hizo zimewezesha ongezeko la udahili wa wanafunzi wa kike Chuoni kutoka **342** mwaka 2015/2016 hadi kufikia **489** sawa na **asilimia 26** ya wanafunzi wote mwaka 2016/2017.

**186.** **Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Machi 2017, Chuo kina watumishi **91** kati yao **60** ni wakufunzi na **31** ni wafanyakazi katika maeneo ya uendeshaji na utawala. Katika kuongeza ufanisi wa utendaji wa Chuo, watumishi wameendelezwa kimasomo ambapo jumla ya watumishi **21** wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu. Kati ya hao watumishi **11** wako katika mafunzo ya Shahada ya Uzamivu (*PhD*), watumishi **saba (7)** ni wa Shahada ya Uzamili (*Masters*) na watumishi **watatu (3)** wapo katika mafunzo ya Shahada. Vilevile, watumishi **22** wakiwemo wajumbe wa Bodi ya Zabuni na wakuu wa idara walipatiwa mafunzo ya muda mfupi kuhusu Sheria ya Manunuzi ya Umma. Orodha ya watumishi wa Chuo imeainishwa katika ***Jedwali Na. 12****.*

**187.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Chuo kimelenga kudahili wanafunzi **900**, kukarabati majengo, kuongeza vifaa vya kufundishia katika maabara na vitabu pamoja na kuwajengea uwezo watumishi kupitia mafunzo

ya muda mrefu na mfupi. Vilevile, Chuo kitakamilisha utafiti wa upotevu wa maji kwenye Mamlaka za Maji za Miji Mikuu ya Mikoa (*non- revenue water for regional water utilities*) na uendelevu wa miradi ya maji vijijini (*sustainability of rural water supply services*) katika Mikoa yote nchini.

### 4.6.4 Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (*DDCA*)

**188.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa iliendelea kutafiti maji chini ya ardhi, kuchimba visima na kujenga mabwawa katika maeneo mbalimbali nchini. Hadi mwezi Machi 2017, Wakala umefanya uchunguzi wa maji chini ya ardhi kwenye maeneo **324** kwa ajili ya uchimbaji wa visima, umechimba jumla ya visima virefu **272**, kufanya ukarabati wa visima **57** na kufunga pampu za mkono na umeme jumla **35** kwa ajili ya kusukuma maji. ***Jedwali Na. 13*** linaonesha orodha ya visima vilivyochimbwa hadi mwezi Machi, 2017.

**189.** **Mheshimiwa Spika**, Wakala umekamilisha ujenzi wa mabwawa **matatu (3)** ya ujazo wa kati kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo. Mabwawa hayo ni Sekeididi lililopo Wilayani Kishapu Mkoani Shinyanga, Habiya **(**Itilima, Mkoa wa Simiyu) na Kwamaligwa lililopo Wilaya ya Kilindi katika Mkoa wa Tanga. Vilevile, Wakala umekamilisha ujenzi wa bwawa dogo la *Buyuni Reddo Farm* kwa ajili ya matumizi ya mifugo na Umwagiliaji katika Wilaya ya Bagamoyo. Kazi zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa bwawa la Matwiga kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo lilipo Wilaya ya Chunya Mkoa wa Mbeya ambao umefikia **asilimia 93**; usanifu wa Bwawa la *Olutakule Ngorongoro Conservation Area* kwa ajili ya wanyama; kufanya uchunguzi wa udongo kwenye maeneo **16** kwa ajili ya ujenzi; kujenga mfumo wa kusambaza maji kwenye maeneo **mawili (2)** ya Kijiji cha Lepampule kilichopo Wilaya ya Kiteto na Kambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania iliyopo Gongo la Mboto katika Manispaa ya Ilala; pamoja na kupima ubora wa mabomba kwa ajili ya miradi **13** ya maji kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*).

**190. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa umepanga kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi kwenye maeneo mbalimbali **300** nchini, kuchimba visima virefu **400**, kukarabati visima **50**, kufunga pampu za maji **35**, kujenga bwawa **moja (1)** la ujazo wa kati na bwawa dogo **moja (1)**, kukarabati mabwawa **manne (4)** ya ujazo wa kati, kujenga mifumo midogo ya kusambaza maji na kufanya uchunguzi wa udongo kwa ajili ya kazi za ujenzi kwenye maeneo **20**. Wakala unatarajia kukusanya jumla ya S**hilingi bilioni 14.05** ikiwa ni mapato yatokanayo na kazi hizo.

### 4.6.5 Bohari Kuu ya Maji

**191. Mheshimiwa Spika**, Bohari Kuu ya Maji imeendelea kuwa msimamizi wa ubora wa nyenzo na msambazaji wa vifaa vya maji nchini *'Centre of exellence'* na kuhakikisha vifaa hivyo vinawafikia watekelezaji wa miradi ya maji kwa wakati. Katika mwaka 2016/2017, Bohari ya Maji imeweza kusambaza mabomba ya urefu wa **kilomita 200,000**, dira za maji **90,000** pamoja na viungio mbalimbali kwenye miradi ya maji inayotekelezwa katika Mamlaka za Maji za Babati, Chalinze, Tanga, Dodoma, Makonde, Igunga, Kigoma, Morogoro, Tanga, Lindi, Mtwara, Njombe, Karatu, Maswa, Ikwiriri, Bukoba, Mugumu, Iringa Arusha, Ulanga, Longido, Bunda, *DAWASA* na *DAWASCO* na kwenye Halmashauri za Wilaya mbalimbali nchini.

**192. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Bohari imeanza kushirikiana na wadau mbalimbali kutoka sekta binafsi katika kutekeleza Sera ya Ubia baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma (*Public Private Partnership – PPP*) kwa lengo la kuboresha utoaji huduma na hivyo kupunguza utegemezi kwa Serikali Kuu. Katika mwaka 2017/2018, Bohari inatarajia kuendelea na kutafuta vifaa vya maji vyenye ubora na unafuu wa bei ili kuvisambaza vifaa hivyo kwenye miradi ya maji inayoendelea kujengwa kwenye maeneo mbalimbali nchini.

## 4.7 MASUALA MTAMBUKA

### 4.7.1 Sheria

**193.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutoa elimu ya Sheria mbalimbali za nchi zinazohusiana na masuala ya Sekta za Maji na Umwagiliaji kwa Halmashauri, Bodi za Maji za Mabonde, Mamlaka za Maji na Wadau wengine nchini. Elimu hiyo ilitolewa kupitia warsha, mikutano, semina, mafunzo, makongamano na vyombo vya habari.

**194.** **Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Machi 2017, Wizara imekamilisha kuandaa Oda **sita (6)** za kutangaza mabonde madogo chini ya Sheria **Na. 11** ya mwaka 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji kwenye Gazeti la Serikali. Mabonde madogo yaliyotangazwa kwenye Oda hizo ni Mto Mara (Tangazo la Serikali Na. 127 la tarehe 22/04/2016); Somoche (Tangazo la Serikali Na. 131 la tarehe 22/04/2016); Tobora (Tangazo la Serikali Na. 134 la tarehe 22/04/2016); Mkondoa (Tangazo la Serikali Na. 235 la tarehe 05/08/2016); na Wami (Tangazo la Serikali Na. 240 la tarehe 05/08/2016). Vilevile, Oda ya kutangaza bonde dogo la Ngerengere ipo katika hatua ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

**195.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha kuandaa Notisi **tisa (9)** za kutangaza maeneo ya hifadhi ya vyanzo vya maji chini ya Sheria **Na. 11** ya mwaka 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji kwenye Gazeti la Serikali. Maeneo ya hifadhi ya vyanzo vya maji yaliyotangazwa kupitia Notisi hizo ni: Bwawa la Mindu (Tangazo la Serikali Na. 221 la tarehe 22/07/2016); Mto Halewa/Swaya (Tangazo la Serikali Na. 231 la tarehe 05/08/2016); Mto Hanzya (Tangazo la Serikali Na. 234 la tarehe 05/08/2016); Mto Imeta (Tangazo la Serikali Na. 230 la tarehe 05/08/2016); Mto Ivumwe (Tangazo la Serikali Na. 236 la tarehe 05/08/2016); Mto Mfwizimo eneo la Iziwa (Tangazo la Serikali Na. 241 la tarehe 05/08/2016); Mto Mfwizimo eneo la Lunji (Tangazo la Serikali Na. 232 la tarehe 05/08/2016); Mto Nzovwe (Tangazo la Serikali Na. 233 la tarehe 05/08/2016); na Mto Sisimba (Tangazo la Serikali Na. 239 la tarehe 05/08/2016).

**196.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha kutangaza Notisi ya kuziunganisha Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira za Vwawa na Mlowo katika Gazeti la Serikali (Tangazo la Serikali Na. 326 la tarehe 23/12/2016) na kuwa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Vwawa-Mlowo. Vilevile, Kanuni **tatu (3)** za Uanzishaji wa Maabara za Ubora wa Maji; Ubora wa Visima vya Maji; na Mfumo wa Kuainisha Rasilimali za Maji katika Madaraja kulingana na ubora wake zimetayarishwa na zinaendelea kuboreshwa kabla ya hatua ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali na kuanza kutumika.

**197.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara ilifanya vikao vya wadau mwezi Oktoba na Desemba, 2016 na kupokea maoni, ushauri na mapendekezo ya wadau kuhusu Kanuni **saba (7)** ambazo ni *The Water Resources Management (Transfer of water use, discharge and groundwater permits) Regulations, 2017; The Water Resources Management (Control and Management of Storm Water) Regulations, 2017; The Water Supply and Sanitation (Provision and Management of Sewage and Waste Water Services) Regulations, 2017; Water Supply and Sanitation (Water Bowsers) Regulations, 2017; Water Supply and Sanitation (Licensing Board) Regulations, 2017; DAWASA (Water Bowsers) Regulations, 2017;* na *Water Supply and Sanitation (Delegation of Powers to Local Government Authorities) Regulations, 2017.* Rasimu za Kanuni hizo zimeboreshwa na zitawasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili ziweze kupitiwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

**198.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Wizara yangu imeendelea kukusanya maoni, ushauri na mapendekezo ya wadau kuhusu marekebisho ya Sheria **Na. 11** ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya mwaka 2009, Sheria **Na. 12** ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009, Sheria **Na. 20** ya DAWASA ya mwaka 2001 na Sheria **Na. 4** ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2013. Vikao vya Wataalam na Wadau vilifanyika mwezi Novemba na Desemba, 2016 ambapo maoni, ushauri na mapendekezo yalikusanywa na kufanyiwa kazi. Rasimu za mapendekezo ya kurekebisha Sheria hizo zipo katika hatua ya kuwasilishwa

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya mapitio na ushauri wa kisheria.

**199.** **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara yangu imeendelea kujadiliana na kutayarisha Mikataba na Randama za Makubaliano ambayo Wizara ya Maji na Umwagiliaji ni sehemu (*party*) ya makubaliano hayo. Mikataba hiyo ni pamoja na Mikataba ya Kimataifa inayohusiana na usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji (*Conventions and Protocols*) ambayo nchi yetu inashirikiana na nchi nyingine. Jumla ya Mikataba na Randama za Makubaliano **151** zimepitiwa na kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya mapitio na ushauri wa kisheria. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefuatilia na kusimamia mashauri **23** yaliyopo mahakamani ambapo mashauri **matano (5)** kati ya hayo yametolewa uamuzi.

**200.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara yangu itaendelea na utayarishaji wa Kanuni za Sheria zinazohusiana na Sekta za Maji na Umwagiliaji kulingana na uhitaji pamoja na kukamilisha utafiti utakaosaidia katika maandalizi ya Kanuni hizo. Vilevile, Wizara itaendelea kukamilisha mapendekezo ya kurekebisha Sheria za Maji ambazo ni Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, Sheria ya *DAWASA* na Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji pamoja na kutoa ushauri wa kisheria kwa wadau wa Sekta ya Maji na Umwagiliaji katika utekelezaji wake.

### 4.7.2 Habari, Elimu na Mawasiliano

**201.** **Mheshimiwa Spika**, elimu kwa umma na taarifa kuhusu maendeleo ya Sekta za Maji na Umwagiliaji ni muhimu kwa jamii kama njia mojawapo ya kujenga uelewa wao katika masuala yanayohusu Sekta hizo. Katika mwaka 2016/2017, Wizara imetoa elimu kwa wananchi kuhusu usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, huduma za maji na usafi wa mazingira vijijini na mijini pamoja na uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji nchini. Elimu hiyo imetolewa kupitia warsha,

tovuti na vyombo vya habari na maonesho mbalimbali yakiwemo Maonesho ya Kilimo ya Nanenane yaliyofanyika Mkoani Lindi mwezi Agosti, 2016. Katika maonesho hayo, vipeperushi, majarida na machapisho mbalimbali yanayohusu kazi zinazotekelezwa na majukumu ya Sekta za Maji na Umwagiliaji vilitolewa. Vilevile, elimu ya Sera ya Maji kwa lugha nyepesi ilitolewa kwa wananchi kupitia majarida na santuri za maigizo ili waifahamu kwa urahisi mipango na mikakati ya Sekta.

**202. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia vyombo mbalimbali vya habari imeendelea kuandaa vipindi mubashara vya ana kwa ana ambavyo vimekuwa vikihudhuriwa na Viongozi wa Serikali pamoja na Wataalam wa Wizara kuwaeleza wananchi kazi mbalimbali zinazotekelezwa na Sekta za Maji na Umwagiliaji. Vipindi hivyo vilirushwa kupitia vituo vya runinga na redio. Vilevile, kupitia vituo hivyo, Wizara ilirusha vipindi maalum kuhusu taarifa za miradi ya maji na umwagiliaji pamoja na maendeleo ya hali ya Sekta za Maji na Umwagiliaji nchini. Aidha, Wizara imeendelea kutumia teknolojia mpya ya mawasiliano kupitia tovuti na mitandao ya kijamii kuwasiliana na wananchi, kupokea kero za wananchi, kuonesha kazi, majukumu na matukio mbalimbali yanayohusu Wizara.

### 4.7.3 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

**203. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano ili kuboresha utendaji kazi katika Sekta za Maji na Umwagiliaji. Katika mwaka 2016/2017, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuandaa rasimu ya Sera ya TEHAMA ya Wizara (*Draft Institutional ICT Policy*); kutumia Mfumo wa Takwimu Huria (*Open Data System*) kwa ajili ya utoaji wa takwimu na taarifa za huduma za Sekta ya Maji; kuboresha na kuoanisha mifumo ya kieletroniki inayotekelezwa ndani ya Sekta ya Maji; na kutoa mafunzo kwa watumishi wa Taasisi zinazotekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ili waweze kutumia vifaa na mifumo ya kielektroniki iliyopo.

**204.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira zinaboresha utendaji na ukusanyaji wa mapato yanayotokana na ankara za maji kwa kutumia vifaa na mifumo ya kieletroniki ili kurahisisha ukusanyaji wa taarifa za wateja na kubaini wateja wanaokwepa kulipia huduma za maji kwenye Mamlaka husika. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo imeanza kuandaa mfumo wa kielektroniki wa utunzaji na ufuatiliaji wa taarifa za rasilimali za Maji na watumiaji (*Electronic Water Register*) ili kurahisisha usimamizi wa rasilimali za maji kwenye Bodi za Maji za Mabonde kote nchini.

**205.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kuboresha mfumo wa kielektroniki wa habari na mawasiliano ikiwa ni pamoja na kuiunganisha Wizara na Taasisi zake kupitia miundombinu ya Serikali Mtandao; kuendelea kutumia Mfumo wa Takwimu Huria ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa na takwimu kwa wananchi na wadau wengine kwa wakati; na kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa utunzaji na ufuatiliaji wa mafaili na majalada.

### 4.7.4 Manunuzi

**206.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara inasimamia utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma kwa misingi ya uwazi, uwajibikaji, pamoja na matumizi mazuri ya fedha za umma. Kwa mujibu wa Sheria **Na. 7** ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011, Kanuni zake za mwaka 2013 na Marekebisho ya mwaka 2016, Taasisi za Umma zinatakiwa kuhakikisha huduma inayopatikana inalingana na thamani ya fedha zinazotolewa (*value for money*). Hadi mwezi Machi 2017, kazi zilizotekelezwa ni uandaaji wa Mpango wa Manunuzi wa Wizara na kuoanisha na miradi itakayotekelezwa kwa kipindi cha mwaka mzima (*Annual Procurement Plan*), nyaraka za zabuni, kuratibu uandaaji wa Hadidu za Rejea (*Terms of references)* kwa ajili ya kupata wataalam washauri, wakandarasi na watoa huduma.

**207.** **Mheshimiwa Spika**, katika Mpango wa Manunuzi wa

mwaka 2016/2017, Wizara ilipanga kutangaza jumla ya miradi ya maji **141** kwenye maeneo mbalimbali nchini. Hadi mwezi Machi 2017, jumla ya miradi **78** imetangazwa na kati ya miradi hiyo mikataba **15** imesainiwa. Katika mwaka 2017/ 2018, Wizara itaendelea na taratibu za kutangaza miradi ya maji, kutoa huduma za ushauri wa kitaalam katika masuala ya manunuzi pamoja na kuandaa mpango wa manunuzi kwa mwaka 2017/2018.

### 4.7.5 Jinsia

**208.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu zinazoelekeza uwiano wa jinsia wa hamsini kwa hamsini. Kwa kuzingatia maelekezo hayo, watumishi hususan wanawake wamehamasishwa kushiriki katika fursa mbalimbali zinazojitokeza zikiwemo nafasi za uongozi, lengo likiwa ni uwepo wa uwiano wa kijinsia baina ya wanawake na wanaume kwenye maeneo ya vyombo vya maamuzi katika usimamizi, uendeshaji na utekelezaji wa miradi ya maji na umwagiliaji nchini. Vilevile, Wizara inazingatia suala la kurithishana madaraka (*succession plan*) kwa kuangalia sifa za miundo na kuweka kipaumbele hususan kwa wanawake wenye sifa, elimu na weledi.

### 4.7.6 UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY)

**209.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea na juhudi mbalimbali za kukabiliana na janga la ugonjwa wa UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) mahala pa kazi. Juhudi hizo ni pamoja na kusambaza mwongozo wa magonjwa hayo uliotolewa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kuzingatia Waraka unaoweka wazi huduma zinazotakiwa kwa watumishi wanaoishi na VVU kwa kuzingatia kiwango cha msaada unaohitajika kwa waathirika ikiwemo kuwapatia fedha kwa ajili ya lishe bora na usafiri pamoja na kuwapunguzia uzito wa kazi. Vilevile, katika kuzingatia agizo la Serikali kuhusu kujikinga na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa, Wizara imehamasisha watumishi kushiriki

mazoezi ya viungo kila Jumamosi ya pili ya mwezi kwa lengo la kupunguza magonjwa ya kisukari, kiharusi, shinikizo la damu, uzito uliozidi na kansa.

### 4.7.7 Maendeleo ya Rasilimali Watu

**210.** **Mheshimiwa Spika**, upungufu wa Wataalam katika Sekta za Maji na Umwagiliaji ni mojawapo ya changamoto katika usimamizi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa nchini. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imepata kibali cha kuajiri wataalam **243** wa Sekta ya Maji mwezi Desemba, 2016 ambapo kati ya wataalam hao, Wahandisi ni **63**, mafundi sanifu **172** na mafundi sanifu wasaidizi **nane (8)**. Watumishi hao wanatarajiwa kuajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi kwenye Ofisi za Mikoa na Halmashauri, Bodi za Maji za Mabonde, Miradi ya Kitaifa, Mamlaka za Maji na wengine kubaki Makao Makuu ya Wizara.

**211.** **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi. Katika mwaka 2016/2017, jumla ya watumishi **51** wamegharamiwa mafunzo mbalimbali yakiwemo ngazi ya Stashahada watumishi **saba (7)**, Shahada **(11)**, Uzamili **(27)**, Uzamivu **wawili (2)** pamoja na Watumishi **wanne (4)** ambao wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi yaliyofanyika ndani ya nchi. Katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watumishi ili kuongeza ufanisi na waledi wa kutekeleza majukumu yao.

### 4.7.8 Mapambano Dhidi ya Rushwa

**212.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaloelekeza kila Wizara, Idara na Taasisi zote za Serikali kuwa na simu za kupokea hoja za wananchi na kuzijibu papo kwa papo. Wizara imeanzisha simu za moja kwa moja (*helpline:* ***+255 22 2452068****;* ***+255 22 2450699****)* ambazo hazitozi malipo pamoja na kuboresha tovuti kwa ajili ya kupokea malalamiko ya wateja. Katika

mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea na mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa kwenye maeneo yote ya kazi. Katika kutekeleza harakati hizo, malalamiko mbalimbali yalipokelewa kwenye Dawati la Malalamiko na kupatiwa ufumbuzi. Vilevile, Mkataba wa Huduma kwa Mteja umeandaliwa kwa Mujibu wa Hati ya Rais ya Mgawanyo wa Majukumu ya mwezi Aprili 2016, kwa kuzingatia hali halisi ya mahitaji ya wateja na maendeleo ya Sekta katika kutoa huduma na kupunguza mianya ya rushwa.

### 4.7.9 Ujenzi wa Ofisi za Wizara

**213.** **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza maelekezo ya **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, **Mheshimiwa Daktari John Pombe Joseph Magufuli** ya kuitaka Serikali kuhakikisha inahamishia shughuli zake Mjini Dodoma, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tarehe 27.02.2017, Wizara ya Maji na Umwagiliaji imehamia rasmi Dodoma. Kufuatia zoezi hilo, Wizara itafanya ukarabati wa jengo la Wizara lililopo eneo la Mlimani Kitalu Na. 487. Wizara ilikuwa inaendelea na mradi wa ujenzi wa Ofisi zake (*Maji House*) katika Jiji la Dar es Salaam na hadi mwezi Machi 2017, ujenzi umefikia ghorofa ya 14 ambayo ni ya mwisho. Wizara imeanza utaratibu wa kuangalia uwezekano wa jengo hilo kutumiwa na Taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo hazitahamia Dodoma kutokana na majukumu yake kuwa na uhitaji wa Ofisi katika Jiji la Dar es Salaam.

### 4.7.10 Uratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji

**214.** **Mheshimiwa Spika**, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*Water Sector Development Program- WSDP),* ilianzishwa kwa ajili ya kutekeleza Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002. Programu hiyo imepangwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka 20 kuanzia mwaka 2006 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2025. Utekelezaji wa Programu hiyo umezingatia ushirikishwaji zaidi wa wadau mbalimbali katika kuibua, kujenga, kuendeleza, kuendesha na kusimamia miradi ya maji nchini kwa lengo la kuhakikisha kuwa miradi hiyo

inakuwa endelevu. Ushirikishwaji huo umelenga kurahisisha utekelezaji na kuondoa dhana iliyokuwa imejengeka miongoni mwa wananchi wengi kuwa miradi ya maji ni mali ya Serikali na hivyo ujenzi, ukarabati, uendeshaji na utunzaji wa miradi ni jukumu la Serikali.

**215.** **Mheshimiwa Spika**, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ni ya kwanza kwa ukubwa ukilinganisha na programu za aina yake zinazotekelezwa katika nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara kutokana na muundo wake unaohusisha idadi kubwa ya wadau katika utekelezaji. Wadau wa programu hiyo ni pamoja na Halmashauri za Wilaya zote nchini, Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Wizara za TAMISEMI; Afya, Jinsia, Wazee na Watoto; Fedha na Mipango; Elimu, Sayansi na Mafunzo ya Ufundi Stadi; Taasisi zisizo za kiserikali, na Wadau wa Maendeleo. Wizara yangu inalo jukumu la uratibu wa wadau wote katika utekelezaji wa Programu kwa kuzingatia miongozo mbalimbali inayoongoza programu kama vile Dira ya Taifa ya Maendeleo (*Tanzania Development vision 2025*), Malengo ya Maendeleo Endelevu, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Sera ya Maji ya Mwaka 2002 na Makubaliano ya Utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kati ya Serikali na Wadau wa Maendeleo. Kwa nafasi hiyo kama Mratibu, Wizara yangu ina jukumu la kutoa takwimu sahihi zinazohusu utekelezaji wa Programu.

**216.** **Mheshimiwa Spika**, katika Hotuba yangu ya Bajeti ya Mwaka 2016/2017, nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Awamu ya Kwanza ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ilikamilika mwezi Desemba, 2015 na kueleza mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho. Hata hivyo, vikao mbalimbali vya Wadau wa Programu vilivyofanyika kupitia na kutathmini hali ya utekelezaji wa Programu kwa kipindi chote cha awamu ya kwanza, Wadau hao walikubaliana kuwa muda wa utekelezaji wa awamu hiyo uongezwe hadi mwezi Juni, 2016. Lengo la makubaliano hayo lilikuwa ni kutoa muda zaidi kukamilisha miradi iliyokuwa ikitekelezwa katika awamu ya kwanza pamoja na kuoanisha mwaka wa Kiserikali na muda wa kuanza kwa Awamu ya Pili ya

Programu. Ongezeko hilo la muda limesababisha mabadiliko ya baadhi ya takwimu za utekelezaji zikiwemo fedha zilizotumika na miradi iliyokamilika kufikia mwezi Juni, 2016.

**217.** **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha awamu ya kwanza ya Programu (mwezi Julai, 2007 hadi mwezi Juni 2016), mafanikio ya utekelezaji kwa upande wa Programu Ndogo ya Rasilimali za Maji ni pamoja na kuanzishwa kwa **Bodi ya Taifa ya Maji**; kuandaliwa kwa Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji kwa Mabonde **sita (6)**; kutangaza maeneo **17** ya vyanzo vya maji kuwa tengefu; kutoa vibali **4,779** vya matumizi ya maji; kuzijengea uwezo maabara za maji nchini; na Bunge kuridhia Mikataba mikubwa **mitatu (3)** ya Kimataifa kuhusu usimamizi endelevu wa rasilimali za majishirikishi. Mikataba hiyo ni ya Matumizi ya Maji ya Mto Nile, Mkataba wa Bonde la Mto Ruvuma, na Mkataba wa nchi zilizopo katika Bonde la Mto Zambezi (*ZAMCOM*).

**218.** **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa uboreshaji wa huduma za maji vijijini, jumla ya miradi **1,210** kati ya **1,810** iliyopangwa kutekelezwa ilikamilika katika Awamu ya Kwanza; vituo **50,995** vya kuchotea maji vimejengwa katika vijiji **1,677** ikilinganisha na vituo **41,900** vilivyopangwa na hivyo kuongeza idadi ya watu **6,707,506** wanaoishi vijijini kupata huduma ya maji safi. Kutokana na ongezeko hilo, idadi ya watu wanaopata huduma ya maji safi maeneo ya vijijini imefikia **22,792,322** sawa na **asilimia 72** ya watu **31,623,999** waishio vijijini kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012.

**219.** **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa huduma za maji mijini, upatikanaji wa huduma ya maji safi katika Miji Mikuu ya Mikoa uliongezeka kutoka **asilimia 80** mwezi Julai, 2007 hadi **asilimia 86** mwezi Juni, 2016. Ongezeko hilo limetokana na kukamilika kwa miradi **47** ya maji mijini. Kwa Jiji la Dar es Salaam, upatikanaji wa huduma ya maji umeongezeka kutoka **asilimia 55** hadi **asilimia 72**. Vilevile, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa upatikanaji wa huduma ya maji umeongezeka kutoka

**asilimia 41** hadi **asilimia 60**. Kwa upande wa huduma ya uondoaji majitaka katika baadhi ya Miji Mikuu ya Mikoa, maunganisho mapya **16,573** yamefanyika na kuongeza idadi ya maunganisho ya majitaka kufikia **44,220** ambapo upatikanaji wa huduma ya uondoaji majitaka imefikia wastani wa **asilimia 20** ya wakazi wa mijini.

**220.** **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hicho cha awamu ya kwanza ya Programu, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; na Wizara ya Elimu, Sayansi na Mafunzo ya Ufundi Stadi imetekeleza Kampeni ya Kuhamasisha Usafi wa Mazingira Kitaifa (*National Sanitation Campaign*). Kampeni hiyo imewezesha kujengwa kwa vyoo **1,662,550** kwenye kaya ikilinganisha na vyoo **1,520,000** vilivyopangwa kujengwa; na kujenga sehemu **1,029,404** za kunawia mikono baada ya kutoka chooni katika shule mbalimbali pamoja na maeneo mengine ikiwa ni sawa na **asilimia 67.7** ya malengo. Kampeni hiyo imesaidia Serikali kuepuka gharama kubwa za kuwatibu wananchi waliokuwa kwenye hatari ya kupata magonjwa ya mlipuko ikiwemo kipindupindu kwa kukosa vyoo na maeneo ya kunawia mikono.

### 11.1 Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP II)

**221.** **Mheshimiwa Spika**, Awamu ya Pili ya Programu inatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwezi Julai, 2016 kwa gharama ya **Dola za Marekani bilioni 3.3** ambapo hadi sasa jumla ya **Dola za Marekani bilioni 1.59** zimeahidiwa kutolewa. Awamu hiyo imegawanywa katika maeneo matano ikilinganishwa na maeneo manne ya kiutendaji yaliyokuwepo katika awamu ya kwanza ya Programu. Maeneo hayo ni utunzaji na uendelezaji wa rasilimali za maji; huduma ya maji vijijini; huduma ya majisafi na usafi wa mazingira mijini; Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira (inayosimamiwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto); na kuzijengea uwezo taasisi zinazotekeleza Programu. Aidha, Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira imepewa mkazo kwa lengo la kuongeza

uelewa kwa wananchi katika hatua za kukabiliana na magonjwa yanayotokana na kutumia maji yasiyo salama na uchafuzi wa mazingira.

**222.** **Mheshimiwa Spika**, Awamu hiyo inatekelezwa kwenye maeneo ya kipaumbele ambayo ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Mipango Shirikishi ya Utunzaji na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji na kuanza utekelezaji wake; kukamilisha miradi ya maji vijijini na mijini ambayo haikukamilika katika awamu ya kwanza; kutekeleza miradi mipya; kuhamasisha matumizi ya vyanzo mbadala vya nishati ili kupunguza gharama za uendeshaji wa miradi ya maji; kupunguza upotevu wa maji; kusimamia mikakati na mipango ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika Sekta ya Maji Kitaifa, Kikanda na Kimataifa; kuongeza nguvu katika kampeni za usafi wa mazingira; na kuzijengea uwezo Taasisi zinazotekeleza Programu ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

**223.** **Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuongeza kasi ya utekelezaji wa Programu, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuhakikisha kuwa malengo yaliyowekwa yanatekelezwa kikamilifu na kwa wakati. Katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa awamu ya pili ya Programu ili iweze kufikia malengo ya muda mfupi na muda mrefu.

## 5.0 USHIRIKI WA SEKTA BINAFSI KATIKA SEKTA ZA MAJI NA UMWAGILIAJI

**224.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhamasisha na kuishirikisha Sekta Binafsi ili kushiriki katika kutekeleza na kuwekeza kwenye miradi ya maji na umwagiliaji nchini. Ushiriki huo unafanyika kwa Sekta Binafsi kufadhili, kuwekeza na kwa utaratibu wa ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Lengo likiwa ni kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji na kuongeza kasi ya uwekezaji katika Sekta za maji na Umwagiliaji. Kupitia uhamasishaji huo, Sekta Binafsi imejitokeza kutaka kushirikiana na Serikali ambapo makampuni **58** yameonesha nia ya kuwekeza katika Sekta

ya Maji yakiwa yametoa mapendekezo mbalimbali ya uwekezaji (*investment modalities*). Majadiliano yanaendelea kati ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Wizara ya Fedha na Mipango; na Wadau wengine wakiwemo *PPRA* kuona utaratibu utakaofaa wa kuishirikisha Sekta Binafsi kuwekeza katika Sekta za Maji na Umwagiliaji.

**225.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara inatekeleza Sera ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*National PPP Policy, 2009*) kwa kuendelea na jitihada mbalimbali za kuwezesha utekelezaji wa miradi kupitia *PPP*. Jitihada hizo ni pamoja na kuwajengea uwezo watendaji mbalimbali katika ngazi ya Wizara ili wapate uelewa wa masuala ya *PPPs*; kuanzishwa kwa Dawati la *PPPs* kwa ajili ya kuratibu miradi ya *PPPs*; kuundwa kwa Kamati Maalum ya Wizara kwa ajili ya kuchambua miradi inayoombwa kutekelezwa kwa ubia; na kuzihamasisha Mamlaka za Maji kupitia mikutano mbalimbali kuhusu umuhimu wa kushirikisha Sekta Binafsi katika utekelezaji wa miradi yao. Vilevile, Wizara kupitia *EWURA* inashirikiana na *GIZ* kuandaa Mwongozo utakaotumika na Mamlaka za Maji katika utekelezaji wa miradi kwa utaratibu wa *PPP*. Hadi mwezi Machi 2017, Mtaalam Mshauri amewasilisha rasimu ya Mwongozo huo ambao umejadiliwa na kurejeshwa kwa Mshauri ili akamilishe kazi hiyo ifikapo mwezi Juni, 2017.

**226.** **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Sekta ya Umwagiliaji, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kushirikiana na *2030 Water Resources Group (2030 WRG)* na *Financial Sector Deepening Trust (FSDT)* iliratibu na kuendesha mkutano uliojadili namna bora ya kugharamia uwekezaji katika Sekta ya Umwagiliaji kwa wadau mbalimbali wakiwemo Sekta Binafsi, Taasisi za Kibenki na Wadau wa Maendeleo. Katika mkutano huo, *2030 WRG* walionesha nia ya kufadhili uandaaji wa mkakati wa kushirikisha Sekta Binafsi katika kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji. Mkakati huo unatarajiwa kuandaliwa katika mwaka 2017/2018.

**227.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara itaendelea kuhamasisha Taasisi zilizo chini yake

kuibua miradi itakayotekelezwa kwa utaratibu wa ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Vilevile, Wizara itaendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika miradi ya maji na umwagiliaji.

## 11.3 6.0 CHANGAMOTO NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA

**228.** **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2016/2017, Wizara ya Maji na Umwagiliaji imeendelea kukabiliana na changamoto mbalimbali wakati wa utekelezaji wa majukumu yake. Changamoto hizo pamoja na hatua zinachokuliwa ni kama ifuatavyo:-

### 6.1 Upungufu wa Wataalam katika Sekta za Maji na Umwagiliaji

**229.** **Mheshimiwa Spika**, Sekta za maji na umwagiliaji nchini zimeendelea kukabiliwa na upungufu wa wataalam kutokana na Serikali kutoajiri kwa muda mrefu; baadhi ya watumishi kufariki, kustaafu na wengine kuacha kazi; uwepo wa ikama mpya ya muundo wa Sekretariati za Mikoa; na kuongezeka kwa idadi ya Mikoa na Halmashauri. Mahitaji ya Sekta za maji na umwagiliaji ni **10,287** ikilinganishwa na wataalam **2,290** waliopo kwa sasa, hivyo kuwa na upungufu wa wataalam **7,997**. Upungufu huo umesababisha usimamizi hafifu wa miradi ya maji na umwagiliaji na kusababisha baadhi ya miradi kutokuwa na ubora unaotakiwa.

**230.** **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara yangu iliendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kupata kibali cha kuajiri wataalam watakaokidhi mahitaji ya Sekta za Maji na Umwagiliaji. Katika mwaka 2016/2017, Wizara imepata kibali cha kuajiri Watalaam **243** wa Sekta ya Maji ambao watapangiwa vituo vya kazi katika ngazi ya Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya. Vilevile, kibali cha kuajiri Wataalam **40** wa Sekta ya Umwagiliaji kimetolewa. Watalaam hao watakaoajiriwa watasaidia kuongeza ufanisi

katika utekelezaji wa majukumu ya Sekta hizo kwenye maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Wizara imeendelea kuwasiliana na Taasisi mbalimbali za elimu ya juu kwa ajili ya uanzishwaji wa fani zinazohusu maji na umwagiliaji ili kuongeza idadi ya wataalam katika fani hizo.

### 6.2 Uwekezaji Mdogo katika Sekta Usiolingana na Mahitaji

**231.** **Mheshimiwa Spika**, Sekta za Maji na Umwagiliaji zinakabiliwa na uhaba wa huduma ya maji unaosababishwa na uwekezaji mdogo kwenye miundombinu ya maji na umwagiliaji ikilinganishwa na mahitaji ya kijamii na kiuchumi katika maeneo ya mijini na vijijini. Miji inakua kwa kasi kutokana na ongezeko la watu na kasi kubwa ya uwekezaji katika viwanda, biashara na ujenzi wa makazi. Vilevile, maeneo mengi ya miji mikuu ya wilaya, miji midogo na vijijini yanakua kwa kasi na idadi ya watu kuongezeka wakati huduma ya maji haitoshelezi. Sababu zilizochangia changamoto ya uwekezaji mdogo usiolingana na mahitaji ni kama ifuatavyo:-

### (a) Upatikanaji Mdogo wa Fedha Kulinganisha na Bajeti

**232.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/2017, Wizara ya Maji na Umwagiliaji ilikasimiwa jumla ya **Shilingi 950,563,467,199** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye Sekta ya Maji na Sekta ya Umwagiliaji. Hadi mwezi Machi, 2017 jumla ya **Shilingi 184,195,914,901** sawa na **asilimia 19.38** zilitolewa. Kwa upande wa Sekta ya Maji, jumla ya **Shilingi 915,193,937,771** ziliidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo **Shilingi 181,209,813,609** sawa na **asilimia 19.8** zilitolewa. Kwa Sekta ya Umwagiliaji, **Shilingi 2,986,101,292** sawa na **asilimia 8.4** zilitolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ikilinganishwa na jumla ya **Shilingi 35,369,529,428** zilizoidhinishwa. Kutokana na hali hiyo ya upatikanaji mdogo wa fedha za Bajeti, miradi mingi ya maendeleo imeshindikana kukamilika kwa wakati.

**233.** **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imeendelea kuhamasisha wadau

wengine kushiriki katika uendelezaji wa Sekta za Maji na Umwagiliaji. Vilevile, Serikali imeanzisha Mfuko wa Taifa wa Maji ambao umeendelea kugharamia utekelezaji wa miradi ya maji pamoja na kupunguza kwa kiwango kikubwa mahitaji ya fedha za kutekeleza miradi ya maji nchini.

### (b) Ushiriki Mdogo wa Sekta Binafsi katika Sekta za Maji na Umwagiliaji

**234. Mheshimiwa Spika**, ushiriki wa Sekta Binafsi umejikita zaidi katika ujenzi wa miundombinu ya maji na umwagiliaji, suala la uendeshaji na usimamizi wa miradi umebaki kwenye Mamlaka za Maji, Halmashauri na Vyombo vya Watumiaji Maji. Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuiwezesha Sekta Binafsi kuongeza ushiriki wake katika uendeshaji wa miradi ya maji vijijini na mijini kupitia Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Hatua hizo ni pamoja na kutunga Sera ya Taifa ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2009, Sheria ya Ubia ya mwaka 2010 na Kanuni zake. Pamoja na jitihada za Serikali kuweka misingi hiyo, Sekta Binafsi bado haijahamasika vya kutosha kushiriki katika uendeshaji na matengenezo ya miradi ya maji na umwagiliaji.

**235. Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto hiyo, Wizara imechukua hatua za makusudi kuhakikisha kuwa Sekta Binafsi inashiriki kikamilifu katika kubuni, kujenga, kusimamia na kuendesha miradi ya maji na umwagiliaji. Katika kutimiza azma hiyo, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo wataalam wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu yanayohusu Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika uwekezaji na hadi sasa Watumishi **watatu (3)** wamepata mafunzo hayo.

## 6.3 Kupungua kwa Rasilimali za Maji

**236. Mheshimiwa Spika**, nchi yetu imebahatika kuwa na rasilimali za maji za kutosha juu na chini ya ardhi ambazo ni pamoja na mito, maziwa, maji chini ya ardhi na maeneo oevu. Hata hivyo, mgawanyiko wa rasilimali hiyo hauko

sawa, yapo maeneo yenye rasilimali nyingi za maji na maeneo mengine yana uhaba wa rasilimali hiyo. Vilevile, rasilimali hiyo imeendelea kupungua siku hadi siku kutokana na uchafuzi wa vyanzo vya maji, uvamizi katika vyanzo vya maji kwa ajili ya shughuli za kibinadamu, matumizi holela ya maji na mabadiliko ya tabianchi. Kupungua kwa rasilimali hiyo, kumeathiri shughuli za kijamii na kiuchumi pamoja na kusababisha migogoro kwenye vyanzo vya maji.

**237.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kushirikiana na wadau wengine katika kukabiliana na changamoto zinazosababisha kupungua kwa rasilimali za maji kwa kutekeleza Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya utunzaji wa mazingira. Kupitia nyenzo hizo, Wizara imekuwa ikifanya ukaguzi wa mara kwa mara wa vyanzo vya maji, maeneo ya viwanda, migodi na mabwawa ya kutibu majitaka ili kuhakikisha vyanzo vya maji vinalindwa na kuhifadhiwa na utupaji wa majitaka unazingatia viwango vinavyotakiwa kisheria. Vilevile, inaendelea kuvitambua vyanzo vya maji, kuviwekea mipaka na kuvitangaza kuwa maeneo tengefu. Hadi sasa, jumla ya maeneo **18** yametangazwa kuwa maeneo tengefu na maeneo **55** yapo katika hatua za kutangazwa. Aidha, Wizara kupitia Bodi za Maji za Mabonde, Jumuiya za Watumia Maji, Halmashauri na wadau wengine imeendelea kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kuhusu matumizi bora ya maji ili kuzuia migogoro inayojitokeza.

**238.** **Mheshimiwa Spika**, mabadiliko ya tabianchi husababisha kutokuwepo kwa uhakika wa majira na mtawanyiko wa mvua, ukame wa muda mrefu na mafuriko ya mara kwa mara. Hali hiyo husababisha uharibifu wa miundombinu ya maji na umwagiliaji. Katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kujenga mabwawa madogo na makubwa, kuimarisha ukusanyaji wa takwimu; kutoa mafunzo kwa wataalam na kuelimisha umma; kuhamasisha utaalam asilia (*Indigenous knowledge*); kutekeleza mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji na kushirikiana na wadau mbalimbali katika

kufanya utafiti kuhusu mabadiliko ya tabianchi na namna ya kukabiliana na athari hizo.

### 6.4 Uharibifu wa Miundombinu ya Maji na Umwagiliaji

**239.** **Mheshimiwa Spika**, imejengeka tabia kwa baadhi ya wananchi ya kuharibu miundombinu ya maji na umwagiliaji ambayo inaathiri upatikanaji wa huduma ya maji safi na uondoaji wa majitaka katika jamii pamoja na huduma za uhakika za umwagiliaji kwa wakulima. Hali hiyo imesababishwa na uwepo wa hujuma kwenye miundombinu ya maji na umwagiliaji ikiwemo biashara ya chuma chakavu pamoja na wananchi kuharibu kwa makusudi miundombinu ya miradi ambayo imechelewa kukamilika.

**240.** **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hiyo, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na Serikali kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa ulinzi shirikishi katika kulinda na kutunza miundombinu ya maji na umwagiliaji kupitia vipeperushi, maonesho na maigizo kwenye shehere mbalimbali za kitaifa pamoja na vipindi kwenye luninga na radio. Vilevile, Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini, Ofisi za Kanda za Umwagiliaji na Wahandisi wa Halmashauri wameendelea kushirikiana na uongozi wa Mikoa, Jeshi la Polisi pamoja na wananchi ili kubaini wananchi wanaojihusisha na hujuma hizo na kuchukua hatua stahiki pamoja na kutoa zawadi kwa watoa taarifa. Aidha, Wizara imeendelea kuzifanyia marekebisho Sheria za Maji ili ziweze kutoa adhabu kali kwa wahujumu wa miundombinu ya maji na umwagiliaji.

### 6.5 Kiwango Kikubwa cha Upotevu wa Maji

**241.** **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka za Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa, Wilaya, Miji Midogo pamoja na miradi ya Kitaifa zimekuwa zikikabiliwa na upotevu mkubwa wa maji (*NRW*) ambao ni wastani wa **asilimia 33** ukilinganishwa na kiwango kinachokubalika Kimataifa cha **asilimia 20**. Hali hiyo inasababisha Mamlaka hizo kutofikia malengo ya makusanyo

ya maduhuli waliyojiwekea na kuathiri shughuli za uendeshaji kutokana na uhaba wa fedha. Hadi mwezi Machi 2017, Mamlaka hizo zinapoteza jumla ya **Shilingi bilioni 1.58** kwa mwezi. Kwa upande wa *DAWASCO***,** wastani wa upotevu wa maji kwa kipindi hicho ni **asilimia 38** ambayo ni sawa na **Shilingi bilioni 2.5** kwa mwezi. Upotevu huo wa maji unatokana na uchakavu wa miundombinu iliyojengwa miaka mingi iliyopita, wizi wa maji unaotokana na wateja wasiokuwa waaminifu kujipatia huduma ya maji kinyume na taratibu (*by-pass, and illegal connection*) pamoja na udanganyifu wa wateja kuchezea dira za maji ili zisitoe taarifa sahihi za matumizi ya maji.

**242.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara inachukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto ya upotevu wa maji hapa nchini. Hatua hizo ni pamoja na uwekezaji katika miundombinu ya majisafi pamoja na ukarabati wa miundombinu, kuhakikisha wateja wote wanafungiwa dira za maji, na kuzielekeza Mamlaka kuwa mikakati ya kupunguza upotevu wa maji hadi kufikia **asilimia 20**. Aidha, Serikali inaendelea kurekebisha sheria za maji ili ziweze kutoa adhabu kali kwa wezi wa maji na wahujumu wa miundombinu ya maji. Vilevile, Wizara inaangalia uwezekano wa kushirikiana na Sekta Binafsi katika kutumia teknolojia rahisi ya kudhibiti upotevu wa maji.

### 6.6 Madeni Makubwa ya Ankara za Maji kwa Taasisi za Serikali

**243.** **Mheshiwa Spika**, Mamlaka za Maji nchini zimeendelea kukabiliwa na changamoto ya malimbikizo makubwa ya madeni ya ankara za matumizi ya maji kwa baadhi ya Taasisi na Idara za Serikali ambazo zimekuwa zikipata huduma ya maji na kushindwa kulipia gharama ya huduma hiyo kwa wakati. Hali hiyo, imesababisha Mamlaka hizo kushindwa kutekeleza majukumu yao ya msingi ambayo ni uendeshaji na matengenezo ya miundombinu. Hadi mwezi Machi 2017, jumla ya madeni ya ankara za maji kwa Taasisi na Idara za Serikali yamefikia **Shilingi bilioni 39.94**.

**244.** **Mheshimiwa Spika**, katika kutatua changamoto hiyo, Wizara yangu imewasilisha Wizara ya Fedha na Mipango orodha ya madeni ya ankara za maji za Taasisi za Serikali na inaendelea kuwasiliana nayo ili kuona uwezekano wa kulipa madeni hayo moja kwa moja kwa Mamlaka za Maji husika badala ya kutuma fedha kwenye Taasisi hizo ili walipe. Vilevile, Wizara imezielekeza Mamlaka za Maji kuanza kutumia dira za maji za mfumo wa malipo kabla ya matumizi (*prepaid meters*) ili kupunguza tatizo la malimbikizo ya madeni ya matumizi ya maji kwa wateja. Hadi mwezi Machi 2017, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa imeanza kutumia dira hizo na kuonesha mafanikio makubwa. Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Miji ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Moshi, Songea na Tanga zimeanza majaribio ya kutumia dira hizo. Vilevile, Serikali imeziagiza Mamlaka za Maji Mijini kuhakikisha kuwa wateja wote wanafungiwa dira hizo za maji ifikapo mwezi Juni, 2018 ili kuwawezesha wateja kulipia huduma ya maji kadri wanavyotumia.

### 6.7 Uendelevu wa Miradi ya Maji na Skimu za Umwagiliaji

**245.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kukabiliwa na changamoto ya uendelevu wa miradi ya maji na umwagiliaji. Hali hiyo imetokana na mapungufu katika uendeshaji na matengenezo ya baadhi ya miradi ya maji na skimu za umwagiliaji; miradi kujengwa kwa kutumia teknolojia zisizoendana na mazingira ya vijijini; kipato kidogo cha watumiaji kulinganisha gharama za usimamizi, uendeshaji na matengenezo; kutopatikana kwa wakati kwa vipuri vya miradi ya maji; kasi ndogo ya uanzishwaji wa vyombo vya usimamizi wa miradi; na usimamizi hafifu wa makusanyo ya fedha za miradi. Changamoto hii imeathiri kwa kiwango kikubwa upatikanaji wa huduma ya maji safi ya uhakika na ufanisi wa skimu za umwagiliaji kwenye maeneo mengi vijijini.

**246.** **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri inaendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji na upatikanaji

wa takwimu ili kuwa na taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu hali ya miradi ya maji nchini. Vilevile, Serikali inatekeleza Mkakati wa Uendelevu wa Miradi ya Maji Vijijini *(National Rural Water Supply Sustainability Strategy)* ambao unaelekeza ushirikishwaji wa wananchi katika kusimamia na kuendesha miradi ya maji. Aidha, Halmashauri za Wilaya nchini zimeelekezwa kuongeza kasi ya uundaji na usajili wa Vyombo vya Watumiaji Maji (*COWSOs*) ili kuongeza ufanisi wa usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji vijijini.

Kwa upande wa uendelevu wa skimu za umwagiliaji, Halmashauri za Wilaya zimeelekezwa kuwa na wataalam wa kutosha wa Sekta ya Umwagiliaji katika maeneo ya miradi; na kusajili vyama vipya vya wamwagiliaji pamoja na kuendelea kuviimarisha vyama vilivyopo ili kusimamia uendeshaji na matengenezo ya skimu za umwagiliaji nchini kwa ufanisi zaidi.

## 11.4 7.0 SHUKRANI

**247.** **Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru wadau wote waliochangia kwa njia moja ama nyingine kufanikisha majukumu ya Sekta za Maji na Umwagiliaji katika kipindi cha mwaka 2016/2017. Shukrani za pekee ni kwa Nchi marafiki, Washirika wa Maendeleo, Mashirika ya Misaada ya kimataifa, Taasisi za Kiserikali, Mashirika ya Kidini pamoja na wadau wengine. Napenda kuwashukuru wananchi wote kwa kushiriki kikamilifu katika kutekeleza miradi ya maji na umwagiliaji nchini bila kujali tofauti zao za kisiasa, kidini, kikabila na kijinsia.

**248.** **Mheshimiwa Spika**, napenda kuzishukuru nchi rafiki ambazo zimesaidia kuchangia maendeleo ya Sekta za Maji na Umwagiliaji nchini zikiwemo Serikali za Ujerumani, Uholanzi, Uingereza, Marekani, Japan, Ufaransa, China, Uswisi, Ubeligiji, Ireland, Korea Kusini, Sweden, Denmark, Norway, India na Misri. Vilevile, natoa shukrani kwa Taasisi za fedha za kimataifa na mashirika ya kimaendeleo kwa misaada na ushirikiano wa kitaalam katika kufanikisha kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara. Taasisi hizo ni pamoja na

Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza *(DFID),* Shirika la Maendeleo la Ujerumani *(GIZ),* Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW),* Benki ya Maendeleo ya Ufaransa (*AFD*), Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya *(EIB)*, Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA)*, Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait *(Kuwait Fund),* Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta *(OPEC Fund for International Development-OFID)*, Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*SFD*), Umoja wa Ulaya (*EU*), Shirika la Maendeleo la Ubelgiji (*BTC*), Shirika la Marekani la Changamoto za Milenia (*MCC*)*,* Benki ya Dunia *(WB)*, Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (*UNDP),* Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan *(JICA)*, Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Makazi Duniani *(UN HABITAT)*, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF),* Shirika la Misaada ya Maendeleo la Sweden *(SIDA)* na Shirika la Misaada la Marekani (*USAID).*

**249.** **Mheshimiwa Spika**, miradi iliyotekelezwa kupitia Mashirika na Taasisi za Kidini imekuwa na mchango mkubwa katika kufikia malengo tuliyojiwekea katika Sekta za Maji na Umwagiliaji. Hivyo napenda kutoa shukrani kwa mashirika na taasisi hizo ambazo ni pamoja na *Catholic Agency for Overseas Aid and Development (CARITAS)*, *Adventist Development Relief Agency (ADRA), Norwegian Church Aid, Livingwater International, World Islamic League,* Shirika la *Ahmadiya Muslim Jamaat Tanzania, Islamic Foundation,* Kanisa la Kilutheri la Ujerumani, Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Kanisa Katoliki Tanzania na Kanisa la Kianglikana Tanzania.

Vilevile, napenda kutambua mchango wa Taasisi zisizo za Kiserikali katika kuendeleza Sekta za Maji na Umwagiliaji. Taasisi hizo ni pamoja na *Tanzania Water and Sanitation Network (TAWASANET);* Wahamasishaji wa Maji, Maendeleo na Afya *(WAMMA); WaterAid*; *World Vision*; *World Wide Fund for Nature (WWF*); *Netherlands Volunteers Services (SNV); Plan International*; *Concern Worldwide*; *Water Mission* (T), Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili na Mali Asili (*IUCN*); *African*

*Medical Research Foundation (AMREF); Clinton HIV Aids Initiative; Bill and Melinda Gates Foundation;* na wote ambao wameendelea kuisaidia Wizara ya Maji na Umwagiliaji katika kufanikisha malengo yake.

**250.** **Mheshimiwa Spika**, naomba sasa nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Mhe. Mhandisi Isack Kamwelwe (Mb)**, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji; **Prof. Kitila Alexander Mkumbo**, Katibu Mkuu; **Mhandisi Emmanuel Masasi Kalobelo**, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, wataalam na watumishi wote wa Wizara; pamoja na Maafisa Watendaji Wakuu na watumishi wa Mashirika, Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano mkubwa walionipatia katika kuhakikisha tunatekeleza malengo na majukumu ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Nawasihi waongeze juhudi katika kutekeleza majukumu yao ili kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata huduma bora na endelevu za maji na umwagiliaji kote nchini. Vilevile, napenda kuwashukuru wananchi wote wa Jimbo langu la Wanging'ombe kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia na wamekuwa nami bega kwa bega katika kuleta maendeleo ya Wilaya yetu ya Wanging'ombe na Taifa kwa ujumla.

## 11.5 8.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/2018

**251.** **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 672,223,100,937** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2017/2018**,** ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

### (a) Fungu 49

**252.** **Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi 648,064,207,705** zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya Sekta ya Maji kwa mwaka 2017/2018. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 24,457,459,705** ambapo **Shilingi 6,636,518,705** sawa na **asilimia 27** ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo

**(*OC*)** na **Shilingi 17,820,941,000** sawa na **asilimia 73** ni kwa ajili ya kulipa mishahara **(*PE*)** ya watumishi wa Wizara na Chuo cha Maji. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni **Shilingi 623,606,748,000** ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi 408,617,643,000** sawa na **asilimia 66** ni fedha za ndani na **Shilingi 214,989,105,000** sawa na **asilimia 34** ni fedha za nje.

**(b) Fungu 05**

**253.** **Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi 24,158,893,232** zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya Sekta ya Umwagiliaji kwa mwaka 2017/2018. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 4,055,481,082** ambapo **Shilingi 585,184,082** sawa na **asilimia 14.4** ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo **(*OC*)** na **Shilingi 3,470,297,000** sawa na **asilimia 85.6** ni kwa ajili ya kulipa mishahara **(*PE*)** ya watumishi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni **Shilingi 20,103,412,150** ambapo kati ya fedha hizo **Shilingi 5,600,000,000** sawa na **asilimia 27.9** ni fedha za ndani na **Shilingi 14,503,412,150** sawa na **asilimia 72.1** ni fedha za nje.

**254.** **Mheshimiwa Spika**, naomba tena nitoe shukrani zangu kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anwani: *www.maji.go.tz*.

**255.** **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na utaratibu unaofuta. Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. *(Makofi)*

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji naomba kuwasilisha na kama muda hautatosha naomba ripoti yote iingie katika *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Kamati na

muundo wa taarifa; kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2016/2017, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia maelezo ya utangulizi, taarifa hii inafafanua mambo matano yafuatayo:

(a) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017;

(b) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017;

(c) Mapitio ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017;

(d) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018; na

(e) Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa masuala mbalimbali, sehemu hii inabainisha masuala muhimu yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Kamati kwa kuzingatia masuala yaliyoorodheshwa katika kipengele cha kwanza na kipengele cha pili cha sehemu ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa ushauri wa Kamati; Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Toleo la 2005 imeipa Bunge mamlaka ya kuisimamia na kuishauri Serikali. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ilichambua bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kutoa maoni na ushauri

kwenye maeneo takribani saba ya kipaumbele ambayo yameainishwa katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri uliotolewa na Kamati kwa kiasi kikubwa umezingatiwa na kufanyiwa kazi isipokuwa ushauri kuhusu makadirio yaliyowekwa na kiasi kilichokusanywa hadi tarehe 31 Machi, 2017.

Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ya Maji na Umwagiliaji Fungu 49, liliidhinishiwa jumla ya shilingi 939,631,302,771; kati ya fedha hizo shilingi 7,075,948,000 ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi 17,361,417,000 ni mishahara. Aidha, kiasi cha shilingi 915,193,937,771 zilitengwa kwa ajili ya bajeti ya miradi ya maendeleo na asilimia 62 ya kiasi kilichoidhiishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa hadi kufikia Machi 2017 zilikuwa shilingi 181,209,813,609 sawa na asilimia 19.8 ya fedha zote za bajeti ya maendeleo. Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Fungu 5 hadi kufikia Machi, 2017 fedha za matumizi ya kawaida kiasi cha shilingi 122,354,224 ambayo ni sawa na asilimia 40.8. na shilingi 2,409,935,000 zilitolewa kwa ajili ya mishahara. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha shilingi 2,986,101,292 zilitolewa ambazo ni sawa na asilimia 8.4 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,334,980,000 sawa na asilimia 39 ya fedha za ndani na shilingi 646,121,292 sawa na asilimia 2.2 ya fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha unaomalizika 2016/2017 jumla ya fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa ni shilingi 181,209,813,609 sawa na asilimia 19.8 mwenendo huu ni wa kusikitisha na hasa ukizingatia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa sehemu kubwa ni miradi ya maji. Kiasi kikubwa cha fedha hizi za maendeleo zimetokana na fedha za Mfuko wa Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maduhuli, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara ya Maji na

Umwagiliaji ilipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi 550,005,000. Hadi kufikia Machi, 2017 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi 467,633,709 ambayo ni sawa na asilimia 85 ya malengo ya ukusanyaji. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kukusanya mapato hayo lakini inahimiza kuongeza juhudi za ukusanyaji ili kufikia malengo iliyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2016/2017; kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) inayoitaka Kamati kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoishia 2016/2017, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi katika Mikoa ya Shinyanga na Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Shinyanga; katika Mkoa wa Shinyanga Kamati ilikagua mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria hadi Miji ya Shinyanga, Mwadui, Kishapu na Maganzo, uliotengewa shilingi 1,000,000,000 na fedha zote kutolewa kwa wakati.

Katika ukaguzi Kamati ilibaini kuwa, mradi huu umetekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha na thamani ya fedha imetumika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa tanki la maji katika Mji wa Kishapu; Kamati ilipokagua ujenzi wa tanki kubwa la maji katika Mji wa Kishapu ilibaini kwamba hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa tanki hilo ni ya kuridhisha. Aidha, kutokana na mji wa Kishapu kutokuwa na miundombinu ya usambazaji maji Kamati inaishauri Serikali kuweka mipango madhubuti itakayowezesha Halmashauri kujenga kwa wakati miundombinu itakayokidhi kusambaza maji hayo pindi mradi huu utakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa maji na usafi wa Mazingira wa Ziwa Victoria Awamu ya Pili *(LV WATSAN II)*; katika mkoa wa Mwanza Kamati ilikagua mradi wa maji na usafi wa mazingira wa Ziwa Victoria Awamu ya Pili *(LV WATSAN II)* mradi unaotekelezwa katika Wilaya ya Sengerema. Mradi ambao unagharimu dola za Kimarekeni milioni 30.4 na

umekuwa ukitekelezwa kwa awamu tangu mwaka 2011 na unategemewa kukamilika mwezi Desemba, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018; Kamati ilipokea na kuchambua Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tarehe 30 na 31 Machi , 2017. Mpango huu wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi umezingatia ukomo wa bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (Awamu II) na Sera na Mikakati ya Kitaifa na Kisekta katika kuandaa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018, ikiwa ni pamoja na kutekeleza Sera ya Maji ya Mwaka 2002 na Sera ya Umwagiliaji ya Taifa ya mwaka 2010 pamoja na Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili *(ASDP II).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Namba 05 linahusu Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, ambapo pamoja na majukumu mengine Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ina jukumu la kuhakikisha Sera ya Umwagiliaji ya Taifa inatekelezwa kwa vitendo. Sera ya Umwagiliaji ya Taifa inahimiza umuhimu wa kuendeleza eneo kubwa lililopo nchini linalofaa kwa umwagiliaji kwa kuweka miundombinu ya umwagiliaji kwa ajili ya kuongeza tija na uzalishaji katika sekta ya kilimo kwenye mazao ya chakula, biashara, malisho na kilimo cha maji. Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2017/2018 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 24,158,893,232; kati ya fedha hizo, shilingi 20,103,412,150 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 4,055,481,082 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, hadi kufikia Juni 2018, Tume ya Taifa inatarajia kukusanya shilingi 15,500,000 kutokana na usajili wa vyama 100 vya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinazoombwa zinakusudiwa kutumika kutekeleza pamoja na kazi zingine vipaumbele vya Wizara kama vilivyoanishwa katika kipengele (a) na (d) ya taarifa ya Kamati. Uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kwamba kwa miaka miwili mfululizo fedha

nyingi zimekuwa zikitengwa kwenye matumizi ya maendeleo ikilinganishwa na matumizi ya kawaida, jambo ambalo limekuwa likipongezwa na Kamati, hata hivyo hali ni tofauti wakati wa utekelezaji wa bajeti; kwa mfano, katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kiasi cha fedha kilichotolewa ni kidogo ikilinganisha na fedha zilizotengwa na kuidhinishwa na Bunge. Aidha, baadhi ya miradi ya maendeleo haikupata fedha yoyote. Maelezo hayo yanathibitishwa na jedwali lililopo katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsri ya jedwali hili ni kwamba Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kulipa watumishi wa umma mishahara pasipo kuwawezesha watumishi kutekeleza majukumu yao kwani kazi nyingi zinazotekelezwa na Tume ya Umwagiliaji ni kazi za vitendo *(field work)* hivyo kukosekana kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kunapelekea mipango iliyopangwa kutotekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji na Umwagiliaji Fungu 49; Sera ya Maji ya mwaka 2002 inaeleza kuwa maji ni bidhaa muhimu kwa viumbe vyote duniani, bila maji hakuna uhai. Hivyo upatikanaji wa maji safi na salama ni mojawapo ya mahitaji ya msingi kwa binadamu wote. Juhudi za upatikanaji wa maji safi na salama zinaweza kuonekana katika hatua ambazo zimekuwa zikichukuliwa ikiwa ni pamoja na mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Pili, Dira ya Maendeleo ya Taifa *Tanzania Development Vision 2025*, Matokeo Makubwa Sasa *(Big Results Now)* na Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi zote hizo zinadhihirisha kwamba maji ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii na kwamba kiwango cha maendeleo ya jamii yoyote kinategemea kuwepo kwa maji ya kutosha na yenye ubora unaotakiwa, lakini bado upatikanaji wa maji safi na salama hapa nchini umethibitika kuwa mgumu hususan maeneo ya vijijini ambapo takwimu zinaonyesha ni asilimia 46 tu ya wakazi wa vijijini ndio wanaopata maji safi na salama na asilimia 74 kwa wakazi wa Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na bajeti inayoombwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 inatarajiwa kwenda kutekeleza miradi itakayosaidia kuongeza kasi ya upatikanaji wa maji safi na salama ili kuhakikisha kufikia dira ya taifa ya maendeleo ya mwaka 2025. Ikiwa ni pamoja na vipaumbele vya bajeti kama vilivyooneshwa katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza kazi zilizopangwa katika mwaka wa fedha 2017/2018; Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi 24,457,459,705 kwa ajili ya matumizi ya kawaida; kati ya fedha hizo, shilingi 6,636,518,705 sawa na asilimia 27 ni kwa ajili ya kugharamia matumizi ya kawaida na shilingi 17,820,941,000 sawa na asilimia 73 ni kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia Fungu 49 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 623,606,748,052; kati ya fedha hizo, shilingi 408,617,643,052 sawa na asilimia 66 ni fedha za ndani na shilingi 14,989,105,000 sawa na asilimia 34 ni fedha za nje. Aidha, fedha zingine za nje shilingi 78,420,000,000 zimetengwa kupitia Mafungu ya Mikoa na Halmashauri, Wizara ya Afya, Elimu na TAMISEMI kwa ajili ya miradi ya maji na kampeni za maji na usafi wa mazingira vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia Fungu Namba 49 imepanga kukusanya shilingi 590,005,000 itakazozipata kutokana na makadirio ya kukusanya maduhuli yatakayotokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, malipo kwa ajili ya leseni kwa kampuni za utafiti na uchimbaji visima vya maji na tozo mbalimbali zitakazotozwa kwa wateja watakaopata huduma za maabara za ubora wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kuwa Serikali imeendelea kutenga fedha nyingi za ndani kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018 Fungu Namba

49 limetengewa fedha za ndani kiasi cha shilingi 408,617,643,052 ambayo ni sawa na asilimia 66 ya fedha zote za maendeleo. Hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo. Hata hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha fedha zinazoidhinihwa zinatolewa kwa wakati. Pamoja na pongezi hizi, Kamati inataka kujua kwa nini bajeti imepungua kutoka shilingi 939,631,302,771 mwaka 2016/2017 na kuwa shilingi 623,606,748,052 kwa mwaka 2017/2018?

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya malengo kwa mwaka 2016/2017 Kamati imepitia, kuchambua na kutathmini malengo yaliyoainishwa katika mpango wa bajeti ya mwaka 2017/2018 na kuridhishwa nayo. Hata hivyo, tathmini ya Kamati katika kufanya ulinganisho wa makadirio ya matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018, umebaini kwamba fedha zinazoombwa hazikidhi mahitaji makubwa ya maji kama yalivyoelezwa katika mipango ya maji ya maendeleo ya miaka mitano awamu ya kwanza na ya pili. Kamati imebaini pia kwamba imekuwa ni kawaida kwa Serikali kutenga kiasi kikubwa cha fedha za miradi ya maendeleo na kushindwa kuzitoa kama zilivyoidhinishwa, kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Bunge liliidhinisha shilingi 915,193,813,609 kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo hadi kufikia Machi, 2017 kiasi cha shilingi 181,209,813,609 sawa na asilimia 19.8 tu ya fedha zote za bajeti ya maendeleo zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kamati kufanya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na maombi ya fedha kwa bajeti ya mwaka 2017/2018. Naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwenye maeneo sita yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni mtiririko wa fedha za miradi ya maendeleo usiokuwa na uhakika. Upo udhaifu mkubwa katika kutoa fedha za maendeleo zinazokuwa zimetengwa na Serikali na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta za maji na umwagiliaji. Kamati inashauri Serikali kutekeleza azma ya

kuhudumia wananchi kwa kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati na kadri zilivyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, kilimo cha umwagiliaji, uhusiano wake na uchumi wa viwanda. Uhaba wa mvua unaotokana na mabadiliko ya tabianchi umepelekea maeneo mengi ya nchi kuwa kame, hivyo kilimo cha kutegemea mvua hakiwezi kukidhi mahitaji ya chakula cha kutosheleza nchi. Hivyo kilimo cha umwagiliaji kina nafasi kubwa ya kuiwezesha nchi kujitosheleza kwa chakula na kupatikana ziada itakayouzwa nje ya nchi na kuliongezea Taifa fedha za kigeni. Hivyo, Kamati inashauri Serikali:-

(a) Kuiwezesha kifedha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ili iweze kujenga miundombinu ya umwagiliaji itakayowezesha Taifa kuwa na kilimo chenye tija katika maeneo mbalimbali nchini kwa mwaka mzima;

(b) Kuainisha na kutenga kanda maalum za kipaumbele zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na kuelekeza fedha katika maeneo hayo ili kuwa na kilimo chenye tija badala ya kuwa na miradi mingi isiyoweza kutekelezwa kwa pamoja; na

(c) Kuainisha vyanzo vya fedha kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Umwagiliaji. Uhakika wa upatikanaji fedha za Mfuko wa Umwagiliaji utapelekea kutekeleza azma ya Serikali ya kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta 468,338 za sasa hadi kufikia hekta 1,000,000 ifikapo mwaka 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba tatu, uchimbaji na ukarabati wa mabwawa na visima kwenye maeneo kame nchini; ukarabati wa mabwawa pamoja na upanuzi wa miundombinu ya maji kutoka kwenye mabwawa na visima vilivyochimbwa ni miongoni mwa vipaumbele vya Wizara katika mwaka wa fedha 2017/2018. Kwa sababu ujenzi wa mabwawa ukikamilika utasaidia kuongeza kasi ya upatikanaji maji kwa ajili ya matumizi ya kilimo cha umwagiliaji, majumbani, mifugo, viwandani na uzalishaji wa

umeme. Aidha, kutokana na mabiliko ya tabianchi visima vingi vya asili na vilivyojengwa na Serikali katika maeneo mbalimbali nchini vimekauka na hakuna hatua za haraka zilizochukuliwa kwa maelezo kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa miradi ya visima na mabwawa kutoka kwa wafadhili na wawekezaji mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilishangazwa na maelezo hayo kwani wapo wawekezaji wenye teknolojia rahisi na ya kisasa na wana fedha za kuwekeza katika sekta ya maji kwa mikopo nafuu na misaada. Kwa mfano, Kamati ina taarifa kuwa Kampuni ya *Investglobal and Associate* imeonyesha nia na iko tayali kuingia ubia na Serikali katika ujenzi wa miradi ya visima. Kwa kutoa mkopo wenye masharti nafuu kwa kipindi cha malipo ya kati ya miaka 10 - 20, mkopo utakaoanza kulipwa kuanzia miaka miwili mpaka mitatu baada ya mradi kukamilika na asilimia 35 ya mkopo huo ni msaada. Vilevile kampuni hii itabeba dhamana ya visima hivyo kuendelea kutoa maji kwa kipindi cha miaka kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na uhaba wa maji katika maeneo kame nchini ikiwa ni pamoja na kuepukana na changamoto zilizopo za miradi mingi ya visima kutotoa maji na mabwawa kukauka muda mfupi baada ya uchimbaji na hivyo kupoteza fedha za Serikali. Kamati inaishauri Serikali kutumia fursa za kushirikiana na sekta binafsi *(Private Public Partnership)* kwa kuchukua hatua ili kujiridhisha na masharti ya mikopo, misaada na faida zinazoonesha kuambatana na wadau wa sekta binafsi walio tayari kushirikiana na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kimkakati wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda; ujenzi wa bwawa la Kidunda ni wazo lililoasisiwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere miaka ya 1980. Bwawa la Kidunda lina umuhimu mkubwa katika uhai wa Mto Ruvu kwani kukamilika kwa ujenzi wa bwawa hili kutawezesha Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kuwa na uhakika wa maji kwa kipindi chote cha mwaka mzima pamoja na kuzalisha umeme wa

megawati 20 ambao utachochea pamoja na mambo mengine utekelezaji wa azma ya Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati imebaini kuwa tarehe 2 Machi, 2015, Tume ya Mipango iliiandikia barua Wizara ya Fedha na kuishauri Serikali kuwa ujenzi wa Bwawa la Kidunda ni moja ya vipaumbele vya Serikali. Aidha, Tume ya Mipango iliishauri Serikali kuendelea na majadiliano na Benki ya Maendeleo ya China ili kupata mkopo wenye masharti nafuu kwa ajili ya kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Exim China imeonyesha utayari wa kugharamia mradi huu ambao ujenzi wake utagharimu dola za Marekani milioni 215 na benki imetoa tarehe ya mwisho ya kusubiri majibu ya Serikali kuwa 17 Agosti, 2017, endapo muda huu utapita bila majibu ya Serikali, nchi itakuwa imepoteza fursa ya kupata fedha za ujenzi wa bwawa hili. Ili kufanikisha upatikanaji fedha za ujenzi wa bwawa hili, Kamati inaishauri Serikali kujiridhisha na masharti ya mikopo kutoka katika mabenki yaliyoonesha nia ya kusaidia ili kukamilisha mapema iwezekanavyo taratibu na makubaliano ya benki hizo ili ujenzi wa mradi huu uweze kuanza katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa fedha zingine za nje kiasi cha shilingi 78,420,000,000 ambazo hazijajumuishwa kwenye bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji zimetengwa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maji kupitia Mafungu ya Mikoa na Halmashauri, Wizara ya Afya, Elimu na TAMISEMI. Kufuatia umuhimu wa miradi ya maji nchini, Kamati inaishauri Wizara kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha hizo na kuwasilisha taarifa kwenye Kamati mapema mwezi Machi na kabla Kamati haijafanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa Mfuko wa Taifa wa Maji katika kuboresha huduma za maji. Kamati ilipowasilisha maoni yake kuhusu utekelezaji wa bajeti ya

Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilipendekeza Serikali ifanye marekebisho kwenye Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 kuweka tozo ya shilingi mia 100. Kwa kila lita ya mafuta ya dizeli na shilingi mia100 kwa kila lita ya mafuta ya petroli. Mapendekezo hayo yangetekelezwa yangewezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Taifa wa Maji ambao ungesaidia kuboresha huduma za maji. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kutekeleza ushauri huu hasa ukizingatia kuwa fedha za Serikali zisizotokana na mfuko inatoka kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji. Napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mheshimiwa Injinia Gerson Lwenge na Naibu Waziri Mheshimiwa Injinia Isack Kamwelwe pamoja na wataalam wote wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati ikichambua na kujadili bajeti ya Wizara ya maji. Kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano wao walioutoa wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake, naomba *Hansard* iweze kuwatambua sitapata muda wa kuwasoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah pamoja na Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndugu Rachel Nyega, Ndugu Virgil Mtui, Ndugu Martha Chassama na Ndugu Mwimbe John kwa kuihudumia Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati. Baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumiziya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja iliyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita na naomba kuwasilisha.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

## MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA

### 1.1 MAJUKUMU YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6 (7) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Maji na Umwagiliaji pamoja na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Kwa madhumuni ya Taarifa hii, Wizara ya Maji ina mafungu mawili ambayo ni:-

- Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Fungu 05 - na
- Wizara ya Maji na Umwagiliaji - Fungu 49.

### 1.2 MUUNDO WA TAARIFA

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia maelezo hayo ya utangulizi, Taarifa hii inafafanua mambo matano (5) yafuatayo:-

(a) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

(b) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

(c) Mapitio ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

(d) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; na

(e) Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MASUALA MBALIMBALI

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu hii inabainisha masuala muhimu yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Kamati kwa kuzingatia masuala yaliyoorodheshwa katika Kipengele 1.2 cha Sehemu ya Kwanza.

### 2.1 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Toleo la 2005 imeipa Bunge mamlaka ya kuisimamia na kuishauri Serikali. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ilichambua bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na kutoa maoni na ushauri kwenye maeneo takribani saba (7) ya kipaumbele. Maeneo hayo yalijumuisha ushauri kuhusu:-

(a) Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wakati;

(b) Mapendekezo ya kuongeza tozo ya shilingi hamsini kwa kila lita ya mafuta ya petroli na diseli ili kutunisha mfuko wa maji;

(c) Hujuma dhidi ya miundombinu ya maji;

(d) Umuhimu wa Serikali na Taasisi zake kulipa Ankara za maji kwa wakati ;

(e) Upungufu wa wataalamu katika sekta ya maji;

(f) Umuhimu wa uvunaji wa maji ya mvua na;

(g) Umuhimu wa matumizi ya rasilimali maji katika kuongeza tija na uboreshaji wa Sekta ya Kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ushauri uliotolewa na Kamati kwa kiasi kikubwa umezingatiwa na kufanyiwa kazi isipokuwa ushauri kuhusu:-

(a) Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo; kwani hadi kufikia mwezi Machi 2017 Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 19.8** tu ya fedha zote za bajeti ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge. Hali iliyopelekea Wizara kushindwa kutekelezwa kwa miradi mingi ya maendeleo.

(b) Kutoongezwa kwa tozo ya mafuta kwa kila lita ya dizeli na petroli kutoka shilingi 50 ya sasa hadi kufikia shilingi 100, ushauri ambao ulipokelewa na Serikali lakini haujatekelezwa kwa maelezo kwamba ushauri huu unaendelea kufanyiwa kazi.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ushauri huo kutotekelezwa, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa mwenendo huu wa kutotoa fedha zote za miradi ya maendeleo kwa wakati kunaathiri kwa kiasi kikubwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Wizara. Vilevile kutoongezwa tozo ya mafuta kwa kila lita ya petrol na diseli kutoka shilingi hamsini (50) hadi shilingi mia moja (100) kunaathiri ufanisi wa Mfuko wa Maji.

### 3.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ulijikita katika kulinganisha kiasi cha fedha

kilichoidhinishwa na Bunge, kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumika hadi mwezi Machi, 2017 na eneo la ukusanywaji maduhuli kwa kulinganisha makadirio yaliyowekwa na kiasi kilichokusanywa hadi tarehe 31 Machi, 2017.

3.1 **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ya Maji na Umwagiliaji- Fungu 49, liliidhinishiwa jumla ya shilingi **939,631,302,771**. Kati ya fedha hizo shilingi **7,075,948,000** ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi **17,361,417,000** ni mishahara. Aidha, kiasi cha shilingi **915,193,937,771** zilitengwa kwa ajili ya bajeti ya miradi ya maendeleo.

3.2 **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji **-** Fungu 05 iliidhinishiwa jumla ya shilingi **39,876,143,028** kati ya fedha hizo shilingi **4,506,613,600** ni fedha za matumizi ya kawaida ambapo shilingi **4,206,825,600** ni fedha kwa ajili ya mishahara na shilingi **299,788,000** ni fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo zilikuwa shilingi **35,369,529,428** kati ya hizo shilingi ni **6,000,000,000** ni fedha za ndani na shilingi **29,369,529,428** ni fedha za nje.

3.3 **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2017 Fungu 49 lilikuwa limepokea fedha za matumizi mengineyo shilingi **3,424,260,246.43** sawa na **asilimia 48**, na mishahara shilingi **10,862,692,720** sawa na **asilimia 62** ya kiasi kilichoidhinishwa. Kwa upande wa Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotolewa hadi kufikia Machi 2017 zilikuwa shilingi **181,209,813,609** sawa na **asilimia 19.8** ya fedha zote za bajeti ya maendeleo.

3.4 **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Fungu 05 hadi kufikia Machi, 2017 fedha za matumizi ya kawaida kiasi cha shilingi **122,394,224** ambayo ni sawa na **asilimia 40.8**. **na shilingi 2, 409, 935, 000** zilitolewa kwa ajili ya mishahara. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha shilingi **2,986,101,292** zilitolewa ambazo ni sawa na **asilimia 8.4** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi **2,339,980,000** sawa na **asilimia 39** ya fedha za ndani na shilingi **646,121,292** sawa na **asilimia 2.2** ya fedha za nje.

**3.5 Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha unaomalizika (2016/2017) jumla ya fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa ni shillingi **181,209,813,609** sawa na **asilimia 19.8** mwenendo huu ni wa kusikitisha na hasa ukizingatia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa sehemu kubwa ni miradi ya maji. Mwenendo huu usioridhisha wa upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge umeendelea kuwa kikwazo katika utekelezaji wa miradi iliyopangwa kutekelezwa. Kamati inaitaka Serikali kulieleza Bunge sababu za kutopeleka fedha kadri zilivyoidhinishwa na Bunge.

**3.6 Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa maduhuli, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara ya Maji na Umwagiliaji ilipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi **550,005,000** Hadi kufikia Machi 2017, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi **467,633,790** ambayo ni sawa na **asilimia 85** ya malengo ya ukusanyaji. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kukusanya mapato hayo lakini inahimiza kuongeza juhudi za ukusanyaji ili kufikia malengo iliyojiwekea.

## 4.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) inayoitaka Kamati kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha (2016/ 2017). Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi katika mikoa ya Shinyanga na Mwanza.

## 4.1 MRADI WA MAJI KUTOKA ZIWA VIKTORIA HADI SHINYANGA

**Mheshimiwa Spika,** katika mkoa wa Shinyanga Kamati ilikagua mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria hadi miji ya Shinyanga, Mwadui, Kishapu na Maganzo, uliotengewa shilingi **1,000,000,000** na fedha zote kutolewa kwa wakati. Katika ukaguzi, Kamati ilibaini kuwa, mradi huu umetekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha na thamani ya fedha imetumika ipasavyo.

## 4.2 UJENZI WA TANKI LA MAJI KATIKA MJI WA KLISHAPU

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokagua ujenzi wa tanki kubwa la maji katika mji wa Kishapu ilibaini kwamba hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa tanki hilo ni ya kuridhisha. Aidha, kutokana na mji wa Kishapu kutokuwa na miundombimu ya usambazaji maji, Kamati inaishauri Serikali kuweka mipango madhubuti itakayowezesha Halmashauri kujenga kwa wakati miundombinu itakayokidhi kusambaza maji hayo pindi mradi huu utakapokamilika.

## 4.3 MRADI WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA WA ZIWA VIKTORIA AWAMU YA PILI (LV WATSAN II)

**Mheshimiwa Spika,** katika mkoa wa Mwanza, Kamati ilikagua mradi wa maji na usafi wa mazingira wa Ziwa Viktoria Awamu ya Pili (LV WATSAN II) mradi unaotekelezwa katika Wilaya ya Sengerema. Mradi ambao unagharimu dola za kimarekeni **milioni 30.4** na umekuwa ukitekelezwa kwa awamu tangu mwaka 2011 na unategemewa kukamilika mwezi Desemba, 2017.
**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 mradi huu, ulitengewa shilingi **1,804,358,000,** hadi kufikia mwezi Machi, 2017, mradi ulikuwa umepokea shilingi **614,966,347** ambazo ni sawa na **asilimia 34** ya fedha iliyotengwa. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha zilizosalia kabla ya kumalizika kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ili kuwezesha mradi huu kamilika kwa muda uliopangwa ambao ni Desemba 2017**.** Vile vile, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji kwenye vijiji vilivyolengwa kufikiwa na mradi huu. Lakini pia kubuni na kutekeleza miradi ya aina hiyo katika maeneo mengine ambayo kuna maziwa, mabonde na mito ili kuwawezesha wananchi wa maeneo hayo kuondokana na uhaba mkubwa wa maji safi na salama ambayo imekuwa ni kero ya muda mrefu.

## 4.4 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Mpango

wa Bajeti wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 tarehe 30 na 31 Machi , 2017. Mpango huu wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi umezingatia Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (Awamu II) na Sera na Mikakati ya Kitaifa na Kisekta katika kuandaa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, ikiwa ni pamoja na kutekeleza Sera ya Maji ya Mwaka 2002 na Sera ya Umwagiliaji ya Taifa ya Mwaka 2010 pamoja na Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II).

### 4.4.1 TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI FUNGU 05

**Mheshimiwa Spika,** Fungu 05 linahusu Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, ambapo pamoja na majukumu mengine Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inajukumu la kuhakikisha Sera ya Umwagiliaji ya Taifa inatekelezwa kwa vitendo.

**4.4.1.1 Mheshimiwa Spika,** Sera ya Umwagiliaji ya Taifa inahimiza umuhimu wa kuendeleza eneo kubwa lililopo nchini linalofaa kwa umwagiliaji kwa kuweka miundombinu ya umwagiliaji kwa ajili ya kuongeza tija na uzalishaji katika sekta ya kilimo kwenye mazao ya chakula, biashara, malisho na kilimo cha majani[1]. Kwa muktadha huu, maombi ya fedha kwa mwaka 2017/2018 na utekelezaji wa bajeti unalenga kuwezesha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Umwagiliaji pamoja na kufanikisha azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda.

**4.4.1.2 Mheshimiwa Spika,** Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **24,158,893,232**. Kati ya fedha hizo, shilingi **20,103,412,150** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **4,055,481,082** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, hadi kufikia Juni 2018, Tume ya Taifa inatarajia kukusanya shilingi **15,500,000** kutokana na usajili wa vyama 100 vya umwagiliaji.

----------------------

[1] Sera ya Umwagiliaji ya Taifa ya Mwaka 2010

**Mheshimiwa Spika,** Fedha zinazoombwa zinakusudiwa kutumika kutekeleza pamoja na kazi zingine vipaumbele vifuatavyo:-

(a) Kuendeleza ujenzi wa mabwawa ya Dongobeshi (Manyara), Itagata (Manyoni) na kujenga bwawa jipya la Tlawi ( Mbulu);

(b) Kuendeleza ujenzi na ukarabati wa skimu za Igenge (Misungwi), Kirya (Mwanga), Kongogo (Bahi), Endagaw (Hanang), Mbogo na Kigugu (Mvomero);

(c) Kujenga na kukarabati skimu za Segeni (Rufiji), Msolwa Ujama, Njage na Mkula (Kilombero) na Mvumi (Kilosa); na

(d) Kujenga uwezo wa vyama 442 vya wamwagiliaji na wataalamu kuhusu uendeshaji skimu za umwagiliaji.

**4.4.1.3 Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kwamba kwa miaka miwili mfululizo fedha nyingi zimekuwa zikitengwa kwenye matumizi ya maendeleo ikilinganishwa na matumizi ya kawaida, jambo ambalo limekuwa likipongezwa na Kamati, hata hivyo hali ni tofauti wakati wa utekelezaji wa bajeti. Kwa mfano katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kiasi cha fedha kilichotolewa ni kidogo ikilinganisha na fedha zilizotengwa na kuidhinishwa na Bunge. Aidha, baadhi ya miradi ya maendeleo haikupata fedha yoyote.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo hayo yanathibitishwa na jedwali lifuatalo linaloonyesha muhtasari wa Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo kwa mwaka 2016/2017

| Kifungu | Idara/ Kitengo | Bajeti iliyoidhinisha 2016/2017 | Fedha zilizotolewa na kutumika hadi Machi,2017 | % ya fedha iliyotolewa |
|---|---|---|---|---|
| 2002 | Ujenzi na Usimamizi wa miundombinu ya umwagiliaji | 16,562,474,928 | 497,000,000 | **3%** |
| 2003 | Ufatifi na Uhamasishaji wa Teknolojia za Umwagiliaji | 200,000,000 | 00 | **0%** |
| 2004 | Huduma za uendeshaji na uwezeshaji wa umwagiliaji | 845,568,000 | 00 | **0%** |

**Chanzo cha taarifa**: Randama ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji Fungu - 05 Machi, 2017.

**Mheshimiwa Spika**, tafsri ya jedwali hili ni kwamba Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kulipa Watumishi wa umma mishahara pasipo kuwawezesha Watumishi kutekeleza majukumu yao kwani kazi nyingi zinazotekelezwa na Tume ya Umwagiliaji ni kazi za vitendo *(field work)* hivyo kukosekana kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kunapelekea mipango iliyopangwa kutotekelezwa.

## 4.4.2 WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI FUNGU 49

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Maji ya Mwaka 2002 inaeleza kuwa maji ni bidhaa muhimu kwa viumbe vyote duniani, bila maji hakuna uhai. Hivyo upatikanaji wa maji safi na salama ni mojawapo ya mahitaji ya msingi kwa binadamu wote[2]. Kwa kutambua hilo ndio maana swala la maji limewekewa mkazo katika malengo ya mahususi ya kitaifa na kimataifa ikiwemo Malengo ya Maendeleo Endelevu. Lengo la sita la maendeleo endelevu linadhamiria kuona kuna upatikanaji wa maji safi na salama kwa wote ifikapo 2030.

-------------------------------------

[2] Sera ya Maji ya Mwaka 2002

**4.4.2.1 Mheshimiwa Spika**, juhudi za upatikanaji wa maji safi na salama zinaweza kuonekana katika kila hatua ya MKUKUTA (Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania) , Dira ya Maendeleo ya Taifa *(Tanzania Development Vision 2025)*, Matokeo Makubwa sasa *(Big Results Now)* na katika ilani zote za uchaguzi wa vyama vya siasa.

**4.4.2.2 Mheshimiwa Spika,** juhudi zote hizo zinadhihirisha kwamba Maji ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii na kwamba kiwango cha maendeleo ya jamii yoyote kinategemea kuwepo kwa maji ya kutosha na yenye ubora unaotakiwa lakini bado upatikanaji wa maji safi na salama hapa nchini umethibitika kuwa mgumu hususan maeneo ya vijijini ambapo takwimu zinaonyesha ni **asilimia 46% tu** ya wakazi wa vijijini ndio wanaopata maji safi na salama na **asilimia 74%** kwa wakazi wa mjini.

**4.4.2.3 Mheshimiwa Spika**, bajeti inayoombwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 inatarajiwa kwenda kutekeleza miradi itakayosaidia kuongeza kasi ya upatikanaji wa maji safi na salama ili kuhakikisha kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 ni:-

(a) Kuwa na huduma bora ya maji kwa wote katika maeneo ya mijini ifikapo mwaka 2025;

(b) Huduma bora za maji vijijini kwa zaidi ya asilimia 90 ya wananchi ifikapo mwaka 2025; na

(c) Kuwa na rasilimali za maji endelevu kwa kuvilinda, kuvitunza, kuviendeleza na kutafuta vyanzo vipya vya maji.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na vipaumbele hivyo, bajeti hii pia itatekeleza malengo ya muda wa kati kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza upatikanaji wa maji safi na usafi wa mazingira kwa **asilimia 85** kwa wakazi wa vijijini na **asilimia 95** kwa maeneo ya mijini ifikapo mwaka 2020;

(ii) Kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta **468,338** za sasa hadi hekta **1,000,000** ifikapo 2021;

(iii) Kuhakikisha rasilimali za maji zinatunzwa, zinasimamiwa, na zinatumika kwa njia endelevu kwa manufaa ya kijamii na kiuchumi; na

(iv) Kuboresha mazingira ya kazi na kuendeleza Watumishi wa Sekta ya Maji na Umwagiliaji ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo yaliyowekwa.

**4.4.2.4 Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza kazi zilizopangwa katika **Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha** shilingi 24,457,459,705 **kwa ajili ya matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo,** shilingi 6,636,518,705 **sawa na** asilimia 27 **ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi ya kawaida (*Other Charges*) na** shilingi 17,820,941,000 **sawa na** asilimia 73 **ni kwa ajili ya kulipa mishahara (PE) ya Watumishi.**

**4.4.2.5 Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia fungu 49 inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 623,606,748,052.** Kati ya fedha hizo, shilingi **408,617,643,052** sawa na **asilimia 66** ni fedha za ndani na shilingi **214,989,105,000** sawa na **asilimia 34** ni fedha za nje**.** Aidha, fedha zingine za nje shilingi 78,420,000,000 zimetengwa kupitia mafungu ya Mikoa na Halmashauri, Wizara ya Afya, Elimu na TAMISEMI kwa ajili ya miradi ya maji na kampeni za maji na usafi wa mazingira vijijini.

**4.4.2.6 Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia Fungu 49 imepanga kukusanya shilingi **590,005,000** itakazozipata kutokana na makadirio ya kukusanya maduhuli yatakayotokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, malipo kwa ajili ya leseni kwa kampuni za utafiti na uchimbaji visima vya maji na tozo mbalimbali zitakazotozwa kwa wateja watakaopata huduma za maabara za ubora wa maji.

**4.4.2.7 Mheshimiwa Spika**, uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kuwa Serikali imeendelea kutenga fedha nyingi za

ndani kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, ambapo katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Fungu 49 limetengewa fedha za ndani kiasi cha shilingi **408,617,643,052** ambayo ni sawa na **asilimia 66** ya fedha zote za maendeleo. Hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo, hata hivyo Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha fedha zinazoidhinihwa zinatolewa kwa wakati.

### 4.4.3 TATHIMINI YA MALENGO KWA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepitia, kuchambua na kutathimini malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2017/2018 na kuridhishwa nayo. Hata hivyo, tathimini ya Kamati katika kufanya ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 umebaini kwamba fedha zinazoombwa hazikidhi mahitaji makubwa ya Maji kama yalivyoelezwa katika Mipango ya Taifa ya Maendeleo ya Miaka Mitano (Awamu ya I&II) ambayo imebainisha maji kama kipaumbele kimojawapo katika kukuza uchumi hasa kwa kuchangia katika uzalishaji wa umeme, kilimo cha umwagiliaji, ufugaji, viwanda, usafirishaji na uchukuzi na kupunguza umaskini.

**4.4.3.1 Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini pia kwamba, imekuwa ni kawaida kwa Serikali kutenga kiasi kikubwa cha fedha za miradi ya maendeleo na kushindwa kuzitoa kama zilivyoidhinishwa. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2016/ 2017 Bunge liliidhinisha shilingi **915,193,813,609** kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo hadi kufikia Machi, 2017 kiasi cha shilingi **181,209,813,609** sawa na **asilimia 19.8** tu ya fedha zote za bajeti ya maendeelo zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

## SEHEMU YA TATU

### 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kufanya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara ikiwa ni

pamoja na maombi ya fedha kwa Bajeti ya Mwaka 2017/ 2018. Naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwenye maeneo sita (6) yafuatayo:-

**1) Mtiririko wa Fedha za miradi ya maendeleo usiokuwa na uhakika**

**Mheshimiwa Spika,** upo udhaifu mkubwa katika kutoa fedha za maendeleo zinazokuwa zimetengwa na Serikali na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta za Maji na Umwagiliaji, Kamati inashauri Serikali kutekeleza adhima ya kuhudumia wananchi kwa kutoa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati na kadri zilivyoidhinishwa na Bunge.

**2) Kilimo cha Umwagiliaji na uhusiano wake na uchumi wa viwanda**

**Mheshimiwa Spika,** uhaba wa mvua unaotokana na mabadiliko ya tabianchi umepelekea maeneo mengi ya nchi kuwa kame, hivyo kilimo cha kutegemea mvua hakiwezi kukidhi mahitaji ya chakula cha kutosheleza nchi, hivyo kilimo cha umwagiliaji kina nafasi kubwa ya kuiwezesha nchi kujitosheleza kwa chakula na kupatikana ziada itakyouzwa nje ya nchi na kuliongezea Taifa fedha za kigeni. Hivyo, Kamati inashauri Serikali:-

(a) Kuiwezesha kifedha Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ili iweze kujenga miundombinu ya umwagiliaji itakayowezesha Taifa kuwa na kilimo chenye tija katika maeneo mbalimbali nchini kwa mwaka mzima;

(b) Kuainisha/kutenga kanda maalum za kipaumbele zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na kuelekeza fedha katika maeneo hayo ili kuwa na kilimo chenye tija badala ya kuwa na miradi mingi isiyoweza kutekelezwa kwa pamoja.

(c) Kuainisha vyanzo vya fedha kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Umwagiliaji. Uhakika wa upatikanaji fedha za Mfuko wa Umwagiliaji utapelekea kutekeleza azma ya Serikali

ya kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta **468,338** za sasa hadi kufikia hekta **1,000,000** ifikapo 2021.

**3) Uchimbaji na Ukarabati wa Mabwawa na Visima kwenye maeneo kame nchini**

**Mheshimiwa Spika**, ukarabati wa mabwawa pamoja na upanuzi wa miundombinu ya maji kutoka kwenye mabwawa na visima vilivyochimbwa ni miongoni mwa vipaumbele vya Wizara katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwasababu ujenzi wa mabwawa ukikamilika utasaidia kuongeza kasi ya upatikanaji maji kwa ajili ya matumizi ya kilimo cha umwagiliaji, majumbani, mifugo, viwandani na uzalishaji wa umeme.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na umuhimu wa ujenzi wa mabwawa nchini mabwawa ya Lugoda (Ndembera), Farkwa (Dodoma), Mbangala (Songwe) na Dongwe (Kiteto) umekuwa ukisuasua. Aidha, kutokana na mabiliko ya tabianchi visima vingi vya asili na vilivyojengwa na Serikali katika maeneo mbalimbali nchini vimekauka na hakuna hatua za haraka zilizochukuliwa kwa maelezo kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa miradi ya visima na mabwawa kutoka kwa wafadhili na wawekezaji mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilishangazwa na maelezo haya kwani wapo wawekezaji wenye teknolojia rahisi na ya kisasa na wana fedha za kuwekeza katika sekta ya Maji kwa mikopo nafuu na misaada. Kwa mfano; Kamati ilikutana na kampuni ya ***Investglobal and Associate*** ambao wako tayari kuingia ubia na Serikali katika ujenzi wa miradi ya visima kwa kutoa mkopo wenye masharti nafuu kwa kipindi cha malipo ya kati ya **miaka 10-20**, mkopo utakaoanza kulipwa kuanzia **miaka 2-3** baada ya mradi kukamilika na **asilimia 35** ya mkopo huo ni msaada. Vilevile kampuni hii itabeba dhamana ya visima hivyo kuendelea kutoa maji kwa kipindi cha miaka kumi.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukabiliana na uhaba wa maji katika

maeneo kame nchini ikiwa ni pamoja na kuepukana na changamoto zilizopo za miradi mingi ya visima kutotoa maji na mabwawa kukauka muda mfupi baada ya uchimbaji na hivyo kupoteza fedha za Serikali, Kamati inaishauri Serikali kuondokana na urasimu usiokuwa wa lazima na kutumia fursa za kushirikiana na sekta binafsi (*Private Public Partnership*)kwa kuchukua hatua ili kujiridhisha na masharti ya mikopo, misaada na faida zinazoonyesha kuambatana na wadau wa sekta binafsi waliotayari kushirikiana na Serikali.

**4) Mradi wa kimkakati wa Ujenzi wa Bwawa la Kidunda**

**Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa Bwawa la Kidunda ni wazo lililoasisiwa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere miaka ya 1980. Bwawa la Kidunda lina umuhimu mkubwa katika uhai wa Mto Ruvu kwani kukamilika kwa ujenzi wa Bwawa hili kutawezesha mikoa ya Dar es salaam na Pwani kuwa na uhakika wa maji kwa kipindi chote cha mwaka mzima pamoja na kuzalisha umeme wa **megawati 20** ambao utachochea pamoja na mambo mengine utekelezaji wa adhma ya Tanzania ya viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** usanifu wa bwawa hili ulianza mwaka 2010 ulikamilika mwaka 2012 ambapo gharama ya ujenzi wa mradi inatarajiwa kuwa **Dola za Marekani milioni 215** sawa na shilingi **bilioni 430**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia umuhimu wa bwawa hili hatua mbalimbali za kutafuta vyanzo vya fedha za kutekeleza mradi huo zimekuwa zikichukuliwa, hata hivyo upatikanaji fedha za uhakika kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hili umekuwa wa kusuasua.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati imebaini kuwa, tarehe 2 Machi, 2015, Tume ya Mipango iliiandikia barua Wizara ya Fedha na kuishauri Serikali kuwa ujenzi wa bwawa la Kidunda ni moja ya vipaumbele vya Serikali. Aidha, Tume ya Mipango iliishauri Serikali kuendelea na majadiliano na Benki ya Maendeleo ya China ili kupata mkopo wenye masharti nafuu kwa ajili ya kutekeleza mradi huu.

**Mheshimiwa Spika,** Benki ya *Exim* China imeonyesha utayari wa kugharamia mradi huu ambao ujenzi wake utagharimu **Dola za Marekani milioni 215** na benki imetoa tarehe ya mwisho ya kusubiri majibu ya Serikali kuwa 17 Agosti, 2017 endapo muda huu utapita bila majibu ya Serikali, nchi itakuwa imepoteza fursa ya kupata fedha za ujenzi wa bwawa hili.

**Msheshimiwa Spika,** ili kufanikisha upatikanaji fedha za ujenzi wa Bwawa hili, Kamati inaishauri Serikali kujiridhisha na masharti ya mikopo kutoka katika mabenki yaliyoonyesha nia ya kusaidia ili kukamilisha mapema iwezekanavyo taratibu za makubaliano na Benki hizo ili ujenzi wa mradi huu uweze kuanza katika Mwaka wa Fedha (2017/2018).

**5) Uratibu wa fedha zingine za miradi ya maendeleo shilingi 78,420,000,000**

**Mheshimiwa Spika,** fedha zingine za nje kiasi cha shilingi **78,420,000,000** ambazo hazijajumuishwa kwenye bajeti ya Wizara ya Maji na umwagiliaji zimetengwa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maji kupitia mafungu ya Mikoa na Halmashauri, Wizara za Afya, Elimu na TAMISEMI. Kufuatia umuhimu wa miradi ya maji nchini, Kamati inaishauri Wizara kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha hizo na kuwasilisha taarifa kwenye Kamati mapema mwezi Machi na kabla Kamati aijafanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2017/2018.

**6) Umuhimu wa Mfuko wa Taifa Maji katika kuboresha huduma za maji**

Kamati ilipowasilisha maoni yake kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ilipendekeza Serikali ifanye marekebisho kwenye Sheria ya Fedha ya Mwaka 2016 kwa kuweka tozo ya shilingi mia moja (100) kwa kila lita ya mafuta ya diseli na shilingi mia moja (100) kwa kila lita ya mafuta ya petroli. Mapendekezo hayo yangetekelezwa yangewezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Taifa wa Maji ambao ungesaidia kuboresha huduma za maji. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kutekeleza ushauri huu.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**6.1 Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mhe. Eng. Gerson H. Lwenge, (Mb) na Naibu Waziri Mhe. Eng. Isack A. Kamwelwe (Mb) pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati Kamati ikichambua na kujadili bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji**.**

**6.2 Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao walioyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-**

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mb | Mwenyekiti |
| 2.Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma,Mb | M/Mwenyekiti |
| 3.Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb | Mjumbe |
| 4.Mhe. Mahmoud H. Mgimwa, Mb | “ |
| 5.Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mb | “ |
| 6.Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb | “ |
| 7.Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb | “ |
| 8.Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb | “ |
| 9.Mhe. Mattar Ali Salum, Mb | “ |
| 10.Mhe. John John Mnyika, Mb | “ |
| 11.Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb | “ |
| 12.Mhe. James Kinyasi Millya, Mb | “ |
| 13.Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb | “ |
| 14.Mhe. Pascal Yohana Haonga, Mb | “ |
| 15.Mhe. Salim Mbaraku Bawazir Mb | “ |
| 16.Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb | “ |
| 17.Mhe. Abdallah Hamis Ulega, Mb | “ |
| 18.Mhe. Haji Ameir Haji, Mb | “ |

19.Mhe. Daniel N. Nsanzugwanko, Mb "
20.Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb "
21.Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb "
22.Mhe. Emmanuel Papian John, Mb "
23.Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb "
24.Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb "

**6.3 Mheshimiwa Spika,** mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah pamoja na Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndg. Rachel Nyega, Ndg. Virgil Mtui, Ndg. Martha Chassama na Ndg. Mwimbe John kwa kuihudumia Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**6.4 Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumiziya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**6.5 Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja iliyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita na naomba kuwasilisha.

Dkt.Christine G. Ishengoma, (Mb)
**MAKAMU MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**
**10 MEI, 2017**

**NAIBU SPIKA:** Nimuite sasa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI – MSEMAJI MKUU KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema inayoniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara hii. Kipekee kabisa naomba nichukue fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Peter Lijualikali

Mbunge, Naibu Msemaji Mkuu wa Wizara hii, kwa kufanikiwa kuandika historia adhimu ya kuhukumiwa kufungwa jela wakati akiwa anapambana kuwatetea wapiga kura wake wa Jimbo la Kilombero, pia akiwa anatetea haki yake ya kupiga kura katika Halmashauri ambayo yeye ni Mbunge wa kuchaguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Lijualikali siyo tu kwa kuwa ameshinda rufaa yake na hivyo kuwa huru kuwatumikia wapigakura wake, bali pia kitendo chake cha kufungwa huku akiwa Mbunge wakati hakuwa na makosa, hii imeionesha dunia kuwa wanaofungwa katika nchi yetu siyo kuwa wote wanakuwa na hatia. Jina lake litakuwa rejea mbalimbali katika vitabu na majarida mbalimbali duniani kote. Lijualikali umekuwa mwakilishi wa wafungwa bila hatia na shujaa wa vijana wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuingia kwa undani katika utoaji wa maoni na uchambuzi wa Wizara, Kambi Rasmi inamtaka Mheshimiwa Waziri awaeleze Watanzania kwa kujibu swali hili, maji ni huduma au biashara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa maji kwa ajili ya uhai wa wanyama, watu, mimea na mazingira kwa ujumla ni jambo lisilopingika. Bila ya maji viumbe vyote vitapotea, mazingira yatakuwa mfu na maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii yatadumaa. Kutokana na umuhimu wa maji, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa katika kikao chake cha tarehe 21 Desemba, 2016 limeridhia kwa kauli moja miaka kumi ya utekelezaji wa Azimio jipya la Maji kwa Maendeleo Endelevu *(International Decade 2018 - 2028 for Action - Water for Sustainable Development).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Dira ya Maendeleo ya Taifa *(Tanzania Development Vision 2025)* imeweka malengo ya maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na ustawi jamii ikiwa ni pamoja na malengo yanayogusa moja kwa moja Wizara na sekta ya Maji na Umwagiliaji. Baadhi ya malengo muhimu katika muhtadha huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati ambapo wananchi wake wanafurahia amani na umoja wa kitaifa.

(ii) Upatikanaji wa maji safi na salama kwa wakazi wote, ambapo kwa wakazi wa mijini watapata maji kwa asilimia 100 na kwa wakazi wa vijijini watapata maji safi na salama kwa asilimia agalau 90 ifikapo 2025.

(iii) Kuhakikisha kwamba raslimali za maji ni endelevu ili kukidhi mahitaji ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia malengo ya dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji inatekeleza programu kuu zifuatazo:-

(i) Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*Water Sector Development Programme – WSDP).*

(ii) Programu ya maendeleo ya sekta ya kilimo, sekta ya umwagiliaji inayosimamiwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji *(Water Sector Development Programme - WSDP)* ni mradi wa muda mrefu wa utekelezaji wa miaka 20. Utekelezaji wake ulianza mwaka 2006 na utafikia ukomo wa utekelezaji mwaka 2025 ambapo inategemewa kuwa viwango vya upatikanaji wa maji safi na salama na usalama wa maji kwa ujumla vitakuwa vimefikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha utekelezaji wa programu kubwa ya kiwango cha *WSDP* ya Tanzania, programmu imegawanywa katika awamu kuu nne za utekelezaji, ambapo kwa sasa awamu ya kwanza iliyochukua takribani miaka minne imemalizika, na sasa awamu ya pili inatekelezwa. Muundo na mfumo wa utekelezaji umeigawanya programu hii katika sehemu kuu zifuatazo:-

(i) Usimamizi wa Rasilimali za Maji.

(ii) Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.

(iii) Huduma ya Maji Usafi wa Mazingira na Uondoshaji wa Maji Taka Mijini.

(iv) Usafi wa Mazingira na Usafi Mashuleni *(National Sanitation Campaign and School WASH).*

(v) Mfumo wa Uwezeshaji wa Utekelezaji wa Programu *(Programme Delivery Support).*

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa programu hii unafanyika kwa kuzingatia sera kuu za maendeleo ya taifa, Sera za kisekta kama vile Sera ya Maji ya mwaka 2002, Sera ya Ugatuaji wa Madaraka *(Decentralization by Devolution),* Mikakati ya Kupunguza Umaskini nchini na Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano. Majukumu na wajibu wa wadau wa sekta ya maji hususan wale wanaohusika na utekelezaji wa programmu hii wanatajwa kuwa katika ngazi ya Taifa ni pamoja na Wizara ya Maji yenyewe, Wizara ya Afya, Elimu na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na washirika wa kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na taasisi za kifedha za kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ngazi za Kanda, Mikoa, Wilaya na Vijiji programu inatekelezwa kupitia Bodi za Mabonde ya Maji *(Basin Water Boards),* Mamlaka za Maji Mijini na kipekee kwa sababu ya unyeti wake, Mamlaka ya Maji ya Jiji la Dar es Salaam; Mamlaka za Maji katika Makao Makuu ya Wilaya na Miji Midogo, na Halmashauri za Wilaya katika Idara ya Mhandisi wa Maji katika ngazi ya kijiji, wadau wakuu wa usambazaji wa maji safi na salama kwa wananchi ni pamoja na Serikali za vijiji na vyombo vya watumiaji wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe ya kwamba utekelezaji wa *WSDP* unafanywa kupitia sheria kuu mbili za maji pamoja na kanuni zake na miongozo mbalimbali yaani Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2009 na Sheria ya Raslimali za Maji ya mwaka huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa na mfumo maalum wa kitaasisi kwenye sekta kwa ajili ya uwezeshaji na uendeshaji wa programu, ufahamu wa Watanzania kuhusu mabadiliko ya kisera, kisheria na kitaasisi ndani ya sekta bado ni mdogo jambo ambalo linadhoofisha kanuni ya ushirikishaji, utawala bora na uwazi katika uboreshaji na utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira mijini na vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa mbalimbali za utafiti kuhusu ushiriki wa jamii na wadau mbalimbali wa sekta ya maji katika utekelezaji wa *WSDP* unaonesha kuwa wadau wengi hawana ufahamu wa miundo na mifumo ya programu jambo linalochangia utekelezaji hafifu wa miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kutambua umuhimu wa maji kwa wananchi wa Tanzania imefuatilia kwa kina utekelezaji wa *WSDP* awamu ya kwanza na *WSDP* awamu ya pili. Kati ya changamoto zilizooneshwa katika utekelezajiwa wa awamu ya kwanza ya programu ni programu awamu ya kwanza na vilevile katika utekelezaji wa mpango na bajeti 2016/2017 suala la uundaji wa vyombo vya watumiaji wa maji limebaki kuwa ni changamoto kubwa na linachangia kwa kuharibika kwa miundombinu ya maji kwa kasi kubwa, kwa kukosekana kwa usimamizi wa karibu miundombinu ya maji karibu na vituo vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na taarifa za hivi karibuni, Tanzania inapiga hatua moja mbele katika kutoa huduma za maji lakini inarudi hatua mbili nyuma katika utoaji wa huduma hiyo hiyo kutokana na kuharibika kwa miundombinu na upotevu mkubwa wa maji safi na salama yanayozalishwa kwa fedha nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalamu na wadau wa sekta ya maji wanajuliza maswali mengi na hivi karibuni kupitia ukurasa wa mtandao wa taasisi bobezi ya maji kumekuwa na swali la msingi kama ifuatavyo na ninanukuu kwa kiingereza kama ilivyo; *"Despite massive investments in*

*rural water supply in Tanzania, the number of people with access to improved water sources has not increased. This begs the question, what could be the reason for this stagnation?"*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara ya Maji ituambie je, ni kwa kiasi gani Wizara ya Maji imewianisha mfumo wake wa tathmini na ule wa ufuatiliaji na tathmini wa kimataifa *Joint Monitoring Programme(JMP).* Je, tuamini kati ya kipi takwimu za Kitaifa na zile za *JMP?* Na sababu ya kuamini kimojawapo ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inaamini kuwa mkakati wa maendeleo endelevu wa sekta ya maji *(sustainability strategy)* ulioandaliwa na kuasisiwa na sekta hii kwa fedha nyingi za walipa kodi wa Tanzania na wale wa nchi za nje haujapewa kipaumbele stahiki hususan katika suala la kuanzisha na kuwezesha vyombo vya usimamizi wa maji. Kwa sababu hiyo, fedha nyingi zinazowekezwa kwenye sekta hii hupotea bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kuuelezea umma wa watanzania masuala yafuatayo:-

(i) Ni kiasi gani cha fedha kimetumika katika kuanzisha na kuimarisha vyombo vya watumiaji maji vijijini?

(ii)Ni mkakati upi unatumika ili kuhakikisha kuwa vyombo ya watumiaji maji vinaundwa, vinaimarishwa na kusajiliwa rasmi ili kuwezesha utekelezaji wenye tija wa *WSDP II* vijijini?

(iii) Kwa vile uwepo wa vyombo vya watumiaji maji ni sehemu ya kigezo cha kupata ruzuku ya maji inayojulikana kama malipo kwa matokeo ni hatua zipi zimechukuliwa kufidia Halmashauri ambazo zimekosa kupata ruzuku hiyo kwa kukosa sifa kutokana na kutokuwepo kwa vyombo vya watumiaji maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka kufikia mwisho wa utekelezaji wa awamu ya kwanza ya programmu ya maendeleo ya maji mnamo tarehe 30 Juni, 2016 fedha zilizowekezwa katika programu zilikuwa ni Dola za Kimarekani 1,713.5. Awamu ya pili ya utekelezaji wa programu ya maendeleo ya ya maji, programu hii ina sifa ya kuwa ni programu kubwa na pengine yenye kugharimu fedha nyingi kuliko programu nyingine za kitaifa Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia kurejea bajeti za Kisekta za Maji na Umwagiliaji kwa mwaka 2016/2017, ili kuweka kumbukumbu vizuri, katika mwaka huo wa fedha, Wizara iliomba na kuidhinishiwa bajeti za Sekta za Maji na Umwagiliaji yaani Fungu Namba 49 na Fungu Namba 05 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Maji Fungu 49 mwaka wa fedha 2016/2017 iliombewa bajeti ya shilingi 939,631,302,000 na kati ya fedha hizo shilingi 915,193,937,771 ni kwa ajili ya maendeleo na shilingi 24,437,365,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida yaani mishahara na matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii ni takriban maradufu ya ile iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha uliopita yaani 2015/2016 ambapo Fungu Namba 49 kiliidhinishiwa jumla ya shilingi 458,900,981,000 ambapo kati ya fedha hizo shilingi 429,257,904,000 zilikuwa ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo na shilingi 31,643,077,000 zilikuwa ni kwa ajli ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu hizo zinaonesha kuwa kuongezeka kwa takwimu za fedha haina maana kwamba fedha hizo zitatolewa kwa uwiano wa bajeti. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuacha kupanga bajeti inayotoa matumaini lakini haina uhalisia katika utekelezaji wa miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiondoa fedha hizo za malimbikizo, fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa

bajeti ya 2015/2016 zilikuwa ni asilimia 64, shilingi 274,855,973,668. Kati ya hizo shilingi 510,377,900,552 zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeleta suala hili hapa ili kuonesha historia ya mkanganyiko katika mwenendo wa matumizi ya fedha za sekta ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kwenda mbele vizuri na mtiririko wa fedha za bajeti na matumizi yake kwa miaka inayofuatia, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata maelezo ya ziada kwa kina kwa niaba ya Watanzania watumiaji wa maji na walipa kodi kuhusu hizo shilingi 235,521,926,883.85 kutoka kwenye *earmarked projects.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarejea na kuelezea kwamba taarifa ya Hali ya Sekta ya Maji *(WSSR)* Oktoba*,* 2016 haijafafanua ni katika miaka ipi malimbikizo hayo ya *earmarked project funding* yamekuwa yakitolewa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali Dkt. Servacius Likwelile, mchana wa tarehe 11 Oktoba, 2014 kwa niaba ya Serikali alitiliana saini makubaliano ya mkataba wa kuanzisha Mradi wa Maji katika Wilaya ya Same na Mwanga na Mfuko wa maendeleo ya uchumi wa Kuwait akiwa Washington D.C.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko huo wa Maendeleo ya Uchumi wa Kuwait ulitoa Dola za Kimarekani milioni 34.0 sawa na shilingi bilioni 56.10 za Kitanzania kwa ajili ya kusaidia mradi wa maji katika Wilaya ya Same na Mwanga. Kambi Rasmi ya Upinzani inafahamu umuhimu wa mradi huo kwa wananchi wa maeneo husika hadi maeneo ya Wilaya ya Korogwe ambapo nao wangekuwa wanufaikaji wa mradi huo wa maji kutoka Bwawa la Nyumba ya Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata mrejesho wa mradi huo mkubwa wa maji

umefikia wapi kwa kuangalia utekelezaji kwa mujibu wa thamani ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu rasilimali za maji na usalama wa maji, hali halisi ya maendeleo ya maji nchini haiakisi Dira ya Maendeleo ya Taifa iliyotajwa hapo juu. Wizara ya Maji na Umwagiliaji inaelezea wazi kwamba Tanzania iliyokuwa na kiwango kikubwa cha uhakika wa maji inaelekea kuwa ni nchi yenye uhaba wa maji *(Water Stressed Country)* iwapo hatua madhubuti na za haraka hazitachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba iliyosomwa Bungeni na Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mei, 2016, inaelezea wazi kuwa kwa sasa rasilimali za maji zinatosheleza kumpatia kila Mtanzania mita za ujazo 1,952 kwa mwaka. Kiwango cha kimataifa za mahitaji ya mtu mmoja ni mita 1,700 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kiashiria cha kustua katika hotuba hiyo ni kile kilichoonyesha kuwa kama hatua za kiutawala, kitaalam na kisiasa hazitachukuliwa, upatikanaji wa maji kwa kila Mtanzania utashuka hadi kufikia mita za ujazo 883 kwa mwaka. Hali hii inatishia usalama na uhakika wa maji *(water security)* inayoweza kusabisha migogoro ya kijamii na mdororo wa uzalishaji katika sekta zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa mbalimbali za Kimataifa juu ya usalama na uhakika wa maji *(water security)* zinaoenesha wazi kuwa upungufu wa maji utachangia kwa kiasi kikubwa kuyumbisha Serikali na Tawala mbalimbali duniani. Inaelezwa bayana kuwa matatizo ya maji yanahitaji utatuzi wa haraka ili kuepusha janga la anguko la utawala wa nchi *(State Failure).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yoyote makini na inayotaka kuimarisha utawala wake ni lazima itambue, izingatie na kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wote bila ya ubaguzi, itatue changamato za umaskini

ikiwa ni pamoja na umaskini wa maji *(water poverty);* misuguano na migogoro ya kijamii itokanayo na masuala ya maji *(water conflicts)* na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ilivyo hivi sasa, haieleweki kama Serikali iliyopo madarakani imejipanga vya kutosha kuwahakikishia Watanzania uhakika na usalama wa maji. Zipo dalili nyingi za kukosekana kwa uhakika na usalama wa maji. Dalili hizo ni pamoja na migogoro kati ya wadau na watumiaji wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, methali ya kiswahili husema ni heri kuzuia kuliko kuponya. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Serikali ya Tanzania kwa msisitizo mkubwa sana kwamba ni lazima Serikali iwekeze rasilimali fedha na watu katika huduma za rasilimali za maji. Rasilimali za maji ndicho kitovu cha maji ya kunywa, kuendeshea viwanda, kilimo cha umwagiliaji na shughuli nyingine za kiuchumi na kijamii. Huduma hii ya rasilimali za maji ndiyo imekuwa ikiwekewa fedha kidogo zaidi katika bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Kwa kutoipa huduma ya raslimali za maji umuhimu unaostahili ina maana upungufu wa rasilimali za maji utageuka kuwa ni tatizo la kutengenezwa na watu kwa makusudi kabisa yaani *(man made problem).* Tatizo hili pia limepewa sifa ya kuwa siyo tu ni tatizo la kimfumo, bali ni tatizo la utawala usio bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti finyu kwa huduma ya rasilimali za maji unaonesha kuwa Serikali inakosa utashi wa kisiasa *(lack of political will)* wa kufanya maamuzi sahihi ya uwekezaji katika maendeleo endelevu ya sekta ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani katika hotuba zake hapa Bungeni imekuwa ikisisitiza na kuitaka Serikali kuanzisha Wakala wa Maji Vijijini na Serikali ilikubaliana na hoja hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi sana zikiwa ni kutoka kwa wahisani kwenye programu mbalimbali zinazohusu upatikanaji wa huduma

za maji vijijini. Kwa bahati mbaya sana, fedha hizo zimekuwa zikitumika vibaya kutokana na kutokuwepo kwa usimamizi wa kutosha na mwisho wa siku tatizo la upatikanaji maji linabakia pale pale. Mifano ni mingi hasa ile ya mradi wa visima kumi kwa kila Halmashauri zilivyotumika na tathmini yake bado wananchi hawana maji, kwani visima vilivyochimbwa havitoi maji na hivyo tatizo limebaki pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo, naomba kunukuu kile ambacho Kambi Rasmi ya Upinzani ilikisema humu Bungeni; katika Bunge la Kumi yaliyotolewa maoni kadhaa ndani ya Bunge lako Tukufu kuhusu uanzishwaji wa Wakala ya Maji Vijijini *(Rural Water Agency)* ikiwa na lengo la kuongeza utoaji na usimamiaji wa huduma ya maji kwa wananchi katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mjadala wa suala hili Serikali ilikubali kuundwa kwa wakala huyu kwa ajili ya huduma ya maji kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Lengo la kuundwa kwa wakala huyu lilitokana na kuwa na Wakala sawa na Wakala wa Umeme Vijijini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuhoji hatua zilizofikiwa na Serikali katika kuanzisha wakala huyu kama ambavyo iliahidi hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya maji, usafi wa mazingira na uondoshaji wa maji taka, ni ukweli kwamba miji mingi hapa nchini inapanuka na kuongeza wakazi wake kwa kasi kubwa kutokana na kukua kwa idadi ya Watanzania. Hivyo huduma ya maji safi na maji taka katika miji ni jambo la muhimu sana katika kuhakikisha afya za wakaazi kwa miji husika.

Kwa ujumla upatikanaji wa maji safi na salama katika miongo miwili iliyopita umepungua kidogo kutoka asilimia 55 hadi asilimia 53, na kwa wananchi wa vijijini, imeshuka kutoka asilimia 46 hadi asilimia 44 japokuwa fedha nyingi sana za walipakodi zimeelekezwa uko. Hii ni kwa mujibu wa utafiti wa TWAWEZA uliotolewa mwezi Aprili, 2014. Swali la kujiuliza tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto kubwa ya usambazaji maji usio na uhakika kwa watumiaji na hivyo kupelekea gharama kubwa za upatikanaji wa maji. Serikali imekuwa na taarifa nyingi zinazokinzana kuhusu upatikanaji wa uhakika wa maji hasa katika Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na mikoa jirani. Tumeambiwa kuhusiana na mradi wa uchimbaji wa visima virefu 20 vya Kimbiji na Mpera kama ndiyo mkombozi au suluhisho la maji kwa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani na kwa mujibu wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Miaka mitano mradi huu uliwekewa jumla ya shilingi bilioni 112. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, je, na Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ulikuwa ni kiini macho kama ulivyo huu wa pili?

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa bwawa la Kidunda ambalo kwa mujibu wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano, mradi uliwekwa kwenye mpango toka mwaka 2011/2012 kwa kuwekewa shilingi 26,800,000,000, na kwa miaka mitano 2015/2016 mradi ungetumia jumla ya shilingi bilioni 134 ikiwa shilingi bilioni 112 ni mchango wa Serikali na shilingi bilioni 22 toka kwa wahisani. Kwa maajabu makubwa, sasa hivi Randama inatuonesha kuwa gharama ya ujenzi wa bwawa hilo inatarajiwa kuwa shilingi bilioni 476.2. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema Serikali itaendelea kupata hasara na kutotimiza wajibu wake kwa Watanzania kama mtindo wa kutokuheshimu utekelezaji wa mipango iliyojiwekea utaendelea. Kupanda kwa gharama za utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda ni matunda ya kushuka kwa bei ya shilingi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa takwimu za Serikali zinaonesha kuwa upatikanaji wa maji safi na salama kwa maeneo ya mijini ni asilimia 59 na 26 kwa vijijini, hii ni takwimu kwa mujibu wa taarifa ya *demographic and socio economic profile* iliyotolewa na Idara kuu ya Takwimu mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifumo ya uondoaji wa maji taka kwa maeneo mengi ya mijini hasa maeneo ambayo

yalikuwa ni mashamba na sasa kutokana na kupanuka kwa miji yamekuwa ni maeneo ya makazi ni tatizo na ni jukumu binafsi la mmiliki wa makazi. Hii inatokana na ukweli kwamba wananchi wako mbele zaidi ya taasisi za Serikali ambazo ndizo zinatakiwa kupanga miji. Kwa upande mwingine tatizo kubwa ni kuwa miundombinu ya majitaka imezeeka kiasi cha kushindwa kuhimili taka zinazotolewa kutokana na ongezeko kubwa la wakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Serikali, kwa maeneo mapya ya makazi waweke mashine za kusafisha majitaka. Katika programu hii, Mradi wa Uboreshaji wa Mfumo wa Uondoaji wa Majitaka Jijini Dar es Salaam inaonesha kuwa mikopo toka Serikali ya Korea Kusini na Benki ya Dunia, lakini ukisoma vizuri Randama ukurasa wa 25 aya ya nne, mikopo hiyo ni kwa ajili ya kutandika mifumo mipya ya kusafirisha majitaka toka majumbani kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji. Kambi Rasmi inashauri maji taka hayo yasafishwe yawe *recycled* na yaingie tena kwenye matumizi, na ndiyo sababu yatatufanya kuwa mfano wa Singapore.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria hadi katika miji ya Nzega, Igunga, Tabora, Sikonge na Uyui. Mradi huu unahusisha malengo ya muda mrefu ya kuwapatia huduma ya maji wakazi wapatao milioni 1.1 kwa miji tajwa hapo awali pamoja na wananchi vijiji vilivyo kandokando ya bomba kuu la mradi wa Kahama. Mradi huu umegawanywa katika vipande vitatu vya ujenzi ili kuhakikisha kukamilika kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu utakuwa na kandarasi zenye thamani ya dola za Marekani 268.35 ambazo ni zaidi ya shilingi bilioni 600 za Tanzania mjini Tabora kwa mkopo wa Benki ya Exim ya nchini India kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzani kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria na kupeleka katika Manispaa ya Tabora na Halmashauri za Igunga, Uyui, Shinyanga Vijijini na Nzega. Kambi Rasmi ya Upinzani imepokea kwa masikitiko makubwa ya harufu za rushwa katika mchakato wa awali wa

kuwapata wakandarasi unaofanywa na watendaji wa Wizara ambao watakuwa ni wasimamizi wakuu wa mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nyaraka zinaonesha kuwa makampuni yaliyohusika katika zabuni ya ujenzi wa vipande vyote vitatu ni makampuni matano, majina tumeyahifadhi kwa usalama wa kibiashara, lakini moja kati ya makampuni hayo kwa ushahidi ilionesha kuwa kulikuwa na mchezo mchafu katika utoaji wa zabuni. Kwani bei ya zabuni kwa makampuni hayo matano zipo lakini vigezo ndivyo havikufuatwa katika utoaji wa zabuni hizo, *not always the lowest is the cheapest, what is needed is the competent supervisor* na hawa *engineers* ambao ni mahiri kusimamia tunao na wanalipwa vema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mlalamikaji alitoa ushahidi wake kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji na hakuna hatua zilizochukuliwa. Hii ni kasoro kubwa sana kwani jambo hili linatupa wasiwasi hata ukamilikaji wa mradi huu. Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa kina suala hili, kwani linamtia doa hata yeye ambaye ndiye msimamizi mkuu wa Wizara hii, kwani miongoni mwa malalamiko yaliyotajwa ni Afisa mmoja Wizarani kughushi *(forge) email* na kutunga uwongo uliotumika kufanya maamuzi ya nani apewe zabuni na nani asipewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Lindi Mjini; Mradi wa Maji Lindi Mjini eneo la Ng'apa unajengwa na Kampuni ya O*verseas Infrastructure Alliance Private Limited* ya India, mkandarasi huyo alianza kazi baada ya mradi kuzinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais Mstaafu Jakaya Kikwete tarehe 8 Agosti, 2015. Mradi huo unatekelezwa kwa mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW)* na Umoja wa Ulaya *(EU)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais katika ziara yake Mkoani Lindi alimtaka mkandarasi huyo kuhakikisha kuwa anakamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji wa Ng'apa

uliopo Mkoani Lindi unakamilika ndani ya miezi minne na si vinginevyo, siyo kuleta visingizio. Mheshimiwa Waziri alisema kuwa hadi sasa mradi huo umefikia asilimia 85 na kwamba mkandarasi amesimamisha kazi kutokana na kuishiwa fedha. Kambi Rasmi ya Upinzani inataarifa kuwa fedha za ujenzi wa mradi huo zimewekwa kwenye akaunti mkandarasi iliyopo nchini India na hivyo fedha hizo kukosa uangalizi wa msimamizi wa mradi huo *(consultant). (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za umwagiliaji; Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Fungu Namba 05. Kilimo cha umwagiliaji katika nchi hii kimekasimiwa chini ya mamlaka ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Fungu Na. 05. Takwimu zinatuonesha kuwa kwa nchi yetu ina jumla la hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa umwagiliaji na hekta milioni 2.3 zina uwezo mkubwa wa kumwagiliwa, hekta milioni 4.8 zina uwezo wa kati na hekta milion 22.3 zina uwezekano mdogo wa kumwagiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inawasiwasi kuwa, lengo la kufikia umwagiliaji wa hekta milioni moja kama litafikiwa, wakati tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda na kilimo ndiyo *engine* ya kutoa malighafi nyingi itakayohitajika katika viwanda. Ni dhahiri kwamba uwezekano mkubwa wa maandiko hayo yatabakia kwenye makabrasha tu na siyo utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni nchi ya kilimo, na uchumi wa viwanda utabebwa kwa kiasi kikubwa na kilimo. Ili kufikia azma ya uchumi wa viwanda, mikakati iliyopo katika sekta ya kilimo hususan kilimo cha umwagiliaji ni kupanua eneo la uzalishaji kwa takriban hekta milioni 1.5 ili kuongeza uzalishaji kwa asilimia 25 na kunufaisha zaidi ya kaya milioni 2.3 au watu wapatao milioni 12. Ndoto hii ya kukuza uzalishaji haitakamilika iwapo fedha zilizoidhinishwa na Bunge hazitatolewa ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa umwagiliaji wa Kiwalala katika Bonde la Lukuledi Halmashauri ya Wilaya ya

Lindi, umegharimu zaidi ya shilingi milioni 600 hadi sasa mradi haufanyi kazi. Na maelezo yanayotolewa ni kwamba mkandarasi alikosea wakati amafanya usanifu, hivyo kwa eneo uliopo haliwezi kutoa tija na hivyo mradi ndio umekufa kifo cha mende kama miradi mingine mingi kama vile Kinyope uliopo katika Jimbo la Mchinga ambao una hekta 400.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu unaonesha bila ya kuwa na uhakika na usalama wa maji, azma ya kupanua kilimo na kukifanya kiwe cha kisasa, endelevu na hatimaye kupata mapinduzi ya viwanda itabakia kuwa ni nadharia kwenye makabrasha tu, bila ya kuwa na utekelezaji wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukweli kwamba tunakokwenda tutakuwa na upungufu mkubwa wa maji kwa ajili ya matumizi ya kibinadamu, kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Hivyo katika kutekeleza jukumu hilo la umwagiliaji ni lazima Tume ya Umwagiliaji ichague aina ya umwagiliaji ambayo itatumia maji kidogo wakati huo kuzalisha kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, *District Agriculture Sector Investment Project (DASIP)* ni mradi uliokuwa wa miaka saba, ulianza mwaka 2006 hadi 2013 na mradi ulihusisha Wilaya 28 za Mikoa ya Kagera, Kigoma, Mara, Mwanza na Shinyanga ambao ulikuwa ni mkopo wa *Unit of Account (UA)* milioni 58.01 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB).* Mradi ulitekelezwa kupitia mfumo wa *ASDP* katika utaratibu wake wa utekelezaji wa miradi chini ya *Project Coordination Unit*. *UA* pamoja ni sawa na dola za kimarekani bilioni 1.567 mwaka 2009 kwa thamani ya mwaka huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ulikuwa na lengo la kuongeza tija na mapato kwa jamii ambazo ni wanufaikaji wa mradi na progamu nzima ya *DASIP*. Mradi huu ulihusisha skimu za umwagiliaji 23 zilizokuwa na thamani ya shilingi 16,600,251,799.40.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hotuba yangu

ni ndefu naomba maelezo yangu yote na hotuba yangu yote yaingie kwenye *Hansard* nan a ninaomba nihitimishe hotuba yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuangalia takwimu za maombi ya fedha za maendeleo kwa Wizara Fungu 49 zinaonesha kuwa ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bobali hutaweza tena kuendelea wewe hitimisha dakika moja nimekupa.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, ni muda muafaka sasa wananchi kushirikishwa katika shughuli za maendeleo yanayowahusu, kwani wao ndiyo watakuwa wasimamizi wakubwa wa miradi husika, badala ya tabia iliyopo sasa ya wao kuona watu wanafanyakazi nao kuwa watazamaji tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI MHESHIMIWA HAMIDU HASSAN BOBALI (MB) WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Yanatolewa chini ya Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99(9), toleo la mwaka 2016)*

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia afya njema inayoniwezesha

kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa naomba nichukue fursa hii adhimu kumpongeza Mhe. Peter Lijualikali (Mb), Naibu Msemaji Mkuu wa Wizara hii kwa kufanikiwa kuandika historia adhimu ya kuhukumiwa kufungwa jela wakati akiwa anapambana kuwatetea wapiga kura wake wa Jimbo la Kilombero, pia akiwa anatetea haki yake ya kupiga kura katika halmashauri ambayo yeye ni Mbunge wa kuchaguliwa.

**Mheshimiwa Spika,** nampongeza Mhe. Lijualikali sio tu kwa kuwa ameshinda rufaa yake na hivyo kuwa huru kuwatumikia wapigakura wake, bali pia kitendo chake cha kufungwa huku akiwa mbunge wakati hakuwa na makosa. Hii imeionesha Dunia kuwa wanaofungwa katika nchi yetu sio kuwa wote wanakuwa na hatia. Jina lake litakuwa rejea mbalimbali katika vitabu na majarida mbalimbali Duniani kote. Lijualikali umekuwa mwakilishi wa wanaofungwa bila hatia na shujaa wa vijana wote wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa ni shukrani kwa wanachama wa CUF na wananchi wa Jimbo la Mchinga kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa katika utendaji kazi wangu wa shughuli za kibunge na kichama, bila kusahau kwa umoja wetu ndiyo silaha ya kuhakikisha bwana Yule anaondoka kwa aibu.

## 2.0 MUUNDO NA MFUMO WA KISEKTA

**Mheshimiwa Spika,** ninapowasilisha hotuba hii ya Wizara Kivuli ya Maji na Umwagiliaji kutoka katika Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ninaomba niazime tamko la kauli mbiu za kitaifa na kimataifa kuhusu umuhimu wa maji. Kauli mbiu hizi ni pamoja na tamko la Kimataifa kwamba ***"Maji ni Haki ya Kibinaadamu, Maji ni Uhai, Maji ni Uchumi; Maji ni Msingi wa Amani na Maji ni Siasa".***

***Mheshimiwa Spika,*** *kabla ya kuingia kwa undani katika utoaji*

*wa maoni na uchambuzi wa wizara, Kambi Rasmi inamtaka Mheshimiwa Waziri awaeleze watanzania kwa kujibu swali hili, maji ni huduma au biashara?*

**Mheshimiwa Spika,** umuhimu wa maji kwa ajili ya uhai wa watu, wanyama, mimea na mazingira kwa ujumla ni jambo lisilopingika. Bila ya maji, viumbe vyote vitapotea, mazingira yatakuwa mfu, na maendeleo ya kiuchumi na ya kijamii yatadumaa.

Kutokana na umuhimu wa maji, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa katika kikao chake cha tarehe 21 Desemba 2016 limeridhia kwa kauli moja miaka kumi ya utekelezaji wa **Azimio jipya la Maji kwa Maendeleo Endelevu (Interational Decade (2018-2028) for Action- Water for Sustainable Development).**

**Mheshimiwa Spika,** Dira ya Maendeleo ya Taifa (Tanzania Development Vision 2025) imeweka malengo ya maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na ustawi jamii ikiwa ni pamoja na malengo yanayogusa moja kwa moja Wizara na Sekta ya Maji na Umwagiliaji. Baadhi ya malengo muhimu katika muktadha huu ni kama ifuatavyo:

i. Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati, ambapo wananchi wake wanafurahia amani na umoja wa kitaifa

ii. Upatikanaji wa maji safi na salama kwa wakazi wote. Ambapo kwa wakazi wa mijini watapata maji kwa asilimia 100 na kwa wakazi wa vijijini watapata maji safi na salama kwa agalau asilimia 90 ifikapo 2025.

iii. Kuhakikisha kwamba raslimali za maji ni endelevu ili kukidhi mahitaji ya kiuchumi na kijamii.

**Mheshimiwa Spika, i**li kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji inatekeleza programu kuu zifuatazo:

i. Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (Water Sector Development Programme- WSDP)

ii. Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (Sekta ya Umwagiliaji inayosimamiwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji).

**Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (Water Sector Development Programme- WSDP) ni mradi wa muda mrefu wa utekelezaji wa miaka ishirini. Utekelezaji wake ulianza mwaka 2006 na utafikia ukomo wa utekelezaji mwaka 2025 ambapo inategemewa kuwa viwango vya upatikanaji wa maji safi na salama na usalama wa maji kwa ujumla vitakuwa vimefikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuwezesha utekelezaji wa programu kubwa ya kiwango cha WSDP ya Tanzania, programmu imegawanywa katika awamu kuu nne za utekelezaji, ambapo kwa sasa awamu ya kwanza iliyochukua takriban miaka minane imemalizika, na sasa awamu ya pili inatekelezwa Muundo na mfumo wa utekelezaji umegawanya programu hii katika sehemu kuu zifuatazo:

i. Usimamizi wa Raslimali za Maji.
ii. Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini
iii. Huduma ya Maji Usafi wa Mazingira na Uondoshaji wa Maji Taka Mijini
iv. Usafi wa Mazingira na Usafi Mashuleni (National Sanitation Campaign and School WASH)
v. Mfumo wa Uwezeshaji wa Utekelezaji wa Programmu (Programme Delivery Support)

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa programu hii unafanyika kwa kuzingatia sera kuu za maendeleo ya taifa, Sera za kisekta kama vile Sera ya Maji ya mwaka 2002; Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (Decentralization by Develution); Mikakati ya Kupunguza Umaskini nchini, na Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano. Majukumu na wajibu wa wadau wa Sekta ya Maji hususan wale wanaohusika na utekelezaji wa programmu hii wanatajwa kuwa katika ngazi ya Taifa ni pamoja na Wizara ya Maji yenyewe, Wizara za

Afya, Elimu na Ofisi ya Raisi Tawala Za Mikoa na Serikali za Mitaa, na washirika wa kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na taasisi za kifedha za Kitaifa na kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002, imeweka bayana umuhimu wa Sekta Binafsi (private sector) katika utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa Tanzania. Hivyo basi sekta binafsi ni mmoja kati ya wadau wakuu wanaotoa huduma kama vile za utafiti; uchimbaji na ujenzi wa miundombinu, fedha, utawala, mafunzo, na upatikanaji wa vipuri.

**Mheshimiwa Spika,** Katika ngazi za Kanda, Mikoa, Wilaya na Vijiji programu inatekelezwa kupitia Bodi za Mabonde ya Maji (Basin Water Boards); Mamlka za Maji Mijini na kipekee kwa sababu ya unyeti wake Mamlaka ya Maji ya jiji la Dar-es-Salaam; Mamlaka za Maji katika makao makuu ya Wilaya na Miji Midogo; na Halmashauri za Wilaya kupitia idara ya Mhandisi wa Maji. Katika ngazi ya kijiji, wadau wakuu wa usambazaji wa maji safi na salama kwa wananchi ni pamoja na Serikali za Vijiji, na Vyombo vya Watumiaji wa Maji (Community Owned Water Supply Organisations) ambavyo ni taasisi rasmi za kijamii zenye mamlaka ya kisheria za kuendesha vituo vya usambazaji wa maji vijijini.

**Mheshimiwa Spika, n**imeona ni vyema kutumia fursa hii kuelezea kwa kina muundo na mfumo wa utoaji wa huduma ya Maji safi na Salama kwa Umma wa Watanzania kupitia Bunge lako Tukufu kwa sababu mpaka hivi sasa bado watanzania wengi wa mijini na vijini bado hawana ufahamu wa mabadiliko yaliyofanywa katika Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002 (National Water Policy – NAWAPO 2002); pamoja na utekelezaji wake kupitia Programmu ya Taifa ya Maendeleo ya Maji.

**Mheshimiwa Spika,** Ikumbukwe ya kwamba utekelezaji wa WSDP unafanywa kupitia sheria kuu mbili za maji pamoja na kanuni zake na miongozo mbali mbali yaani Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2009; na Sheria ya Raslimali za Maji ya Mwaka huo huo.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kuwa na mfumo maalum wa kitaasisi kwenye sekta kwa ajili ya uwezeshaji na uendeshaji wa programmu, ufahamu wa watanzania kuhusu mabadiliko ya kisera, kisheria na kitaasisi ndani ya sekta ya bado ni mdogo, jambo ambalo linadhoofisha kanuni ya ushirikishaji, utawala bora na uwazi katika uboreshaji na utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira mijini na vijijini.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa mbali mbali za utafiti kuhusu ushiriki wa jamii na wadau mbali mbali wa Sekta ya Maji katika utekelezaji wa WSDP unaonesha kuwa wadau wengi hawana ufahamu wa miundo na mifumo ya programmu jambo linalochangia utekelezaji hafifu wa mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Nitatoa mifano michache kuhusu jambo hili. Hali halisi ilivyo huko vijijini inaonesha kuwa bado vijiji vingi nchini vinatekeleza shughuli za usambazaji wa maji kupitia "kamati za maji' na siyo Vyombo vya Watumiaji wa Maji (COWSOs) kama inavyotakiwa kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kutambua umuhimu wa maji kwa wananchi wa Tanzania imefuatilia kwa kina utekelezaji wa WSDP awamu ya Kwanza na WSDP awamu ya II.

**Mheshimiwa Spika**, Kati ya changamoto zilizooneshwa katika utekelezajiwa wa awamu ya kwanza ya Programu ni programu awamu ya kwanza na vile vile katika utekelezaji wa mpango na bajeti 2016/17 suala la uundaji wa Vyombo vya Watumiaji wa Maji limebaki kuwa ni changamoto kubwa na linalochangia kwa kuharibika kwa miundobinu ya maji kwa kasi kubwa, kwa kukosekana ka usimamizi wa karibu wa miundo mbinu ya maji karibu na vituo vya kuchotea maji.
**Mheshimiwa Spika,** kulingana na taarifa za hivi karibuni, Tanzania inapiga hatua moja mbele katika kutoa huduma ya maji lakini inarudi hatua mbili nyuma katika utoaji wa huduma hiyo kutokana na kuharibika kwa miundombinu na upotevu mkubwa wa maji safi na salama yanayozalishwa kwa fedha nyingi

**Mheshimiwa Spika,** Wataalamu na Wadau wa Sekta ya Maji wanajuliza maswali mengi na hivi karibuni kupitia ukurasa wa Mtandao wa taasis bobezi ya Maji kumekuwa na swali la msingi kama ifuatavyo na ninanukuu kwa kiingereza kama ilivyo:

> *"Despite massive investments in rural water supply in Tanzania, the number of people with access to improved water sources has not increased. This begs the question, what could be the reason for this stagnation?"*
>
> (http://www.ircwash.org/blog/rural-water-supply-access-tanzania-why-has-it-stagnated)

**Mheshimiwa Spika**, taarifa iliyotolewa na wataalmu hao ni kwama kwa kila mtanzania mmoja anayepata huduma ya maji safi na salama, wapo wawili wanaokosa huduma hiyo, hususan vijijini. Taarifa hiyo ikinukuu taarifa za mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa kimataifa juu ya maendeleo ya maji na usafi wa mazingira unaonesha kuwa upatikanaji na usambazaji wa maji ni mdogo sana kulinganisha na takwimu zinazotolewa na Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka wizara ya Maji ituambie je, ni kwa kiasi gani Wizara ya Maji imewianisha mfumo wake wa tathmini na ule wa Ufuatiliaji na Tathmini wa kimataifa (joint Monitoring programme au JMP?). Je tuamini kipi kati ya takwimu za Kitaifa na zile za JMP? Na sababu ya kuamini kimojawapo ni nini?

**Mheshimiwa Spika,** Kambi ya Upinzani Bungeni inaamini kuwa Mkakati wa Maendeleo Endelevu wa Sekata ya Maji (Sustainability Strategy) ulioandaliwa na kuasisiwa na Sekta hii kwa fedha nyingi za walipa kodi wa Kitanzania na wale wa nchi za nje haujapewa kipaumbele stahiki hususan katika suala la kuanzisha na kuwezesha Vyombo vya Usimamizi wa Maji. Kwa sababu hiyo fedha nyingi zinazowekezwa kwenye sekta hii hupotea bure.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kuuelezea umma wa watanzania masuala yafuatayo:

i. Ni kiasi gani cha fedha kimetumika katika kuanzisha na kuimarisha vyombo vya watumiaji maji vijijini?

ii. Ni mkakati upi utatumika ili kuhakikisha kuwa vyombo ya watumiaji maji vinaundwa, vinaimarishwa na kusajiliwa rasmi ili kuwezesha utekelezaji wenye tija wa WSDP II vijijini?

iii. Kwa vile uwepo wa vyombo vya watumiaji maji ni sehemu ya Kigezo cha kupata Rusuku ya Maji inayojulikana kama "malipo kwa Matokeo" ni hatua zipi zimechukuliwa kufidia halmashauri amabzo zimekosa kupata ruzuku hiyo kwa kukosa sifa kutokana na kutokuwepo kwa vyombo vya watumiaji maji ?

## 3.0 UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA MAJI: BAJETI ZA SEKTA NA MWENENDO WAKE

**Mheshimiwa Spika,** Mpaka kufikia mwisho wa utekelezaji wa Awamu ya kwanza ya Programmu ya Maendeleo ya maji mnamo Juni 30 2016,fedha zilizowekezwa katika programu zilikuwa ni Dola za Kimarekani 1,713.5

Awamu ya pili ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya ya Maji. Programu hii ina sifa ya kuwa ni programu kubwa na pengine yenye kugharimu fedha nyingi kuliko programu nyingine za kitaifa barani Afrika *(MoWI: 2013 'WSDP Tanzania Evaluation of Phase 1).*

**Mheshimiwa Spika,** Ninaomba pia kurejea bajeti za Sekta za maji na umwagiliaji kwa mwaka 2016/17, ili kuweka kumbukumbu vizuri. Katika Mwaka huo wa fedha, Wizara iliomba na kuidhinishiwa bajeti za Sekta za Maji na Umwagiliaji yaani kifungu namba 49 na kile cha namba 05 kama ifuatavyo:

### 3.1 HUDUMA ZA MAJI

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya maji (kifungu 49) mwaka wa fedha 2016/17 iliombewa bajeti ya Tshs 939,631,302,771 ambapo kati ya hizo, Tshs 915,193,937,771 ni kwa ajili ya maendeleo na Tshs 24,437,365,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida yaani mishahara na matumizi mengineyo.

Bajeti hii ni takriban maradufu ya ile iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha uliopita yaani 2015/2016, ambapo kifungu namba 49 kiliidhinishiwa jumla ya Tshs 458,900,981,000 ambapo kati ya fedha hizo Tshs 427,257,904,000 zilikuwa ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo na Tshs 31,643,077,000 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, lakini hadi mwisho wa mwaka wa bajeti 2015/16 Wizara ilipokea fedha za maendeleo jumla ya shilingi 141,244,873,622 ambazo ni sawa na asilimia 33.06 ya fedha zilizokuwa zimeidhishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2017 fedha za maendeleo ambazo zilikuwa zimepokelewa na Wizara ni shilingi 181,209,812,609 sawa na asilimia 19.8 tu ya fedha zilizokuwa zimetengwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu hizo zinaonesha kuwa kuongezeka kwa takwimu za fedha haina maana kwamba fedha hizo zitatolewa kwa uwiano wa bajeti. Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuacha kupanga bajeti inayotoa matumaini lakini haina uhalisia katika utekelezaji wa miradi.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya hali ya Sekta ya Maji ya Oktoba 2016 (Water Sector Status Report October 2016) imedhihirisha kuwa kufikia Juni 2016, fedha zilizopokelewa na Wizara kwa ajili ya utekelezeji wa programmu zilikuwa ni Tshs 510,377,900,552.22, ambapo kati ya hizo Tshs 235,521,926,883.85 zilitokana na malimbikizo ya fedha za nyuma kutoka kwa washirika wa maendeleo wanaotekeleza miradi maalum

yaani ***earmarked projects***. Ukiondoa fedha hizo za malimbikizo, fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya 2015/2016 zilikuwa ni aslimia 64, yaani Tshs 274,855,973,668.37 kati ya 510,377,900,552.22, zilizoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeleta suala hili hapa ili kuonesha historia ya mkanganyiko katika mwenendo wa matumizi ya fedha za sekta ya Maji.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kwenda mbele vizuri na mtiririko wa fedha za bajeti na matumizi yake kwa miaka inayofuatia, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata maelezo ya ziada /kina kwa niaba ya watanzania watumiaji wa maji na walipa kodi; kuhusu hizo Tshs Tshs 235,521,926,883.85 kutoka kwenye ***earmarked projects.***

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inarejea na kuelezea kwamba taarifa ya Hali ya Sekta ya Maji (WSSR Ocober 2016) haijafafanua ni katika miaka ipi malimbikizo hayo ya ***"earmarked project funding"*** yamekuwa yakitolewa taarifa. Pili tunataka maelezo ya kina namna ambavyo fedha hizo zilivyoidhinishwa na baadaye kuingizwa kwa ujumla wake katika taarifa hiyo ya WSSR ya Okoba 2016.

**Mheshimiwa Spika,** Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa serikali Dr. Servacius Likwelile, mchana wa tarehe 11.10.2014 kwa niaba ya Serikali alitiliana saini makubaliano ya mkataba wa kuanzisha Mradi wa Maji katika Wilaya ya Same na Mwanga, na Mfuko wa maendeleo ya uchumi wa Kuwait akiwa Washington D.C

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko huo wa Maendeleo ya Uchumi wa Kuwait ulitoa Dola za Kimarekani milioni 34.0 sawa na shilingi Bilioni 56.10 za Kitanzania kwa ajili ya kusaidia mradi wa maji katika Wilaya ya Same na Mwanga. Kambi Rasmi ya Upinzani inafahamu umuhimu wa mradi huo, kwa wananchi wa maeneo husika hadi maeneo ya Wilaya ya Korogwe ambao nao wangekuwa wanufaikaji wa mradi huo wa maji kutoka bwawa la Nyumba ya Mungu.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata mrejesho wa mradi huo mkubwa wa maji umefikia wapi kwa kuangalia utekelezaji kwa mujibu wa thamani ya fedha?

### 3.1.1 Raslimali za Maji na Usalama wa maji

**Mheshimiwa Spika,** Hali halisi ya maendeleo ya maji nchini haiakisi Dira ya Maendeleo ya Taifa iliyotajwa hapo juu. Wizara ya Maji na Umwagiliaji inaelezea wazi kwamba Tanzania iliyokuwa na kiwango kikubwa cha uhakika wa maji inaelekea kuwa ni nchi yenye 'UHABA wa MAJI" ***(Water Stressed Country)*** iwapo hatua mathubuti na za haraka hazitachukuliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Hotuba iliyosomwa Bungeni na Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mei 2016, inaelezea wazi kuwa kwa sasa, raslimali za maji zinatosheleza kumpatia kila Mtanzania mita za ujazo 1,952 kwa mwaka. Kiwango cha kimataifa za mahitaji ya mtu mmoja ni mita 1,700 kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo kiashiria cha kustua katika hotuba hiyo ni kile kinachoonesha kuwa kama hatua za kiutawala, kitaalamu na kisiasa hazitachukuliwa, upatikanaji wa maji kwa kila Mtanzania utashuka hadi kufikia mita za ujazo 883 kwa mwaka. Hali hii inatishia usalama na uhakika wa maji ***(water security)*** inayoweza kusabisha migogoro ya kijamii na mdororo wa uzalishaji katika sekta zote.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa mbali mbali za kimataifa juu ya usalama na uhakika wa maji (***Water Security***) zinaoenesha wazi kuwa upungufu wa maji utachangia kwa kiasi kikubwa kuyumbisha Serikali na Tawala mbali mbali duniani. Inaelezewa bayana kuwa matatizo ya maji yanahitaji utatuzi wa haraka ili kuepusha janga la anguko la utawala wa nchi yaani '***State Failure'***

**Mheshimiwa Spika,** Serikali yoyote makini na inayotaka kuimarisha utawala wake ni lazima itambue, izingatie na kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wote bila ya ubaguzi; itatue changamato za umasikini ikiwa ni

pamoja na umasikini wa maji yaani ***Water Poverty***; misuguano na migogoro ya kijamii itokanayo na masuala ya maji (***Water Conflicts)***, na uharibifu wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa hali ilivyo hivi sasa, haieleweki kama Serikali iliyopo madarakani imejipanga vya kutosha kuwahakikishia Watanzania uhakika na usalama wa maji. Zipo dalili nyingi za kukosekana kwa uhakika na usalama wa maji. Dalili hizo ni pamoja na migogoro kati ya wadau na watumiaji wa maji

**Mheshimiwa Spika,** Methali ya Kiswahili husema 'ni heri kuzuia kuliko kuponya', Kambi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Serikali ya Tanzania kwa msisitizo mkubwa sana kwamba ni lazima zerikali iwekeze raslimali fedha na watu katika huduma za Raslimali za Maji. Raslimali za Maji ndicho kitovu cha maji ya kunywa, kuendeshea viwanda, kilimo cha umwagiliaji na shughuli nyingine za kiuchumi na kijamii. Huduma hii ya raslimali za maji ndiyo imekuwa ikiwekewa fedha kidogo zaidi katika bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kutoipa huduma ya Raslimali za Maji umuhimu unaostahili ina maana upungufu wa raslimali za maji utageuka kuwa ni tatizo la kutengenezwa na watu kwa makusudi kabisa yaani ***'man made problem'. Tatizo hili pia limepewa sifa ya kuwa siyo tu ni tatizo la kimfumo, bali ni tatizo la utawala usio bora***. Bajeti finyu kwa huduma ya Raslimali za Maji unaonesha kuwa Serikali inakosa utashi wa kisiasa (lack of political Will) wa kufanya maamuzi sahihi ya uwekezaji katika maendeleo endelevu ya Sekta ya Maji.

### 3.1.2 Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani katika Hotuba zake hapa Bungeni imekuwa ikisisitiza na kuitaka Serikali kuanzisha wakala wa maji vijijini, na Serikali ilikubaliana na hoja hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi

sana zikiwa ni kutoka kwa wahisani kwenye programmu mbalimbali zinazohusu upatikanaji wa huduma za maji vijijini. Kwa bahati mbaya sana fedha hizo zimekuwa zikitumika vibaya kutokana na kutokuwepo kwa usimamizi wa kutosha na mwisho wa siku tatizo la upatikanaji maji linabakia pale pale. Mifano ni mingi hasa ile ya mradi wa visima 10 kwa kila Halmashauri zilivyotumika na tathmini yake bado wananchi hawana maji, kwani visima vilivyochimbwa havitoi maji na hivyo tatizo kubakia pale pale.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muktadha huo, naomba kunukuu kile ambacho Kambi Rasmi ya Upinzani ilikisema humu bungeni ;

> *"**Mheshimiwa Spika**, katika Bunge la kumi yaliyotolewa maoni kadhaa ndani ya Bunge lako tukufu kuhusu uanzishwaji wa Wakala ya Maji Vijijini (**Rural Water Agency**) ikiwa na lengo la kuongeza utoaji na usimamiaji wa huduma ya maji kwa wananchi katika maeneo ya Vijijini.*
>
> ***Mheshimiwa Spika**, katika mjadala wa suala hili serikali ilikubali kuundwa kwa Wakala huyu kwa ajili ya huduma ya maji kwa mwaka wa fedha 2015/2016.*
>
> ***Mheshimiwa Spika**, lengo la kuundwa kwa Wakala huyu lilitokana na kuwa na Wakala sawa na Wakala wa Umeme Vijijini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuhoji hatua zilizofikiwa na serikali katika kuanzisha Wakala huyu kama ambavyo iliahidi hapa Bungeni."*

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu mchakato wa uanzishwaji wa wakala huu wa maji vijijini umefikia wapi?

### 3.1.3 Huduma ya Maji, Usafi wa Mazingira na Uondoshaji wa Maji Taka Mijini

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kwamba miji mingi hapa nchini

inapanuka na kuongeza wakazi wake kwa kasi kubwa kutokana na kukua kwa idadi ya watanzania, hivyo huduma ya maji safi na maji taka katika miji ni jambo la muhimu sana katika kuhakikisha afya za wakaazi kwa miji husika.

**Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa maji safi na salama ni changamoto kubwa kwa watu wengi nchini Tanzania. Ingawa kimataifa, Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDG) ya usambazaji wa maji yamefikiwa, upatikanaji wa maji safi nchini Tanzania umezorota. Kwa miongo kadhaa nchi imekuwa nyuma zaidi ya nchi nyingine ambazo ziko kwenye ngazi sawa kimaendeleo na kijiografia.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla, upatikanaji wa maji safi na salama katika  miongo miwili iliyopita umepungua kidogo kutoka 55% hadi 53%, na kwa wananchi wa vijijini, imeshuka kutoka 46% hadi 44%. Japokuwa fedha nyingi sana za walipakodi zimeelekezwa uko. Hii ni kwa mujibu wa utafiti wa Twaweza uliotolewa mwezi Aprili 2014, swali la kujiuliza tatizo liko wapi?

**Mheshimiwa Spika,** tafiti za twaweza zinazidi kuonesha kuwa zaidi ya Watanzania watatu kati ya wanne (76%) wanakiri kuwepo kwa changamoto za aina mbalimbali za upatikanaji wa maji. Changamoto kubwa inayotajwa na idadi kubwa ya wakazi mijini na vijijini ni umbali wa kuvifikia vyanzo vya maji. Pia ongezeko kubwa la bajeti ya maji kwa kila Mtanzania kutoka chini Tsh 1,000 hadi zaidi ya Tsh 3,000 katika miaka kumi iliyopita wakati kuna maboresho kwa mujibu wa bajeti zinazopitishwa.

**Mheshimiwa Spika,** kuna changamoto kubwa ya usambazaji maji usio na uhakika kwa watumiaji na hivyo kupelekea gharama kubwa za upatikanaji wa maji. Serikali imekuwa na taarifa nyingi zinazokinzana kuhusu upatikanaji wa uhakika wa maji hasa kwa Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na mikoa jirani. Tumeambia kuhusiana na mradi wa uchimbaji wa visima virefu 20 vya Kimbiji na Mpera kama ndio mkombozi au suluhisho la maji kwa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani na kwa mujibu wa Mpango wa Kwanza

wa Maendeleo ya miaka mitano mradi huu uliwekewa Jumla ya shilingi bilioni 112. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, je na mpango wa kwanza wa maendeleo ulikuwa ni kiini macho kama ulivyo huu wa pili?

**Mheshimiwa Spika**, Ujenzi wa bwawa la Kidunda ambalo kwa mujibu wa mpango wa kwanza wa maendeleo wa miaka mitano mradi uliwekwa kwenye mpango toka mwaka 2011/12 kwa kuwekewa shilingi 26,800,000,000, na kwa miaka mitano 2015/16 mradi ungetumia jumla ya shilingi bilioni 134 ikiwa shilingi bilioni 112 ni mchango wa Serikali na shilingi bilioni 22 toka kwa wahisani. Lakini kwa maajabu makubwa, sasa hivi Randama inatuonesha kuwa gharama ya ujenzi wa bwawa hilo inatarajiwa kuwa shilingi bilioni 476.2

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, Serikali itaendelea kupata hasara na kutotimiza wajibu wake kwa watanzania kama mtindo wa kutokuheshimu utekelezaji wa mipango iliyojiwekea utaendelea. Sasa kupanda kwa gharama za utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bwawa la Kidunda ni muda na kushuka kwa bei ya shilingi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** ni muda mwafaka kwa Serikali kuwapa taarifa zenye uhakika wananchi kuhusu upatikanaji wa uhakika wa huduma za maji kwa wakazi wa maeneo ya miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, japokuwa takwimu za Serikali zinaonesha kuwa upatikanaji wa maji safi na salama kwa maeneo ya mijini ni asilimia 59 na 26 kwa vijijini, hii ni kwa mujibu wa taarifa ya “demographic and socio economic profile” iliyotolewa na Idara kuu ya Takwimu mwaka 2014.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Utafiti wa Sauti za Wananchi-Twaweza, uliotolewa mwezi Mach,2017 umeonesha ya kwamba Upatikanaji wa maji vijijini ulikuwa asilimia 55 mwaka 2014 na asilimia 46 mwaka 2016 – **Ofisi ya Taifa ya takwimu** inaonyesha tofauti ya upatikanaji wa maji kuwa kati ya asilimia 40 na 50 kwa zaidi ya miaka 10 ambapo tafiti tisa kati ya kumi zimeonesha uwiano wa takwimu ndani

ya kiwango hiki. **Wizara ya Maji** nayo imeripoti upatikanaji mkubwa wa maji wa kati ya asilimia 50 na 60 ndani ya kipindi tajwa.Takwimu za **Matokeo Makubwa Sasa** zinaripoti kuongezeka kwa kasi ya upatikanaji wa maji kutoka asilimia 40 mwaka 2013 hadi asilimia 67 mwaka 2015. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hali halisi ilivyo kwa sasa mwaka 2017.

**Mheshimiwa Spika,** mifumo ya uondoaji wa maji taka kwa maeneo mengi ya mijini hasa maeneo ambayo yalikuwa ni mashamba na sasa kutokana na kupanuka kwa miji yamekuwa ni maeneo ya makazi ni tatizo na nijukumu binafsi la mmiliki wa makazi.

**Mheshimiwa Spika,** Hii inatokana na ukweli kwamba wananchi wako mbele zaidi ya taasisi za serikali ambazo ndizo zinatakiwa kupanga miji. Kwa upande mwingine tatizo kubwa ni kuwa miundombinu ya maji taka imezeeka kiasi cha kushindwa kuhimili taka zinazotolewa kutokana na ongezeko kubwa la wakaazi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Serikali, kwa maeneo mapya ya makazi waweke mashine za kusafisha maji taka na maji hayo kuingia kwenye mzunguko mpya wa matumizi. Mfano mzuri ni nchi ya Singapore, ambapo maji taka tani milioni 7.5 huzalishwa kwa mwaka na kila mtu anazalisha kilo 1,370 kwa mwaka. Lakini uchafu huo 60% unawekwa kwenye mzunguko na kuwa na matumizi mapya kwa maendeleo ya nchi, ni vyema tukaangalia mbele zaidi katika mipango yetu.
**Mheshimiwa Spika**, katika program hii, Mradi wa Uboreshaji wa Mfumo wa Uondoaji wa Majitaka Jijini Dar es Salaam inaonesha kuwa mikopo toka Serikali ya Korea Kusini na Benki ya Dunia, lakini ukisoma vizuri Randama uk.25 aya ya (iv) mikopo hiyo ni kwa ajili ya kutandika mifumo mipya ya kusafirisha majitaka toka majumbani kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji. Lakini Kambi Rasmi inashauri maji taka hayo ya safishwe au “recycled” na yaingie tena kwenye matumizi. Na ndio sababu iliyotufanya kuweka mfano wa Singapore

### 3.1.4. Mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Viktoria hadi katika miji ya Nzega,Igunga, Tabora,Sikonge na Uyui

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusisha malengo ya muda mrefu ya kuwapatia huduma ya maji wakazi wapatao milioni 1.1 wa miji tajwa hapo awali pamoja na wananchi vijiji vilivyo kandokando ya bomba kuu la mradi wa Kahama. Mradi huu umegawanywa katika vipande vitatu vya ujenzi ili kuharakisha kukamilika kwake.

**Mheshimiwa Spika**, mradi mzima utakuwa na kandarasi zenye thamani ya dola za Marekani Milioni 268.35 ambazo ni zaidi ya Shilingi bilioni 600 za Tanzania mjini Tabora kwa mkopo wa benki ya Exim ya nchini India kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzani kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji kutoa Ziwa Victoria na kupeleka katika Manispaa ya Tabora na Halmashauri za Igunga, Uyui, Shinyanga Vijijini na Nzega.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani imepokea masikitiko makubwa ya harufu za rushwa katika mchakato wa awali wa kuwapata wakandarasi unaofanywa na watendaji wa Wizara ambao watakuwa ni wasimamizi wakuu wa mradi huu.

**Mheshimiwa Spika,** nyaraka zinaonesha kuwa makampuni yaliyohusika katika zabuni ya ujenzi wa vipande vyote vitatu ni makampuni matano (5),majina tumeyahifadhi kwa usalama wao kibiashara, lakini moja kati ya makampuni hayo kwa ushahidi ilionesha kuwa kulikuwa na mchezo mchafu katika utoaji wa zabuni. Kwani bei ya zabuni kwa makampuni hayo matano zipo lakini vigezo ndivyo havikufuatwa katika utoaji wa zabuni hizo, ***"not always the lowest is the cheapest, what is needed is the competent supervisor" na hawa ma-engineers ambao ni mahiri kusimamia tunao na wanalipwa vyema.***

Mlalamikaji alitoa ushahidi wake kwa Mheshimiwa Waziri na hakuna hatua zilizochukuliwa. Hii ni kasoro kubwa sana kwani, jambo hili linatupa wasiwasi hata ukamilikaji wa mradi huu.

Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mhe.Waziri aliangalie kwa kina suala hili, kwani linamtia doa hata yeye ambaye ndiye msimamizi mkuu wa wizara hii. Kwani miongoni mwa malalamiko yaliyotajwa ni Afisa mmoja Wizarani kufoji email na kutunga uongo uliotumika kufanya maamuzi ya nani apewe zabuni na nani asipewe.

### Mradi wa Maji Lindi Mjini

**Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji Lindi Mjini eneo la Ng'apa unajengwa na kampuni ya Overseas Infrastructure Alliance Private Limited ya India, mkandarasi huyo alianza kazi baada ya mradi kuzinduliwa rasmi na Mhe Rais Mstaafu Jakaya Kikwete Agosti 8,2015.** Mradi huo unatekelezwa kwa mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KFW) na Umoja wa Ulaya (EU)

**Mheshimiwa Spika,** Mheshimiwa Spika, tukumbuke kuwa Mhe WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, mwezi Oktoba mwaka 2016 alimsimamisha kazi Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Lindi (LUWASA), Mhandisi Adam Alexander kwa matumizi mabaya ya ofisi pamoja na kushindwa kusimamia ujenzi wa kituo cha kuzalisha maji katika manispaa hiyo (Mradi wa Ng'apa).

**Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Rais katika ziara yake mkoani Lindi alimtaka mkandarasi huyo **kuhakikisha kuwa inakamilisha ujenzi wa** Mradi wa Maji wa Ng'apa uliopo mkoani Lindi unakamilika ndani ya miezi minne na si vinginevyo **huo na sio kuleta visingizio.**

**Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Waziri alisema kuwa hadi sasa mradi huo umefikia asilimia 85 na kwamba mkandarasi amesimamisha kazi kutokana na kuishiwa fedha. Kambi Rasmi ya Upinzani inataarifa kuwa fedha za ujenzi wa mradi huo zimewekwa kwenye Akaunti Mkandarasi iliyopo nchini India, na hivyo fedha hizo kukosa uangalizi wa msimamizi wa Mradi huo (Consultant).

### 3.2 Huduma za Umwagiliaji- Tume ya Taifa ya Umwagiliaji- (Fungu 05)

**Mheshimiwa Spika,** kilimo cha umwagiliaji katika nchi hii kimekasimiwa chini ya mamlaka ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (fungu 05), takwimu zinatuonesha kuwa kwa nchi yetu ina jumla la hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa umwagiliaji, na hekta milioni 2.3 zina uwezekano mkubwa wa kumwagiliwa, hekta milioni 4.8 zinauwezekano wa kati na hekta million 22.3 zina uwezekano mdogo wa kumwagiliwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa ifikapo 2021 eneo lenye ukubwa wa hekta milioni 1 liwe limeendelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji, lakini kwa sasa ni eneo la hekta 468,338 ndilo linamwagiliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inawasiwasi kuwa, lengo la kufikia umwagiliaji wa hekta milioni 1, wakati tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda na kilimo ndio injini ya kutoa malighafi nyingi itakayohitajika katika viwanda. Ni dhahiri kwamba uwezekano mkubwa wa maandiko hayo yatabakia kwenye makabrasha tu na sio kwa utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya huduma za umwagiliaji maji (kifungu 05) iliombewa bajeti ya Tshs 39,876,141,428 ambapo kati ya hizo, Tshs 35,369,529,428 ni kwa ajili ya maendeleo na Tshs 4,206,827, 000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Bajeti hii ni pungufu ya ile ya mwaka uliopita kwa asilimia 26.

**Mheshimiwa Spika,** Mwenendo wa miezi tisa yaani kati ya Julai 2016 na Machi 2017, ni wa kustua na kusikistisha, hususan ukilinganisha umuhimu wa Sekta ya Umwagiliaji katika muktadha wa mapinduzi ya viwanda yanatarajiwa kutokea nchini Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni nchi ya kilimo, na uchumi wa viwanda utabebwa kwa kiasi kikubwa na kilimo. Ili kufikia azma ya uchumi wa viwanda, mikakati iliyopo katika Sekta ya Kilimo hususan kilimo cha umwagiliaji, ni kupanua eneo la uzalishaji kwa takriban hekta millioni 1.5 ili kuongeza

uzalishaji kwa asilimia 25 na kunufaisha zaidi ya kaya 2.3 milioni au watu wapatao milioni 12.

**Mheshimiwa Spika,** Ndoto hii ya kukuza uzalishaji haitakamilika iwapo fedha zilizoidhinishwa na Bunge hazitatolewa ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kuna matatizo mengi ya matumizi ya fedha zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji hapa nchini, Naibu waziri ofisi ya rais, Tamisemi, Mh.Seleman Jaffo katika ziara yake katika jimbo la Mwanga alisikitishwa na utekelezaji wa mradi wa maji ya umwagaliji katika kijiji cha Kivulini wilaya ya Mwanga kujengwa chini ya kiwango huku halmashauri ikishindwa kujua thamani halisi ya mashine zilizofungwa katika mradi huo ambao unatarajia kugharimu zaidi ya shilingi bilioni 1.6

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa umwagiliaji wa Kiwalala katika bonde la Lukuredi halmashauri ya wialaya ya Lindi, umegharimu zaidi ya shilingi milioni 600 lakini hadi sasa mradi haufanyikazi. Na maelezo yanayotolewa ni kwamba Mkandarasi alikosea wakati amafanya usanifu, hivyo kwa eneo uliopo haliwezi kutoa tija na hivyo mradi ndio umekufa kifo cha mende kama miradi mingine mingi kama vile Kinyope mradi wa hekta 400 katika Jimbo la Mchinga.

**Mheshimiwa Spika,** Katika hali kama hii ni halmashauri ngapi zinapoteza fedha za walipa kodi wan chi hii kwa kushindwa kusimamia fedha za miradi?

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2016/2017 vitengo/Idara nne kati ya saba hazikupatiwa fedha kabisa kwa ajili ya kuendesha shughuli zake. Idara/Vitengo hivyo ni Uhakiki na Udhibiti wa Ubora, Huduma za Uedeshaji na Uwezeshaji wa Umwagiliaji, Utafiti na Uhamasishaji wa Teknolojia za Umwagiliaji na Mazingira na Jamii.

**Mheshimiwa Spika,** Ni jambo la kushangaza na fedheha kuona kwamba pamoja na Serikali iliyopo madarakani kusistiza uchapaji kazi wa hali ya juu, sekta muhimu kama hii

ya umwagiliaji ambayo inategemewa katika kuinua productivity ya kilimo iliyodorora katika miaka ya karibuni, inanyimwa fedha za kuweka miundombinu inayohitajika kwa kazi hiyo. Itakuwaje kutekeleza ***"Kauli mbiu ya Hapa Kazi Tu"*** kama vitendea kazi havipatikani?

**Mheshimiwa Spika,** Uzoefu unaonesha bila ya kuwa na uhakika na usalama wa maji, azma ya kupanua kilimo na kukifanya kiwe cha kisasa, endelevu na hatimaye kupata mapinduzi ya viwanda itabakia kuwa ni nadharia kwenye makabrasha tu bila ya kuwa na utekelezaji wowote.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ukweli kwamba, tunakokwenda tutakuwa na upungufu mkubwa wa maji kwa ajili ya matumizi ya kibinadamu, kutokana na mabadiliko ya Tabianchi. Hivyo katika kutekeleza jukumu hilo la umwagiliaji ni lazima Tume ya umwagiliaji ichague aina ya umwagiliaji ambayo itatumia maji kidogo wakati huo kuzalisha kwa tija. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa kufanya ufuatiliaji wa miradi ambayo ilikwisha pata fedha za utekelezaji na kuona ni kwa vipi miradi hiyo ya umwagiliaji inawanufaisha wananchi katika maeneo husika.

**Mheshimiwa Spika,** District Agriculture Sector Investment Project (DASIP) ni Mradi uliokuwa wa miaka saba (7) ulianza mwaka 2006 hadi 2013 na mradi ulihusisha wilaya 28 za mikoa ya Kagera, Kigoma, Mara, Mwanza na Shinyanga ambao ulikuwa ni mkopo wa (***Unit of Account)*** UA million 58.01 kutoka Benki ya Maendeleo ya Africa (ADB). Mradi ulitekelezwa kupitia mfumo wa ASDP katika utaratibu wake wa utekelezaji wa miradi chini ya Project Coordination Unit (PCU).

***NB:*** *UA moja ni sawa na 1.567 US$ kwa mwaka 2009 kwa thamani ya mwaka huo.*

**Mheshimiwa Spika,** Mradi ulikuwa na lengo la kuongeza tija na mapato kwa jamii ambazo ni wanufaikaji wa mradi na progamu nzima ya DASIP. Mradi huu ulihusisha skimu za umwagiliaji 23 zilizokuwa na thamani ya shilingi

16,600,251,799.40 (AfDB funds) na fedha zilizolipwa kwa skimu hizo 23 lakini hadi sasa hakuna hata skimu moja iliyokamilika kwa asilimia 100 ilikuwa ni shilingi 9,209,934,228.16 (AfDB & DIDF). Zifuatazo ni baadhi tu ya Skimu hizo kati ya zile 23; Pia Jumla ya shilingi 1,521,699,500.00 zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya utaalam ushauri (consultancy) na kiasi cha shilingi 1,408,742,558.00, kililipwa kwa wataalam washauri wa miradi hiyo. Hapa ni baadhi ya skimu zilizokuwemo ndani ya Programu hiyo na thamani ya kila skimu na fedha zilizolipwa kwa mkandarasi;

i. Kahanga iliyopo Kahama ya thamani ya shilingi 774,164,345 na mradi ulisainiwa tarehe 20.03.2013 na ulitakiwa kuchukua siku 210, hadi mkandarasi anaondoka alilipwa shilingi 273,149,775. Lakini mradi hadi sasa haufanyikazi.

ii. Kinamwigulu skimu-Maswa, mradi ulikuwa na thamani ya shilingi 698,189,988. Na mkataba wa ujenzi ulisainiwa 01.02.2013 na ulitakiwa kukamilika 07.08.2013, mkandarasi alilipwa shilingi 628,361,988.3 mradi hadi sasa haufanyikazi kwa ukamilifu wake.

iii. Kisangwa Skimu-Bunda, thamani ya mradi ilikuwa ni shilingi 385,901,500. Mkataba ulisainiwa 07.05.2012 na ulikuwa wa siku 150 kukamilisha mradi. Mkandarasi alilipwa shilingi 259,653,118. Mradi haufanyikazi

iv. Kyakakera Skimu –Misenyi mradi uliokuwa na thamani ya shilingi 497,120,784 na ulisainiwa 20.3.2013 na ulitakiwa kukamilika ndani ya siku 150. Serikali ilimlipa Mkandarasi jumla ya shilingi 429,268,874.4 wakati kazi kwa mujibu wa mkataba ilikuwa imekamilika kwa asilimia 31 tu.

v. Lutubiga Skimu –Busega, mradi ulikuwa na thamani ya shilingi 799,047,665. Ulisainiwa 5.2.2013 na kazi ilitakiwa kukamilika ndani ya siku 240. Lakini hadi mkandarasi anaondoka site kazi ilikamilika kwa asilimia 49 tu.

vi. Lwenge Skimu-Geita, mradi ulikuwa na thamani ya shilingi 434,637,358. Na ulitakiwa kukamilika ndani ya siku 150

baada ya kusini mkataba hapo tarehe 01.02.2013. Lakini hadi Mkandarasi anaondoka site kwa kukamilisha asilimia 59 tu ya kazi na alilipwa shilingi 391,125,000.

vii. Masinono Skimu- Musoma, mradi ulikuwa na thamani ya shilingi 1,248,038,427.67 na mkataba ulifungwa 09.05.2013 na kazi ilitakiwa kukamilika kwa muda wa siku 270. Serikali ililipa jumla ya shilingi 265,681,080. Hadi sasa mradi haufanyikazi.

viii. Mgondogondo Skimu-Kibondo, mradi ulikuwa na thamani ya shilingi 330,453,742. Mradi ulitakiwa kukamilika ndani ya siku 180 tu, lakini hadi mkandarasi anaondoka site alikwishalipwa jumla ya shilingi 297,407,107.8 wakati kazi ilikamilika kwa asilimia 53 tu.

ix. Mwagila Skimu-Meatu, uliokuwa na thamani ya shilingi 1,165,132,300. Na ulisainiwa 05/02/2013 mradi ulitakiwa kukamilika ndani ya siku 180, lakini Serikali ililipa shilingi 1,164,006,962. Lakini hadi sasa mradi haufanyikazi.

x. Mwasubuya Skimu-Bariadi, mradi ulikuwa na thamani ya shilingi 1,204,646,601. Ulisainiwa tarehe 20.03.2013 na ulitakiwa ukamilike ndani ya siku 270. Serikali ilimlipa mkandarasi shilingi 215,884,150.71. lakini mradi huo hadi leo haufanyikazi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge wahusika wa upotevu wa / hasara ya fedha kama zilivyowekwa hapo awali ni hatua gani zimechukuliwa kwani hadi sasa miradi hiyo ya skimu za umwagiliaji haifanyikazi na fedha hizo zilikuwa ni mkopo toka Benki ya Maendeleo ya Afrika.Wataalam washauri wa miradi hiyo ambao walikuwa ndio wasimamizi wakubwa wa miradi hiyo ni hatua gani zimechukuliwa dhidi yao?

**Mheshimiwa Spika,** Mpaka hivi sasa kilimo cha umwagiliaji kinatumia kiwango kikubwa cha maji kuliko sekta nyingine yoyote, lakini ni kiwango kidogo sana cha maji kinatumika kwa tija.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Wizara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula zinaonesha kuwa ni asilimia 15 tu ya maji yanayochukuliwa kutoka katika vyanzo mbali mbali vya maji ndiyo inayotumika vizuri (Wizara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula, ACRP 2014). Miundombinu ya umwagiliaji ni chakavu na ile mipya ina makosa mengi ya kiufundi (ASDP II).

**Mheshimiwa Spika,** Kilimo cha umwagiliaji vilevile kimegubikwa na migogoro kati ya watumiaji wa maji, na kimesababisha nadhara makubwa. Kati ya watumiaji wa raslimali za maji. Tumeona madhara makubwa ya mapigano kati ya wakulima na wafugaji wakigombea maeneo yenye maji kwa ajli ya kilimo na mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** *"Integrated Water Resource Management (IWRM) Integrated Water Resources Management (IWRM) is a comprehensive approach to water resource management that views water as a single resource with competing uses and inter linkages with the ecological, social and economic systems. Through IWRM, water is treated as an economic, social, and environmental good; and IWRM helps ensure that policies and options that guide water resources management are analyzed within an integrated framework"*

**Mheshimiwa Spika,**Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze wananchi ni kwa vipi Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji inapambana na mabadiliko ya Tabianchi jambo ambalo ni kisababishi kikubwa cha upungufu mkubwa wa maji kwa makundi mbalimbali ya watumiaji, hasa katika kuchagua na kuhamasisha aina ya kilimo cha umwagiliaji kinachotumia maji kidogo na kutoa tija kubwa?

### 4.0: Mapitio ya Maombi ya Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuangalia takwimu za maombi ya fedha za maendeleo kwa wizara (fungu 49) zinaonesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2015/16 ilipewa shilingi 141,244,873,622 kati ya hizo fedha za ndani ziliwa shilingi 100,394,810,359 na

za nje zikiwa shilingi 40,860,063,263. Mwaka 2016/17 ilitengewa jumla ya shilingi 915,193,937,771 kati ya hizo za ndani zikiwa ni shilingi 690,155,000,000 na za nje zikiwa shilingi 225,038,937,771.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2017/18, Wizara inaomba kupatiwa jumla ya shilingi 632,606,748,000 kati ya hizo shilingi 408,617,643,000 ni fedha za ndani na shilingi 214,989,105,000 zikiwa ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuwa fedha za ndani kwa wizara kwa kulinganisha mwaka jana na mwaka huu kuna tofauti ya shilingi 281,537,357,000. Kambi Rasmi inataka kufahamu kama Serikali inavyodai kila mara kuwa makusanyo ya mapato ya ndani yanaongezeka kila mwaka inakuwaje inapunguza mgawo wa fedha za maendeleo kwa sekta muhimu kama maji, ambayo inawagusa watanzania wote na pia ndiyo injini ya kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa Kati?

## 4.0 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, ni ukweli kuwa, Serikali pamoja na wadau wa maendeleo, taasisi zisizo za kiserikali pamoja na taasisi za kidini kwa muda tofauti zimeweka fedha zao kwenye miradi kadhaa inayodhamiria kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wetu, Kambi Rasmi ya Upinzani inaliona jambo hili sio suala la kujadili kwani liko wazi.

**Mheshimiwa Spika**, ni miradi mingi sana ambayo imetumiwa fedha nyingi sana za walipa kodi wa nchi hii, hasa miradi ya vijiji 10 kwa kila wilaya, ambapo Serikali ilishindwa kusimamia miradi hiyo na sasa hivi takwimu zinaonesha kuwa miradi imekamilika wakati huohuo wananchi wengi katika vijiji husika hawana maji.

**Mheshimiwa Spika**, sio hilo tu, skimu nyingi za umwagiliaji katika nchi yetu, fedha za mikopo au halmashauri au fedha za misaada toka kwa wadau wa maendeleo zimezama na

miradi imekuwa kama magofu hakuna uzalishaji unaofanyika.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kuishauri Serikali kwamba miradi itakpokuwa inafaanza ni vyema wananchi wakapewa taarifa kuhusu thamani halisi ya mradi na unatakiwa kumalizika lini ili nao kwa nafasi zao wawe ni wasimamizi vivuli wa raslimali za Serikali. Mfano ni mradi wa maji wa Kahama Tabora na wilaya zake, randama haioneshi ni mradi wa shilingi ngapi kwa kila hatua japokuwa zabuni tayari zimefunguliwa na wakandarasi tayari wamepewa kazi na hivyo waheshimiwa wabunge wasaidie katika ufuatiliaji.
Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, ni muda mwafaka sasa wananchi kushirikishwa katika shughuli za maendeleo yanayowahusu kwani wao ndio watakuwa wasimamizi wakubwa wa miradi husika, badala ya tabia iliyopo sasa ya wao kuona watu wanafanyakazi nao kuwa watazamaji tu.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

**............................**
**Hamidu Hassan Bobali (Mb)**
**Waziri Kivuli na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-Wizara ya Maji na Umwagiliaji**
**10/05/2017**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge sasa tutaendelea na utaratibu wa uchangiaji, tutakuwa na kwa muda uliopo nadhani ni mchangiaji mmoja na mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Charles Kitwanga.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kutoa shukrani kwa nafasi hii. Nianze tu kwanza kwa kutoa shukrani angalau safari hii nimeona hela katika kusaidia kupata maji katika Jimbo langu la Misungwi. Kwa masikitiko makubwa sana vilevile lile swali nililouliza la nyongeza kwamba, pale Ihelele ambapo ndipo

chanzo cha maji hata leo hii pamesahaulika. Sasa safari hii patachimbika na mimi sitatoa shilingi, nitakachofanya nitakwenda ku-*mobilize* wananchi wa Misungwi kama 10,000 tukazime ule mtambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mwaka 2008 tunaendelea kusubiri, tunaendelea kusubiri na leo mmethubutu kuandika huku kijiji cha Nyanhomango kimepata maji wakati hakina. *It's so disgusting* kwamba *World Bank* walikuja pale wakasema *this is inhuman,* halafu sisi tunaona ni *human*. *World Bank* wamefika pale wakaona kwamba hawa watu ambapo maji yanatoka hawana maji, wakasema *this is inhuman,* lakini wafanyakazi waliokuwa nao wameendelea kuona huo ni ubinadamu. Siwezi kukubali na sitakubali na hili lazima libadilike, kwa sababu hii nchi ni yetu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia huku pesa nyingi zimepelekwa sehemu ambazo siwezi kuzitaja na maji labda yapo, ni vema tukatendeana haki. Inanipa shida zaidi kuona kwamba hata mahala ambapo Mheshimiwa Rais aliahidi maji pale Usagara hamna senti iliyowekwa humo, kama imo mnionyeshe. Ninachowaomba jamani tutendeane haki. Huwezi kuwa na mradi wa kwenda mpaka Tabora unatumia bilioni 600 unashindwa kuwapa hawa watu wa pale ambapo maji yanatoka hata bilioni kumi? *Very unfair,* ninazungumza hili likitoka moyoni mwangu kabisa. Nakipenda sana chama changu, naipenda sana Serikali yangu, nampenda sana Mheshimiwa Magufuli lakini ninyi watu wa Wizara lazima mtende haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hapo hata ile barabara inapokwenda chanzo cha maji sasa hivi haipitiki kwa sababu ile ni ya tani 10, lakini yale malori yanayobeba yale madawa ni *28 tons, 40 tons*, sasa Halmashauri kila ikijaribu kutengeneza inashindikana. Nashukuru Wizara ya Ujenzi angalau wameweza kui-*upgrade* ile barabara kuwa ya *TANROADS.* Niseme tu kwamba haki haijatendeka hapa na mimi sitatoa shilingi wala nini dawa yenu ni kwenda kuzima ule mtambo, eeh. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dawa yenu ni kwenda kuzima ule mtambo wote tukose, eeh! Kwa sababu gani, kama tunasema na mmeniahidi hapa kwamba na mimi nimekwenda nimeongea na watu wa *KASHWASA* wakaniambia *it is 4.2 billion,* ziko wapi? nimeona hapa bilioni 3.9 najua ni za kutoka Mbalika kuja Misasi. Halafu sasa tutakuwa tunapoteza hata hela, kwa sababu kutoka Mbalika kuja mpaka Misasi tayari mabomba yamewekwa, kutoka kwenye chanzo cha maji kuja hapa Mbalika, hamjaweka, hata *common sense* jamani hatuna? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine inanishangaza sana, yaani mnishukuru tu nilikuwa Waziri zamani nilikuwa siwezi kusema, sasa nimetoka tutapambana. Ninachosema ni lazima tuwe *good planner*, lazima tuwe na mipango mizuri, tuwe na mikakati mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbona kwenye *REA* tume-*perform* vizuri tu, kwa nini tusi-*perform* vizuri hata kwenye maji vijijini, tuna matatizo hapo kidogo. Sasa mpaka nashangaa wakati mwingine, niliomba mradi kwa rafiki zangu kutoka Austria nikawa nimepewa, baadae nikapigwa figisu figisu eti kwamba wewe una-*interest*, ndiyo nina *interest!* Kwa sababu watu wangu wa Kolomije wanahitaji maji! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wangu wa Bukumbi wanahitaji na tulipokuwa Bukumbi na Mheshimiwa Rais akawambia wananchi huyu ana marafiki zake wengi nchi za nje. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikawa nimetafuta kule mara ya kwanza wakasema kwanza Tanzania ichangie *20 percent* kwenye *design* hela kidogo, sasa hivi wamesema hivi hata hiyo *20 percent* tunawasamehe kamilisheni hiyo miradi awamu ya kwanza ili nami Bukumbi wapate maji, Kolomije wapate maji, Ibongoya wapate maji. Kwa sababu waliishaniahidi kwamba tukiishamaliza tu hiyo awamu ya kwanza na wewe utapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namuuliza mmojawapo ya wakubwa hapo kwamba hebu vipi huu mradi wa Austria ananiambia achana na huo mradi wa Austria. Sasa hatuwezi kutajana majina, *I was a little bit disappointed.* Niombe tu huo mradi na wenyewe tuupe, kwa sababu sasa hivi wameshakubali, kinachotakiwa ni sisi ku-*respond* kwa Serikali ya Austria kusema kwamba *go ahead,* halafu wakishamaliza hapo wanachosema pelekeni ombi lingine sasa la hivyo vijiji vyangu ambavyo nimevitaja.

**MBUNGE FULANI:** Kolomije. *(Kicheko)*

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Hamia huko kama unataka, ni pazuri sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ndugu zangu wapendwa sitajihangaisha kutoa shilingi, lakini mjue mtajua sasa maharage ni mboga au ni zao la biashara. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto Kabwe dakika tano.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, leo sikupanga kuzungumza lakini nimeomba kuzungumza kutokana na hali halisi ya bajeti ya Wizara ya Maji.

Kwanza kabisa kwa mara nyingine binafsi kama Kiongozi wa Chama cha ACT Wazalendo, napenda kumshukuru sana Mheshimwa Rais kwa uteuzi wa Profesa Kitila Mkumbo kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji. Ninaamini kabisa kwamba kutokana na uwezo wake, umahiri wake na weledi wake ataweza kuisaidia nchi na ujumbe utakwenda duniani kwamba ndani ya Vyama vya Upinzani kuna watu wazalendo na uwezo wa kufanya kazi, ninamtakia kila la heri Profesa Kitila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa ambalo

tunaliona na naomba Waheshimiwa Wabunge tuelewane katika hili, Mheshimiwa Rais alikuja hapa Bungeni, katika moja ya jambo ambalo lilikuwa ni *very emotional* kwa Watanzania ni pale Rais alipoahidi kuwatua akina mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona Makamu wa Rais akizunguka kila kona ya nchi hii kufanya kazi hiyo, hata bajeti ya mwaka jana picha iliyokuwa mbele ya kwenye bajeti ilikuwa ni picha ya Makamu wa Rais anamtua mama ndoo kichwani, lakini kwa masikitiko makubwa sana bajeti ya Wizara ambayo ndiyo inawahusu Watanzania moja kwa moja imeshuka kutoka bilioni 915 za maendeleo mpaka bilioni 623 za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unatafsiri vipi uwekezaji wa rasilimali fedha namna hii kwenye ajenda ya kuwashusha na kuwaondolea kina mama ndoo kichwani. Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nawaomba kwa siku tatu hizi za bajeti hii, najua tuna kero zetu kwenye majimbo, najua tuna matatizo kwenye mikoa yetu na kila mtu ataanza kuongelea mradi wake, iwapo hatutaungana pamoja na kutaka bajeti ya Wizara hii irudishwe angalau kwa mpango ule wa mwaka jana, hayo malalamiko yote mtakayoyatoa kwenye majimbo yenu hayatakuwa na maana yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Bunge tunayo hayo mamlaka, Kanuni za Bunge zinaturuhusu kuitaka Serikali ikapange upya bajeti hii, kama unaguswa na kero ya maji kwenye eneo lako, kama unaguswa na kero ya maji kwenye mkoa wako au jimbo lako au kijiji chako una njia moja tu ya kufanya ya kumsaidia Waziri bajeti hii iende ikaandikwe upya, tupate bajeti angalau ile ya mwaka jana iweze kurudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo siyo la Vyama, wanaoumia na maji ni watu wa vyama vyote na watu wasio na vyama vilevile. Nimeomba dakika hizi tano kwa ajili ya kui-*set* hiyo *trend* na tuweze kuiambia Serikali, kuna mapendekezo mengi Kamati ya Maji imetoa maependekezo kuhusiana na *Rural Water Agency*, imetoa mapendekezo

kuongeza fedha kwenye mafuta kwa ajili ya kuweza kuelekeza maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hiyo bajeti ya mwaka jana ya bilioni 915 ni asilimia 19.8 tu ya miradi ya maendeleo ndiyo imepelekwa kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ambayo imetueleza hapa. Hata Waziri mwenyewe kwenye hotuba yake ukurasa wa 120 ameeleza, tuchague, tupige kelele humu ndani, tulalamike, halafu tuonekane tumesemea watu wetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto sekunde tano malizia sentensi.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, au tuchukue hatua ya kuhakikisha kwamba bajeti ya Wizara ya Maji inakwenda kurudishwa angalau kwenye kiwango cha mwaka jana. Naomba Waheshimiwa Wabunge huo ndio uwe mjadala wetu na huko ndiko ambako twende, tuweze kuwatua akina mama ndoo kichwani. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha kwanza kwa leo, nitawataja baadhi ya wachangiaji wa mchana halafu tutaendelea na mengine yaliyo mezani, Mheshimiwa Mary Nagu, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mheshimiwa Allan Kiula, Mheshimiwa Josephine Chagula, Mheshimiwa Azza Hillal, Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, Mheshimiwa Rose Kamil, Mheshimiwa Julius Kalanga, Mheshimiwa Tunza Malapo, Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mheshimiwa Suleiman Said Bungara na Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Hawa watakuwa baadhi ya wachangiaji wetu wa mchana.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mawili, tangazo la kwanza linatoka kwa Mheshimiwa Jasson Rweikiza anawatangazia Wabunge wote wa CCM kuwa leo tarehe 10 Mei, 2017 saa 8.30 mchana, kutakuwa na kikao *White House,* ni muhimu sana kila Mbunge wa CCM kuhudhuria mkutano huu.

Tangazo la pili linatoka kwa Mheshimiwa Joseph

Selasini ambaye ni Mwenyekiti Jumuiya ya *St. Thomas Moore* Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wakristo wakatoliki, leo Jumatano tarehe 10 Mei 2017, kuwa kutakuwa na ibada maalum ya misa ya kuwaombea watoto na walimu wao waliofariki katika ajali huko Arusha. Ibada hii itafanyika mara baada ya kuahirishwa Bunge saa saba mchana katika kanisa dogo lililoko ghorofa ya pili, ukumbi wa Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wengine wote mnakaribishwa kushiriki ibada hii takatifu. Raha ya milele uwape ee bwana na mwanga wa milele uwaangazie wapumzike kwa amani, amina.

Waheshimiwa Wabunge, ninayo mambo matatu kwa haraka, moja ni la kukumbusha hapa mbele ya Siwa kwenye huu mzunguko wanaoruhusiwa kukatiza hapo ni watumishi wanaozunguka, siyo Wabunge, ndiyo maana Siwa iko hapa mbele. Sasa usitoke mahali upande mmoja ukakatiza hapa ukaona ni njia ya mkato, tafadhali zunguka ndiyo utaratibu tuliojiwekea, hilo ni moja.

Jambo la pili, kwa kuwa limezungumzwa hapa Bungeni Mheshimiwa aliyechangia kwanza Mheshimiwa Mbunge ametoa maelezo mazito sana hapa ya kwamba ataenda kuwaleta watu wake kama elfu kumi hivi ili wakazime mtambo. Waheshimiwa Wabunge hilo jambo sheria yetu ya mwenendo wa makosa ya jinai unakataza wewe kuwaweka watu ama kuwashawishi watu kufanya kosa la kijinai. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikasema nikukumbushe tu hilo kwa sababu hatua zinaweza kuanza kuchukuliwa kabla hata hujawafikia hao watu unaotaka ukawakusanye pamoja, kwa sababu sheria inakataza. Ni muhimu kujua jambo hili.

Waheshimiwa Wabunge, lingine si kwa udogo nalo ni la muhimu, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Kivuli wa Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji kwa hotuba yake ambayo pengine ni ya kwanza, sina uhakika kama ni ya pili ambayo hatujapata taabu nayo ya watu kusimama na kuanza kuomba hili na lile. Kwa hiyo nikupongeze sana. Jambo moja dogo lililojitokeza kwenye hotuba hiyo si kwa lengo la kufuta

lakini kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawa za Bunge, hotuba hii inaeleza kwamba Mheshimiwa Peter Lijualikali aliachiwa na Mahakama Kuu kwa kuwa hakuwa na makosa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ni vizuri tukiwa tunataka kuzungumza sisi kama viongozi tuwe tunajiridhisha mambo haya. Mheshimiwa Lijualikali ameachiwa na Mahakama Kuu haikuzungumza juu ya kosa lililofanywa, isipokuwa ameachiwa kwa kuwa Hati ya Mashtaka ilikuwa na matatizo. Kwa hiyo, lazima uwe unaweka vizuri tusije tukajikuta sisi hapa tunakuwa kama Mahakama ya Rufani wakati Mahakama Kuu ilitoa hukumu yake vizuri kabisa. Hivyo, tuwe tuna uhakika na mambo haya tunapo zungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa maji kwa sababu tutaendelea na mjadala na wataalam wako utakapopata fursa mchana huu, ukurasa wa 174 mpaka ukurasa wa 184 Jedwali la Nane yapo maelezo mengi tu ya kutosha ambayo yanaonekana miradi haijafanyiwa kazi ya hizo skimu za umwagiliaji kwa sababu taratibu za manunuzi zimechelewa katika Ofisi za Wakurugenzi wa Wilaya, inaonekana ni za muda mrefu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mambo kama haya yameletwa kwenye bajeti kwamba wamechelewa Wakurugenzi ambao tunaamini kwamba mamlaka zao zipo na kama ni hatua basi zichukuliwe kwa sababu kama ni mwaka mzima hakuna maelezo na bajeti yetu hii ndiyo inayosema kwamba imechelewa kwa Mkurugenzi na mpaka leo inasema hivyo kwamba imechelewa kwa Mkurugenzi, tungetamani kujua kwamba hawa Wakurugenzi ni vipi wamecheleweshа, kwa sababu maana yake siyo fedha tatizo, tatizo ni Wakurugenzi. Nadhani hilo likae vizuri ili mjadala wetu uweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni leo.

*(Saa 7.05 Mchana Bunge lilisitishwa Mpaka Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Tukae. Katibu!

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano ya Hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji. Tutaanza na Mheshimiwa Mary Nagu, atafuatiwa na Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mheshimiwa Mattar Ali Salum ajiandae.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii ya awali kabisa kukushukuru kwa dhati kabisa kwa kunipa nafasi ya mwanzo jioni ya leo ili kujadili hoja ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijafika huko, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia na wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kuwapa pole wale wote waliofiwa na wanafunzi wa shule ya St. Vincent na wengine wote waliopata ajali kwenye maafa mbalimbali na kufariki. Mwenyezi Mungu alaze roho zao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naupongeza sana uongozi wa Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania kwa kutambua umuhimu na unyeti wa Sekta ya Maji na kuipangia Sekta hii siku tatu za majadiliano. Naomba Waheshimiwa Wabunge wasirudi nyuma kutumia siku hizi tatu kuijengea hoja ili Mheshimiwa Rais wetu mwema aweze kumtua mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vile vile kumpongeza Mheshimiwa Rais na Serikali kusikiliza ushauri wa Wabunge wetu. Vile vile kwa kututeulia Waziri Lwenge na Naibu Waziri Kamwelwe ambao ni mahiri sana katika kuongoza Wizara hii pamoja na watendaji wote; na Mungu awape afya njema waweze kusikiliza wanayosema Wabunge na watekeleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwamini sana Mheshimiwa Rais na nampongeza sana. Naisihi Serikali yake kuona kwamba inapokea kilio cha Wabunge kuhusu Bajeti ya Maji kwa sababu maji ni uhai na usafi wa mazingira ni utu wa binadamu. Hivyo sina shaka changamoto nitakazozitoa hapa zitachukuliwa na kufanyiwa kazi kwa kuzitolea uamuzi kwa manufaa ya Taifa letu na wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya 2016/2017 iliyotengwa ilikuwa sh. 939,631,302,771 na kati ya hizo fedha zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni sh. 915,193,937,771. Hata hivyo, fedha zilizotolewa kwa Miradi ya Maendeleo mpaka Machi mwaka 2017 ni sh. 181,209,313,609 sawa na asilimia 19 peke yake. Mbaya zaidi Bajeti ya Mwaka huu wa 2017/2018, iliyotengwa ni sh. 623,606,748,052 ambayo ni ndogo ukilinganisha na mwaka uliopita lakini mahitaji ya maji yameongezeka, *population* nayo imeongezeka, mahitaji ya viwanda yameongezeka na mahitaji ya jumla ya maendeleo yameongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, kwa sababu mwenendo huu unasikitisha na utawasikitisha Watanzania, naomba Serikali bajeti yetu irudi kama ilivyokuwa mwaka jana ili kuona kwamba ndoo hii ambayo mwanamke ameteseka nayo kwa muda mrefu inatua kutoka kwenye kichwa chake. Naomba bajeti hii iongezeke kama ilivyokuwa bajeti ya mwaka jana. Maji ni uhai narudia tena na usafi wa mazingira ni utu. Bila maji hakuna maendeleo, bila maji hakuna uhai, bila maji jamani viwanda hivyo tunavyovisema haviwezi kuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ili tuwe na uhakika wa kutekeleza miradi ya maji na maendeleo ya maji ambayo matokeo yake ni maji kupatikana, naomba sana kama tulivyoomba mwaka jana na Kamati yangu imerudia mwaka huu kwamba Mfuko ule wa Maji unaochangiwa sh. 50 kwa kila lita ya *diesel* na *petrol* uongezewe sh. 50 ili iwe sh100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu Serikali yenyewe iliahidi kuifanyia kazi. Nina hakika kwa mwaka mmoja hiyo kazi itakuwa imefanyika na naomba mwaka huu tufanye hivyo hasa tukizingatia bajeti yenyewe inayotengwa huwa haitolewi na fedha hizi zitasaidia sana miradi ya maji iende kwa kasi zaidi. Ukiangalia mpaka mwisho wa mwezi Machi, 2017 utaona kwamba hela iliyotolewa ni kidogo sana. Nchi hii inakabiliwa na njaa na inakabiliwa na ukame, hakuna kitu ambacho kitai-*rescue* au itasaidia nchi hii kama miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuone kwamba fedha zinazotengwa kwenye umwagiliaji zitasaidia kuongezeka kwa uhakika wa chakula, uhakika wa kupata mazao ya biashara unaongezeka. Kwa hiyo, naomba Tume ya Umwagiliaji nayo iangaliwe kwa jicho la huruma na kuongezewa fedha ili nchi hii iwe na uhakika wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshukuru sana kuona kwamba katika bajeti hii, bwawa ambalo nimeliomba kwa miaka saba lingelijitokeza lakini sikuona na nimekuwa nikiomba kila mwaka hata pale ambapo nipo kwenye Sekta hiyo ya Maji, bwawa la Gidahababiel halikuonekana na nasema naipenda sana Serikali, naiamini sana lakini kwa bwawa hili la Gidahababiel nitatoa shilingi kwa sababu watu wa Hanang hawawezi kuelewa hili, wataniona naimba tu halafu Serikali haichukui hatua yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mjue kwamba bwawa hili lilikuwepo toka wakati wa ukoloni lakini likapasuka wakati wa *el-nino.* Mpaka leo hakuna ambaye amelihangaikia bwawa hili. Namuomba Waziri na Watendaji wake waone umuhimu wa bwawa hili. Sisi tuko kwenye bonde la ufa na wilaya ambazo ziko kwenye bonde la ufa zina matatizo makubwa sana ya maji. Hanang ikiwa moja ya Wilaya ya Bonde la Ufa haina maji ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile zaidi ya bwawa la Gidahababiel naomba visima vile ambavyo tumeviomba viweze kuchimbwa ili wananchi wa Hanang waweze kupata

maji. Mpaka hapa tulipo wananchi wanaopata maji kwenye Wilaya ya Hanang nafikiri ni asilimia 46, na sisi ni wilaya ya mifugo. Wananchi wa Hanang wamehama wilaya ile kutokana na ukame na kwenda wilaya zingine na kutoa adha kwa watu wengine. Naomba sana, wale waliobaki na mifugo, wasihame, wabakie Wilaya ya Hanang kwa kuhakikisha kwamba mabwawa na visima vinachimbwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hapo naomba vile vile katika kuimarisha Sekta ya Maji, tunaomba kuwe na maafisa wa kutosha wa maji, wahandisi wenye uwezo wa kukabiliana na tatizo la ukame. Sasa hivi tuna wahandisi wachache, Wilaya ya Hanang ilikuwa na wahandisi wazuri, wamehamishwa, basi na mimi ningeomba TAMISEMI ione umuhimu wa kuwaleta wahandisi imara ambao watakabiliana na tatizo hilo ambalo ni kubwa katika wilaya yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge waone umuhimu wa kuongeza bajeti ya maji iwe angalau kama ile ya mwaka jana. Naomba Waheshimiwa Wabunge waunge mkono hoja ya kuongeza sh. 50 kwa kila lita ya *diesel* na *petrol* ili mfuko wa maji uwe na fedha za kutosha kutekeleza miradi mbalimbali. Tukifanya hivyo, Mheshimiwa Rais wetu atakuwa na uwezo, na ana upendo mkubwa sana na wananchi wake wa kutua ndoo kwenye kichwa cha akinamama ambao ndio wanapata adha kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nishukuru sana kwa nafasi hii na naunga mkono Bajeti hii ya Sekta ya Maji au ya Wizara ya Maji kwa moyo wangu wote, lakini yale niliyoyasema myazingatie na wakati wa kutoa majibu myatolee majibu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jasson Rweikiza, atafuatiwa na Mheshimiwa Mattar Ali Salum. Mheshimiwa Allan Kiula.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia Bajeti hii ya Wizara ya Maji ambayo kwangu mimi ni moja ya Bajeti muhimu sana kwa nchi hii, ni muhimu sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na wasaidizi wake wote katika Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya. Maji ni tatizo kubwa sana kwa nchi yetu. Maeneo mengi sana hayajapata maji safi na salama, hasa hasa majimbo ya vijijini. Ukiwauliza Waheshimiwa Wabunge wote hapa, wa vijijini, wote kilio ni maji. Kilio kikubwa sana ni kuhusu maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyoongea waliotangulia, inasikitisha sana kwamba bajeti ya mwaka huu tunayoijadili imepungua kutoka ile ya mwaka jana tunayomalizia. Kutoka bilioni 900 na pointi kwenda bilioni 600, hiki ni kitu cha kusikitisha na kwa kweli si jambo zuri. Serikali iangalie kwa makini hizi fedha zirudishwe katika bajeti ya maji angalau basi ifikie ile ile kama ya mwaka tunaoumalizia huu. Hata kama haikutoka yote lakini ifikie pale ikipatikana, itumike. Bajeti imepanda kutoka trilioni 29 hadi 32, kwa nini ya maji ipungue? Bajeti nzima ya Serikali ikipanda maana yake na za Wizara zote zinapanda, lakini ya maji imepungua, hili sio jambo jema hata kidogo ukizingatia kwamba uko tunakotoka vijijini hali ya maji ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulizungumza humu siku nyingi tu kuhusu Wakala wa Maji, tuwe na Mfuko wa Maji. Bahati nzuri ukaanzishwa lakini hauna pesa, kwa hiyo hauwezi kufanya kazi inayotakiwa au inayotegemewa kwa sababu hakuna pesa. Yale aliyoyasema Mheshimiwa Nagu kwamba tulisema itoke sh. 50 iende sh.100 na naiunga mkono. Tuongeze tozo katika mafuta ya *diesel* na *petrol* badala ya sh. 50 iwe sh. 100 ili angalau mfuko huu upate fedha ya kutosha kuhudumia maji vijijini. Hili ni jambo kubwa na litasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata habari kwamba jambo hili lilipofika kwa Waziri wa Fedha akasema kwamba si zuri maana tukiliruhusu litaleta *inflation,* si kweli! Hakuna *inflation* kwenye jambo hili. Leo unga umepanda mara nne kutoka bei ya mwaka jana je, ni kwa sababu ya *petrol* kupanda? Petrol haijapanda. Unga umepanda mara nne kutoka sh. 1,800 mpaka karibu sh. 2500. Kwa hiyo si sababu ya mafuta kupanda ndiyo maana unga umepanda, *inflation* iko pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukisema watu waendelee kunywa maji machafu vijijini maji ambayo sio safi na salama wataugua matumbo, *typhoid,* kuharisha na kadhalika utatumia shilingi ngapi kuwatibu hawa? Madawa, vifaa tiba, kulaza hospitalini, gharama yake ni kubwa kuliko hiyo ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha anasema kwamba itatokana na kupandisha bei ya mafuta kutoka sh. 50 kwenda sh. 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo si kweli kwamba kutakuwa na *inflation* isipokuwa kutokupandisha tozo hii ndiko kunasababisha *inflation* iwepo kwa sababu watu wanaugua sana. Zahanati na hospitali zinajaa wagonjwa, *ambulance* zinatumika sana kwa hiyo hali inakuwa ngumu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna miradi ya maji kwa vijiji 10 kwenye kila Halmashauri, yote imekwama. Miradi hii si ya leo wala si ya jana, ina miaka minne, mitano, nane, imekwama. Pale kwangu kuna kijiji kimoja Ibwera kuna mabomba yaliletwa pale mengi sana, mabomba ya kutosha mradi mzima yako pale kando ya barabara yamekaa miaka minne hadi yamebadilika rangi kutoka nyeusi yamekuwa meupe na yametoboka. Sasa hasara kubwa sana kwa sababu ya kutokuwa na fedha za kumalizia mradi ule. Nashauri sana kwamba bajeti ya maji kwa kweli tuizingatie na tuongeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya Kibirizi kule kwangu imekwama, miradi ya Bituntu imekwama, Lubafu,

Katoma yote imekwama; Miradi yote vijiji 10 haija-*take off* haijaweza kukamilika kwa sababu chanzo cha fedha kutoka Benki ya Dunia kimekoma. Lazima tusimamie Mfuko wa Maji upate fedha. Pamoja na kupandisha sh. 50 kwenda sh. 100 kwenye mafuta ya magari *diesel* na *petrol* mimi napendekeza yafuatayo yaongezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni hilo, hiyo tozo mafuta toka sh. 50 kwenda sh. 100 iongezwe. Pia maji haya tunayokunywa mjini haya ya chupa, vijijini hamna maji ya chupa, yako mjini, watu wenye fedha wako mjini; wananunua maji nusu lita sh. 2000. Huku nako tuweke tozo angalau kwa lita sh. 50 kwenye maji ya chupa. Maji ya chupa yawe na tozo sh. 50 iende kwa Wakala wa Maji Vijijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bia; wanywaji wa bia wako mjini, nako kuwe na tozo kwa lita moja ya bia angalau sh. 50 iende Mfuko wa Maji Vijijini. Soda; wanywaji soda wako mijini, angalau kwa lita nzima ya soda sh. 20. Pendekezo langu, kiasi hicho kiende kwenye Mfuko wa Maji Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipendekeze pia kwamba kwenye *bill* za maji, mijini kuna maji, miji yote ina maji ya bomba mazuri safi na salama. Kuna *bill* za maji za kila mwezi au za kila wakati angalau asilimia tano ya ile *bill* ikatwe iende katika Mfuko wa Maji Vijijini ili nao wapate maji. Wakazi wa mjini ni wa vijijini hawa, wanatoka vijijini wanakuja mjini, walipe angalau asilimia tano ya zile *bill* ziende kwenye Mfuko wa Maji Vijijini ili Wakala wa Maji Vijijini uwe na uwezo wa kuhudumia miradi ya maji vijijini. Vile vile wakala huu uimarishwe, watafutwe watu wenye uwezo, wajitegemee, watafute fedha ndani na nje ya nchi. Waombe kwa wafadhili, waseme tuna shida vijijini, watu wanaugua matumbo sababu ya maji machafu tutafute fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo *REA,* tujifunze *REA, REA* imefanikiwa baada ya miaka michache, sasa hivi imefanikiwa kwa asilimia 70% nchi nzima. Kwa hiyo wakala

uimarishwe uweze kufanya kazi ya kusaidia kupata maji vijijini. Hata hivyo, Serikali na yenyewe kwa kweli kama nilivyosema mwanzoni, kupunguza bajeti ya kutoka milioni 900 kwenda 600 si sahihi. Fedha irudishwe, ibaki angalau 900 hiyo hiyo na itoke; kwa sababu ilikuwa milioni 900 lakini iliyotoka ni asilimia 19, ni kiasi kidogo sana itoke iende kwenye miradi ya maji ili wananchi wa vijijini wapate huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ni muhimu sana, mimi ukiniuliza kati ya maji na umeme nitakwambia maji ni muhimu kuliko umeme. Umeme unaweza ukaona kwa kibatari lakini huwezi kuishi bila maji, kwa hiyo tuyape uzito unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa mradi wangu wa maji pale Bukoba Vijijini, mradi wa maji wa miaka mingi, miaka ya 60 na 70 mwanzoni, wa pale Maruku. Nimeshamwambia Mheshimiwa Waziri, mradi huu ni mzuri, ulijengwa na Serikali ya Awamu ya Kwanza, ukafanya kazi nzuri sana, lakini miaka mingi imepita umechakaa. Mradi ule umechakaa yale mabomba tu, matanki yako vizuri na chanzo kiko vizuri. Kama tukipata milioni 300 ama 400 mradi ule unakarabatiwa unakuwa mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mradi huu ufufuliwe, upate fedha kidogo ili na wenyewe uweze kuhudumia Kata mbili, Maruku na Kanyangereko...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mattar Ali Salum atafuatiwa na Mheshimiwa Adamson Emanuel Mwakasaka na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar ajiandae.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii kwa ajili ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jina langu naitwa Mattar Ali Salum, kwa hiyo naomba kidogo tuliweke sawa ili tuweze kufahamika vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi yake nzuri ambayo anaifanya katika kushughulikia tatizo la maji katika nchi yetu, maji ni uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nigusie sana katika suala la Mfuko wa Maji. Ni suala ambalo ni *sensitive* sana ambalo Serikali lina haki sana ya kutusikiliza kwa macho mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Maji ndio mkombozi wa nchi hii. Kwenye ziara yote ambayo tumeifanya, ukaguzi tulioufanya Kamati katika maendeleo yaliyofanywa katika miradi ya maji yote asilimia kubwa imetoka katika mfuko wa maji. Kwa hiyo niiombe sana Serikali iangalie huu mfuko wa maji ili uweze kuendelea kuweza kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali na maombi yangu haya naamini yatakuwa ni ya Waheshimiwa Wabunge wengi ambao walichangia Bunge lililopita na hata Bunge hili. Tunaiomba sana Serikali iongeze sh. 50 ili ifike sh. 100 ili Mfuko wa Maji uwe mkubwa ili uweze kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba sana Serikali suala hili la kuongeza hii sh. 50 itimie sh. 100 kwenye kila lita ya *petrol* na *diesel* hili liwe *important* sana. Serikali tunaiomba sana iweze kusikia tatizo hili, iweze kusikia maoni ya Waheshimiwa Wabunge na hivyo kuhakikisha maji yanapatikana kwa ufasaha.

Mheshimiwa Naibu Spika tumeiona bajeti ya Serikali ilivyo ndogo, lakini tukipata pesa katika mfuko huu, ukikaa vizuri basi tunaweza tukafika katika hatua kubwa katika kutatua tatizo la maji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la maji bado ni sugu sana ambalo kutatulika kwake ni kazi ngumu sana, inahitaji kazi ya ziada ili tuweze kutatua tatizo hilo la maji. Tumefanya ziara katika vijiji vingi, katika Wilaya nyingi tumekuta tatizo la maji linaendelea kusumbua sana. Niiombe sana Serikali iweze kusikia kilio hiki cha kuongeza hizi sh. 50 ili iwe sh. 100 kwa lita ya *petrol* ili iweze kufikia hatua ya kutatua tatizo hili la maji hasa katika vijiji vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, katika uongezaji wa sh. 50 hii ikawa sh. 100, nashauri shilingi 70 iende vijijini shilingi 30 ije mijini kwa kuwa vijijini ndiko kuna kero kubwa ya maji kuliko mjini. Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri pesa hii iweze kugawia vizuri na niiombe Serikali iweze kutukubalia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuendelea nigusie tatizo la pesa za Benki ya India zinazokwenda Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni zito sana. Bajeti iliyopita fedha hizi zililetwa ndani ya vitabu tukaambiwa fedha hizi za Benki ya India zinazokwenda Zanzibar zimeshakuwa tayari; lakini kitu kikubwa mpaka sasa fedha hizi hatujui zipo wapi, hatujui zimefikia vipi. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri juu ya hili suala la pesa hizi za Benki ya India zinazokwenda Zanzibar ambazo ni mkombozi wa matatizo ya maji kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; wananchi wa Zanzibar wana matatizo makubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, fedha hizi za Benki ya India aje atuambie zimefikia hatua gani na ni lini fedha hizi zinaweza kwenda Zanzibar ili ziweze kutatua kero Zanzibar?

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee na umwagiliaji wa maji. Hali ya hewa ya nchi yetu sio shwari, kwa hiyo tunaomba suala la umwagiliaji wa maji ni suala nyeti sana, lazima tuongeze suala la umwagiliaji kwa nguvu zetu zote angalau tufikie hekta milioni moja, tunaweza ku-*save* matatizo ya maji tuliyo nayo. Mheshimiwa Waziri nimwombe sana, hali ya hewa iliyokuwepo nchini kwetu si shwari na tukitengemea kilimo cha mvua hatuwezi kufika mahali ambapo tunapatarajia. Nchi yetu inaendelea na ukame na matatizo ni mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, tuliangaliengalie kwa macho mapana suala la umwagiliaji ili tuweze kufikia hatua ya kuhakikisha wananchi wetu wanaweza kupata kilimo cha umwagiliaji kwa asilimia kubwa. Hii itawezesha nchi yetu kuwa na kilimo cha mafanikio. Kilimo cha kutegemea mvua hakiwezi kuondoa hali ya njaa katika nchi yetu; lazima tugeukie upande wa kuangalia kilimo cha umwagiliaji kwa nguvu zote na tuhakikishe kwamba wananchi wetu wameelekea katika kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie na miradi ya vijijini. Hii miradi ya vjijini bado ni tatizo sugu; wananchi wetu wa vijijini wanapata miradi hii kwa gharama sana na kwamba inawasumbua sana kupatikana kwake. Tunaomba sana Mheshimiwa Waziri, katika hii miradi ya vijijini tuache kutumia majereta twende katika *system* ya *solar* ili tuweze kupata maji kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya ziara, tumeona faida ya matumizi ya *solar* katika miradi ya vijijni, kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri juu ya hili suala la kutumia *solar* katika miradi yetu hasa ya vijijini. Tuache matumizi wa majenereta kwa sababu wananchi wetu wanapata maji kwa gharama zaidi, lakini tukitumia *solar* watapata maji kwa urahisi, watapata maji kwa bei rahisi, watapata maji kwa uhakika. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri akisikilize kilio hiki kwa makini ili aweze kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirejee tena kukazia suala la fedha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja (Makofi).

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka atafuatia na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud ajiandae.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kujadili bajeti hii ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Nami nianze kwa kuwapa pole wale wote ambao wamepata majanga mbalimbali yakiwemo haya ya ajali ambazo zimewakumba watoto wetu kule Arusha, lakini na zingine mbalimbali ambazo zimetokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nitumie fursa hii kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na Baraza lake lote la Mawaziri kwa jinsi wanavyotutendea haki kwa jinsi sisi wawakilishi. Kipekee niipongeze Wizara hii na hasa Waziri wake *Engineer* Lwenge pamoja na Naibu, Katibu Mkuu wake kwa kutukumbuka sisi wana Tabora.

Sisi Tabora kwa muda mrefu tumekuwa na matatizo ya maji na tatizo hili tumekuwa tukiliimba hapa kila mara na hata waliotangulia ni tatizo lililokuwa sugu. Sisi wana Tabora tunaendelea kusema tunaomba mtufikishie salamu za shukrani kwa Mheshimiwa Rais kwa kutimiza Ilani na Sera za Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo pale Tabora kwenye upande wa maji juzi juzi tu tumetoka kushuhudia

mkataba wa mradi wa Ziwa Victoria wa bilioni 600 ambazo zimesemewa semewa hapa; nazidi kuishukuru Serikali. Pia siku chache zilizopita Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu Hassan alikuwepo pale kwa ajili ya kuzindua mradi wa maji kule Mabama Mkoani Tabora. Tunasema ahsante Serikali kwa kuijali Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna matatizo ya maji ambayo kwa kutumia lile ziwa moja la Igombe maji yetu yamekuwa hayana uhakika na hasa yamekuwa ni maji machafu ambayo hata rangi yake mara nyingi utaona ni ya kijani. Sasa tumepata fursa hii tunasema ahsante. Hata hivyo, nitakuwa sijaitendea haki nafsi yangu na hata wananchi wa Tabora kama sitazungumzia hili lililojitokeza leo kwa baadhi ya Wabunge wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mbunge mwenzetu tena naomba ku-*declare interest* kwamba nipo naye kwenye Kamati ya Miundombinu, bahati mbaya hayupo hapa, Mheshimiwa Kitwanga, alizungumzia suala la kwa nini ule mradi wa Tabora umepewa hela nyingi kiasi hicho, amesahau kwamba Tabora ilikuwa imesahaulika miaka mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napata mashaka Mheshimiwa ambaye ameshakuwa hata Waziri, kauli alizozitumia hapa hazipaswi kabisa kutumiwa na mtu yoyote ambaye ni kiongozi wa Serikali, ambaye amewahi kuwa kiongozi wa Serikali na pia ni Mbunge. Unapo sema kwamba mradi ule umepita kwao, kule Kolomije na kwamba mradi ule kwa kuwa unakuja Tabora, yeye yuko tayari kuhujumu mradi ule kuzima mitambo. Kwanza huu ni uasi, lakini si tu uasi ni kuchochea mambo ambayo katika nchi yetu hatujayazoea kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyofahamu kuna miradi mingi imepita nchi hii ambayo haijawanufaisha watu ambao wanaokaa maeneo yale, kwa mfano mradi wa *REA*, hata nguzo za umeme zinapita mahali pengine ambapo watu hawapati mradi huo, lakini sijawahi kusikia wakisema watang'oa nguzo za umeme. Sasa yeye akisema yuko tayari

ule mradi aweze kuzima zile mashine huu ni uchochezi ambao haukubaliki kabisa. Pia unaposema kwamba mimi nikiwa Waziri kule ndani nilikuwa sisemi nitasema nje anataka kutupa *message* gani? Kwamba wakiwa kule ndani wanakuwa waoga? Sidhani kwamba lile suala linapaswa kuzungumza namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kutokana na mradi huu, kuna Mheshimiwa Mbunge mwingine ameongelea mpaka mchakato wake wa mradi wa maji wa Tabora kwamba mchakato wake ana taarifa kwamba haukwenda vizuri na kwamba kulikuwa na waombaji watano na kwamba wengine hawakutendewa haki. Nashangaa pilipili usiokula inakuwashia nini?

Sisi ambao ndio wenye mradi ule tunaona kila kitu kimekwenda vizuri na ule mradi tayari na ule mradi tayari umesainiwa na watu sasa hivi karibu wanaanza kazi. Atuachie sisi wana Tabora tuamue kwamba wale waliopewa ule mradi hawapaswi kuwa na ule mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Tabora tuna tatizo moja wakati tuanasubiri huo mradi wa Ziwa Victoria. Tabora ile mamlaka yetu ya maji *TUWASA* imekuwa na madeni makubwa wanaidai Serikali zaidi ya shilingi bilioni 3.3 ambazo ni malimbikizo ya madeni ya muda mrefu. Sasa naiomba Serikali, ili kuwe na ufanisi na ile Mamlaka ya Maji Tabora, basi deni hili lilipwe ili angalau tuweze kuwa na huduma ya maji ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema asiyeshukuru kwa dogo hata kwa kubwa hawezi kushukuru. Mimi kwa upande kwa Mkoa wa Tabora kwa hapa ambapo Wizara na Serikali yetu imetufikisha kwenye suala la maji, niendelee kuipongeza Wizara pamoja na Chama chetu cha Mapinduzi kwa sababu tunatekeleza sera yake na Ilani pamoja na ahadi mbalimbali zilizoahidiwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, atafuatia Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa Nape Nauye ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kwa kuchangia kuhusu bajeti. Bajeti kwa kweli ni ndogo na inashangaza kabisa. Tunasema kuwa maji ni uhai na kila mmoja anajua kuwa maji ni uhai. Maji ni uhai kwa binadamu, maji ni uhai kwa kila kiumbe na maji ni uhai kwa viwanda ambavyo tunasema tunaenda kwenye Tanzania ya Viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya kuwa na maji ya kutosha hatuwezi kuendeleza haya mambo mazuri ambayo tunayopanga. Bajeti ya mwaka huu ni ndogo ukilinganisha na ya mwaka wa jana, nawaomba Waheshimiwa Wabunge kila mmoja atakayesimama aiongelee hii bajeti kusudi tuweze kuiongeza na kufikia angalau ya mwaka wa jana ili tuweze kufikia malengo mazuri ya mwaka 2021 ya kuwa na maji ya kutosha na kuweza kumtua mwanamke ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naomba kuongelea ni tozo. Mwaka wa jana tuliongelea kwamba tozo kwa ajili ya Mfuko wa Maji iwe sh. 100, lakini haikupitishwa. Sasa hivi nazidi kuongelea zaidi na zaidi na naungana pamoja na Kamati ya Kilimo na Maji kusudi iweze kufikia lita moja ya *diesel* na lita moja ya mafuta ya *petrol* kuwa sh. 100. Kwa namna hiyo tutakuwa tumekuza Mfuko wa Maji. Vijijini akinamama wanapata shida sana na hata watoto wa kike ambao ndio wanatumika kuchota maji hawaendi mashuleni kwa sababu ya kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 70 ya fedha ambazo zitakuwa zimekusanywa tuzipeleke huko vijijini na asilimia 30 ziweze kupelekwa mijini. Kwa nini nasema hivi, ni kwa sababu mijini kuna miradi mingi ya maji na wafadhili ni wengi ambao wanafadhili mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukipata maji safi na salama tutaweza kupunguza magonjwa nyemelezi hasa ya tumbo, kwa mfano kipindupindu ambacho kimekithiri kwenye miji yetu pamoja na kuhara kwa tumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuongelea juu ya Halmashauri zetu. Kwenye Halmashauri zetu ilikuwepo sheria ndogo ya uvunaji maji, naomba sheria hii irudishwe kwenye hizi Halmashauri zetu. Kama haipo kwenye Halmashauri nyingine itungwe na kama kwenye Halmashauri nyingine ipo isimamiwe vizuri sana kusudi wananchi waweze kuvuna maji kwenye nyumba wanazojenga na pia kwenye mabwawa ambayo watakuwa wameyatengeneza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukipata maji safi na salama tutakuwa tumepunguza mambo mengi. Tutakuwa tumeimarisha afya yetu na familia na wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha za maendeleo. Tunapanga fedha za maendeleo na zinapitishwa vizuri sana, lakini ukiangalia haziji kama tunavyopanga. Kwa mfano mwaka jana fedha za maendeleo ambazo zimetolewa ni aslilimia 19.8 tu kwa upande wa maji na upande wa kilimo cha umwagiliaji ni asilimia 8.4 tu ambazo zimetoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya kuwa na fedha za maendeleo miradi yetu yote ambayo tutakuwa tunapanga haiwezi kukamilika, ndiyo sababu unakuta tuna miradi mingi viporo. Kwa mfano miradi mingi ya Benki ya Dunia bado haijakamilika kwa sababu fedha tunazotenga hazitoshi na hazitoki.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zote za ndani hasa ndizo zinazopaswa kutoka kwa sababu fedha za ndani tunakuwa na uhakika nazo. Kwa mfano, mwaka huu, Serikali imetenga asilimia 66 ya fedha za maendeleo za ndani. Kwa hiyo naiomba Serikali, kuwa hizi fedha ambazo zimetengwa

tuzisimamie na kwa sababu ni za ndani tunaamini kuwa zitatoka; fedha hizi ziweze kutoka ili zikamilishe miradi yetu ambayo tutakuwa tumetenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo cha Umwagiliaji. Hatuwezi kusema kuwa tutaweza kufanikiwa katika kilimo kwa kutegemea mvua na kwa kutegemea jembe la mkono. Kwa hiyo naomba Serikali yetu, kwamba miradi mizuri iliyopangwa ikiwemo ya Mkoa wangu wa Morogoro, kama ile ya Mikula pamoja na miradi mingine, itekelezwe kusudi tuweze kutoka kwenye hekta 468.338 mpaka kwenye hekta milioni moja mwaka 2021. Ukame ulitunyemelea kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi, nyote mnajua. Nchi zote zilizoendelea zinatumia kilimo cha umwagiliaji pamoja na kulima kwa matrekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Umwagiliaji. Nashauri; kwa sababu hela tunazotenga hazitoshi na hazitoki kutoka Hazina; kwamba uanzishwe Mfuko wa Umwagiliaji. Tukiwa na Mfuko huu tutakuwa na uhakika kuwa hela tunazotoa kwenye mfuko huo tunaweza kulima na kupata chakula cha kutosha na hivyo tutapata chakula cha uhakika kwa mwaka mzima na tutainua lishe yetu, hasa Mkoa wetu wa Morogoro pamoja na Tanzania kwa ujumla, ambapo sasa hivi tuna utapiamlo unaokaribia asilimia 34 ambayo si nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tufanikiwe kwenye kilimo cha umwagiliaji lazima tuwe na watalaam. Hata hivyo, mpaka sasa hivi tuna watalaam wachache; *engineers, surveyors* ni wachache sana kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, naomba kuiuliza Serikali, je, ina mkakati gani? Kwa sababu tuna vyuo vichache vinavyotoa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia naomba mradi wangu wa Chalinze namba..

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umemalizika

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Khadija Aboud atafuatiwa na Mheshimiwa Nape Nnauye, Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka ajiandae.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie bajeti hii ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa niaba ya wananchi wangu wa Mtama nitoe pole kwa wenzetu wa Arusha kwa msiba mkubwa walioupata kutokana na ajali na kufiwa na wanafunzi karibu 32, tunaamini Serikali itachukua hatua kuzuia hizi ajali ambazo zimeendelea kutokea siku hadi siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani ilianza kuchukua hatua kadhaa za kuongeza mapato ya Serikali ikiwa ni pamoja na kubana mianya ya wakwepa kodi. Pia kupunguza matumizi ikiwepo kupunguza safari, kupunguza sherehe na matumizi ambayo kwa kweli pengine kwa namna moja au nyingine hayakuwa ya lazima; ikiwemo kushughulika na wafanyakazi hewa na hatua mbalimbali ambazo zilichukuliwa na Serikali katika kipindi ambacho Serikali imekuwepo madarakani. Pia kwa takwimu tunaambiwa uchumi unakua kwa asilimia 7.2. Haya yote hayatakuwa na maana kama hayatatafsiriwa kwenye maboresho kwenye huduma za jamii na hasa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hizi lengo lake lilikuwa ni kuongeza uwezo wa Serikali. Sasa kama hatua hizi zimechukuliwa na matokeo yake ni chanya tunapaswa tuyaone kwenye ongezeko la huduma za jamii, na hapa tuanze na suala la maji ambalo linagusa kila mtu. Tusipofanya

hivi hatua tulizochukua hazitakuwa na maana hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti iliyopita tumetenga bilioni mia tisa. Bajeti hii tukiwa tumesimamia hatua tulizozichukua ambazo kwa kweli zingeongeza uwezo wa Serikali; tunatoka 900 kwenda 600, hatujatafsiri mafanikio ya hatua tulizozichukua, kwa vyovyote vile Watanzania hawawezi wakatuelewa. Ukuaji wa uchumi wetu hauwezi ukabaki kwenye makaratasi peke yake, hatuna tunayemfurahisha, tunataka tuwafurahishe wananchi wetu na hivyo, lazima tutafsiri ukuaji huu kwenye huduma za jamii na hapa kwenye sekta ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wito wangu wa kwanza, naamini Serikali ni sikivu. Watu wamepiga kelele juu ya jambo hili lakini lazima pia tuone matokeo yake, wananchi hawataelewa hatua tunazozichukua kama haziwezi kwenda kubadilisha maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Ilani ya Uchaguzi ya CCM, ambayo bahati nzuri kwa mujibu wa Katiba ya CCM ilani hii inatengenezwa na kusimamiwa na Idara ya Itikadi na Uenezi, ambapo wakati ikitengenezwa mimi nilikuwa mkuu wa idara hiyo.

Vile vile nilibahatika kuzunguka nchi nzima, jimbo kwa jimbo na kwa kila jimbo nimelala siku moja. Tatizo la maji liko kila jimbo katika nchi hii, hakuna mahali ambako hakuna tatizo hili. Tunapishana ukubwa wa tatizo lakini umegusa kila mahali na mimi nimeshuhudia kwa macho yangu. Ndiyo maana tulipokuwa tunatengeneza ilani ya uchaguzi moja ya jambo kubwa ambalo tumelizungumza kwa kina ni suala la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani hii ya Uchaguzi, iliyotengenezwa na Chama cha Mapinduzi ndio mkataba wetu kati ya CCM na wananchi. Tusipoitekeleza wananchi hawataturudisha na huu ndio ukweli, kwa sababu tuliwaahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya tatizo la maji pamoja na kuathiri watu wote lakini akinamama ambao ndio wapiga kura wakubwa wa CCM ndio waathirika wakubwa wa tatizo hili. Ndiyo maana sina mashaka kwamba Serikali itasikiliza iende ikaongeze pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ilani hii tumeahidi kwamba tutatoa kiwango cha upatikanaji wa maji vijini kutoka asilimia 67 kwenda 85. Dar es Salaam pale ambapo *DAWASCO* na Luhemeja wanajitahidi kufanya vizuri lakini kama hakuna hela mambo yatakwama; tunataka kutoa 68 kwenda 95. Kwenye miji na makao makuu ya mikoa kutoka 86 kwenda 95, miji midogomidogo kutoka 57 kwenda 90. Hili halitafanikiwa tukienda na bajeti hii. Ndiyo maana naunga mkono hoja Serikali wasione aibu wala wasijisikie vibaya kurudi kwenda kuongeza pesa hapa. *(Makofi)*

Mwishoni nitatoa mapendekezo. Eneo la pili ni kwenye umwagiliaji. Umwagiliaji ukiangalia hapa hela iliyotengwa ilikuwa kidogo, hela iliyopelekwa asilimia 8.4 lakini hela yenyewe sijui kama wanajua kwamba sehemu kubwa imekwenda kuliwa. Tunayo miradi ya umwagiliaji; jimboni kwangu nina miradi mitatu ya umwagiliaji mradi mmoja umetumia miaka nane haujakwisha, mingine ipo kisingizio kikubwa ni kwamba ilibuniwa vibaya .

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya sana pale jimboni kwangu wakamfukuza Mkurugenzi ambaye hakuwepo, ambaye siye aliyebuni, waliobuni miradi na pesa zikazama wapo na wanaendelea kula nchi hawaguswi kwa lolote. Leo mafuriko tunayoyaona ni kwa sababu tumeshindwa ku-*manage* maji yanayotokana na mvua ambayo yanatiririka kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama tunaendelea kuona umwagiliaji kama kasehemu kadogo sana kwenye Wizara, nadhani pengine *either it is wrong placed,* tuipeleke mahali sahihi ili umwagiliaji ufanye kazi iliyokusudiwa, tukienda hivi hili eneo hatutafika. Sasa napenda nitoe mapendekezo yafuatayo:-

La kwanza, hili…

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Unga mkono hoja

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Kamili ambaye atachangia kwa dakika tano, dakika tano nyingine anampa Mheshimiwa Julius Kalanga, kwa hiyo, Makatibu hapo muangalie. Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Na mimi niungane na wenzangu kutoa pole sana kwa wafiwa wote waliofiwa na watoto wetu wale waliofariki kule Arusha kwa ile ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nielekeze mchango wangu katika upande wa umwagiliaji maana najua hapa ndio kwenye maisha yetu Watanzania wote. Ukiangalia tafiti ambazo zimefanyika za *REPOA* na *ESRF* zote zimeonesha kwamba, Tanzania kama tunataka kutoka katika umaskini lazima msisitizo uwe katika kilimo cha umwagiliaji, kama hatukuweka msisitizo katika kilimo cha umwagiliaji hata tukitengeneza barabara kiasi gani tutakuwa tunajidanganya, maana nchi ambayo haiwezi kujilisha haina heshima yoyote hapa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hata Jarida la *Economist* la 2012 linatueleza jinsi ambavyo Tanzania ni nchi ya kumi na moja duniani ya kuwa na maji mengi ambayo ni maji yale tunasema maji ya baridi au maji ambayo hayana chumvi. Ukiangalia Ziwa Tanganyika peke yake lina asilimia 17 ya maji yote masafi katika ulimwengu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiweka na Mito ya Pangani, Rufiji na Maziwa mengine tuliyonayo hakika utajua kwamba Tanzania tuna utajiri mkubwa sana wa maji. Licha ya maji tuna mabonde makubwa sana yanayofaa kwa

umwagiliaji. Tafiti pia zimeonesha na Mheshimiwa Waziri amezungumza, kwamba tuna mabonde hekta milioni 29.4 yanayofaa kwa umwagiliaji. Lakini inasikitisha kwamba mpaka sasa ni hekta 468 tu ambazo zimejengewa miundombinu, na hiyo ni kama asilimia mbili tu ya sehemu yote ambayo imejengewa miundombinu ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunauliza hivi kweli Watanzania tunatakaje kuondokana na umaskini wakati hatutilii mkazo zile sekta ambazo zitatutoa kwenye umaskini? Unaangalia unajua je, ni kwamba hatutaki kutumia akili zetu tuko tayari tukaombe misaada kutoka nje, tukachukue misaada kutoka nje? Tungekuwa kama nchi za huko Ethiopia, Sudan, hivi nchi hii si tungekuwa tumeshakufa wote. Kwa hiyo, ninachosema, ni kwamba nchi yetu bado hatujatumia busara, hekima na akili Mungu alizotupa kwa ajili ya kuona vipaumbele vyetu viwe katika nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kilimo kwa mwaka 2010 kilikua kwa asilimia 2.7 lakini mwaka jana kimeshuka hadi asilimia 1.7, tatizo unaambiwa uhaba wa mvua, ni aibu. Maji yamejaa tunazungumzia uhaba wa mvua kwa nini akili zetu zote tunapeleka kwenye mvua? Haya mambo ya kilimo cha umwagiliaji tumezungumza miaka nenda, rudi tangu kilimo kwanza, lakini mpaka leo tuna tatizo hilo, sijui tusemeje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija Jimbo la Same Mashariki Mungu ametujalia tuna mito mikubwa ukichukulia Nakombo, Hingilili, Saseni, Yongoma lakini mito yote hii inakwenda baharini, mito yote inapita kwenye vichaka. Tumeomba tujengewe mabwawa ili akinamama ambao wengi ndio wanaolima wapate nafuu, akinamama ndio watekaji maji wengi ndio wanahangaika. Watoto wetu wa shule wako wengine *boarding* wanafuata maji kilometa nzima au mbili, ugonjwa wa *UTI* haupungui kwenye *boarding schools,* ugonjwa wa kuharisha watoto, akinamama kila siku wako hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba bajeti ya Wizara ya Afya iongezwe. Tunasema hapa Wizara ya Afya iongezewe pesa kumbe yote inaenda kutibu kuharisha, matumbo, kwa nini tusingeboresha maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nasema, nchi yetu tukiendelea kwa mtindo huu, tusipojali maji na hasa tuseme maji ya kumwagilia akina mama, mboga mboga, akina baba mashamba, vijana wetu hasa kule Jimbo la Same Mashariki kilimo cha tangawizi ambapo *LAPF* wanataka wajenge kiwanda kikubwa, hakiwezi kufanya kazi kama tangawizi haitapata maji ya umwagiliaji. Kwa hiyo naomba wenzetu walione hilo tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishuke kuangalia nini kinachotufanya Tanzania tunarudi nyuma. Hata tukisema bajeti ya Wizara ya Maji iongezwe, ambavyo naunga mkono, je, ubadhirifu ambao uko katika Wizara ya Maji nao tutaufanya nini? Ukiangalia ukaguzi wa ufanisi wa ujenzi wa miradi ya maji hasa ya mijini kwa mwaka 2010/2011 na mwaka 2013/2014 imeonesha katika miradi tisa, miradi nane iliongeza gharama zake kuanzia asilimia 10 mpaka asilimia 229 sawa na ongezeko la shilingi bilioni 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa je, Wizara ikiongezewa bajeti sasa hivi itatuhakikishiaje kwamba haya maji yatawafikia hasa akina mama ambao katika Tanzania wako asilimia 51 na na kati yao asilimia 60 wako vijijini? Tupunguze bajeti ya kwenda huko kwenye miji ili asilimia 30 iende mjini, 70 iende vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nasisitiza kwamba tungeanzisha Wakala wa Maji Vijijini badala ya Mfuko wa Maji ili tuwe na uhakika maji kweli yanaenda vijijini na kwamba maji yatawafikia wananchi vijijini. Kinyume cha hapo fedha itawekwa kwenye mfuko halafu hela zitakwenda ndivyo sivyo. Kwa hiyo, ningeomba sana, hata kama tukisema tunaweka umeme mwingi, barabara za lami kama akina mama vijijini watakuwa wanahangaika na maji, hakika nchi hii hatutaendelea. Akina mama ndio wenye uchumi mkubwa

katika nchi hii, ndio wakulima wadogo wadogo. Tume-*fail* katika mambo mengi lakini hebu tuwape akinamama *chance*, tupeleke maji vijijini, tuanzishe huu Wakala wa Maji Vijijini ili tuwe na hakika hela kweli inaingia huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rose Kamili dakika tano, Mheshimiwa Julius Kalanga dakika tano, watafuatiwa na Mheshimiwa Tunza Malapo.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Naomba pia iwe nafasi pekee ya kuwapa pole ndugu zangu wapendwa wa Arusha, Walimu na wazazi waliopotelewa na watoto wao. Mwenyezi Mungu awape faraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata hii fursa ya kuchangia bajeti ya Wizara hii ya maji ambayo naita kwamba iko *ICU*. Sababu ya kusema iko *ICU,* ukweli ni kwamba kama mwaka jana ilitolewa au iliidhinishwa bajeti ya bilioni 915.2 na haikutolewa yote na leo tena tunaidhinisha bajeti ya bilioni 632.6 ambayo hatuna uhakika wa kutolewa; na tena iko pungufu ya bilioni mia mbili themanini na moja ya bajeti iliyopita mwaka jana, maana yake Serikali yetu haifanyi kazi ya kukusanya mapato nchi hii.

Mhesimiwa Naibu Spika, sisi Watanzania hapa tuna vitongoji 64,677, hivi vitongoji vyote vinahitaji maji, lakini ukiangalia wanasema wametoa miradi 1,333 ndani ya vitongoji 64,677, ndiyo maana nimesema wako *ICU.*

Mheshimiwa Naibu Spika, maji tukubaliane ni uhai na kwa kuwa maji ni uhai, ni uchumi, ni msingi wa amani na ni haki za binadamu, nadhani sasa ifike mahali tuangalie ni jinsi gani tukomboe nchi hii kwa ajili ya maji. Mbinu pekee ya kuikomboa ni kuhakikisha kwamba, hii bajeti inarudiwa upya, hii bajeti ikarekebishwe upya tuijadili ili Watanzania waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maana kwamba, Mheshimiwa Rais mwenyewe alitoa Kauli Mbiu kwa wanawake kwamba, nitawatua ndoo za maji vichwani. Sasa hapo ni kutua ndoo za maji au ni kuwawekea ndoo za maji? Labda hatujui Kiswahili! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo napenda tulijue vizuri kwamba, kama ni kutua hizo ndoo basi nendeni kwenye sera ya maji ya mwaka 2002, kuhusu suala la miradi ya maji vijijini, kila mwananchi aweze kupata maji isizidi mita 400. Je, mpaka sasa hivi mna mita mia ngapi ambazo zimewafikia hao akinamama, kama mnataka kuendelea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namna pekee ya kuokoa hii Wizara, nawaombeni sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa pamoja hasa sisi wanawake, ili tuwakomboe wanawake wenzetu vijijini; mimi nina uhakika asilimia 99 tumetoka vijijini ndipo tukaenda mjini. Sasa mjue kabisa kwamba, akinamama wanachota maji kwa umbali mrefu sana, sio chini ya kilometa 20 wengine, wengine kilometa tano na kadhalika wanaamka saa 9.00 kwenda kuchota maji. Namna pekee ya kuwasaidia ili waweze kuleta maendeleo ni sisi kuhakikisha kwamba, tunaliomba Bunge hili kwamba hizi fedha ziongezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namna pekee ya kuongeza kwenye huo mfuko, tunaomba kuuliza ile tozo ya sh. 100/= tuliyoiomba kwa nini mliikataa? Kama mnaweza kufanya maendeleo au mnaweza kutoa zile fedha za maendeleo, ni kwa nini mlikataa ile tozo ya Sh. 00/= tusiitoze kwenye mafuta, badala yake mkakaa kimya? Mngetueleza tena kwamba haiwezekani kwa sababu bei ya mafuta inapanda. Bora tupande bodaboda kuliko kukosa maji. Kama tungekosa maji humu ndani nyie wanaume mngekuwa na vikwapa na sisi wanawake ni uvundo mtupu; sasa kwa nini tusiangalie suala la maji kwa wenzetu na tuwaokoe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namna pekee ya kuboresha huo Mfuko wa Maji, basi tutafute namna nyingine ya Mfuko

wa Barabara ichangie Mfuko wetu wa Maji sh. 100 ile ipatikane ili maji yapatikane vijijini. Mfuko wa Umeme upatikane, kwa sababu barabara huwezi kujenga bila maji. Kwa hiyo nao wachangie kwenye ule Mfuko wetu wa Maji ili tuweze kuboresha hiyo miradi ya maendeleo kwenye vijiji vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kujua...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Julius Kalanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Tunza Malapo na Mheshimiwa Magdalena Sakaya ajiandae.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote niungane na wenzangu kuwapa pole wazazi wote waliopoteza watoto wao katika ajali mbaya. Mungu aendelee kuwafariji na kuwatunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kila mtu na hakuna hata Mbunge mmoja anayekataa kwamba, kuna tatizo la maji nchini, kila mtu anakiri hilo na tatizo hapa inaonekana ni fedha. Kama kweli Bunge hili lina wajibu wa kuisimamia Serikali na kupitisha bajeti ya Serikali ni lazima tuungane kwa pamoja kuhakikisha Serikali inaongeza fedha katika bajeti ya maji ili kuwasaidia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni mama na bahati nzuri kuna Wabunge wengi wa Viti Maalum wanaotokana na akinamama. Mimi kwa umri wangu huu sijawahi kuchota maji hata bombani kwangu pale ndani, nje ya nyumbani kwangu. Ni utamaduni na desturi ya Watanzania na ya

Waafrika wengi kwamba, akinamama ndio sehemu kubwa wanashughulikia matatizo ya watu majumbani. Kama kweli tunataka tuwasaidie kama sio kuwatwisha ndoo kichwani ni kuwatua ndoo kichwani, tuongeze bajeti kwa ajili ya kuwanusuru akinamama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata nyakati nyingine hata kazi za kufanya za kuwasaidia watoto wao hawafanyi, kwa hiyo jambo hili ni *serious* sana. Kama kweli, tuna nia njema ya kulisaidia Taifa hili, tuisaidie Serikali ikaongeze bajeti, heri hata ikasimamisha shughuli nyingine ili wananchi wakapate maji. Wakati wa kiangazi mwaka huu mnajua jinsi nchi yetu ilivyopita katika janga la ukame; kama hali ikiendelea hivyo nani atakuwa salama katika nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naamini kama tukiamua kama Bunge, tuirudishe bajeti Serikali ikaongeze fedha katika Wizara hii ya Maji ili wananchi wetu wapate maji. Kama tunakubaliana kuwasaidia akinamama hawa na si kwa unafiki, turudishe bajeti hii ili Serikali ione ni namna gani itafanya ili kuwasaidia akinamama kuondokana na tatizo la maji. Kama ni punda anayeswaga ni mama, kama ni ndoo ni mama anayebeba kichwani, kwa sababu hiyo na sisi wote tunatokana na mama, naomba tuungane kuwasaidia akinamama kuondokana na tatizo hili la maji. Hatujui mateso ya mtu anayebeba ndoo ya lita 20 kichwani kwa kilometa mbili au tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni uchungu wanajua hawa akinamama, tuwasaidie kuondokana na tatizo hili la maji nchini. Sikusudii kuzungumza matatizo ya maji kwenye jimbo langu kwa sababu hata fedha mlizotenga hazifai hata kuzungumza, lakini kama tuna nia njema turudishe bajeti hii, Serikali ikapitie upya, ili jambo hili lipate kufikia muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kama Serikali ina nia ya dhati ya kuwasaidia Watanzania; kama Serikali ina nia ya dhati ya kusimamia suala la maji nchini itasikiliza kilio cha Waheshimiwa Wabunge wengi hapa ndani ambao kila

mmoja kwenye jimbo lake anajua adha ya kwanza tunayokutana nayo kama Wabunge wa vijijini ni suala la maji vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu hata kwenye mikutano hawaendi kwa sababu ya maji; na naamini hata Waheshimiwa Wabunge hawa wanaosimamia Wizara hiyo wanatoka vijijini, wanajua matatizo na adha ya maji. Naibu Waziri alikuja Monduli, aliona mazingira ya Jimbo lile; miaka 50 ya uhuru wananchi wetu bado hawajui watachota maji wapi, miaka 50 ya uhuru tunahangaika na akinamama wanaendelea kununua ndoo sh. 500/=, hii haikubaliki mahali popote, lazima kama Bunge tuisaidie Serikali kutafuta Suluhu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Monduli maeneo ya Mfereji, maeneo ya Sepeko, maeneo ya Moita, maeneo ya Esilalei na maeneo mengine ya Lepurka ambayo ni kame, miaka 50 ya uhuru wananchi wale hawajawahi kuona maji ya bomba. Naomba Serikali isikie kilio cha Waheshimiwa Wabunge ikarekebishe bajeti hii ili iwafae wananchi wa leo na vizazi vijavyo kwa ajili ya maisha yao ya sasa na maisha yao ya baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge tuache itikadi katika hili, tuisimamie Serikali ikarekebishe bajeti yake. Haiwezekani bajeti ya bilioni mia tisa unapunguza kwa asilimia 30 halafu hata ya mwaka jana umepeleka kwa asilimia 19 halafu upunguze, leo utapeleka kwa asilimia ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali itwambie ni kwa nini bajeti ya maji ambayo imetekelezwa kwa asilimia 20 imeshushwa kutoka ile bilioni mia tisa kuja bilioni mia sita, ni kwa nini? Ni vigezo gani vinatumika? Au ni mpango gani Serikali inao katika kuondokana na tatizo la maji nchini? Kama haiwezekani tu-*admit* kwamba hili ni Janga la Kitaifa na hili tatizo la maji sasa Serikali imeshindwa, ili tutafute namna nyingine hata wahisani kutusaidia. Hatuwezi kwenda

kwa namna hii kama hatukubaliani kusimamia suala la maji ambalo ni tatizo kubwa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nitangaze majina ya wachangiaji wengine wa *CUF* maana naona wote wanatawanyika hapa mbele, sasa msije mkajikuta hamna watu wengine! Mheshimiwa Mussa Mbarouk na Mheshimiwa Suleiman Said Bungara watafuata baada ya Mheshimiwa Magdalena Sakaya, maana msije mkajikuta wote mmeshatoka nje.

Mheshimiwa Tunza Malapo!

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia naomba tu niwaulize hawa Mawaziri wa Maji, hivi ni kwa nini ninyi hampewi hela? Kuna tatizo gani? Labda wakitueleza tutatoka hapo tukajua tuwasaidie vipi, kwa sababu tunajua sekta ya maji ni sekta muhimu, lakini ukienda kwenye pesa walizopewa za maendeleo ni asilimia 19.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunakaa hapa tunajadili, tunafanya nini, lakini mwisho wa siku utekelezaji finyu, kwa hiyo, wakati wanakuja kujibu watueleze kwa nini Wizara ya Maji haipewi pesa za kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo ni lazima nichangie tu. Kuhusu Mfuko wa Maji, naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba, pesa ziongezwe kwa ile tozo kutoka shilingi 50/= kwa lita mpaka shilingi 100/=, lakini katika kuongeza huko naomba ile pesa ikiongezwa ikafanye jambo lililokusudiwa. Sisi lengo letu watu wa vijijini wapate maji, angalau ile pesa asilimia 70 ikatumike vijijini ili kuwawezesha akinamama wa vijijini wapate maji; isiwe kwamba ile pesa ichukuliwe ikafanye mambo mengine kama *administration* na vitu kama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Mto Ruvuma. Mimi Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa kuhitimisha hii hoja naomba aje na majibu. Kila siku wanatwambia mkandarasi yuko *site* anafanya hivi, anafanya hivi. Tunataka tupate jibu la uhakika, pesa ya kufanya huu mradi ipo ama haipo? Swali la kwanza. Hata hivyo, pale unapopita mradi wamewaambia watu wasiendeleze, lakini mpaka leo hakuna fidia yoyote waliyolipwa? Watu wale mnawaachaachaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Serikali ya China na Serikali ya Tanzania kwenye mradi huu tunaomba sisi watu wa Mtwara tupate maelezo ya kina kwa sababu mradi huu ukikamilika, kama kweli tunasema tunaitaka Mtwara ya Viwanda maji haya yatatusaidia kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye Manispaa ya Mtwara Mikindani; pale maji yapo ya kutosha, tatizo miundombinu. Miundombinu ya tangu mwaka 47 wakati watu wanavaa kaptula badala ya suruali ndiyo hiyo hiyo iko mpaka sasa hivi, haitoshelezi. Huwezi kuamini watu wa Mtwara Mjini kuna watu wengine ukienda mitaa ya Komoro wanachota maji, kule kwetu tunaita ya kuokota; unasubiri mvua inyeshe unachimba kisima unachota, hiyo ndiyo Manispaa ya Mtwara Mjini. Sasa nafikiri kuna haja ya makusudi kabisa Mheshimiwa Waziri wa Maji atueleze mikakati thabiti ya kuitekeleza ili kusudi tuepukane na matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Mkoa wa Mtwara kwa matokeo ya elimu kila siku ni karibu unashika nafasi za chini; kwa mfano mwaka jana shule tisa katika 10 za mwisho zimetoka Mkoa wa Mtwara kwenye mtihani wa *form two;* na waathirika wakubwa ni watoto wa kike. Wanaathirika kwa sababu, pamoja na mambo mengine maji hakuna, wanatumia muda mwingi kwenda kutafuta maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa cha kusikitisha Mheshimiwa Rais ametoa amri ya Kata Umeme. Kweli umeme

umekatwa, umekatwa mpaka kwenye vyanzo vya maji, ukienda kwenye Mradi wa Makonde umeme umekatwa, wananchi wamehangaika maji hakuna.

Sasa najiuliza mwananchi wa kawaida akipelekewa maji nyumbani kwake bili analipa, wale wanaenda kukata umeme kwenye chanzo ambacho maji yale wanaowadai si wananchi wa kawaida; wanadai Jeshi, wanadai Polisi, wanadai Hospitali, lakini wanaenda kukata maji ambayo wananchi wote hawapati; wanaenda kukata umeme kwenye ule mtambo ambapo unasababisha wananchi wengine huku wote wasipate maji, hata wale ambao wanalipa bili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hilo hilo la kukata maji; kwa mfano ukienda katika Manispaa ya Mtwara Mikindani watu wa maji wanadai sana madeni. Ukiangalia wanadai Jeshi, wanadai Polisi, wanadai Hospitali, lakini na wao kwa sababu hawalipwi, wanadaiwa umeme! Ikafikia *stage* wakakata maji Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Ligula siku nne. Niambie yule mama yule tunayemtaka akajifungue, yule mtoto anayeumwa anatibiwa katika mazingira gani? Mpaka maabara ilifungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo mimi nayaongea kwa uchungu sana kwa sababu wale watu wanateseka tatizo sio la kwao, tatizo la Serikali hii hampeleki hela za kulipia hizi huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Umwagiliaji. Naomba nipate maelezo ya kina, inavyoonekana *issue* ya umwagiliaji kwetu si kipaumbele. Sasa kama si kipaumbele watu wakilalamika njaa msiwazuie waacheni waseme, kwa sababu nina mfano. Kuna Skimu ya Umwagiliaji Mtwara Vijijini katika Bonde la Mto Kitere, ile skimu ilifunguliwa na mbio za mwenge mwaka 2014, lakini cha ajabu sijui walifungua kitu gani. Ndiyo maana *sometimes* tunasema mwenge tuuweke makumbusho! Walienda pale wametumia hela chungu nzima, wamefungua, lakini hakuna kinachofanyika. Sasa walifungua ili iweje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bonde lile likitumiwa vizuri sisi watu wa Mikoa ya Kusini naamini hatutahangaika kwenda kufuata mchele Ifakara, hatutahangaika kwenda kufuata mchele Mbeya. Mheshimiwa Waziri anakiri kabisa kwamba miradi mingi ya umwagiliaji ilifanyika kifisadi.

Sasa tunamwomba afanye jitihada za makusudi kuhakikisha miradi ile inafanya kazi na wale watu ambao walihusika katika kuhujumu miradi ile wachukuliwe hatua za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, magonjwa mengi, karibu asilimia tisa ya wagonjwa wanaolazwa hospitali matatizo yao yanatokana na kutumia maji ambayo si safi na salama. Serikali inatumia pesa nyingi kutibu watu wetu. Kwa hiyo, ushauri wangu tuwekeze kwenye maji kwa sababu tutapunguza kutibu watu na kuwafanya watu wakose vizazi, kwa sababu haya magonjwa ya *UTI* na nini yanaenda kusababisha watu wengine wakose vizazi kwa sababu, vinakuwa vinapata matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia suala la uvunaji wa maji ya mvua, nafikiri wenzangu wengi wameliongea, tuweke msisitizo kabisa, tuweke mkakati maalum kama tunavyofanya mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Magdalena Sakaya atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Bakar Mbarouk na Mheshimiwa Selemani Bungala ajiandae

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba iliyoko mbele yetu. Niungane na Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania kuwapa pole wazazi wa watoto wetu ambao wametutoka kule Arusha, Mwenyezi Mungu awape faraja na awapumzishe watoto wetu kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, natamani sana akinamama tungeungana leo, ukiwepo na wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dakika moja angalau tuangue kilio kwenye Bunge hili kwa niaba ya akinamama wa Taifa hili wanaoteseka na kuhangaika kwa adha ya maji kwenye nchi nzima.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walitoa sauti ya kilio kwa niaba ya akinamama wanaohangaika kwa adha ya maji)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania shida ya maji ni kubwa kupita maelezo. Ukiangalia hivi vitabu vya maji kwa miaka karibu mitatu, minne iliyopita unakuta mambo mengi yanayojirudia ni yale yale.

Kiukweli ni jambo la ajabu, Watanzania wanaongezeka kwa milioni moja kwa mwaka. Wakati watu wanaongezeka, mahitaji ya maji yanaongezeka, bajeti ya maji inashuka; haingii akilini kabisa. Kwa mwaka mmoja tunaongezeka watu milioni moja Tanzania na Mheshimiwa Waziri kasema, yaani hata ule uwezo wa ongezeko la watu, tofauti na namna ya kuweza kumudu gharama za huduma kwa wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini mahitaji yanaongezeka wakati huo bajeti inapungua? Wale wanaoongezeka hawahitaji kunywa maji? Hakuna kitu muhimu kwa Mtanzania na mwananchi yeyote wa Tanzania na binadamu yeyote kama maji. Kwa hiyo, tunaomba sana suala la bajeti ya maji iongezwe, hakuna *discussion,* liongezwe kwa sababu watoto wa Tanzania wengi hawaendi shule kwa sababu ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, akinamama wanaamka saa 10.00 ya usiku kufuata maji visimani, wengine wanabakwa. Huwa tunasema, hatufichi, wanabakwa usiku wakifuata maji kwenye visima; watoto wanachelewa shule hawapati elimu wanayostahili. Suala la maji lazima Serikali

ije na mkakati maalum wa namna ya kuhakikisha akinamama wa Tanzania wanapata maji ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Malagarasi. Nimewahi kusema Bungeni hapa mara nyingi, karibu miaka mitano sasa. Ardhi ya Kaliua na ardhi ya Mkoa wa Tabora haiwezi kuchimbwa maji kwenye ardhi yakapatikana, ndiyo maana kwa Kaliua nzima na hata Urambo hatukunufaika na mradi wa *World Bank* kwa sababu, visima vingi vilivyochimbwa havikutoa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haijasema njia pekee ya kutupatia maji Kaliua, Urambo na Nguruka ni kutupatia maji ya Malagarasi. Tangu miaka mitatu iliyopita, kuanzia 2014 tunaambiwa utafiti unafanyika, leo tunaambwa kwamba mpango unafanyika ili kumpata mshauri mwelekezi haweze kufanya *environmental impact assessment,* wakati huo akinamama Kaliua hawana namna.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nategemea angalau wangetuambia mwaka huu tumetenga angalau kuanza zile hatua za awali; lakini Mheshimiwa Waziri hata shilingi. Bahati nzuri hata nimeongea naye hata kabla ya bajeti hii; anasema wanategemea kutafuta fedha. Miradi inayotegemea sana fedha kutoka nje nyingi haitekelezeki. Kwa adha wanayopata akinamama wa Kauliua, Nguruka na Urambo ningetegemea Serikali itoe kipaumbele kwa fedha ya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa Serikali imezindua miradi miwili ya Mkoa wa Tabora, Mradi wa Victoria na ule Mradi wa pale Mabama, Kaliua na Urambo hawamo, sisi hatumo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ripoti aliyoandikiwa Mheshimiwa Waziri, pengine ameandikiwa hakujua; kwamba mradi uliozinduliwa pale Mabama unalisha wilaya zote saba za Tabora si kweli, ni pale Uyui tu na ni baadhi ya vijiji, siyo vyote, lakini ripoti inasema Wilaya

zote saba zitanufanika na mradi uliozinduliwa Mabama, kitu ambacho siyo kweli na kama ni kweli basi watuambie ndani ya Kaliua ni vijiji vingapi vimeingia kwenye mradi wa pale Mabama na pale Uyui?

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha, tutalia mpaka lini hapa Bungeni, ni kweli tulikuwa tunategemea mwaka huu uwe ni mwaka wa matumaini kidogo kwa wananchi wa Kaliua. Kweli naomba Mheshimiwa Waziri bajeti hii ikiisha twende na yeye Kaliua akawambie Wanakaliua wanapata maji safi na salama. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifumo ya Maji Taka na Safi. Ni kweli kwamba kwa maeneo ambayo yameunganishwa na maji taka mifumo yake imechakaa na mingine imeoza. Nikianzia hapa Dodoma, wananchi wanalipa gharama kwa ajili ya maji taka kila bili inapokuja lakini mabomba yamepasuka yanavuja ovyo na bahati mbaya sana wakiitwa kuja kurekebisha wanachukua zaidi ya miezi miwili, miezi mitatu, wananchi wana adha kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua zile fedha zinazolipwa kwenye kila bili kwa ajili ya maji taka nilijua ni kurekebisha mifumo iliyooza, kuondoa mabomba yaliyochakaa kuweka mabomba mengine lakini mabomba ya miaka thelathini yako pale pale tunalipa gharama tunapata usumbufu kila siku ni gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atakapo-*wind up* atuambie kwamba lini mifumo ile ya maji chafu kwenye maeneo ambayo kumeunganishwa *system* ya maji chafu itaondolewa na kuwekwa mingine kwa sababu ile iliyopo imechoka imeoza na inaleta shida kwa wananchi karibu kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upotevu wa Maji. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema upotevu sasa hivi ni asilimia 38 na hivyo imepungua. Upotevu wa maji ni mkubwa kweli kweli na kwa bahati mbaya bomba linaweza likapasuka katikati ya barabara Mawaziri wanapita pale, viongozi

wanapita pale, inachukua *almost* miezi mitatu wakati maji yanatiririka, yanapotea Watanzania wengine wana-*share* maji na ng'ombe kwenye vijiji vya maeneo mbalimbali. Nikikutana na maji yanayomwagika mahali huwa naumia sana; kwa sababu nawaangalia wananchi wangu wanavyotesa nikikuta maji yanamwagika huko barabarani roho inauma sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo bado Serikali lazima inatakiwa iweke mifumo. *Standard* inayotakiwa kitaifa upotevu wa maji ni asilimia 14, kwa hiyo sisi asilimia 38 bado ni kubwa sana. Maji mengi tunayagharamia lakini yanapotea barabarani wakati huo huo kilio cha maji kinaongezeka kila kukicha; kitu ambacho ni hasara kwa Serikali na ni maumivu kwa Watanzania ambao hawana maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Gharama za Kuunganisha Maji. Gharama hizi zinazidi kuongezeka kila siku na zinakuwa kubwa kiasi kwamba mwananchi wa kawaida; kwa mfano hapa Dodoma gharama za kuunganisha zimezidi kuongezeka. Mwanzo utaratibu ilikuwa Mwananchi ananunua vifaa anakwenda kulipa gharama kule *DUWASA* anakuja kufungiwa maji.Leo unaambiwa ukalipe moja kwa moja kila kitu kule. Nimejaribu kwenda mimi mwenyewe, unajaribu kuangalia gharama ulizoandikiwa milioni moja na ushee wananchi wangapi wa hali ya chini wanaweza kuvuta maji? Ni wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ukiangalia vile vifaa bei ya madukani na bei ambayo umeandikiwa pale ni tofauti. Kwa hiyo, naomba suala la maji si biashara, maji ni huduma. Kila Mtanzania apate maji. Kwa hiyo tatizo la kuweka gharama kubwa wananchi wengi wanashindwa kugharamia ni maumivu kwa Watanzania lakini pia tunafanya huduma ya maji kuwa ni biashara na si huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho, Madawa ya Kutibu Maji. Tumekuwa tukilalamika hapa Bungeni miaka mingi gharama za madawa ya kutibu maji inakuwa ni kubwa

kiasi kwamba kuna maeneo mengine kuna wakati inafika maji yatoka machafu, yanatoka yananuka, yanatoka yana udongo kwa sababu halmashauri na miji zinashindwa kumudu gharama, matokeo wanaweka dawa kidogo wananchi wanakunywa maji machafu. Kwa hiyo naiomba Serikali, kwa kutambua umuhimu waweze kupunguza gharama za kutibu maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante. (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Said Bungala na Mheshimiwa Seif Gulamali ajiandae.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia kuwa na afya njema na kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Maji. Vile vile nami niungane na Wabunge wenzangu na Watanzania kwa ujumla kutoa pole kwa wazazi, ndugu, jamaa na marafiki ambao watoto wao wamefariki katika ajali kule Mkoani Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo pia natoa nyingine kule kule Arusha, kama tulivyoona katika vyombo vya habari kuwa kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha mti umeanguka na msiba mwingine umetokea wakiwemo watoto wamefariki. Pia nitumie fursa hii kutoa pole za dhati kabisa kwa wananchi wangu wa Jimbo la Tanga kwa mafuriko makubwa yaliyotokea ambapo yamesababisha uharibufu wa mali, maisha na vile vile pia madaraja yamekatika na kukata mawasiliano kati ya mji wa Tanga na Pangani na vilevile Lushoto na Tanga Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nianze kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha Mwenyenzi Mungu cha Qurani kwenye *Surat Anbiyaa* aya ya

thelathini Mwenyezi Mungu anasema *wajaalna minal-mai kul shaiyn hai;* kwamba ametujalia sisi binadamu kwamba maji ni uhaki kwa kila kitu. Utaoa ni namna gani Mwenyezi Mungu mwenyewe ametoa umuhimu kwa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji hayana mbadala, umeme ukikatikaunaweza ukaweka kibatari, lakini maji yakikatika hakuna mbadala. Kwa hiyo, naitaka Serikali ijue kwanza umuhimu wa maji kwa maisha ya binadamu. Vile vile mahitaji ya si kwa binadamu tu, wanyama, wadudu, ndege na kadhalika na kadhalika wote wanahitaji maji; mpaka vyombo vya moto tunavyovitumia pia vinahitaji maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inashangaza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya maji na mifugo kupunguza bajeti ya maji kutoka Shilingi za Kitanzania bilioni mia tisa thelathini na tisa na kurudi chini hadi bilioni 623, hilo jambo haliingii akilini hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nami niungane na Mheshimiwa Zitto Kabwe na Waheshimiwa Wabunge wengine waliosema kwamba bajeti hii irudi ili ikarekebishwe iongezwe; kwamba kutoka shilingi milioni mia sita za mwaka 2017/2018 ipande. Haiingii akilini kwamba ikiwa maji yanamhusu kila mtu lakini bajeti tunaipunguza wakati ndiyo sehemu muhimu katika maisha ya binadamu. Kwa hiyo naungana na wale wote waliosema kwamba bajeti hii irudi na ikongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, siishii hapo. Jambo lingine kwenye suala zima la maji, sasa hivi maji katika baadhi ya mikoa kwa mfano katika jimbo langu bei ya maji sasa hivi imekuwa ghali kuliko umeme; na wananchi wanahitaji maji kwa shughuli za kimaendeleo lakini maji yamekuwa hayapatikani kama yanavyokusudiwa. Pia katika jimbo langu siku za karibuni maji yamekuwa ni machafu kuliko maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namtaka Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa; nilitoa mwongozo siku moja akasema alikuwa hana habari; sasa nataka pia

anijibu kupitia majibu yake kwamba amegundua nini mpaka Tanga iliyokuwa na historia ya maji safi kabisa leo yanatoka machafu kama chai ya maziwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalotaka kulizungumzia ni miradi ya maji vijijini. Miradi ya maji vijijini Serikali imepata ufadhili wa Benki ya Dunia, sasa kinachotushangaza Benki ya Dunia wametoa fedha kwa nini miradi ile haikamiliki? Kwa mfano mimi nina miradi ya vijiji kumi, kuna mradi unaoelekea kaskazini na kuna mradi unaelekea kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi wa Kaskazini maji yameishia sehemu moja inaitwa Mabokweni ambayo ndiyo jina la kata vile vile; lakini mradi unatakiwa ufike mpaka Kata ya Chongoleani kwenye Vijiji na Vitongoji vya Mpirani, Kibafuta, Mchanga Mweupe, Mchana Mwekundu, Putini, Helani hadi Chongoleani kwenyewe na kufikia Bagamoyo; lakini mradi kule Mkandarasi ameondoa mpaka vifaa anasema anaidai Serikali na hajalipwa fedha zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napata kigugumizi hapa kujiuliza, fedha tunaambiwa zimeletwa na benki ya dunia kwa nini mradi haukamiliki na wananchi wanapata shida? Wameeleza wengi hapa; akinamama kule Tanga wamekuwa na vipara kama wanaume kwa kubeba ndoo za maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa Mawaziri nao ni watoto waliozaliwa na mama, binadamu wote wamezaliwa na mama, kwa nini basi hata kama wao hawana huruma, wangewaonea huruma hawa akinamama ambao ndio waliotuleta sisi hapa duniani. Maji ni bidhaa muhimu katika maisha ya kila siku ya binadamu. Kwa hiyo, namtaka Mheshimiwa Waziri, hili la kwamba bajeti irudi ili iongezwe alizingatie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine linahusu miradi ya maji vijijini; baadhi ya *contractors* wa miradi ile ya maji wamefikishwa mahakamani kwa sababu na wao

wamekopa *materials* ili wakaendeleze ile miradi, hawajalipwa na Serikalini kwa kwa muda mrefu kumekuwa kuna ubabaishaji hapa. Naomba hilo pia Mheshimiwa Waziri atueleze kwa nini wakandarasi wale wa maji hawalipwi na ikiwa fedha za *World Bank* zimetoka na wao kwa kuisaidia Serikali yao lakini wanapelekwa mahakamani kwa kuwasaidia wananchi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Maji Taka. Wamesema wazungumzaji wengi hapa kwamba hata mifumo ya maji taka katika mikoa yetu, majiji yetu na manispaa zake si mizuri na lazima tujue tukiwa na mfumo mbaya wa maji taka ndicho kinakuwa chanzo kikubwa cha malaria. Kwa sababu kama utakuwa na mfumo nzuri wa maji taka maji yatakakuwa hayasimami, hayatuami, yatakuwa yanakwenda ambapo mbu hawatoweza kuzaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, maji taka yanayotuama na kumwagika hovyo kwanza yanaharibu mandhari ya miji yetu lakini pia harufu na pia kusababisha magonjwa ya milipuko kama kuhara na kutapika. Kwa hiyo, lazima wizara inayohusika ihakikishe inatilia nguvu ama kwa kutafuta wafadhili au kupeleka fedha pia katika miradi ya maji taka.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wananchi wanahitaji kuwekewa mfumo wa majitaka kwa mfano katika jiji letu la Tanga lakini Mamlaka ya Majisafi na Majitaka hawana uwezo, wanasema tu tuna uwezo wa kukarabati si kuanzisha miradi mipya ya mifumo ya majitaka. Naitaka Wizara pia ipeleke fedha katika Mamlaka ya Majisafi na Majitaka kwa Jiji la Tanga ili iweze kuweka mfumo wa maji taka na hivyo tuondokane na maradhi ya milipuko pia na masalia ya mbu yanayosabisha malaria.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kuzungumzia katika suala la maji ni kwamba maji katika Halmashauri ya Tanga ilikuwa ni historia. Halmashauri nyingi na Waheshimiwa Wabunge watakuwa ni mashahidi hapa walikuja kujifunza ku-*treat* maji kutoka Mamlaka ya Majisafi

na Majitaka ya Tanga. Leo wananchi wanapata tabu mpaka maji yanatoka machafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile pia nimuulize Mheshimiwa Waziri kupunguza bajeti haoni kwamba hili ni tatizo? Leo tuna miaka 56 ya uhuru maji wanayokunywa wanyama wa porini ndiyo hayo hayo maji wanayokunywa binadamu. Yapo baadhi ya maeneo unakuta watu wanachota maji kwenye madimbwi ya barabarani au kwenye mifereji pembeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii hali ni mbaya, haiingi akilini nchi kama Tanzania iliyojaliwa raslimali lukuki lakini tunashindwa kusimamia hata maji; mimi nasema hili jambo ni la aibu sana. Lazima Mheshimiwa Waziri aliyepewa dhamana utuletee mfumo mpya; pamoja na kurudi na bajeti lakini ukija uje na mikakati mipya ya kuwasaidia wananchi wetu wa vijijini. Sote hapa tunatokea vijijini lakini kama vijijini ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umemalizika.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** ...kutakuwa hakuna maji safi nasalama ina maana watu wote watazidi kuathirika na maradhi yataongezeka... *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Said Bungara.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza natoa shukurani kwa kunipa nafasi hii ili nichangie. Pili, namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameumba mbingu na ardhi ili tuitumie sisi binadamu katika maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia habari ya maji na kila kiumbe ana asili ya maji, sisi binadamu tumepatikana kutoka na asili ya maji. Hata hivyo miaka 56

ya Serikali ya CCM tunazungumzia habari ya maji. Tunakwenda vijijini kuomba kura ajenda yetu kubwa ni kwamba mkinichagua kuwa Mbunge mtapata maji, miaka 56.

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema Mheshimiwa wa Mtama hapa, Ilani ya CCM mliwaahidi Watanzania kwamba mtapata maji kutoka asilimia 67 mpaka 85. Mimi Jimbo langu au Wilaya yangu ya Kilwa maji vijijini ni asilimia 48.3. Tunaomba sana...

**MBUNGE FULANI:** Maji safi na salama?

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Maji safi na salama ndiyo. Tunaomba sana, bajeti ya maji lazima iongezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa 2016/2017 tulipangiwa au tulipitisha bajeti ya bilioni mia tisa hamsinitukapata asilimia 19, mwaka huu bilioni mia sita sasa ukipata asilimia 16 utajua mwenyewe itakuwa shilingi ngapi maana itapungua. Naomba sana bajeti hii ya maji irudi iende ikaongezwe fedha kama zilivyoongezwa mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia Mradi wa Maji wa Mavuji. Katika bajeti ya 2016/2017, ukurasa wa 142 kulikuwa na mradi wa maji katika Mji wa Kilwa Masoko. Kazi zitakazofanyika ni ujenzi wa chanzo, mitambo ya kusafishia na kutibu maji, ulazaji wa mabomba, ujenzi wa matanki, ukarabati wa upanuzi wa mabomba ya kusambaza maji. Mahitaji ya fedha *euro* milioni 61.67. Maelezo, majadiliano ya Serikali na Ubeligiji kupitia kampuni ya *Aspec international* yanaendelea. Usanifu umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya! Nataka nijue toka kwa Mheshimiwa Waziri, mazungumzo kati ya *Aspec* na ninyi yameishia wapi? Mradi huu ungesaidia upatikanaji wa maji katika miji midogo miwili ya Kilwa Kivinje na Mji Mdogo wa Kilwa Masoko, lakini sasa hivi ni miaka mitano maneno tu,

maneno tu, kesho, kesho kutwa, kucha maneno tu. Oh haa! Mheshimiwa Waziri leo nataka aniambie mchakato huu umefikia wapi ama sivyo kwa mara ya kwanza nataka nitoe shilingi;.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana. Serikali ya CCM kwa miaka 56 imeshindwa, tunataka kuiangalia Serikali ya Magufuli, maana Serikali CCM haipo, sasa hivi kuna Serikali ya Magufuli. Tunataka tuione Serikali ya Magufuli kwa miaka hii mitano itamaliza tatizo la maji? Kama haikumaliza tatizo la maji katika Tanzania, basi Magufuli *bye bye (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana Serikali ya Magufuli ikishindwa kutatua tatizo la maji *bye bye* mwaka 2020, kwa herini. Waheshimiwa maji si mchezo, huwezi kuishi bila maji, huwezi kulala na mama bila maji. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana, bila maji hakuna kila kitu, watoto hawapatikani bila maji. Tunaomba hilo jambo la maji na hii bajeti lazima irekebishwe ili Watanzania tupate maji. Naunga mkono kabisa; utampata wapi mtoto bila maji? *(Vicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kule Kilwa kuna mradi wa maji tangu mwaka 1992, Kilwa sehemu ya Mpala. Watu walitathminiwa lakini tangu 1992 mpaka leo hawajalipwa fidia, mpaka leo! Maji wameyachukua Mpala wameyapeleka Masoko lakini Mpala penyewe pale maji hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana katika majumuisho leo Mheshimiwa Waziri aniambie watu wa Mpala fidia yao watalipwa lini? Naomba sana na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji alikuja Mpala na akawaahidi watu wa Mpala kwamba lazima hela zao watapata, nataka nijue leo Serikali sikivu ya Mheshimiwa Magufuli mtoe kauli leo nisikie kama si hivyo sijapata jibu sawasawa nasema kweli Serikali ya Mheshimiwa Magufuli si Serikali sikivu. Kama sikivu kweli nijue kwamba watu wale fidia zao zimetoka au zitatoka lini. *(Makofi)*

Mheshimia Naibu Spika, naomba sana msimtie aibu Mheshimiwa Magufuli, Magufuli ni mzuri pengine wabaya ni ninyi hapo. Magufuli mzuri ana tatizo moja tu, anabinya demokrasia, hapo tatizo analo, lakini mengine hana matatizo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana; kuna matatizo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bungara muda wako umemalizika.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, aah! bado bwana! *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Tukumbushe tu jina lako lile lingine bado unatumia au umeacha?

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Ninalo Bwege na wewe mjinga sawasawa tu. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Seif Gulamali atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Lupembe. Kama muda utaruhusu basi Mheshimiwa Josephine Genzabuke atazungumza pia.

**MHE. SEIF K.S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia leo katika Wizara hii ya Maji na Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipotoa shukrani zetu hasa kwa watu wa Manonga, Wilaya ya Igunga ama Mkoa wa Tabora kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli, lakini pia kwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji hasa baada ya kusaini ule mkataba wa maji ya Ziwa *Victoria* Mkoani Tabora hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini mradi huu wa maji ya Ziwa *Victoria* unaenda kupunguza uhaba ama tatizo la maji hasa kwa wananchi wetu ambao ni wa hali ya chini sana. Mradi huu katika kupita utapita katika maeneo ya vijijini, kwa hiyo vijiji ambavyo vitapitiwa na mradi ule vitapata maji. Hii yote ni shukrani kwa Mheshimiwa Rais kwa kuamua kujitoa kwa hali na mali kuhakikisha kwamba analitatua tatizo hili la maji katika maeneo ambayo yalikuwa yana shida ya maji kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme, mradi huu wakati unakwenda pale Igunga maeneo kama Ziba, Ibologelo, Nyandekwa, Ndembezi pamoja na Kata zilizopo jirani pale maana ni kilometa kumi na mbili yatapata maji ya Ziwa Victoria. Vile vile naamini mpaka Nkinga pale kwenye Hospitali yetu ya Rufaa maji yatafika kwa sababu ni Hospitali ya Rufaa ambayo inatoa huduma maeneo mbalimbali, maji na wao watapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo maji ni uhai na kama alivyosema Mheshimiwa aliyetoka hapa bila maji huwezi kufanya mambo yoyote, lakini kwa programu hii namshukuru sana Mheshimiwa Rais na Wizara. Niombe tu hii progamu iende kama ilivyopangwa na naamini kufikia 2018 maji yatakuwa yanatiririka katika maeneo yetu. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie mambo machache ambayo napenda leo nichangie, ni kuhusu masuala ya uchimbaji wa mabwawa. Tumeona kila Mbunge anazungumzia maji hapa na tumeona kuna baadhi ya maeneo mvua zinanyesha kwa kasi sana kiasi kwamba inapeleka mpaka mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe Wizara hii iangalie katika masuala kama haya maji mengi yanapotea; tungechimba mabwawa makubwa ambayo yangesaidia kuhifadhi haya maji kwa sababu maji mengi yanapotea. Sehemu nyingine Mwenyezi Mungu amejalia tuna mvua za kutosha lakini baada ya mvua kukatika na maji yanapotea

na shida ya maji inaendelea kuwepo katika yale yale maeneo ambayo mvua nyingi zilinyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Wizara iliangalie jambo hili kwa macho mawili. Hata nikitolea tu mfano pale kwetu Choma Chankola kulikuwa na *survey* ilifanyika ilitolewa milioni thelathini na tano ya kuchimba bwawa na usanifu ukafanyika, lakini ule uchimbaji wa bwawa sijui umepotelea wapi, imekuwa kimya. Kila mwaka tunaulizia. Mwaka jana nilizungumza hili suala na mwaka huu tena nagusia Mheshimiwa Waziri amesahau ama ile fedha iliyotolewa milioni thelathini na tano walitoa sadaka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini wanavyotoa fedha baadaye inafuata mipango ya utekelezaji. Sasa tumetoa milioni thelathini na tano, isipotee, naomba mabwawa haya yachimbwe katika maeneo ambayo maporomoko ya maji yapo mengi hasa Choma, Ziba pale kuna maji mengi sana na kilimo cha mpunga, lakini pia mabwawa maeneo ya Simbo nashukuru sasa hivi kuna *NGO* ya *World Vision* wana programu ya uchimbaji wa bwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sasa Serikali mshirikiane na hii *NGO* ili tuweze kuhakikisha kwamba hii programu yao ya uchimbaji wa bwawa kubwa pale Simbo iweze kukamilika na kufikia mwisho ili kuhakikisha kwamba maeneo jirani yanapata haya maji ambayo yatawasaidia kwenye kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na kuchangia kwenye ishu ya mabwawa Mheshimiwa Waziri mimi nigusie; tuna miradi inayofadhiliwa ama tunaopata miradi katika maeneo yetu ya maji vijijini. Tunatumia fedha nyingi sana kutengeneza miradi ya maji katika vijiji vyetu, lakini tuna shida ya kukosa wataalam wa kusimamia ile miradi na inapelekea miradi ile baada ya muda mfupi inakufa. Kwa mfano kuna mradi wa usambazaji wa maji katika Kijiji cha Choma namba sita pale Matinje, ukienda Ziba mradi wa maji upo, ukienda Ndembezi, Nkinga na Simbo kote kuna miradi wa maji. Tatizo wanakosa wataalam wanaachiwa Serikali za Vijiji wale

Wenyeviti wa Vitongoji na Wajumbe mwisho wa siku wanakusanya fedha na baada ya kupata mapato wanazila zile hela.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sisi Wizara, katika maeneo ambayo kuna miradi, tuajiri au tupeleke mtaalam pale aweze kusimamia na kuwaongoza hawa viongozi na watu ambao wanasimamia huu mradi wa maji. Niiombe Wizara iliangalie hili suala ili ihakikishe kwamba inaokoa fedha ambazo zimekwishatumika katika uchimbaji ama uwepo wa miradi ile ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niiombe Wizara katika ile miradi yao wanayopata ya ufadhili wa *World Bank* ya uchimbaji wa visima virefu, niombe watuangalie na sisi pale Igunga hasa Manonga kwa sababu yako maeneo yana shida sana ya maji. Tuna shida kweli ya maji hasa ukiangalia kuna baadhi ya vijiji; naweza nikamtajia ama nitamletea Mheshimiwa Waziri kwenye taarifa yake atusaidie. Kuna maeneo kama Kata za Mwamala, Uswaya, Igoweko, Kitangili, Nyandekwa na Mwansugho Ngulu, maeneo yote hayo hayana maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuiombe Wizara katika ule ufadhili wanaoupata kutoka *World Bank* na maeneo mengine waiangalie Wilaya yetu wahakikishe kwamba tunapata visima hivyo virefu angalau; maana bajeti imekwisha sijaona kisima hata kimoja ndani ya Wilaya yangu ya Igunga. Sasa niiombe Wizara iangalie hili suala na iweze kupitia ili waweze kutusaidia kutatua hii changamoto ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine nipende kushauri tu kwa Mheshimiwa Waziri, waliangalie kwenye Wizara. Nilihudhuria kwenye bajeti moja ya Kamati ya Fedha Wilayani pale Igunga. Tumekaa zimekuja fedha za maji milioni ishirini nafikiri, kuna mradi fulani wa maji vijijini; lakini wanasema katika hii milioni ishirini mwongozo kutoka Wizarani asilimia 30 ya fedha ni kwa ajili ya usimamizi wa miradi hii. Milioni ishirini, usimamizi ni milioni sita maana yake

ni kwamba kwenye milioni ishirini unatoa sita inabaki milioni 14. Sasa kwa vijiji sijui 14 vile vitagawana shilingi ngapi ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuangalie kama ni mwongozo kweli wa asilimia 30 kama ni kweli, maana wameniambia wataalam wilayani, huu ni mwongozo wa Wizara, tunakata asilimia 30 kwa ajili ya usimamizi; nikauliza usimamizi gani? Wanasema kwamba sijui kuna mafuta na posho, ukipiga mahesabu hazifiki milioni sita au saba. Sasa leo tuna programu ya bilioni...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali muda wako umemalizika.

**MHE. SEIF K.S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja, niiombe Wizara ifuatilie hizi fedha ambazo zinakuja kwenye Halmashauri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Anna Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuzungumza bajeti hii muhimu sana ya maji, kwa sababu maji ni uhai, bila maji hatuwezi kuishi, kila binadamu lazima atumie maji ili aweze kuishi. Bajeti hii tunaiomba Serikali kwa ajili ni jambo muhimu sana kwa binadamu tunaomba iongezwe kama ilivyokuwa 2016/2017 kwa sababu maji ni uhai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya, tunaona jinsi gani wanavyoipigania Wizara yao kwa ajili ya kufungua miradi mbalimbali. Hata hivyo, bado kaka zangu wana kazi kubwa sana kwa sababu Wizara waliyokuwa nayo ni ngumu sana inawagusa wananchi moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeomba bajeti iongezwe kwa sababu kama nilivyosema maji ni muhimu sana kwa binadamu. Vilevile ukiangalia kuna mifuko mbalimbali ambayo tunaiona imefanya kazi vizuri. Tukizingatia *REA* imefanya kazi vizuri sana kwa upande wa umeme. Tulikuwa tunaiomba Serikali kwenye tozo ya Mfuko wa Barabara tutoe *at least* shilingi hamsini, Mfuko wa Umeme tutoe shilingi hamsini ili iwe shilingi mia iende kwenye Mfuko wa Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona ni jinsi gani *REA* ilivyofanya kazi vizuri ndani ya vijiji vyetu; leo hii wananchi wanafurahi wanapata huduma safi ya mwanga. Sasa maji ni uhai, kila mtu anahitaji maji na tukiangalia maeneo yetu ya vijijini hakuna maji kabisa, akina mama wanahangaika. Tukienda kwenye ziara zetu, ndiyo maana unakuta Waheshimiwa Wabunge wengi wanapiga kelele kwa sababu ya maji kwa kuwa tunapokwenda kwenye ziara zetu huko tunaona hali halisia ya jinsi gani maji hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, akinamama wanatoka saa tisa za usiku, vijiji vingine saa nane za usiku wanakwenda kutafuta maji na akienda kutafuta maji hapati yale maji safi na salama anapata maji machafu. Matokeo yake sasa unakuta asilimia kubwa ya maji yale ya vijijini ambayo ni ya vijito kuna maradhi mengi yanapatikanika huko, watu wanaumwa vichocho na kuharisha. Halafu sasa hivi mpaka mijini kwa sababu hatutumii maji safi na salama, mjini sehemu nyingi maji hayatibiwi matokeo yake watu asilimia 90 tunapata magonjwa ya *UTI.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba Serikali kwa hili sasa hivi lazima tujipange vizuri, bajeti ongezeke ili nchi yetu ya Tanzania tuweze kujivunia kwa hilo. Tunaomba asilimia 70 iende vijijini na asilimia 30 ibaki mjini kwa sababu mijini kuna miradi mbalimbali mikubwa ambayo inatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende sasa kwangu Mpanda. Naomba niishukuru Serikali kwa sababu Mpanda tuna miradi mikubwa kama vile mradi wa Ikolongo ambao umefanyika na sasa asilimia 60 ya wananchi wa Mpanda wanapata maji, lakini asilimia 40 pale Manispaa hawapati maji. Hapa ndani ya ukurasa wa 66 Mpanda kuna huu mradi wa mwaka 2016/2017 tulipangiwa bilioni mbili. Huwezi ukaamini kuna watu wanatafuta maslahi yao wenyewe badala ya kutafuta maslahi ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa hizi zilivyofika Mpanda *Tender Board* imerudiwa mara tatu, mpaka leo ninavyokwambia mradi huu unakutana na pesa za bajeti hii ya 2017/2018. Mradi haujatekelezeka kwa sababu ya ubinafsi; watu wanataka maslahi yao wenyewe binafsi badala ya maslahi ya wananchi. Wananchi wa Mpanda wanahangaika maji wenyewe wanataka waweze kupata mradi wajinufaishe wao. Inasikitisha sana kwa Mpanda! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali Mheshimiwa Waziri, najua sasa hivi *Tender Board* ime-*tender* mara tatu kiasi ambacho wamekwenda kushtakiana kwa ajili ya ubinafsi. Naomba Mheshimiwa Waziri alifuatilie hili jambo ili wananchi wa Mpanda Mjini waweze kupata maji, mradi huu uweze kufanyika na hizi bilioni mbili ziweze kufanya kazi kutoka Kanoge mpaka Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Hospitali ya Mpanda Mjini ambayo wananchi tunaitegemea haina maji, na huu mradi wa bilioni mbili ulitegemewa ukifika pale maji yafike kwenye Hospitali yetu ya Mpanda Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hizi bilioni mbili ambazo zilikuwa za bajeti iliyopita ziweze kufanya kazi na kama safari hii wametupangia bajeti vilevile iweze kufanya kazi kwa sababu wananchi wa Mpanda Mjini wanapata tabu

kwa sababu ya watu wachache ambao wanataka maslahi yao binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii sisi Mkoa wa Katavi tuna Ziwa Tanganyika; sisi tunafurahi wenzetu hapa wana Ziwa *Victoria* leo ziwa lile limewapa manufaa. Hata hivyo, sisi Wanakatavi tuna Ziwa Tanganyika ambalo lina kina kirefu, kina chake kirefu kushinda Ziwa Victoria. Kwa nini sasa Serikali na Ziwa Tanganyika... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Josephine Genzabuke, kama bado tutakuwa na nafasi Mheshimiwa Edward mwalongo ajiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba niipongeze Serikali ya awamu ya tano kwa jinsi inavyofanya kazi vizuri, na Serikali hiyo inayoongozwa na Mheshimiwa John Pombe Magufuli na kama anavyosema sisi Watanzania tuendelee kumuombea na kweli sisi tunamwombea Mwenyezi Mungu amjalie afya ili aweze kuendelea kuwatumikia Watanzania. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuendelea na hotuba yangu naomba niunge mkono hotuba hii kwa ajili ya wanawake wa Tanzania. Naomba niunge mkono hotuba hii kwa ajili ya wanawake wa Mkoa wa Kigoma na Wilaya zake zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini naunga mkono bajeti hii? Wakati naunga mkono bajeti hii, naomba bajeti hii iongezewe pesa ili iweze kumkomboa mwanamke wa Tanzania kwa kumpatia maji. Tusipojipanga kuongeza bajeti hii, tujipange kuja na bajeti ya dharura ya kutibu kipindupindu. Kwa maana hiyo, naomba pesa ziongezwe kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme yafuatayo:-

Naishukuru Serikali kwa sababu mwaka 2016/2017 ilitupangia pesa Mkoa wa Kigoma, nawashukuru kwa hilo. Naomba niseme, pamoja na pesa hizo zilizopangwa, bado lipo tatizo la maji. Kwa hiyo, naendelea kusisitiza kwamba pesa zikipangwa zipelekwe ili kuweza kukamilisha miradi iliyokwishaanzishwa katika Mkoa wa Kigoma. Nimeona wakati Waziri anatoa hotuba yake amesema tumepangiwa pesa nyingine, namwomba Mheshimiwa Waziri pesa hizo zipelekwe ili kuweza kukamilisha miradi iliyopo Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, maji ni uhai. Sisi wote tunafahamu maji ni uhai na maji ni kila kitu. Kwa hiyo, naomba bajeti hii iongezewe pesa kwa sababu wanawake wanapojifungua wanahitaji maji. Wanawake pamoja na watu wengine wanaotunza familia; zipo familia ambazo zina wagonjwa wanaohitaji kutumia maji na wanatumia muda mwingi kwenda kutafuta maji. Wakati mwingine wanatafuta maji na wanakosa muda wa kwenda kufanya shughuli za ujasiriamali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maji ni kila kitu. Maji yanachangia wananchi kuweza kuongeza kipato chao. Kwa mfano, sasa hivi tunahamasisha vikundi, wanawake

waanzishe vikundi. Wakitumia muda mwingi kwenda kutafuta maji, watashindwa kufanya shughuli za uzalishaji na watashindwa kujiunga kwenye vikundi na hata wakijiunga hawataweza kurejesha mikopo katika vikundi vyao kwa sababu muda mwingi watakuwa wanautumia kwenda kutafuta maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upo mpango wa kutafuta maji kutoka Mto Malagarasi. Kwa sasa hivi, maji katika Mto Malagarasi yanapungua na vyanzo vingi vinaendelea kuharibika kwa sababu wafugaji wanapeleka mifugo kwenye vyanzo vya maji. Naomba basi tunapopanga bajeti kwa ajili ya kupeleka maji vijijini tupeleke na pesa kwa ajili ya kwenda kuhamasisha wananchi kutunza mazingira kwa ajili ya kuhifadhi misitu ili maji yasipotee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mipango mizuri ya kutoa maji Mto Malagarasi lakini tusisahau kufanya mipango ya kutumia Ziwa Tanganyika, kwa sababu Ziwa Tanganyika ni ziwa kubwa ambalo linaweza likasambaza maji maeneo mengi. Maji hayo yakisambazwa katika maeneo mbalimbali, tutafanikiwa katika kilimo cha umwagiliaji. Kwa maana hiyo, Tanzania yenye viwanda itawezekana kwa sababu wananchi watakuwa wanazalisha mazao yao na kupelekea viwanda kuanzishwa kwa sababu vitu ambavyo vitakuwa vimelimwa kutoka mashambani vitakuwa vinapatikana kutokana na kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali ipeleke pesa hizo ili kuweza kukamilisha miradi katika Mji wa Kasulu na viunga vyake ambako bado kuna maeneo yana matatizo ya maji. Mji wa Kibondo nao unahitaji pesa kwa ajili ya kukamilisha miradi ya maji. Vile vile Mji wa Kakonko unahitaji pesa. Kwa mfano, upo mradi mkubwa wa Mgembezi ambapo mradi huo ukikamilika utaweza kuhudumia Kata karibu tano. Kwa mfano Kata ya Kasuga, Kata ya Kakonko, Kata ya Kanyonza, Kata ya Kiziguzigu na Kata ya Kasanda. Kwa hiyo, tunaomba kabisa pesa hizo zikipatikana zielekezwe huko kwenda kukamilisha miradi ambayo tayari imeshaanzishwa. Ipo miradi mingine iliyoanza

kutoka miaka takriban mitano hadi kumi, lakini bado haijaweza kukamilika. Tunaomba pesa zikipatikana zipelekwe zikakamilishe miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iongeze bajeti kwa ajili ya Wizara ya Maji ili tuweze kupeleka maji katika maeneo mbalimbali kumsaidia mwanamke wa Tanzania aweze kupata maji na kumtua ndoo kichwani kama Mheshimiwa Rais wetu alivyoahidi. Nami naamini Rais wetu akiahidi, kwa sababu tumeona mambo mengi aliyoahidi, aliahidi ndege, tayari sasa hivi ndege zipo. Zamani ilikuwa ni shida kutoka Dar es Salaam kwenda Kigoma, lakini kwa ahadi aliyoahidi, sasa hivi *bombardier* inaenda Kigoma, inaenda Tabora na maeneo mengine. Kwa maana hiyo, naamini hata tatizo la maji litakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, lakini atakuwa mchangiaji wetu wa kwanza kesho kwa ajili ya kukamilisha uwiano wa wachangiaji humu ndani.

Sasa tunaendelea na shughuli iliyopo mbele yetu. Katibu.

**NDG. NENELWA WANKANGA – KATIBU MEZANI:**

**UCHAGUZI WA WABUNGE WA BUNGE LA AFRIKA MASHARIKI (EALA)**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nitampisha sasa Mheshimiwa Spika ili aweze kuendelea na hiyo hoja iliyo mbele yetu sasa.

*Hapa Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Kabla hatujaendelea, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana wasaidizi wangu wote hapa Mezani kwa kazi nzuri sana ambayo wamekuwa wakiifanya; Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Chenge, Mheshimiwa Zungu na Mheshimiwa Najma. Naomba niseme nawashukuru sana na tuendelee kuchapa kazi hapa Mezani kama kawaida. Katibu.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, maelezo ya Spika.

## MAELEZO YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa mtulie kwenye viti vyenu, tupunguze hii tembea tembea kwa sababu tuna zoezi maalum na muhimu. Kama hatutasikilizana, itatuchukulia muda mrefu bila sababu. Naomba sana kila Mheshimiwa akae kwenye kiti chake. Wale ambao hawakai, nitaanza kuwataja majina.

Niwakumbushe, kwa wakati fulani shughuli hii itakuwa *Live.* Kwa hiyo, ukitajwa jina hapa wapiga kura wako wakikusikia, itakuwa tabu. Naomba wale mnaoongea, mwambie mwenzako kwamba akae chini. Pia naomba utulivu, kutembeatembea kuishe. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nina maelezo machache kabla hatujaanza kwenye zoezi letu lililo mbele yetu nalo ni kuhusiana na uchaguzi wa Wabunge wawili wa Afrika ya Mashariki.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba tarehe 4 Aprili, 2017 wakati wa Kikao cha Kwanza cha Mkutano huu wa Saba Bunge lilifanya uchaguzi wa kuwapata Wabunge wa Bunge la Nne la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki *(EALA)* chini ya masharti ya Ibara ya 50 (1) na ya (2) ya mkataba wa kuanzisha Jumuiya hiyo na Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Waheshimiwa Wabunge, katika uchaguzi huo, Bunge lilifanikiwa kuwapata Wabunge kutoka kundi A ambapo Wabunge wawili wanawake walichaguliwa; Kundi B ambapo Wabunge wawili kutoka Tanzania, Zanzibar walichaguliwa; Kundi C Vyama vya Upinzani, *CUF* ambapo Mbunge mmoja alichaguliwa; na Kundi D ambapo Wabunge wawili wa Tanzania Bara walichaguliwa. Kupitia mchanganuo huo tukawa tumepata wawakilishi wetu saba.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, mtakumbuka kwamba katika uchaguzi huo wa kundi C sasa, Vyama vya Upinzani; kwa upande wa CHADEMA uchaguzi huo haukukamilika, baada ya wagombea wawili wa chama hicho kushindwa kupata kura za kutosha na hivyo kutochaguliwa na Bunge wakati huo.

Baada ya hatua hiyo nilielekeza kwamba uchaguzi huo utafanyika baadaye baada ya Chama cha CHADEMA kufanya mchakato upya wa kuwapata wagombea wengine na hatua nyingine za kikanuni za kufanya uchaguzi upya kukamilishwa na Msimamizi wa Uchaguzi ambaye ni Katibu wetu wa Bunge.

Kwa hiyo, napenda kuwajulisha kuwa sasa mchakato huo umekamilika na uchaguzi huo wa kuwapata Wabunge wawili kutoka CHADEMA utafanyika leo kama inavyoonekana kwenye orodha ya shughuli za leo ili Bunge letu liweze kukamilisha nafasi tisa za Wabunge zinazotakiwa kwa kila nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hivyo basi, ili tuweze kuendelea na zoezi hili la uchaguzi, sasa nimpe nafasi Katibu wa Bunge ambaye ndiye msimamizi wa uchaguzi, awasilishe maelezo na utaratibu mzima wa uchaguzi.

Katibu, karibu.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Maelezo ya Msimamizi wa Uchaguzi kuhusu mchakato wa uteuzi wa utaratibu wa kuwapata Wabunge wawili wa Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naomba nirejee maelezo ili kuweka rekodi sahihi. Tarehe 4 Aprili, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilifanya uchaguzi wa kuwachagua Wabunge tisa wa Bunge la Afrika Mashariki watakaowakilisha katika Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, katika uchaguzi huo, Bunge liliwachagua Wabunge sita kutoka Chama cha Mapinduzi na Mbunge mmoja kutoka Chama cha Wananchi *CUF.* Wabunge wawili kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo walikosa kura za kutosha kuwapatia ushindi. Hivyo Bunge lilipaswa kufanya uchaguzi kwa ajili ya kuwapata wawakilishi wawili kutoka katika kundi la Vyama vya Upinzani ambapo Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ndicho chenye haki ya kujaza nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira hayo na kwa kuzingatia masharti ya sheria na kanuni zinazotawala uchaguzi huu, nilitoa taarifa ya siku ya uteuzi na siku ya uchaguzi kwenye Gazeti la Serikali Na. 537 la tarehe 21, Aprili, 2017. Taarifa hiyo ilitaja siku ya uteuzi *(nomination day)* kwa Wagombea kuwa ni tarehe 3 Mei, 2017 saa 1.00 jioni na siku ya uchaguzi *(election day)* kuwa ni tarehe 10 Mei, 2017.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tarehe 28, Aprili, Chama cha CHADEMA kiliniandikia barua iliyopokelewa na ofisi yangu siku ya tarehe 2 Mei, jioni. Barua hiyo ilitoa maelezo kwamba muda niliowapa kuwasilisha majina ya Wagombea kupitia kwenye taarifa hiyo ni finyu kutokana na kuathiriwa na kuwepo kwa siku za mapumziko ya mwisho wa wiki pamoja na sikukuu ya Mei Mosi iliyoangukia siku ya Jumatatu, hivyo kuwepo kwa ugumu wa kufanya vikao vyao vya kichama.

Hivyo, chama hicho kiliomba kuongezewa muda usiopungua wiki mbili ili kuweza kufanya uteuzi wa Wagombea, kupata uthibitisho wa uraia kutoka Idara ya Uhamiaji na uthibitisho wa sifa za Wagombea kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mujibu wa Ibara ya 50(2) ya

mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ikisomwa pamoja na Ibara ya 67 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu zilizotolewa, niliongeza muda wa siku nne, kuanzia tarehe 3 - 7 Mei, 2017 ili kukiwezesha Chama cha CHADEMA kukamilisha taratibu hizo za kisheria na hivyo kukitaka chama hicho kuwasilisha kwangu majina na nyaraka za Wagombea waliowateua tarehe 8 Mei, 2017 kabla ya saa 10.00 jioni ambayo ilikuwa siku ya uteuzi. Chama cha CHADEMA kiliwasilisha kwangu majina sita ya Wagombea ambapo kati yao Wagombea wanne ni wanaume na Wagombea wawili ni wanawake. Majina hayo ya Wagombea yaliwasilishwa kwangu tarehe 8 Mei, 2017 kabla ya saa 10.00 jioni kama ambavyo nilikuwa nimeelekeza.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, nilifanya uchambuzi wa nyaraka na kuridhika kwamba Wagombea wote wametimiza masharti ya kugombea baada ya kupata uthibitisho wa uraia kutoka Idara ya Uhamiaji na uthibitisho wa sifa za kugombea kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa mujibu wa Ibara ya 50 ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ikisomwa pamoja na Ibara ya 67 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nimeridhika kuwa uteuzi wa Wagombea umezingatia na kuakisi *(reflect)* uwepo wa jinsia zote mbili ambapo Wagombea wanne ni wanaume na wawili ni wanawake kama inavyoelekezwa na masharti ya Kifungu cha (4) cha Sheria ya Uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nimepokea nyaraka zote muhimu zinazohitajika kwa mujibu wa Kanuni ya 5(1), (2) na (3); na Kanuni ya (6) ya Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016. Hivyo, nimeridhika kuwa mchakato wa uteuzi wa Wagombea hao katika Chama cha CHADEMA ulikuwa wa kidemokrasia na wa wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo, nilitoa taarifa na kuwatangazia wafuatao kuwa Wagombea katika

uchaguzi huo wa leo; naomba niwataje. Profesa Abdallah Jumbe Safari... *(Makofi)*

**SPIKA:** Hapana, hapana, msipige makofi wala nini. Ninyi sikilizeni majina tu.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Ndugu Ezekia Dibogo Wenje, Ndugu Josephine Sebastian Lemoyani, Ndugu Lawrence Kego Masha, Ndugu Pamela Simon Massay na Ndugu Salum Mwalim Juma.

Mheshimiwa Spika, baada ya zoezi hilo, naomba sasa nieleze utaratibu wa uchaguzi:-

Mheshimiwa Spika, Wagombea kujieleza na kuomba kura. Kila Mgombea ataitwa na kuingia ndani ya Ukumbi wa Bunge kwa kusindikizwa na Mpambe wa Bunge. Mgombea atapewa nafasi ya kujieleza na kuomba kura kwa lugha ya Kiingereza kwa muda usiozidi dakika tatu.

Mheshimiwa Spika, maswali kwa Wagombea. Baada ya kujieleza, Mgombea anaweza kuulizwa maswali yasiyozidi matatu kutoka kwa wapigakura kwa kadri itakavyoelekezwa na Mheshimiwa Spika. Maswali yatakayoulizwa yanapaswa kuwa ya msingi na siyo yale yanayohusu masuala binafsi ya Mgombea. Maswali hayo yatajibiwa na Mgombea kwa kadri ya uelewa wake kuhusiana na swali aliloulizwa. Maswali yataulizwa na kujibiwa kwa lugha ya Kiingereza na kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge. Mara baada ya kujibu maswali atakayoulizwa Mgombea, Spika atamruhusu Mgombea kutoka nje ya Ukumbi wa Bunge na kuelekea eneo ambalo atakuwa ameandaliwa kwa ajili ya kusubiri.

Mheshimiwa Spika, kupata idadi ya wapigakura. Baada ya Wagombea kujieleza na kuulizwa maswali, kengele itapigwa ili Wabunge wote waingie ndani ya ukumbi kuanza zoezi la upigaji kura. Katika hatua hii, Maafisa watakaokuwa wameandaliwa watahesabu Wabunge walioko ndani ili kupata idadi kamili ya Wabunge waliohudhuria na kupiga kura. Lengo la zoezi hili ni kujiridhisha na uwepo wa akidi

inayotakiwa kwa ajili ya kuwezesha kikao cha uchaguzi kufanyika. Akidi inayohitajika kwa mujibu wa Ibara ya 94 ya Katiba na Kanuni ya 77(1) ya Kanuni za Bunge ni nusu ya Wabunge wote ambayo ni 197. Aidha, zoezi hili litawezesha kupata idadi kamili ya Wabunge waliohudhuria na kupiga kura. Idadi hiyo itatumika kama idadi ya wapigakura katika zoezi la kuhesabu kura.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kupiga kura. Naomba mnisikilize kidogo, zoezi la kupiga kura litakuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, masanduku *(Ballot boxes)* yatakaguliwa mbele yenu. Pili, ugawaji wa karatasi za kura na utaratibu wa kupiga kura. Utaratibu wa leo utakuwa na mabadiliko. Wagombea watakapomaliza kujieleza, kila mpiga kura, kwa utaratibu utakaokuwa umeandaliwa watakuja mbele ya meza, utachukua karatasi ya kura, utapiga kura na kuidumbukiza ndani ya *box* mbele ya meza jirani na siwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nirejee tena. Karatasi za kura zitatolewa mbele ya meza na kila mpigakura atakuja kupiga kura mbele ya meza na kuitumbukiza ndani ya *box*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upigaji kura na idadi kamili ya kura zinazotakiwa kupigwa. Kila mpiga kura atatakiwa kupiga kura mbili kwa siri, kwa utaratibu niliouainisha kwa kuweka alama ya vema kwenye jina la Mgombea anayemtaka kama inayooneshwa kwenye karatasi ya kupigia kura. Mpiga kura ambaye kwa bahati mbaya ataharibu karatasi yake ya kupigia kura wakati wa zoezi la kupiga kura likiwa linaendelea, anaweza kuirejesha karatasi iliyoharibika na kupewa karatasi nyingine.

Mheshimiwa Spika, kuhesabu kura. Baada ya wapiga kura wote kupiga kura na kuzitumbukiza kwenye masanduku kama nilivyoainisha, Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 12(1) atawateua Wabunge wawili; mmoja kutoka

Chama Tawala na mwingine kutoka Kambi ya Upinzani kuwa Mawakala wa kuhesabu kura kwa Wagombea wote. Vile vile uzoefu unaonesha kuwa Mheshimiwa Spika anaweza kuruhusu Wagombea kushuhudia zoezi la kuhesabu kura wao wenyewe. Mara baada ya kura kukusanywa katika masanduku, mimi na wasaidizi wangu tutahesabu kura zilizopigwa mbele ya Mawakala walioteuliwa kwa zoezi hilo katika chumba maalum kitakachokuwa kimeandaliwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya zoezi hilo la kuhesabu kura kukamilika, tutatoa maelezo ya Wabunge watakaokuwa wamechaguliwa na kuwatangaza rasmi kuwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo maelezo ya utaratibu wa zoezi la upigaji kura.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo yangu ya utangulizi na baada ya maelezo ya Msimamizi wa Uchaguzi ambaye ni Katibu wetu, endapo kuna ufafanuzi wa ziada unaohitajika kabla zoezi letu halijaendelea natoa dakika chache sana kwa Mheshimiwa Mbunge yoyote ambaye kwa hatua hii anadhani kuna jambo halijakaa vizuri kidogo au linahitaji ufafanuzi wa namna moja au nyingine.

Nimewaona watatu. Mbona wanaongezeka! Makatibu niandikieni tu orodha sasa. Ukitajwa jina unakaa chini.

**NDG. NENELWA M. WANKANGA - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa Getere, Mheshimiwa Ikupa, Mheshimiwa Yussuf, Mheshimiwa Bobali, Mheshimiwa Maftah, Mheshimiwa Kadutu, Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Mulugo na Mheshimiwa Haonga.

**SPIKA:** Ahsante sana. Naomba sasa tuweze kuanza. Ni dakika mbili mbili tu, Mheshimiwa Lubeleje uanze.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nataka nipate maelezo tu kidogo kwamba tutakwenda kupiga kura

pale mbele. Je, meza itakuwa inatuita jina moja moja au tutakaa foleni? *(Makofi)*

**SPIKA:** Niseme tu, wakati huo utakapofika, Katibu atafafanua vizuri utaratibu mzuri ambao hauna tatizo, lakini *emphasis* ni kwamba tunataka uchaguzi wa uwazi, hatutaki mtu tena apige kelele wala aseme sijui nilionewa kwa namna moja au nyingine. Vitu vinafanyika, vinaonekana, sisi wote tukiwepo ni mashahidi wa kinachotokea kwa utaratibu mzuri kabisa ataueleza wakati huo Katibu. Waheshimiwa naomba kwa hilo msiwe na wasi wasi nalo.

Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujua tu kwamba wakati tumefanya uchaguzi wa kwanza tulipewa karatasi hapa mezani na uchaguzi wa leo unasema mtu mmoja mmoja ataitwa. Je, uchaguzi wa kwanza ulikuwa umekosewa, utaratibu haukufuatwa?

**SPIKA:** Hilo siyo swali. Mheshimiwa Ikupa. *(Kicheko)*

**MHE. STELLA A. IKUPA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Langu ni dogo, ni ombi tu, kwamba mimi nitaomba nipigie kura hapa nilipo na kura yangu iletwe hapo mbele. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, tunatambua hilo. Utaratibu wa wale wenzetu na ndugu zetu ambao tunawapenda kabisa, Msimamizi wa Uchaguzi atauweka kwa utaratibu mzuri na tutatangaza wakati huo kwamba kura hii moja inaenda kule kwa ajili gani; wakati huo itakapofika.

Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, swali langu lilikuwa linafanana kidogo na Mheshimiwa Getere, lakini kwa kuwa sisi wengine ni Wabunge wapya, tulitaka tujue tu utaratibu kwa nini siku ile tulipigia huku na leo

tunakwenda pale? Angalau kidogo, Wabunge wengi hapa ni wapya, ungetoa ufafanuzi tu kidogo ukaturidhisha maana tumekuwa *so confused* katika hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maftaha.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nilitaka niulize swali ambalo Mheshimiwa Lubeleje kauliza, kwa hiyo, siwezi kuuliza tena. Ahsante.

**SPIKA:** Labda nilijibu hili, hivi; mtaona katika uchaguzi ambao tunapeleka ma-*box* kura zinazunguka huko, inafika mahali mtu mwingine anaweza akapewa hata kura mbili au tatu huko, Katibu asione wala mimi nisione; inatupa wasiwasi wa kuelewa kama kweli kura zetu ni hizo.

Wasiwasi wake mwingine mkubwa ni kwamba, wakati wa kwenda kuhesabu tumeshawaambieni wapiga kura ni wangapi, inaweza ikajitokeza tofauti ya kura tatu, nne. Unajua kura hizo zinamfanya mtu aende Mahakamani na inakuwa ni kesi nzito! Kwa hiyo, tunataka kuhakikisha kwamba zoezi linaenda katika namna ambayo sote kabisa tunashuhudia hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Maftah, kama huna lingine ili tuokoe muda! Ndio aliongea mwisho eeh!

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, sina lingine ni lile la Mheshimiwa Lubeleje.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kupata ufafanuzi kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge tunachaguliwa kwa sifa ya kujua kusoma na kuandika na Wagombea watajieleza kwa Kiingereza. Tunasikia Kiingereza lakini hatuwezi kuuliza maswali: Je, kwa mwongozo wako, hatuwezi kuwauliza kwa Kiswahili? *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Jamani, msema kweli mpenzi wa Mungu, sasa ninyi mnacheka nini? Wako wengine hapa wanajifanya wanajua Kimombo kumbe hamna kitu! Afadhali hata mtani wangu Musukuma ame-*declare interest.* Hilo Katibu ambaye ni Msimamizi wa Uchaguzi atalijibu. Msimamizi wa uchaguzi katika hilo. *(Kicheko/Makofi)*

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH-KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa mamlaka uliyonayo unaweza ukaruhusu swali liulizwe kwa Kiswahili, lakini anayejibu ajibu kwa Kiingereza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nini tena Mheshimiwa Nassari?

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa maelezo yaliyotolewa na Katibu wa Bunge, lakini kama ni kweli amejibu hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Musukuma kwamba anayeuliza swali aulize kwa lugha ya Kiswahili kwa kutokujua Kiingereza kwa ile sifa ya K3 (Kusoma, Kuandika na Kuhesabu) kwa maana ya sifa za Wabunge kwenye Bunge hili, sasa swali langu kwako ni moja kwamba; kama anayeuliza anaruhusiwa kuuliza kwa Kiswahili, lakini anayejibu anajibu kwa Kiingereza, kuna *translator* humu ndani wa kusaidia kumjibu basi yule aliyeuliza swali ajue alichojibiwa ni kitu gani? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, nami ilikuwa hoja yangu kwa alilokuwa amelifanya Mheshimiwa Getere, lakini baada ya wewe kulifafanua, nimelielewa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, ili tuweze kuokoa muda, kwa sababu umeshatoa ufafanuzi, naomba niseme tu kwamba nami kidogo niliingiwa na hofu kwamba wale Wabunge wenzetu ambao tulishawachagua tayari siku za nyuma hatukutumia utaratibu kama wa leo;

sasa nilidhani labda kama utaratibu ulikosewa na wenzetu wale labda warudi ili tuweze kuwachagua upya. Sasa kwa sababu umeshatoa ufafanuzi, nashukuru sana. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Sasa Waheshimiwa Wabunge, kwa ajili ya kuokoa muda...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**SPIKA:** Hapana, muda sasa umeenda. Upo kwenye orodha yangu, lakini muda Waheshimiwa.

Niseme mafupi yajayo ili tuweze kuanza zoezi, kwamba zoezi hili linatokana na Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika Nchi zetu sita (Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Sudan ya Kusini) wanachagua Wabunge tisa tisa wa kutuwakilisha kwenye Bunge la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Leo sisi hapa tunakamilisha zoezi kwa kuchagua wale wawili waliokuwa wamebaki kwa maelezo ambayo Katibu ameyaeleza kwa ufasaha mkubwa.

Kama kawaida kila nchi inajaribu kupeleka watu ambao inaamini kabisa kwamba watafanya kazi nzuri kule kwa kupambana na wale wengine wa nchi jirani katika mambo ambayo yana maslahi ya Tanzania. Kwa hiyo, nawaombeni Waheshimiwa Wabunge na kuwakumbusha, tuwasikilize kwa umakini, tuache kuongea ongea, tuwasikilize wanapokuja hapa, tuwaulize maswali, tupige kura, zihesabiwe tupate matokeo.

Sasa baada ya kuwa tumeulizana hapa, hakuna neno lingine, nimruhusu Katibu sasa kama ana lolote aseme, basi baada ya hapo tuanze kuita Wagombea wetu kwa mpangilio ambao Katibu ataueleza. Katibu.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH-KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nadhani umeyaeleza yote isipokuwa baada ya zoezi la Wagombea kujieleza na kuuliza maswali, nitarejea tena baadhi ya vipengele ili kuweka vizuri utaratibu

utakaotumika katika kupiga kura na Waheshimiwa muwe na amani tu kwamba kila Mbunge atapiga kura kwa utaratibu tulioandaa.

Pili, utaratibu tunaotumia ni utaratibu wa kawaida wa Kibunge ambao tumekuwa tukiutumia kwa mujibu wa kanuni. Hakuna jambo jipya katika utaratibu tunaoutumia.

Mheshimiwa Spika, zoezi la Wabunge kuja kupiga kura mbele ya meza hii kama ulivyoliweka vizuri ni kuondoa hisia ya uwepo wa kura ya ziada baada ya Wabunge kuhesabiwa na kupata idadi ya kura tofauti na kinyume na hesabu tunayokuwa tumehesabu. Tunashukuru kwa utaratibu huu, sasa kura zitahesabiwa kwa wale watakaokuja kuchukua mbele na kupiga kura na ndiyo itakayokuwa idadi kamili tutakayoitumia katika kuhesabu.

Mheshimiwa Spika, niliomba na hili nilieleze vizuri ili niwarejeshe Waheshimiwa Wabunge kwenye kanuni kwa maana huu ni utaratibu wa kawaida wa upigaji wa kura. Tunaweza tukaeleza wakati mwingine taratibu nyingi za kupiga kura ndani ya nyumba yako hii.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa ili kuokoa muda, tuite Wagombea waje kwa utaratibu tuliouandaa, mmoja baada ya mwingine kama tulivyoeleza.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nafikiri mmemsikia Katibu. Kwa utaratibu huu, maana tunaweza tukawa idadi fulani humu ndani tukaitangaza, lakini mtu mwingine hapa akaondoka zake au watatu, wanne, watano wakaondoka; matokeo yake ile idadi tuliyoitaja kama akidi na karatasi ambazo zinakwenda kuhesabiwa kule ndani zikawa na tofauti, ikatuletea shida. Kwa utaratibu huu, mtu akitumbukiza mle ndani ndiyo anatengeneza akidi.

Kwa hiyo, zile kura tutakazotokanazo hapa, ndiyo akidi yenyewe na ndiyo kura zote, kwa sababu wote tumeshuhudia kwamba hawa kweli ndio waliopiga kura na hakuna aliyerudia kupiga kura. Isipokuwa kama nilivyosema,

kwa wenzetu wenye mahitaji maalum tutawapelekea kura pale kwa kutangaza kwamba kura hiyo moja inaenda pale, ni fulani anakwenda kupiga kura na kadhalika.

Naamini kwa sasa tumefika pazuri, tumetumia nusu saa kwa ajili ya haya mambo ya utangulizi, sasa tuanze kazi ya kuwasikiliza Wagombea wetu. Katibu tuitie wa kwanza.

**NDG. NENELWA M. WANKANGA - KATIBU MEZANI:** Tunaomba *Seargent-at-arms* amwite Profesa Abdallah Jumbe Safari.

**SPIKA:** Mpambe naomba uokoe muda, tuitie Mgombea Profesa Abdallah Safari. Wanatoka mbali kidogo Waheshimiwa, kwa hiyo, tuvumilie. Hatukutaka kulikisha mtihani.

*(Hapa Mgombea Profesa Abdallah Jumbe Safari aliingia Ukumbini na Waheshimiwa Wabunge walianza kumpigia makofi)*

**SPIKA:** Hapana, hapana!

*You are cordially welcome. In front of you are members of Parliament, you will be given three minutes to explain why you are here and certainly identify yourself. After that if there are one, two or three questions you will be asked and I will ask you to answer them, after that you will be required to excuse yourself. The floor is yours now.*

***PROF. ABDALLAH JUMBE SAFARI:*** *Honourable Speaker, Honourable Prime Minister, Honourable Leader of the Opposition; my name is Abdallah Safari. Before I proceed with my request to be elected to the East African Legislative Assembly, I wish to sincerely convey my condolences to the family of the 33 students and their two teachers and a driver who were tragically killed in a road accident that took place in* Arusha.

*Honourable Speaker, I am attending here to appeal to your Parliament to be elected to represent this honourable country to the East African Legislative Assembly. My profile is contained in the CV which has been distributed to the Members of this Assembly as well as a leaflet that I tried to distribute to most of the Members of this Honorable Assembly.*

*I hold a PHD from the University of Sussex in UK where I also taught a course known as "Comparative Criminal Justice Systems in the World." I am also a Professor of Law, I have taught in many academic institutions including the University of* Dar es Salaam *where I taught The Law of Evidence and some of the best students are currently here, for instance Honorable* Rweikiza *and Honorable* Adadi. *I also taught The International Law at* Mozambican - Tanzania *Centre for Foreign Relations where I saved as the Director of Studies and Programmes.*

*I am author of about six books, one of each is being used in all Universities to teach criminal procedure and it is also used at The Law School of* Tanzania *and my other two books including* "Harusi" *was used as A-levels and to teach subject known as Stylistics at The University of* Dar es Salaam *Department of Literature. And my other book called* "Joka la Mdimu," *is currently being used to teach literature at A-levels...*

***HON. SPEAKER:*** *Honourable Professor, the three minutes are over. Now is time for questions if there are any. One from that corner, please proceed.*

***HON. OSCAR R. MUKASA:*** *Honourable Speaker, Thank you. I am Oscar Mukasa from Biharamulo.*

*Yes Sir, the candidate, in a mixture of factors that can produce success with those that can produce failure, the product is failure. This statement was made by someone in the name of Jethro Spear and I would like to use it as a preamble before I pose my question to you.*

*In my opinion, we are failing quite well as a group of countries in this block in terms of the political will from the individual countries. But we are not moving on the same page when it comes to economic interest of the block as opposed to interest of the individual countries. Can you prove me wrong or right as you are asking for for my vote to represent our country in the council of Law makers in East Africa? Thank you. (Applause)*

**HON. SPEAKER**: *Thank you contestant. Can you respond to that question!*

**PROF. ABDALLAH JUMBE SAFARI :** *Honourable Speaker, the objects of the East African Community is clearly stipulated in article 5 of the Treaty for The Establishment of The East African Community. And one of the main objectives is to ensure that the East African States will forge strategies to ensure proper political, economic and cultural development activities to benefit the people of these countries.*

*Therefore, what I am going to do if I will be elected to this August Assembly is to ensure that the interest of Tanzania are going to be best represented in the East African Legislative Assembly for the benefits of all Tanzanians.*

**HON. SPEAKER:** *The second question was from your neighbor there.*

**A MEMBER:** *Thank you Honourable Speaker. I have been going through the very big CV of the Professor, and my question does not intend to change the opinion of the voters in this House. Professor, do you believe in succession plan?*

**PROF. ABDALLAH JUMBE SAFARI :** *Sorry!*

**HON. SPEAKER:** *understood, understood. Can you respond that question? Are you a believer in the concept called succession plan?*

**PROF. ABDALLAH JUMBE SAFARI :** *I didn't hear him properly. What did he say?*

**HON. SPEAKER:** *He asked you a simple question, are you a believer in the philosophy or a concept called succession plan? That is his question.*

**A MEMBER:** Hilo ni swali hilo?

**PROF. ABDALLAH JUMBE SAFARI:** *Honorable Speaker, succession plan! You see, succession can mean a lot of things, for example in law there is doctrine of state succession. If you mean succession in law, it means that this smooth transition of governments from one epoch to another. I am sure there could be other types of succession in other disciplines. Therefore, unless the question is much more specific on what type of successions it is intended. It is a bit vague. (Applause)*

**SPEAKER:** *The last question from HonoUrable Member.*

**HON. JOSEPH K. MUSUKUMA:** *Thank you Mr. Speaker. (Laughter/Applause)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Vipi? *(Kicheko/Makofi)*

*Thank you Mr. Speaker. (Kicheko)*

**HON. SPEAKER:** *Order in the House! Proceed please.*

**HON. JOSEPH K. MUSUKUMA:** *Thank you Mr. Speaker. Mr Safari I want to know your weakness before I vote. Thank you. (Laughter/Applause)*

**HON. SPEAKER:** *Order! Order! Order! The Member wants you HonoUrable Professor to tell him, what are your weaknesses and convince him to vote for you. (Laughter)*

**PROF. ABDALLAH JUMBE SAFARI - CANDIDATE:** *My weaknesses; I am not quite aware of any weakness. I am not*

*quite aware I have any tangible weakness that I have. (Applause)*

**HON. SPEAKER:** *Thank you very much. Now I am giving you two minutes to wind up and ask for votes once more.*

**PROF. ABDALLAH JUMBE SAFARI - CANDIDATE:** *Ok. Honourable Speaker, I had distributed a leaflet spelling out my program at the East African Legislative Assembly. I am sure that Honourable Members of Parliament have gone through them and I don't have to epitomize them. But finally I must say that the preamble to the East African Charter says that, the past East African Community failed because of certain factors. I am going to ensure that this East African Community is not going to fail and finally I am going to play the role of the link between this National Assembly and the East African Legislative Assembly.*

*I honourably request that you vote for me. I can assure you that I am going to represent this country very consciously and with a professional mind and integrity. Thanks a lot. (Makofi)*

**HON. SPEAKER:** *Thank you very much. You can now take your leave please. (Applause)*

Jamani, makofi yaacheni. Mgombea wa pili, Katibu.

***MR. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - CLERK AT THE TABLE:*** Ezekia Dibogo Wenje.

**HON. SPEAKER:** *Ezekiel* Wenje, *you are welcome. In front of you, beside you, behind you are Members of Parliament who are waiting eagerly for you to identify yourself and explain why you are here. After that exercise of three minutes, if there are some questions you will be asked to answer them, not more than three. Later on, you will have to leave us for the rest of the activities. The floor is now yours please. You have three minutes to explain.*

***MR. EZEKIA DIBOGO WENJE:*** *Thank you Mr. Speaker Sir, thank you Honourable Prime Minister, thank you the Leader of Opposition, Honourable Freeman Mbowe, Ministers present and the Honourable Members of this House. My names are Ezekia Dibogo Wenje. Here I am again today before you to seek your votes to enable me represent our great Nation in the East African Parliament.*

*Mr. Speaker Sir, this election is very emotional but I want to tell you, it is just a day's event. It will end today and we will be the same people tomorrow in the same country.*

*Mr. Speaker Sir, I stand here today with a strong conviction that East Africa and its people are one. We have a common shared history under common destiny as people of East Africa. Both of you are aware that long time ago before the Berlin Conference which divided East Africa into what it is today, East African people were one. We were only separated by rivers and valleys and beautiful mountains which our people could easily cross in search of pastures and food without being subjected into the colonial passports and visas.*

*Mr. Speaker, we are one and that is why the founders of these great Nations had this truth at heart and that is why immediately few years after independence they started beating drums loud, the drums of integration because they had this truth at heart.*

*Honourable Speaker, the seeds of integration that they sow, is the new East African Community that we have today. We are here before this House, both of us, to participate in this history to rewrite this history today, to water the seeds of integration that these great men sow those years back.*

*Mr. Speaker, I stand here today as a proud son of Africa, the writings are on the wall right now. Nobody can dispute the fact that we need to take strong men and women with strong characters...*

***HON. SPEAKER:*** *Can you wind up now.*

***MR. EZEKIA DIBOGO WENJE:*** *... into the East African Parliament to go and defend our country and our sovereignty.*

*Honourable Speaker Sir, thank you. (Makofi)*

***HON. SPEAKER:*** *Thank you very much. Any questions to the candidate! Three questions already, we start from there, and then there, we will finish up here. You are welcome Honourable Member.*

***HON. JOSEPH G. KAKUNDA:*** *Honourable Wenje, The United Nations Agreement on the application of sanitary and phytosanitary standards demands equality among Nations in its enforcement. Now this agreement is appurtenant to the EAC Treaty and its subsequent protocols....*

***MR. EZEKIA DIBOGO WENJE:*** *Honourable Speaker, I did not get him properly, can he come again? I can't hear properly.*

***HON. JOSEPH G. KAKUNDA:*** *Honourable Speaker, let me make it close here.*

*The United Nations Agreement on the Sanitary and Phytosanitary Standards demands equality on its application.*

***MR. EZEKIA DIBOGO WENJE:*** *.. Sanitary standards and what?*

***HON. JOSEPH G. KAKUNDA:*** *Sanitary and phytosanitary standards.*

***MR. EZEKIA DIBOGO WENJE:*** *Sanitary?*

***HON. JOSEPH G. KAKUNDA:*** *Yes! You understand now? Ok! Demands equality in the enforcement. Now as an EALA MP, this agreement which is appurtenant to the EAC Treaty and its protocols, how are you going to stand to make sure that our products like meat and fish get through to the market without getting hard to these measures? (Makofi)*

***HON. SPEAKER:*** *Can you respond to that question please.*

***MR. EZEKIA DIBOGO WENJE:*** *Thank you Mr. Speaker Sir. If you read the East African protocols like chapter five and if you read about the Customs Union that includes the so called rules of origin, the best thing that our country can actually benefit from the regional product that we have like fish as he has said, is to make good use of the so called Rules of Origin which is in the Customs Unions Treaty. You see, as a country, for our products to be competitive we cannot compromise the sanitary standards set internationally. (Applause)*

*Honourable Speaker, no matter what, we just have to encourage the manufacturers or producers of our products to put them to that good standard so that we be competitive.*

*Thank you Mr. Speaker Sir. (Applause)*

***HON. SPEAKER:*** *The second question, Honourable Maige.*

***HON. ALMAS A. MAIGE:*** *Thank you very much Honourable Speaker. I have the following question to the candidate. You know that there is imbalance of labor force among the East African Member States; what do you understand by the term free labor movement protocol in the East African Member States. Thank you.*

***SPEAKER:*** *Free labor movement, can you explain.*

***MR. EZEKIA DIBOGO WENJE:*** *Thank you Mr. Speaker Sir. There has been this notion that our people in our country are not getting jobs in other countries across the region simply because some people think we are not competent enough and that is why our people still feel that, you know if you go back to the economic protocol, one of the things that they talk about is free movement of persons and free movement*

*of labor. Our people still have reservations and feel that if we allow free movement of labor then our people will not get jobs elsewhere and some people from Kenya, Uganda, Rwanda will come in and take our jobs. This is not correct! I believe we have strong and competent manpower in this country, we have the same Universities as like* Nairobi, *we have the same Universities as like* Kampala, *we have the same Universities as like Rwanda University. We have competent young men and women in this country who can fight for the jobs not only in Tanzania and even across, even in Uganda we can go! We have competent people here. (Applause)*

*Honourable Speaker, I can assure you, we have very competent Members of Parliament here. They have gone through the same Universities which I have also gone through. I believe if we are put on the same table with Kenyans, Ugandans, we can prove them wrong, that is why some of us who believe we are competent, take us there, we go and prove to them that we have strong men and women in this country, we can defend our sovereignty, we can defend our integrity.*

*Thank you Mr. Speaker Sir.*

***HON. SPEAKER:*** *Thank you very much. The last question from this side.*

***HON. MAFTAHA A. NACHUMA:*** *Honorable Speaker, thank you very much. I would like to ask a question to the contestant right here. Mr. Wenje, you just seem to be a worshipper of commonalities in East Africa and you are talking about...*

***SPEAKER:*** *Worshipper of what?*

***HON. MAFTAHA A. NACHUMA:*** *Commonalities...*

***SPEAKER:*** *Commonalities?*

***HON. MAFTAHA A. NACHUMA:*** *Yes! Commonalities in East Africa. You are talking about this integration just you want people to integrate equally within East African Regional Integration. So my question is; so long as we have started to talk about the Former East African Integration that was declined in 1977 if I am not mistaken and there were some kind of problems that made to decline that kind of integration…*

***HON. SPEAKER:*** *I am sorry, can you wait a little bit. Member, can you listen to me before you proceed? What you are doing is, you are addressing the candidate. Can you put forward a question, straightforward, no organization. Put the question forward, you will be answered, it is over.*

***HON. MAFTAHA A. NACHUMA:*** *Thank you Honorable Speaker. My question is, how are you going to assure us that if we are just going to elect you as a Member of Parliament in EALA that you are going to defend Tanzania interest in East African Community? (Makofi)*

***HON. SPEAKER:*** *Can you respond to that question?*

***MR. EZEKIA DIBOGO WENJE:*** *Mr. Speaker Sir, if I heard him correctly, it is like he doubts my ability to go and represent our country.*

*Mr. Speaker Sir, he also talked about commonality. I am a strong believer that Africa and its people are one and in East Africa in particular, and that is why if you go across border you will find some Maasais in Tanzania ana some are in Kenya. You will find Luos like me here, some are in Shirati and some are in Kenya; you will find Kuryas some are in Tanzania and some are in Kenya; you will find the Kondes, some are there and some are in Zambia. We are one people! What divide us is only colonial boundaries.*

*Mr. Speaker, I am a son of this land. This is the land of my ancestors; this is the land of my fore fathers. I can defend the sovereignty of our country at any cost across our borders.*

*Give me the opportunity to fly high the flag of our country and I will do it without any doubt.*

*Thank you. Mr. Speaker Sir. (Applause)*

***HON. SPEAKER:*** *Thank you very much, thank you candidate. I am now giving you two minutes to wind up your speech and ask for votes once more. After that I will ask you to leave.*

***MR. EZEKIA DIBOGO WENJE:*** *Honourable Speaker, Honourable Prime Minister, Members of Parliament here; as I said earlier, this an election is just a day's event. We will be the same people tomorrow, in the same country; you will be the same Members of Parliament tomorrow in the same Parliament. The writings are on the wall, let us arise all together to do justice to our country by sending competent and strong people who can defend the sovereignty of this country. I believe I am such one character who can go and work for our country. I ask you to support me and I request your votes. Thank you so much. (Applause)*

***HON. SPEAKER:*** *Thank you very much and now you are free to leave. Thank you very much. (Applause)*

Waheshimiwa Wabunge, bado naendelea kuwaomba, Wagombea wanapojieleza hapa na wamekuja kwa ajili yetu, ni vizuri tukawasikiliza. Pana minong'ono mingi, husikilizi! Kama nilivyosema, huenda tunaonekana huko, sasa Watanzania wanashangaa, hivi hawa watu wanashindwa kuwa na dakika mbili, tatu tu za kumsikiliza mtu? Katibu, anayekuja mwingine!

***MR. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - CLERK AT THE TABLE:*** Josephine Sebastian Lemoyan.

**HON. SPEAKER**: *Josephine, in front of you are members of parliament. In a few minutes I will ask you to speak to them, introduce yourself and explain your mission here. Later on there are might be some questions up to three of which you*

*will asked to answer them and later on you will leave. I am now giving you three minutes, the floor is yours, please proceed.*

**MS. JOSEPHINE SEBASTIAN LEMOYAN:** *Thank you very much your Honor Speaker of the United Republic of Tanzania; your Honor the Prime Minister of The United Republic of Tanzania; I recognize the presence of the Leader of the Opposition in the House; Honourable Members of the Parliament; members of Media Houses; good evening ladies and gentlemen.*

*My names are Josephine Sebastian Lemoyan. I am standing before you with deep heart felt sympathy towards the calamities and demise of our children following the accident that has occurred a few days ago in Karatu. Let me offer my heart felt deep sympathy to you, your Honor Mr. Speaker Sir, as well as the parents, friends, relatives and the family of Tanzania as a country.*

*My credentials has been presented, but I would like to go back to them just to set the record right. I am a woman, a mother and a daughter of Tanzania, holding a Master's degree in Sociology and Master of Science in Applied Social Research.*

*Mr. Speaker Sir, I am coming before this August House of the Parliament of United Republic of Tanzania requesting very humbly that I am sent on a mission to go and represent Tanzania in East African Legistrative Assembly whereby I am going to join fellow colleagues whom you have elected a few days ago. My mission and why am I interesting to go to EALA is because I red the strategic plan for East Africa Community 2015 which has a number of issues which I think, I can contribute to.*

*My background is in Social Sciences and I think I can make a contribution using experience expertise and my knowledge.*

**HON. SPEAKER:** *Can you windup your speech now! Windup.*

***MS. JOSEPHINE SEBASTIAN LEMOYAN :*** *I think I can make that contribution because I have done well and I have done so much not only because I have the education, but the experience in working with the government for more than 30 years where by issues of policy analysis, research were done. (Applause)*

***HON. SPEAKER:*** *Thank you very much. Three questions if any? I have seen three candidates now. We will start from that end and then come from that middle position then the last question will come from hear. The man behind in black please.*

***HON. RICHARD P. MBOGO:*** *Thank you Honorable Speaker...*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

***SPEAKER:*** *Proceed!*

***HON. RICHARD P. MBOGO:*** *My name is Mbogo. I would like to ask Madam; you have said that you have good experience and knowledge but we know we have four pillars in East Africa Community. Now, can you tell us what challenges do we have on the current pillars we have adopted and if we elect you as EALA member, how are you going to address these challenges?*

***MS. JOSEPHINE SEBASTIAN LEMOYAN:*** *I could not hear you properly.*

***SPEAKER:*** *Did you hear, his question?*

***MS. JOSEPHINE SEBASTIAN LEMOYAN:*** *Not quite really, I did'nt hear the question.*

***SPEAKER:*** *Speak closer, put closer that microphone or you use the neighbouring one.*

***HON. RICHARD P. MBOGO:*** *Alright. I can just go back again. You have said that you have good experience and knowledge on various matters and you have gone well on the East Africa Communities as our Regional Integration East Africa. There are almost four pillars and two already adopted but we have challenges. Now can you tell us how are you going to address these challenges we have; and how are you going to attack the remaining two pillars which are not yet adopted by the East Africa Community?*

***HON. SPEAKER:*** *He means adopted. Can you answer?*

***MS. JOSEPHINE SEBASTIAN LEMOYAN:*** *Thank you very much Honorable Speaker and thank you very much for your question. Yes indeed, there are four pillars of integration for our East Africa Community and the first one is custom union, which paves the way towards Common Market and the third one is the Monitory Unification and lastly is about the Political Federation. (Applause)*

*Now, the quiet a number of challenges across the four pillars and in so far as second pillar is concern and first one as well, there are quiet a number of non-tariff barriers as well as tariff barriers that have not been addressed. The recent report on East Africa Community annual performance indicates that 104 non-tariff barriers has been actually addressed and between 16 and 20 are not yet addressed, a new ones are emerging. Now, how am I going to...*

***HON. SPEAKER:*** *Thank you very much. Thank you member. Thank you candidate.*

*Matha Umbulla I saw you.*

***MS. JOSEPHINE SEBASTIAN LEMOYAN:*** *Mr. Speaker Sir...*

***HON. MARTHA J. UMBULLA:*** *Thank you Honourable Speaker. The land scarcity in other East African countries may force the citizens of other East African countries to forge in the strategies of intermarriage so that to attain a land*

*ownership from Tanzania. Now as a woman MP in EALA, in case of such behavior, how are you going to discourage it?*

**HON. SPEAKER:** *Can you respond to that question?*

**MS. JOSEPHINE SEBASTIAN LEMOYAN:** *Yes Mr. Speaker Sir. Thank you very much for your question. I think you are talking about the land issues and land grabbing, and if that is the question as a woman MP what I am I going to do in order to address the question of land grabbing in our country?*

*First of all, I had been working for quite some time on land issues and woman participation on land issues and just recently on the 18th of March, 2017, a new Act on gender and Non-discrimination Act has been passed. I am going to facilitate and contribute towards making that legislation known to the women as well as making it popular so that women understand what they have to do in so far as land issues are concern. Thank you. (Applause)*

**HON. SPEAKER:** *The third question. No clapping please! Honorable Saada.*

**HON. SAADA SALUM MKUYA:** *Thank you Honourable Speaker. Miss Josephine, if I am not mistaken, one of your researches during your education background was about drug abuse among the young generation particularly in Tanzania. As a woman, as a mother, as well we expect I do know if you are going to pass through well as a woman MP, what is your take about the challenge of drug abuse among the young generation? And what are you going to do; your special initiative to address the challenges among East Africa countries and as well as a region? Thank you.*

**HON. SPEAKER:** *Can you respond to that question, candidate?*

**MS. JOSEPHINE SEBASTIAN LEMOYAN:** *Honourable Speaker and Madam Saada thank you very much for the question. Yes indeed, child abuse is a critical issue and in a*

*young block like the East African Community we have more than 33 percent of its population as children. My take is going to be working together with the team of Tanzania as well as other country MPs to ensure that we legislate on issues of child abuse taking on board lessons that we have learnt from Tanzania so that we make our country proud. Thank you very much. (Applause)*

***HON. SPEAKER:*** *Thank you candidate. No clapping. I am now giving you two minutes to windup your presentation and once more ask for votes before you leave. Go ahead.*

***MS. JOSEPHINE SEBASTIAN LEMOYAN*** **:** *Thank you, Mr. Speaker Sir, Honourable Members of the Parliament, Josephine comes forward to you pleading that you send me to become a servant in EALA, holding hands together with other colleagues whom you have been elected just a few weeks ago. I am humble woman, I am very much willing to run when I am told to run, I can walk from here to Juba if that is necessary; and I am going to make sure that I hold my country dear in my heart and work together as a team with others.*

*Ladies and Gentlemen, Honourable Speaker Sir, Honourable Member of Parliament, I bag for your votes. (Applause)*

***HON. SPEAKER:*** *Thank you very much. No clapping! Thank you Josephine, now I ask you to leave and wish you all the best. Please!*

Katibu, mwingine.

***MR. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - CLERK AT THE TABLE:*** Lawrence Kego Masha.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nime-*notice* kitu kimoja, kumbe tungefanya sheria hapa tuwe tunachangia Kiingereza, ule ukorofi wote ungekwisha humu ndani.

**MBUNGE FULANI:** Kesho! *(Kicheko)*

**SPIKA:** Kesho eeh? Wanaoafiki kesho! *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Ndiyooo!

**SPIKA:** Wooote mmekataa. *(Kicheko)*

*Lawrence, in front of you are Members of this August House, you will be given three minutes to identify yourself and then explain your mission why you are here and later on if there are any questions not more than three, you will be asked to answer them. You have the floor.*

***MR. LAWRENCE KEGO MASHA:*** *Thank you, Mr. Speaker.*

*Honorable Speaker, Honorable Prime Minister, Honorable Leader of the Opposition, Ministers, Members of the Parliament; my name is Lawrence Kego Masha, I am aspirant the office of being a member of East Africa Legislative Assembly.*

*However, Honorable Speaker, though you I would like to take this opportunity to give my heartfelt condolences to the President of United Republic of Tanzania, the people of Tanzania and particularly the people of Arusha and most importantly to the families who lost the beloved ones and that fateful vehicular accident that took place in Karatu the other day. May the Lord bless the souls of the departed in ever last in peace.*

*Mr. Speaker, three to four weeks ago I stood in this August Hall to request the votes to become a member of the East African Legislative Assembly. Unfortunately, the vote was insufficient and hence I stand before for you once again. My cv has been circulated, my record well known, so I will take one or two minutes simply to give you additional inside as to who I am and my character.*

*Mr. Speaker, in 1960 my father left Sengerema for the United States, he was inspired by John F. Kennedy who is inaugural address said don't ask what your country can do*

*for you but ask what you can do for your country. It is a sentiment my father lived by, it is a sentiment he has embeded in his children. My father came back to this nation saved as a Member of Parliament; I was fortuned enough to save in fourth phase government an opportunity for which I am trully grateful. And my young brother is a Colonel in Tanzanian Army, ready and willing to die for this country as when required.*

*I am standing before you to ask to save my nation once again, I am patriotic Tanzanian I would like to use the skills which I have to save the nation I love.*

*Mr. Speaker, Honorable Prime Minister, Honorable Leader of the Opposition, Ministers and Member of Parliament, my I kindly have your votes. (Applause)*

***HON. SPEAKER:*** *Questions if any?* Hapa *CUF* kiingereza tatizo? Maana sioni maswali. Naona maswali CCM tu, inaelekea... Leo ndiyo tutajuana hapa leo! *(Kicheko)*

Haya, tuanze Mheshimiwa pale kwanza, halafu tutakuja mitaa hiyo.

***HON. SALOME W. MAKAMBA:*** *Thank you Honorable Speaker for giving me a chance to ask the candidate a question.*

*Mr. Masha, you know that South Sudan is one of the country that join East African Community very recently. But we all know that they are still in war and lot of human rights abuses in South Sudan. What is your take in this, do you think it was bit premature to invite it in the treaty? Thank you.*

***HON. SPEAKER:*** *Your opinion is thought, candidate can you respond to that?*

***MR. LAWRENCE KEGO MASHA:*** *Yes Honorable Speaker.*

*One must be understood is that, the strategic reasons in letting South Sudan to become a member of East African*

*Community, part of the very issues you have just raised are some is very reasons South Sudan was allowed to come in, so they could be closely monitored, so that we can actively take part in ensuring that there is peace in South Sudan; ensuring that they would not be able to disrupt neighbours within the region. I am sure although there are problem in South Sudan you are aware that there are problem in Burundi as well and the potentially problems in some of the other states. These are not reason for exclusion, what we must do is insure that, one, we work with our government to ensure as best as possible we can facilitate peace in South Sudan as we have tried in the past.*

***HON. SPEAKER:*** *The two gentlemen, did you say CUF? Okay CUF Ally Saleh yes.*

***HON. ALLY S. ALLY:*** *Mr. Speaker Sir, thank you, my name is not CUF, my name is Ally Saleh, secondly I thank you for seeing me after fourth try you to notice me. (Laughter)*

*My question is Dar es Saalam Community is heading towards political federation and this is after other steps are completed. First, what is your take on this, but secondly, how best do you think Tanzania can protect her interest if this happens, if the political federation comes into being?*

***HON. SPEAKER:*** *Before you respond I want to assure Honorable Ally Saleh, it is not the first time that I saw you, I saw you the first time in late 1980's when we were together at the University of Dar es Salaam while we were leading all the boycotts there and we were some of the followers. Candidate can you answer? (Laughter)*

***MR. LAWRENCE K. MASHA:*** *Honorable Speaker, the question which has been put forth by my colleague counsel Honorable Ally Saleh is a very delicate question, and quiet honestly I am not sure under normal circumstances had I been the Minister for Home Affairs for example in this body, whether I would be willing to answer within an open session my thought will go to political federation. It's a very delicate situation.*

*The political situation of the six countries which we are dealing with is all very different. The levels of the democracy differ and if we go into political federation without naming each country piece by piece, we may actually suffer some problems. I would actually, if I was elected into the East African Legislative Assembly I would work very closely with our Department of Foreign Affairs to determine how best this should be handled because I think it is a matter of state security and it is a matter which should be handled very carefully.*

***HON. SPEAKER:*** *The second question, Honorable Kakunda.*

***HON. JOSEPH G. KAKUNDA:*** *Honorable Speaker, thank you.*

*Mr. Masha, you know that Tanzania is an LDC, is a Least Developed Country, and we are struggling to industrialize but Kenya is non-LDC country and it has about tens of thousands of industries now. Now if we treat equally the place of origin and rule of origin principles of the common market, how are you going to ensure that our products get same treatment in the market without getting some difficulty in the marketing share?*

***HON. SPEAKER:*** *Can you now respond candidate?*

***MR. LAWRECE K. MASHA:*** *Honorable Speaker, yes I can, if I can respond to the Honorable Member of Parliament as follows:-*

*Honorable Speaker, first and foremost we have seen for example when it came to the customs union our Ministers worked very carefully with their colleagues around these five states at the time in order to ensure that we are protected those items in terms of tariffs that we needed to protect prior to entering our budgetary phases.*

*Honorable Speaker, It is absolutely necessary within the stage of the common market that a variety of things be*

*protected. If you take into account that the common market is an agreement of free movement of goods, services and people all of these things we must sit back and figure out at what level we are at both economically in terms of our service ability and look at the protection people within the region in order to determine what we allow to partake at certain times. As I have said previously, when you are a member of the East African Legislative Assembly you are not going there to represent your personal ideas, you are going there to represent your nation. The nine people who will be chosen to go to the East African Legislative Assembly must work hand in hand with their government in order to be mouth pieces for the government in the Legislative Assembly, I am not going to the Legislative Assembly to speak on my behalf.*

***HON. SPEAKER:*** *Thank you, thank you very much. Honorable Zitto Kabwe, the last question.*

***HON. KABWE Z. R. ZITTO:*** *Honorable Speaker, bonus question, thank you very much, tuendelee tu.*

***HON. SPEAKER:*** La kwanza aliuliza nani, sio Mheshimiwa Ally Saleh? Katibu wetu, Mheshimiwa Salome aliuliza? Aah, basi.

***HON. KABWE Z. R. ZITTO:*** *Honorable Speaker, thank you very much for a bonus question to Mr. Masha...*

***HON. SPEAKER:*** *Mheshimiwa Zitto inatosha, inatosha nimeambiwa kumbe ni swali la nne, I am sorry.*

*Candidate, I am now giving you two minutes to windup your speech and ask for the votes once more.*

***MR. LAWRENCE K. MASHA:*** *Thank you very much Honorable Speaker.*

*My request to the Members of the Parliament here today is that they take full cognisance of the fact that the East African Legislative Assembly is not apartisan Parliament.*

*The East African Legislative Assembly is a Regional Parliament where we are supposed to send our best. We shouldn't make decisions based on political party lines, we shouldn't make decisions where we take people who we also understand are not the best. (Applause)*

*Honorable Speaker, my humble is to request you, CHADEMA has brought you six candidates who I believe are all good. My request is, you seat back and look who can best protect the interests of this country across our borders to ensure that Tanzania is stable country, is peaceful country and secure country. I believe I have the experience to do so and I humbly request Mr. Speaker, Honorable Prime Minister, Leader of the Opposition, Ministers and Members of Parliament, please make the right choice.*

*Thank you, can I have your votes.*

**HON. SPEAKER:** *Thank you very much. I now ask you to leave. Thank you. Ahsante sana.*

*Katibu, mwingine.*

***MR. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - CLERK AT THE TABLE:*** *Pamela Simon Massay. (Applause)*

**HON. SPEAKER:** *Pamela, you are welcome. Infront of you or before you are members of this August House. You will be given three minutes to introduce yourself and tell us why you are here. Let on there are might be some questions up to three of which you will be asked to answer. You are now having the time to address the House. Please proceed.*

***MS. PAMELA SIMON MASSAY:*** *Thank you. Honorable Speaker, Honorable Prime Ministers, Honorable Leader of the Opposition, Honorable Members of Parliament, Ladies and Gentleman, I salute you.*

*First of all I would like to send my condolences to all Tanzanians, parents, friends who lost their children, the teachers*

*and the driver to the accident which happen last week. May their souls rest in peace.*

*In front of you, I am Pamela Massay, a Tanzanian lady, energetic one, holding a Bachelor of Food and Bio-Chemical Engineering and currently I am pursuing my Masters in Public Health. I am working with Coca Cola Kwanza as a Business System Coordinator who is ensuring the compliance of the products and services which are being implemented in the company and ensuring all Tanzanian are getting product which are of high quality and safety one. (Applauses)*

*Honorable Speaker, I am also an expert in the risk assessment, hazard analysis, I am conducting allied auditing on the issues of the systems meaning the International Standard Organization Systems. So as an expert, I am a member of Technical Committee under Tanzania Bureau of Standards who we are reviewing the East African Standards ensuring that all member countries from East Africa are producing products and services of high quality which can be sold inside the member countries and outside the country.(Applause)*

***HON. SPEAKER:*** *Thank you. Thank you Pamela! The three minutes are over. I hope you are heard the bell. Now is time for the questions. The first question will go to Honorable Zitto Kabwe and then I will announce the other ones later on. Honorable Zitto.*

***HON. KABWE Z. R. ZITTO:*** *Honorable Speaker, and thank you Pamela for your presentation. The previous EALA had different challenges. The first one develop the Customers Union, the second one develop the Common Market and the EALA that you are contesting for is going to approve a Monitory Union where we are going to have one Central Bank, one currency and we are going integrate our whole economy.*

*Tanzanian interests in the Monitory Union is to protect the capital flows within the Community, but also to protect the labour movement. As our representative there, what are you going to do to ensure that the interest of Tanzania as far*

*as the Monitory Union is concerned are highly protected, regarding that Rwanda has sent highly qualified people there, Burundi has sent its former Ministers there, Uganda has sent its former Ministers there, Kenya is going to send highly qualified there.*

*What are you going to do as a member from Tanzania to protect the interest of Tanzania as far as Monitory Unions is concerned?*

***MS. PAMELA SIMON MASSAY:*** *Okay. Thank you Honorable Zitto Kabwe.*

***HON. SPEAKER:*** *Candidate Pamela, you don't speak in this House before you are allowed. Is time now to answer the question. Can you respond please!*

***MS. PAMELA SIMON MASSAY:*** *Thank you.*

*As I have told you before, as an expert I am currently working in a committee which is reviewing the EAC Standards whereby we are going to ensure that, the member countries they are going to produce the products and services which is going to be competent in the EAC. I also asked, how am I going to protect it?*

*Honorable Speaker, I am going to protect as a technical personnel, because I am a technical personnel, I am going to convince them that all those things which we are going to discuss there, I am going to take them, first of all I will bring them to this Parliament because I know, we have to work hand in hand with this Parliament and also together with my President Dr. Magufuli. I will ask the support and will give me your inputs and then I will ensure that the implementation is going to be done. (Applauses)*

***HON. SPEAKER:*** *Mnavunja utaratibu. The second question Honorable member right behind there.* Naomba tusikilizane, tumtendee haki mgombea. Tusikilize!

***HON. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI:*** *Thank you Honorable Speaker for giving me the chance to ask the question to this young lady Pamela. Pamela!*

***MS. PAMELA SIMON MASSAY:*** *Yes!*

***HON. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI:*** *After seeing your cv, you are quite capable of getting this post, but... (Applause)*

***HON. SPEAKER:*** *Please don't clap for anything. Let us listen to each other, please.*

***HON. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI:*** *...assure me before getting my vote in this House, how are you going to walk or to boost the Tanzania economy in EALA?*

***HON. SPEAKER:*** *Honorable Member, where you reading or you were... (Laughter)*

*Can you answer the question? (Laughter)*

***MS. PAMELA SIMON MASSAY:*** *I didn't hear it well on the last two sentences. The last ones.*

***HON. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI:*** *How are you going to walk or to boost our economy in EALA?*

***MS. PAMELA SIMON MASSAY:*** *In what?*

***HON. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI:*** *Economy in EALA?*

***HON. SPEAKER:*** *Pamela, how are you going to boost our economy, Tanzanian economy in the contest of the East African Legislative Assembly?*

***MS. PAMELA SIMON MASSAY:*** *Okay, thank you. Because we are going to ensure Tanzania is one of the country which is going produce the better and best quality product*

*and services, we are going to get many market outside Tanzania within EAC and we will sell to highest level and ensure that we are going to bring back the money.*

**HON. SPEAKER:** *Last question, Honorable Selemani Jafo.*

**HON. SELEMANI S. JAFO:** *Thank you Honorable Speaker.*

*Madam Pamela, because you talked about the nutrition factors, I would like to know what are success story from Tanzania do you expect to share with your colleagues in the EALA? The success story from Tanzania which you do expect may be to share with others in the EALA.*

**HON. SPEAKER:** *What success story are you going to carry with you to the East African Legislative Assembly? Can you respond to that?*

**MS. PAMELA SIMON MASSAY:** *Okay. As a stakeholder I have been practicing many things which are within the agenda of EAC. I have many experiences, I have examples, for example this year I have the campaign which is called Make Tanzania Goes Green. This is one of my success, when I am on that side, I am going to push it. We will put something within the EALA and I will come back again to this Parliament to give you some hints on how are we going to tackle the issue of ensuring environmental conservation of Tanzania is going to be implemented in a proper way, because we have seen we are backing behind our friends. (Applause)*

**HON. SPEAKER:** *Please hold on! Order in the House.I am giving you time to wind up and ask for votes once more very shortly.*

**MS. PAMELA SIMON MASSAY:** *Thank you!*

*Honorable Members of Parliament, I am begging for your votes because I am energetic lady, I am very competent, I have the capabilities, I am sure that I can convince other members to make sure that all the interest of my country, all*

*the things which will be needed by my country especially the issue of industrialization which has been pushed by our President, is going to be implemented in a proper way. (Applause)*

*I beg you, I am asking for your all votes. (Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumpe nafasi tumsikie anachosema. Sasa kama hamsikii!

**MBUNGE FULANI:** Imetosha! Aombe kura aondoke!

***HON. SPEAKER:*** *Candidates time is up, you can now leave please. (Applause)*

Mimi nawashangaa wale ambao mnavunja utaratibu, mnaweza mkamharibia mgombea hivi hivi. Acheni watu wanaotaka kusikiliza, wasikilize. Kumbukeni wanaosikiliza sio ninyi peke yenu hapa, Taifa linasikiliza. Kama wewe huna *interest,* kaa kimya tu, mgombea ajieleze. Anajieleza kwa Watanzania, siyo kwenu peke yenu. Kumbukeni, Watanzania wanataka kujua mwisho wa siku mmechagua watu gani? Kwa hiyo, wapeni haki hiyo.

**MBUNGE FULANI:** Haiko *live*.

**SPIKA:** Hiyo mtajua wenyewe. Hata kama haiku *live* sasa hivi, inaweza ikawa *live* kesho. *(Kicheko)*

Eeeh, si linaandikwa tu neno *live?* Katibu.

***MR. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – CLERK AT THE TABLE:*** Salum Mwalimu Juma.

**SPIKA:** Tuwasikilize Wagombea tafadhali, nawaombeni sana.

**MBUNGE FULANI:** *(Aliongea bila kutumia kipaza sauti)*

***HON. SPEAKER:*** *Naam.*

*Mr. Salum you are welcome. Before you are members of this August House. You will be given three minutes to explain why you are here and certainly identify yourself, after that there might be some questions of which you will have to answer. There are not going to be more than three. I am now giving you the floor to proceed. Please, you have the time.*

***MR. SALUM MWALIMU JUMA:*** *Thank you Honorable Speaker. I understand the challenge of being the last person to represent yourself in this kind of process; but since I am a person of accountancy, I believe being the last one I will be the first one to be remembered when people start voting. (Laughter)*

*Honorable Speaker, Job Ndugai the right Honorable Prime Minister, Kassim Majaliwa Majaliwa, Honorable Leader of the Opposition,Freeman Aikaeli Mbowe, Honorable Members of the Cabinet, Deputy Speaker, Honorable Members of the Parliament, Ladies and Gentlemen; good evening.*

*My names are Salum Mwalimu, I was born in 1979 in Zanzibar, I am honored to stand before you to humbly request for your votes as I contest for a seat in the East African Legislative Assembly.*

*Honorable Speaker and Honorable Members of the Parliament, I understand in today's world the regional integration has proved without reasonable doubt that is a very necessary tool for a country to advance in economical and political interest for its people, the East African Community is therefore a core for a Tanzanian.*

*Honorable Speaker, and the right Hounourable Prime Minister and the Leader of the Opposition, if I succeed today to have more enough votes from you, I promise you that I will try to work hard to the best of my ability to ensure that we have a meaningful and strong East African Community for the interest not only for Tanzania but the interest of the East African Community.*

*Honorable Speaker and Members of Parliament, thank you for your attention.*

***HON. SPEAKER:*** *Thank you, thank you very much candidate. Now it is time for questions. I have seen you Honorable Mary Mwanjelwa, please proceed.*

***HON. DR. MARY M. MWANJELWA:*** *Mr. Speaker, thank you for having an eye on me.*

*The East African Community collapsed 40 years ago, the treaty was signed and ratified a year later that was in 1999.*

*Now Mr. Candidate, if you are to be elected today for EALA, what will be your key legacy and patriotism in terms of our countries or East African Community four pillars? Thank you.*

***SPEAKER:*** *Can you respond to that question?*

***MR. SALUM MWALIMU JUMA:*** *Thank you Honorable Speaker, with your permission allow me to respond as follows:-*

*Honorable Speaker, first of all I think Honourable Member of Parliament will agree with me, we cannot measure the patriotism of any candidate today this evening but our history and background, the experience and the way we have been living and serving this country as boys and girls of this country is very important to measure our patriotism. (Applause)*

*Honorable Speaker, I served this country over the last fifteen years, I started as a journalist whereby I had an opportunity to travel all over this country including your constituencies to raise on social economic problem and inturn to share about the government and public sector initiative how to solve or how to provide solution for their social economic problems.*

*But again, I got an opportunity to work with Vodacom Tanzania whereby you can all be witnesses of what I am saying here, I had an opportunity to travel to your constituency to share with you how to transform the people from your constituencies. And as of now when I am serving as the capacity of a Deputy Secretary General I have again been traveling all over the country to promote justice, democracy and civil education to our people. (Applauses)*

*But again, let me assure Honourable Member of the Parliament that...*

***HON. SPEAKER:*** *Thank you, thank you, Honourable candidate. Thank you very much. Now we are going for the second question, I think we will have to go for the newest member in the House. Is that Catherine!*

***HON. CATHERINE N. RUGE:*** *Yes.*

***HON. SPEAKER:*** *Yes, okay.*

***HON. CATHERINE N. RUGE:*** *Honourable Speaker thank you very much for this opportunity. I would like to ask the following question to the candidate.*

*Mr. Salum, you have been senior and an experienced journalist with a knowledge of international trade, what are you going to do to ensure that you will make the opportunities available in East African Countries known to Tanzanians? Thank you. (Applauses)*

***HON. SPEAKER:*** *Can you now respond now to that question?*

***MR. SALUM MWALIMU JUMA:*** *With your permission Honorable Speaker, allow me to respond as follows:-*

*It is true that I am a very experienced journalist in this country and what will I do? I think it is very obvious that I will cooperate with the Ministry of International Cooperation and*

*Ministry of Information to come up with the very beautiful and attractive sensitization programs through media to make our integration very active and popular in our people*.

*Not only that, but also to promote the opportunity that are available in East Africa to be known by everybody in our country and for that I think Honourable Mwakyembe and Honorable Ambassador Mahiga will be ready to receive me and to sit down with me to come up with the very good media stratergy in responce with the question. (Applauses)*

*Thank you Honorable Speaker. (Applauses)*

***HON. SPEAKER:****Thank you very much. Honorable Sixtus Mapunda.*

***HON. SIXTUS R. MAPUNDA:*** *Thank you Honourable Speaker for giving me this chance.*

*Mr. Salum, one of the issue affecting cooperation and common stand in East African Community is the signing of Economic Partnership Agreement. Can you tell this House your views about the position of our country as a sovereign state basing on statism, self help and survival?*

***HON. SPEAKER:*** *Can you respond to that question candidate?*

***MR. SALUM MWALIMU JUMA:*** *Honourable Speaker, thank you. It is true that one of the challenges that we are currently facing in East African Community is the signing of Economic Partnership Agreement which is known as EPA. But let me say one thing, as a nation we have to have our own position. It is very true when you look at it as something that can provide market opportunity for our local producers but when you look deeply in EPA you can see that we have to provide or to open access for European market to about 80 percent of our market and then they will provide the free market to our product.*

*But again Honourable Speaker and Members of the Parliament, this thing is very sensitive not only for our producers but even to our sovereignity as a state. I don't think we should run. I completely agree with the position of the government right now, we should not run to sign EPA until when we are assured that the opportunity that we are given by the European Union is very fair and will actually ending up supporting our local producers and not otherwise. It is not everything we are offered by Europeans we should easily accept it.*

***HON. SPEAKER:*** *Thank you, thank you candidate, thank you very much.*

Waheshimiwa Wabunge, kwanza naongeza muda hadi tutakaporidhika kwamba zoezi hili limekwenda vizuri. Kwa hiyo, tuendelee kuwa pamoja.

*Candidate now I am giving you the last two minutes to wind up your presentation and then after that I will ask you to leave.Please can you proceed!*

***HON. SALUM MWALIMU JUMA:*** *Honorable Speaker, right Honorable Prime Minister, Honorable Leader of Opposition, this is Salum Mwalimu. You knew Salum Mwalimu not today, we have been working together, as I said in my initial explanation, that I started as a journalist whereby I had an opportunity to work with some of you. Again I had an opportunity to work with Vodacom Tanzania whereby I had an opportunity to work with you and now as a politician as well we are working together.*

*My commitment, passion, integrity and respect in my country have never been questionable at any point of time in my life. The same Salum Mwalimu I promise you that I am going to be your representative, as a country and not from my party neither from anybody else. When we are crossing the border, we have only President John Pombe Magufuli and when we are crossing the border we have only one Prime Minister Kassim Majaliwa Majaliwa, when we are crossing the*

*border we have only one Leader of Opposition from Tanzania, Freeman Aikaeli Mbowe the role and the responsibility of protecting their image and reputation of our country is the role of everybody of us. (Applause)*

*So I guarantee you, I am going to be a country representative and not otherwise. I humbly request for your votes. Please, remember Salum Mwalimu while you are voting.(Applauses)*

***HON. SPEAKER:** Thank you very much candidate. Now, I am asking you to leave. Please order! Order! Now you can leave.*

***MR. SALUM MWALIMU JUMA:** Thank you Honorable Speaker.*

**SPIKA:** Ahsante sana, Katibu, sasa ni wakati wako.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, tunaomba kengele ipigwe. Waheshimiwa Wabunge, tunaomba mtulie kidogo ndani. Wakati kengele inapigwa, nitaomba walioandaliwa walete masanduku ya kura karibu na meza hii, tutayaonyesha. Naomba Maafisa Wasaidizi mliopo mkae katika mistari mliyopangwa.

Mheshimiwa Spika, wakati zoezi likiendelea, lengo letu ni kupata akidi kwa mujibu wa Ibara ya 94 kwamba Mkutano huu ni halali kufanya uamuzi. Nitaomba nichukue muda kidogo niielezee karatasi ya kura. Wenzangu kwenye *control room* naomba wanioneshe karatasi ya kura ili niweze kutoa melezo kwa ufupi.

Waheshimiwa Wabunge, mnaona karatasi yangu ya kura inaonekana, ina majina yote sita yamepangwa kwa utaratibu wa *alphabet,* inaanza na Profesa Safari, anakuja Mheshimiwa Wenje, Josephine Sebastian, Lawrence Kego Masha, Pamela Simon Massay na Salum Juma Mwalimu. Unachotakiwa kufanya ni kuchagua au unapiga kura mbili.

Narejea tena, unapiga kura mbili kwa kuweka alama ya vema kwenye kisanduku kilicho sanjari na jina la mgombea, unapiga kura mbili (hiyo ni tafsiri ya Kanuni) pembeni au sanjari ya jina la kila mgombea. Ukipiga kura tatu, kura yako imeharibika. Narejea tena, ukipiga kura tatu, kura yako imeharibika. Nadhani nimeelezea kiasi cha kueleweka.

Mheshimiwa Spika, karatasi hii ya kura itapatikana kwenye meza ya Bunge. Utaratibu ulioandaliwa ni kwamba tunaanza na meza mbili au mistari miwili, mstari wa kwanza aliko Waziri na Mkuu wote walioko katika mstari huo watakuja kupiga kura. Mstari wa pili ni wa Kiongozi wa Upinzani. Ni mstari mmoja tu, halafu tutawaeleza utaratibu mwingine wa kufuata.

Mheshimiwa Spika, Maafisa watakuwa wameandaliwa, watakaa kwenye kila mstari watawaondoa Wabunge kwenye kila mstari kwa utaratibu watakuja mbele, Mbunge atapewa karatasi ya kura, atapiga kura. Wapigaji kura watakuwa ni wanne kwa wakati mmoja na masanduku ya kura yatakuwa yako mezani.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa ambao wana mahitaji maalum naomba niwataje. Mheshimiwa Ikupa Alex, Mheshimiwa Ally Saleh, Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Riziki Lulida watapelekewa karatasi za kura pale walipo, watapiga kura na watatumbukiza katika masanduku ya kura yatakayokuwa pembeni watakapokuwa wakipiga kura.

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo utaratibu ambao umeandaliwa kwa uchaguzi huu. Naomba twende vizuri na nina hakika tunaweza kumaliza kama tutakwenda haraka. Tunaomba Waheshimiwa mtulie na mtaongozwa mstari kwa mstari katika kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa tupate orodha ya akidi iliyoko ndani ili tujue kama

Mkutano wetu ni halali kuendelea na utaratibu wa uchaguzi. Naomba akidi.

Mheshimiwa Spika, nimejulishwa kwamba Wabunge mliopo ndani kwa wakati huu ni 280. Akidi inayotakiwa ni 197. Kwa hiyo, Mkutano huu ni halali kufanya uamuzi. Naomba sasa tufanye zoezi la pili.

Tunaomba masanduku ya kura yainuliwe yaonyeshwe; kama Mjumbe ana wasiwasi na mwonekano wa sanduku atuambie labda kuna kura imeng'angania ndani. Tunaomba masanduku ya kura yawekwe katika eneo linalotakiwa, mawili kila upande. Tunaomba Maafisa mjipange katika mistari mliyoelekezwa.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa. Kuhusu Utaratibu.

**SPIKA:** Namtafuta anayeongea, maana waliosimama ni wengi. Hebu ongea huko huko uliko na ujitambulishe wewe ni nani.

**T A A R I F A**

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Spika, naitwa Seif Khamis Gulamali, nataka tu kujua utaratibu wa namna ya kupiga kura pale mbele kwa sababu, kama mlivyotoa maelekezo kwamba kura yetu ni siri sasa tunapokuja kupiga kura hapo, kamera hizi zinatuonyesha hapo. Kwa hiyo, inakuwa tena siyo siri kwa sababu inaonekana nampigia nani. Ningepigia huku, maana yake ingekuwa siri zaidi. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kuna wakati mnapenda kweli kupoteza muda. Hivi hiyo kamera iliyoko hapo juu, inakuona hapo zaidi au inaona huyu aliyeko huku zaidi? Nani anayeonekana zaidi anavyopiga kura kati ya benchi hilo au hawa walioko huku? Hawa walioko huko, inaweza ikamulika hapo zaidi au huku zaidi? *(Kicheko)*

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, tuendelee.

**SPIKA:** Naomba tuendelee na shughuli. Naomba Waheshimiwa kama huna jambo la lazima sana tuendelee na utaratibu. Kwani unaogopa ikijulikana na mtu yeyote umempigia fulani, Watanzania watakufanyaje?

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, tuendelee tu basi.

**SPIKA:** Nawaomba watu wa kamera, mnajua *discipline* ya uchaguzi. Pamoja na kamera ambazo mnaendelea kuchukua picha humu ndani na hatuwazuwii kwa sababu Watanzania lazima waone kitu gani kinachoendelea, tunachowaomba tu msilenge kwenye karatasi ya mpiga kura, ile ni siri ya mpigakura. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Walenge!

**SPIKA:** Sasa Waheshimiwa Wabunge, naomba tusaidiane jambo moja, wenzetu wa Jumuiya ya Ulaya *(EU)* na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge vijana wameandaa mchapalo, *(cocktail party)* hapo nje mara tu baada ya shughuli zetu kwisha. Hapa shughuli zetu zinaweza zikachukua muda kidogo. Sasa naomba tu mwongozo wenu kwa ujumla wake, mnaonaje? Twende hadi mwisho au mkiishapiga kura kwa sababu wale wasimamizi watakuwepo, tuahirishe shughuli ili majibu yatolewe kesho?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo! Ndiyo! Ndiyo! Tunaenda kwenye mchapalo halafu tunarudi.

**SPIKA:** Kwa hiyo, naomba kuhoji kama ifuatavyo:-

**MBUNGE FULANI:** Wakahesabu wenyewe leo leo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, hizi ni kura za CHADEMA tu, ni tofauti na zile kura tulizopiga wakati uliopita. Ni kura ambazo hazitachukua lisaa limoja kuhesabu. Labda useme, wale watakaotaka kuondoka, waondoke, lakini matangazo lazima yatangazwe leo leo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Kwa hiyo, tunafanya hivi, tutapiga kura, tutapata wadhamini, wataenda kuhesabu, kwa anayejisikia kwenda kwenye mchapalo anaweza akawahi akaendelea na mchapalo. Wanaotaka kushuhudia waendelee kubaki na mimi nitakuwepo na tutatangaza matokeo jioni hii hii. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Katibu sasa tuendelee na utaratibu, nilikuwa nashauri tuanze na zile kura nne tu, tuwapate Makatibu wanne wapeleke zile kura nne kwa Mheshimiwa Stella Ikupa, Mheshimiwa Ally Saleh, Mheshimiwa Amina Mollel na kwa Mheshimiwa Riziki Lulida. Hao wanne wapige kura kwanza tuzione hizo nne tu, zikirudi mgawane mmoja mmoja katika wale wanne asiende mmoja tu, muende wanne tofauti. Eeeh, haya kila mtu atawanyike kwa kila mmoja wao.

Aaah, masanduku mnapeleka wapi? Masanduku hapa hapa. Zile kura zitaletwa, watu wote wataona kwamba ni kura moja, kura moja, kura moja. Msiwasimamie hapo ili muone wanavyopiga kura, kaeni pembeni. Wale mnaopeleka kura, kaeni pembeni wapige kura kwa siri.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, swali la uchokozi.

**SPIKA:** Subiri hapo hapo ukishapiga kura yako. Nimekuona lakini subiri kidogo. Nimekuona.

Na wewe jiunge hapo. Tunamsubiri wa nne. Yuko wapi? Yule wapi yule wa nne? *Okay!* Jiunge na wenzako pale. Eeh, jiunge hapo.

Waheshimiwa Wabunge, hizi ndiyo zile kura nne tulizosema za Mheshimiwa Ikupa Alex, Mheshiniwa Ally Saleh, Mheshimiwa Amina Mollel na Mheshimiwa Riziki Lulida. Nadhani mnaniruhusu sasa watumbukize kwa niaba yao, si ndiyo! Haya tumbukizeni hapo. Siyo lazima kwenye sanduku moja, sanduku lolote tu. Ahsante sana.

Baada ya hapo sasa namuachia Katibu aendelee na wengine wote. Ila kabla Katibu hujaendelea, ulisimama Mheshimiwa.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshmimiwa Spika, samahani. Nilikuwa naomba baada ya upendeleo kwa watu wenye ulemavu, basi wapewe upendeleo wale akina mama wanaonyonyesha ili wapige kura baadae wakawahi watoto. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Katibu, tuendelee na utaratibu.

**DKT. THOMAS KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba sasa tuanze, mstari wa kwanza ni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunaomba mstari wote mje kupiga kura. Mstari wa Kiongozi wa Upinzani tunaomba wote mliosimama pale, mje kupiga kura. Mheshimiwa Waziri wa Maji tunaomba urudi kidogo.

Sasa tunaweza tukaendelea kama mlivyojipanga, samahani sana. Waheshimiwa tunaomba msogee, ni kutengeneza tu mstari usiwe mrefu sana, kulia na kushoto.

**SPIKA:** Kwa upande wangu wa kulia ukifika kwa Waziri Mkuu ubaki hapo hapo, usimame hapo kwa Waziri Mkuu mpaka ukiona nafasi ndiyo usogee na upande huu ukifika kwa Kiongozi wa Upinzani usipitilize, bakia hapo hapo mpaka ukiona nafasi ndiyo usogee.

Yule mtu wa *IT* wa Bunge, onesha Bunge na siyo kuonesha hapo wanapopiga kura. *(Makofi/Kicheko)*

Kushoto kwangu, Makatibu wazuieni hapo, asivuke mtu mpaka kuwe na nafasi hapo ya kupiga kura ndiyo asogee mbele. Kushoto kwangu usitoe karatasi mpaka kuwe na nafasi ya mtu huku.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Utaratibu umeanza kuvurugwa.

**SPIKA:** Mnaotoa karatasi za kura msitoe mpaka pawe na *vacancy*, maana yake utaratibu ukivurugika ni ninyi mnaotuvuruga. Usitoe karatasi mpaka pawe na nafasi ya kupiga kura. Kama nilivyosema, kwa wale Waheshimiwa ambao mmeshapiga kura na mnaona mnaweza mkapata chochote kitu, kuna mchapalo hapo nje.

Nakuomba Mheshimiwa Naibu Spika kama utaweza kujiunga na wenzetu wa *European Union* pale na utuwakilishe na Waheshimiwa Wabunge kama umeshapiga kura ruksa kupata chochote kitu pale halafu baadaye tena unarudi humu ndani au ukaamua kwenda moja kwa moja, yote ruksa tu. Wale ambao wanataka kubaki na sisi waendelee kubaki na sisi.

Mheshimiwa ambaye hujapata karatasi sasa sogea mbele. Wewe mwenyewe mtoa karatasi sogea hapo mbele sasa, kwa sababu mstari wako ni huo unaokuja huko sasa.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Ndaki anawaomba kama kuna Mbunge yeyote ameokota funguo za gari, itakuwa ni gari yake alete hapa mezani ili tuweze kumpatia. Ufunguo wa gari endapo kuna Mheshimiwa yeyote ameuona mahali au ameokota anaweza kutuletea kwa Katibu hapa mezani ili tuweze kumpatia Mheshimiwa Ndaki. Tuendelee kupiga kura, naona tunaendelea vizuri, karibu tutamaliza zoezi.

Katibu wangu wa kulia huku unatoa karatasi nyingi kwa wakati mmoja, toa karatasi pale tu panapokuwa na nafasi ya kupiga kura ambayo iko wazi.

Ahsante sana, picha ninayopata hapa ni kwamba Wabunge wote wameshapiga kura Makatibu, sogeeni pembeni kabisa kwanza. Eeh, sogeeni kwangu huku.

Mheshimiwa Mbowe na Mheshimiwa Jenista Mhagama mpaka sasa, kila mmoja kwa nusu dakika, tuwasikie. Mpaka sasa *are you okay?* Mheshimiwa Mbowe.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE - KIONGOZI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi *process* ni salama na sahihi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jenista Mhagama, mpaka sasa?

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, kama kawaida ya viwango vyako vya usimamizi na upangaji wa mambo na umahiri wako katika kazi hii ya Uspika na usimamizi wa shughuli za Bunge, mpaka sasa tuko sawa sawa kabisa na umelisimamia jambo hili vizuri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, nashukuru. Katibu kinachofuata.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, sasa ni kupata Mawakala kutoka upande wa Chama Tawala na Chama cha Upinzani na wagombea wenyewe au kama wanawateua wawakilishi. Baada ya hapo, tunakwenda kwenye zoezi la kuhesabu kura.

**SPIKA:** Ahsante. Naomba wagombea waruhusiwe sasa na *Sergeant-At-Arms* waingie hapa ndani wote. Hamkuwaweka kwenye chumba maalum hapo jirani au wameenda kwenye mchapalo! *(Kicheko)*

Karibuni sana wagombea kama mko, karibu hapo. Wagombea, mnakaribishwa tafadhali. Ahsante sana. Mnaweza kusimama hapo hapo. Karibuni sana wagombea. Kuanzia sasa ndiyo tunaanza ile *process* ya kuhesabu kura.

Kura zimeshapigwa, maboksi hayo manne mnayoyaona hapo ndiyo yenye kura zenye uamuzi wa nani ni nani katika zoezi hili.

Sasa tuanze na wale Wawakilishi wa Kambi. Katibu ulisema mmoja kila upande, au! Lakini ili kufanya zoezi hili liwe zuri zaidi, nami nawaongezeni tena mmoja, yaani upande huu leteni wawili na CCM leteni wawili. Tutajieni wasimamizi *apart from* watakaowataja wao.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE - KIONGOZI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshiniwa John Mnyika na Mheshimiwa Kunti Yusuph.

**SPIKA:** Nawaomba Mheshimiwa Kunti na Mheshimiwa John Mnyika msogee mbele, mje msimame hapo mbele ya Kiongozi wa Upinzani. Mheshimiwa Jenista kwa upande huu.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, tutampeleka Mheshimiwa Ester Mahawe na Mheshimiwa Khadija Aboud.

**SPIKA:** Nawaomba watajwa wasogee hapa mbele. Karibuni sana Mheshimiwa Ester na Mheshimiwa Khadija, karibuni sana mkae hapo mbele ya dawati la Mheshimiwa Waziri Mkuu, msimame hapo. Karibuni hapo mbele, mbele zaidi, karibu na kwa *PM* hapo ili kila mtu awaone. Sogeeni tu, msiyaogope hayo masanduku, ndiyo kazi yenu, ndiyo maana mmeitwa. Eeh, hapo hapo hapo.

Sasa Wagombea mnaruhusiwa ama kwenda ninyi wenyewe ama kutuma wawakilishi wenu. Kwa hiyo, twende kama tulivyokuwa tunaingia hapa ndani. Tuanze na Profesa Safari halafu anayefuata, anayefuata. Kama unaingia mwenyewe au kama mwakilishi, ruksa.

**PROF. ABDALLAH JUMBE SAFARI:** *(Aliongea bila kutumia kipaza sauti).*

**SPIKA:** Profesa, sasa bahati mbaya hayupo, inabidi uangalie katika walioko humu ndani. Nenda mwenyewe Profesa, eeh kabisa! Upendo tafadhali songa mbele ahsante, aliyefuata tafadhali mtajwa njoo mbele. Anayetajwa maana yake ukimtaja mtu maana yake wewe hutashiriki huku ndani utakaa nje kusubiria.

Aliyefuata! *Thank you,* songa mbele huku, sogea.

Anayefuata, tafadhali Mheshimiwa Halima jiunge nasi. Anayefuata, ahsante, songa mbele, ahsante sana. Eeh, Pamela, Pamela, *sorry.* Ahsante, songa mbele. Ahsante sana.

Basi kwa ninyi nawaruhusu. *Sergeant* kuna chumba chetu mahali pale, wanaweza wakakaa kwenye chumba chetu kulia pale, hawa wagombea wakapumzika pale ili wasi-*hang*. Ahsante sana. Basi Katibu sasa maelekezo yako ili zoezi liweze kuendelea.

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Kuna chumba kilichoandaliwa nyuma yangu hapo, *Speaker's Lounge.* Msiondoke kwanza, yabebeni hayo masanduku. Mnaobeba, wale Makatibu kila mmoja awe na lake, baada ya hapo twende upande mmoja. Upande gani tunaenda? Ehe, haya. Tufuatane na myasindikize masanduku ninyi wenyewe. Karibuni sana na mnaruhusiwa kupata chai ya Spika huko. Kuna mchapalo mdogo huko ndani. *(Kicheko)*

Katibu tunakuomba timu yako ifanye *chap chap* kwa sababu bahati nzuri kura za leo wala siyo nyingi. Wanahesabu kura mbili mbili tu, naamini hata nusu saa inaweza isifike tutakuwa tumeshapata majibu.

Nashukuru sana Mheshimiwa Jenista wewe unaweza kubaki, lakini Mheshimiwa Mbowe akitaka anaweza akatoka kidogo. *(Kicheko)*

Ahsante sana, nawashukuru. Sawa sawa. *(Kicheko)*

*(Hapa zoezi la kuhesabu kura lilianza)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nafurahi kuwafahamisha kwamba zoezi la uhesabu kura limekamilika. Kwa hiyo, sasa ni wakati muafaka tumruhusu Katibu wetu ambaye ndiye Msimamizi wa Uchaguzi aweze kutusomea matokeo ya kazi yetu. Katibu wa Bunge, tafadhali.

## MATOKEO YA UCHAGUZI

**DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba sasa nitoe matokeo ya uchaguzi Kundi C - Vyama vya Upinzani Chama cha CHADEMA kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, idadi ya Wabunge wote Kikatiba ni 393, idadi ya Wabunge waliopo na kuapishwa 391, idadi ya kura zilizopigwa 296, idadi ya kura halali 296, hakuna kura iliyoharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo ya kura ni kama ifuatavyo:-

(a) Profesa Abdallah Jumbe Safari amepata kura 35;
(b) Ezekia Dibogo Wenje amepata kura 34;
(c) Josephine Sebastian Lemoyan amepata kura 219;
(d) Lawrence Kego Masha amepata kura 44;
(e) Pamela Simon Massay amepata kura 200; na
(f) Salim Mwalimu Juma amepata kura 59.

Matokeo haya yamethibitishwa na Wasimamizi wa uchaguzi na wametia saini zao katika karatasi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo basi, Mheshimiwa Josephine Sebastian Lemoyan na Mheshimiwa Pamela Simon Massay ndio washindi wa uchaguzi huu. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, ni vizuri kuweka kumbukumbu sahihi, kwa kuwa hawajatangazwa kuwa washindi. Kwa hiyo basi, kwa mamlaka niliyopewa chini ya Kanuni ya 13(b) ya

Nyongeza ya Tatu ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, napenda kuwatangaza Wabunge hao kuwa ni Wabunge wa Bunge la Nne la Afrika Mashariki. *(Makofi/ Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo na matokeo haya naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa matokeo ya uchaguzi huu wa leo, napenda kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekamilisha kazi yake ya kuchagua Wabunge tisa wa Bunge la Afrika Mashariki kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Ibara ya 50 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wajumbe waliochaguliwa na Bunge hili katika uchaguzi uliofanyika tarehe 4 Aprili na uchaguzi uliofanyika leo tarehe 10 Mei, 2017 ni kama wafuatao:-

Mheshimiwa Fancy Haji Nkuhi, Mheshimiwa Happiness Elias Lugiko, Mheshimiwa Dkt. Abdullah Hasnu Makame, Mheshimiwa Mariam Ussi Yahya, Mheshimiwa *Engineer* Habib Mohamed Mnyaa, Mheshimiwa Dkt. Ngwaru Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Adam Omari Kimbisa, Mheshimiwa Josephine Sebastian Lemoyan na Mheshimiwa Pamela Simon Massay. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukurani kwako wewe binafsi kwa kuongoza kikao hiki vizuri na kwa kuzingatia Kanuni.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Taarifa.

**SPIKA:** Ahsante sana, Katibu wa Bunge. Nami napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana kwanza Wagombea wote waliojitokeza kugombea nafasi hii ya kutuwakilisha kama Wabunge katika Bunge la Afrika Mashariki kupitia vyama mbalimbali, kutoka kwenye michakato ya ndani ya vyama na hata wale ambao waliweza kufika hatua ya kufika mbele ya Bunge letu na kupigiwa kura na Waheshimiwa Wabunge, nawapongeza wote kabisa kwa kujitokeza kutumia haki yao ya kidemokrasia na

ninavipongeza vyama kwa michakato mbalimbali ambayo wameitumia katika kuleta wagombea. Kipekee nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwachekecha na kuwachuja na kuona hawa tisa waliosomwa na Msimamizi wa Uchaguzi kwamba ndiyo waliochaguliwa na Bunge hili kutuwakilisha katika Bunge la Afrika Mashariki kwa miaka mitano ijayo.

Kwa hiyo, nawapongeza sana waliochaguliwa na ninawaomba wale ambao hawakupata fursa hii wasivunjike moyo, huu ndiyo utaratibu wa demokrasia yetu. Tuendelee kujaribu wakati mwingine, nafasi nyingine zikitokea. Bunge hili kama alivyotangaza Katibu, katika Wabunge wale tisa wanaokwenda Afrika Mashariki, watano ni wanawake na wanne ni wanaume. *(Makofi/Vigelegele)*

Kwa hiyo, cha muhimu tu kwetu sisi kwa Wabunge wote hawa tisa na kipekee kwa Wabunge hawa wanawake waende kule wakatubebe kwa heshima kubwa. Wakienda kuleta za kuleta kule, safari ijayo sidhani kama Bunge hili litaenda njia hiyo. Kwa hiyo, wanabeba dhamana kubwa sana. Uzoefu umeonesha wanaume hawana matatizo. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli kwa muda ulipofika hapa na kwa kuwa shughuli ambazo tulipanga siku ya leo zimekamilika, naomba sasa nichukue fursa hii kuwataarifu kwamba kesho tutaendelea na Wizara ya Maji, mijadala kama kawaida na kesho kutwa pia. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote ambao mmejiorodhesha, kwa kiasi kikubwa karibu wote mtaongea katika Wizara hii muhimu sana kwa zile siku tatu ambazo tulikuwa tumezipanga tangu mwanzo.

Kwa jinsi hiyo basi, nichukue fursa hii sasa kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 3.54 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 11 Mei, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*